

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Ishirini na Nane – Tarehe 15 Mei, 2019

(Bunge Lillianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Tukae. Katibu!

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani:-

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Randama za Makadirio ya Mapato na matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali. Tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, sasa aulize swali lake.

Na. 230

**Kununua Hospitali ya Wilaya inayomilikiwa na
Kanisa la KKKT**

MHE. OMARI M. KIGUA aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa Wilaya ya Kilindi haina Hospitali ya Wilaya lakini wanayo Hospitali ya Rufaa inayomilikiwa na Kanisa la KKKT, lakini watumishi wote na huduma zote za Hospitali hiyo zinagharamiwa na Halmashauri ya Wilaya (*DED*) na wao KKKT ni wamiliki wa majengo:-

Je, Serikali haioni imefika wakati wa kufanya makubaliano ya kununua Hospitali hiyo ili kupunguza gharama kwa Serikali ya kujenga Hospitali ya Wilaya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA
SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2010 Serikali kupitia Halmashauri ya Kilindi iliingia mkataba na Kanisa la Kilutheri Dayosisi ya Kaskazini Mashariki kwa lengo la kutumia majengo yanayomilikiwa na kanisa hilo kwa ajili ya utoaji wa huduma za afya kwa wananchi wa Kilindi. Hospitali hiyo Teule ya Wilaya (*DDH*) ya Kilindi inahudumia wananchi wapatao 264,000. Serikali inatumia utaratibu huo ikiwa ni ushirikiano na Taasisi binafsi yakiwemo Mashirika ya Dini pale ambapo hakuna Hospitali ya Wilaya ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hospitali hiyo, Serikali inalipa mishahara ya baadhi ya watumishi walioajiriwa na Serikali na kupeleka fedha kwa ajili ya uendeshaji wa hospitali ambazo zinatumiwa kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, hospitali hiyo

iliidhinishiwa shilingi 153,646,500/= kutoka Mfuko wa Pamoja wa Afya ambapo ni asilimia 25 ya fedha zote za Mfuko wa Afya kwa Hospitali ya Wilaya. Vilevile, katika mwaka wa fedha 2019/2020, hospitali hiyo imetengewa jumla ya shiligni 153,646,500/= kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haina mpango wa kununua Hospitali ya Wilaya ya Kilindi inayomilikiwa na KKKT. Mpango wa Serikali ni kuhakikisha kila Halmashauri inakuwa na Hospitali ya Halmashauri ya Serikali. Pale ambapo bado Serikali haijajenga, itaendelea kushirikiana na sekta binafsi kama inavyofanyika sasa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Omari Kigua, swali la nyongeza.

MHE. OMARIM. KIGUA: Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kabisa nami naungana na Serikali kwamba kuna umuhimu wa Serikali kushirikiana na sekta binafsi katika kuwaletea Watanzania huduma. Pamoja na hali hiyo, zimejitokeza changamoto nyingi sana sana katika Hospitali hii ya KKKT mojawapo ni suala la utawala.

Swali: Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari sasa kuangalia utaratibu ulio mzuri ili dhana hasa ya ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi iweze kufikiwa? (*Makofi*)

Swali la pili, kwa kuwa Kilindi haina Hospitali ya Wilaya: Je, Serikali iko tayari sasa kuitengea fedha Wilaya ya Kilindi ili iweze kupata Hospitali ya Wilaya? Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa

Naibu Spika, ni azma na lengo la Serikali kuhakikisha kwamba zile hospitali ambazo tunashirikiana katika kutoa huduma kwa maana ya *DDH*, suala la utawala bora inakuwa ni kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawe ni shuhuda kwamba katika swali lake amesema kuna tatizo la utawala. Sasa ni vizuri Mheshimiwa Kigua tukitoka hapa tuelekezane hasa tatizo ni nini ili tuweze kutoa ufumbuzi ili wafanyakazi nao waweze kuona ni sawa na ambavyo wanafanya katika hospitali zetu za Wilaya. Kwa sababu suala la kuwa na utawala bora ni jambo la msingi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kigua atakubaliana na Serikali kwamba azma ya kuhakikisha kwamba hospitali zinajengwa katika maeneo yote ambayo Halmashauri hazina Hospitali za Wilaya inafikiwa. Kwa kuanzia, yeye mwenyewe ni shuhuda, katika bajeti ambayo Bunge lako Tukufu limetupitishia, tumeweza kuwatengea kwa kuanzia shilingi milioni 200 kwa ajili ya kujenga Kituo cha Afya cha Msente. Naamini baada ya kuhakikisha kwamba tunakamilisha ujenzi wa hospitali 67 tulizoanza nazo na 52, hakika naomba nimtoe shaka kwamba na Kilindi tutakwenda. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa, nimwite Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa Bunga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 231

Hitaji la Barabara – Tarafa ya Mgeta Mvomero

MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA aliuliza:-

Barabara zinazotoka Kidiwa hadi Tandali, Daraja la Mgeta hadi Likuyu, Visomolo hadi Lusungi na Langali *SACCOS* hadi Shule ya Sekondari Langali Tarafa ya Mgeta Wilayani Mvomero zimejengwa kwa nguvu za wananchi, lakini bado

hazipitiki kutokana na vikwazo vya miundombinu na madaraja:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara hizo ili kuondoa adha wanazopata wananchi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Jasmine T. Bunga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kidiwa – Tandali – Maguruwe yenye urefu wa kilometa 13.8 imefanyiwa upembuzi yakinifu na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (*TARURA*) na kubaini zinahitajika shilingi bilioni 2.81 kwa ajili ya matengenezo makubwa (*Rehabilitation Works*) kwa kiwango cha zege katika sehemu za maeneo ya milimani na ujenzi wa miundombinu ya madaraja. Serikali inaendelea na mpango wa kutafuta fedha kwa kizingatia uwingi wa fedha zinazohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 34.6 kwa ajili ya matengenezo ya muda maalum (*Periodical Maintenance*) kwenye barabara za kibaoni – Lukuyu na barabara ya Visomoro – Bumu – Mwalazi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa daraja (*vented drift*) katika Mto Songa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Jasmine Bunga, swali la nyongeza.

MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri yenye matumaini hasa kwa mwaka huu kutengewa hizo shilingi milioni 34, lakini hii barabara ya Kidiwa - Tandali

imeshafanyiwa upembuzi yakinifu, ingawa sasa hizo fedha zitatafutwa mpaka lini? Hapo sasa napenda kufahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba Tarafa ya Mgeta kama alivyotembelea miaka ya nyuma, *landscape* yake bado ni ile ile ya milimani na watu wanaishi milimani. Kwa sasa tunategemea barabara hii kubwa moja toka Sangasanga kwenda mpaka Nyandila - Kikeo. Barabara hii ni mbovu sana hasa wakati wa masika; na tulishaahidiwa. Nakumbuka miaka ya 1970s alipokuja Mheshimiwa Abdu Jumbe aliahidi kwamba tutatengenezewa kwa kiwango cha lami. Ni kweli naweza nikalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Rais Mstaafu, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete alipokuja aliahidi kwamba barabara hii itatengenezwa kwa kiwango cha lami kulingana na ubovu wake na nauli inakuwa kubwa: Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kujenga barabara hii ya Sangasanga mpaka Nyandila kwa kiwango cha lami?

Swali la pili. Katika kutatua changamoto za usafiri katika Tarafa hii ya Mgeta, wananchi wamejitolea kutengeneza barabara nyembamba za kupita pikipiki, lakini wanakutana na changamoto ya utaalumu; wakati mwingine hawajui barabara iende hivi, kwa hiyo, wanakutana na changamoto hizo, lakini pia wanakutana na changamoto sehemu nyingine inabidi ijengwe madaraja au karavati.

Je, Serikali sasa iko tayari kuungana na wananchi hawa wa Tarafa ya Mgeta ili kupeleka wataalam pamoja na kuwajengea madaraja ili tuweze pia kutumia usafiri wa pikipiki kuunganisha vijiji na Kata? Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Naibu Spika, machozi tuliyoshuhudia yakitoka kwa

Mheshimiwa Mbunge wa Mlimba pale, yanatosha kwa Mkoa wa Morogoro. Kwa hiyo, isingependeza tukapata machozi mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Dkt. Tisekwa akubaliane nami kwamba ahadi zote zinazotolewa na Viongozi Wakuu kwa maana ya Marais, hata kama Rais aliyetangulia ndio aliyetoa ahadi, sisi kama Serikali, ahadi hizo tunazitunza na ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba ahadi za viongozi wetu tunazitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Mheshimiwa Mbunge atakuwa shuhuda, katika ahadi ambazo zimetolewa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, katika bajeti ambayo tumepitisha, tumeanza kutekeleza katika maeneo yote ambayo ahadi zimetolewa. Tumeanza kujenga lami kwa kilometa moja moja. Kwa muungwana ahadi ni deni, naomba nimtoe mashaka Mheshimiwa Mbunge, tutatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili suala la pili ambapo wananchi wameanza kutengeneza barabara kwa ajili ya kupita angalau kwa pikipiki, lakini kinachokosekana ni utaalim, naomba nichukue fursa hii kumwagiza *coordinator* wa Mkoa wa Morogoro ahakikishe kwamba anamwagiza Meneja wa Wilaya husika ili kwenda kutoa utaalim ili wananchi pale ambapo wanatoa nguvu yao isije ikapotea na aone namna ambavyo na Serikali tunaweza tuka-*complement* ili kazi nzuri iweze kuonekana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Antony Komu, swali la nyongeza.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kama ilivyo kwenye swali la msingi, kule Moshi Vijijini katika Kata ya Mabogini iko barabara inayotoka Mabogini inakwenda Chekereni mpaka Kahe. Ile barabara huwa inakarabatiwa na wananchi na wakati mwingine na *TARURA* lakini kwa fedha kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kuuliza swali la msingi hapa, nikaahidiwa kwamba *TARURA* inao mpango mkubwa wa kuifanyia kazi hiyo barabara ili iweze kupitika katika kipindi chote cha mwaka. Sasa hivi tunavyoongea, ile barabara haipitiki kabisa kwa sababu imebadilika kuwa mfereji. Naomba ...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Komu, uliza swali tafadhali.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumwuliza Naibu Waziri, ni lini hiyo kazi ya kuitengeneza hiyo barabara itaanza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ni jana tu Mheshimiwa Komu aliuliza swali kuhusiana na barabara ya Jimboni kwake na tukakubaliana kwamba ni vizuri tukaenda kwenye uhalisia. Naamini na hili anaongezea ili wakati tutakavyokuwa tunaenda Moshi tukashughulikia barabara zote mbili, tukitizama tujue suluhu ipi ambayo inatakiwa? Tujue tukiwa *s/te*. Mheshimiwa Komu, naomba niipokee katika lile la jana na la leo, kwa hiyo, tunakuwa na barabara mbili.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Daimu Mpakate, swali la nyongeza.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Tatizo lililopo kwenye Tarafa ya Mgeta linafanana kabisa na tatizo lililopo kwenye katika Tarafa ya Namasakata, katika Jimbo la Tunduru Kusini. Barabara ya Chemchem - Ligoma inazaidi ya miaka 10 tangu 2007 haijawahi kutengenezwa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza barabara ile ili wananchi waweze kufaidika na Uongozi wa Awamu ya Tano.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge ni mashuhuda kwamba tangu tulivyoanzisha chombo chetu kwa maana ya *TARURA*, wengi wamekuwa wakipongeza ufanisi ambao umetokana na chombo hiki. Kwa hiyo, ni vizuri sasa tusiishi kwa historia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni vizuri tukawasiliana na Meneja wa *TARURA* ili atupe uhalisia katika barabara hii ambayo anaongelea na hiyo miaka 10 ambayo iliahidiwa, hakika kwa Serikali ya Awamu ya Tano tunaahidi na kutekeleza.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Allan Joseph Kiula, Mbunge wa Iramba Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 232

Umeme wa REA – Vijiji vilivyopo Wilayani Mkalama

MHE. ALLAN J. KIULA aliuliza:-

Serikali ya Awamu ya Tano inatekeleza mpango kabambe wa kusambaza umeme vijijini chini ya mpango wa *REA*:-

(a) Je, ni lini vijiji vyote 70 vya Wilaya ya Mkalama vitapata umeme wa *REA II*?

(b) Je, Serikali ipo tayari kuweka umeme katika vitongoji vinavyopitiwa na njia ya umeme wa *REA*?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Allan Joseph

Kiula, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) inatekeleza dhamira yake ya kufikisha umeme katika vijiji vyote nchini ifikapo mwezi Juni, 2021 vikiwemo vijiji 70 vya Wilaya ya Mkalama. Katika Awamu ya Pili ya utekelezaji wa mradi wa kusambaza umeme vijijini (*REA II*), jumla ya vijiji 14 vya Wilaya ya Mkalama viliwekwa katika mpango wa utekelezaji wa kupatiwa umeme kupitia Mkandarasi *M/S JV EMEC & Dynamics*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2019 vijiji vinne vya Nkito Kinyantungu, Nkito Nkurui, Ibaga Sekondari na Ibaga *Centre* viliwashwa umeme na wateja zaidi ya 100 wameunganishwa umeme. Kwa sasa, Mkandarasi anaendelea na kazi ya kuunganisha umeme katika vijiji 10 vilivyobaki ambapo kazi hiyo itakamilika ifikapo mwezi Juni, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji na vitongoji vilivyopitiwa na miundombinu ya umeme katika Wilaya ya Mkalama vimejumuisha katika mpango wa kupatiwa umeme kupitia Mradi wa Ujazilizi (*densification*) awamu ya pili unaotarajia kuanza mwezi Julai, 2019. Aidha, mradi huo utahusisha pia kuvipatia umeme vitongoji vyote vya Wilaya ya Mkalama vilivyopitiwa na njia za umeme kupitia utekelezaji wa mradi wa *REA III* mzunguko wa kwanza unaoendelea. Mradi huu utakamilika mwezi Juni, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Allan Kiula, swali la nyongeza.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa tena nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Namshukuru Naibu Waziri alishafika maeneo hayo na kesho Mheshimiwa Waziri atakuwa yuko Mkalama kwa suala hili hili.

Maswali mawili ya nyongeza; katika suala zima la mradi wa ujazilizi hasa katika vijiji vya Iguguno, Kinyangiri, Nduguti, Gumanga, Iyambi, Nkalakala, wananchi wameshaelimishwa? Kwa sababu wananchi wanalalamika. Sasa *REA* wamechukua hatua gani kuwaelimisha wananchi kwamba ujazilizi unakuja? (*Makofi*)

Swali la pili. Ziko sehemu ambazo umeme umeshawaka, lakini kumekuwa na maeneo ambayo yamerukwa na Naibu Waziri anafahamu na alifika. Ni lini umeme utawaka kwenye Kanisa la *TAG Ibag*a, Mkalama Kituo cha Afya, Matongo, Kijiji cha Kidi na Kitongoji kimoja cha Gumanga?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana kwa kazi nzuri anayoifanya. Ni kweli tuliambatana pamoja katika maeneo ya Nkito kama ambavyo nimeyataja katika swali langu la msingi, Ibag na tukawasha umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maswali yake mawili, ameulizia mradi wa ujazilizi. Kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, ni kwamba Mradi wa Ujasilizi awamu ya pili unaanza Julai, 2019 kwa gharama za shilingi bilioni 197 kwa mikoa tisa ikiwemo Singida Tabora, Shinyanga, Dodoma, Kilimanjaro, Tanga, Pwani na maeneo mengine.

Kwa hiyo nataka nimthibitishie katika huu ujazilizi ya awamu ya pili katika Vijiji alivyovitaja ikiwemo cha Iguguno na Ibagala vitapatiwa umeme na nataka nielekeze *REA* pamoja na *TANESCO* ifanye uhamasishaji katika maeneo haya na kwamba *TANESCO* Mkoa wa Singida ijipange sasa kwa ajili ya vitongoji vyote ambavyo vinatakiwa viingie katika mradi wa ujazilizi, awamu ya pili, mzunguko wa kwanza na mikoa mingine 16 itapatiwa mradi wa ujazilizi, awamu ya pili, mzunguko wa pili, ambao utagharimu zaidi ya bilioni 460 na mazungumzo yanaendelea na Serikali ya Ufarasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili ameuliza katika maeneo Mbaga na Mkalama kikiwemo na kituo cha afya, nataka nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge, kwa kuwa katika Wilaya ya Mkalama kwa mradi wa REA awamu ya tatu imegusa vijiji 30 na mradi wa REA awamu ya kwanza vilikuwa vijiji 14 na kwa kuwa wilaya yake ina vijiji takribani 70, ni wazi vijiji 26 vitaingia katika rea awamu ya tatu, mzunguko wa pili ambao pia unaanza sambamba mwezi Julai, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi inayoendelea sasa hivi katika Wakala wa Nishati Vijijini ni kuandaa makabrasha kwa ajili ya kutangaza zabuni na kuwapata wakandarasi wa kuanza mradi huu ili iwezeshe nchi yetu ifikapo 2020/2021 Juni, tuwe tumemaliza vijiji vyote nchini ambavyo havikuwa na umeme. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kata ya Lumuma inayotoka Wilaya ya Kilosa ni mashuhuri sana kwa kilimo cha vitunguu, lakini kata hii haina umeme na inategemea umeme kutoka Wilaya ya Mpwapwa ambayo ipo kwenye mkoa mwingine wa Dodoma. Je, kata hii ni lini itapatiwa huduma ya umeme ili iweze kupata huduma ya umeme?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa mama yangu Dkt. Christine Ishengoma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naye pia naomba nimpongeze kwa kufanya kazi nzuri kama Wabunge wengine wa Viti Maalum kufuatilia sekta mbalimbali. Katika swali lake hili la nyongeza ameuliza hii Kata ya Lumuma ambayo ipo

jirani kabisa na Wilaya ya Mpwapwa nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge hata Diwani wa Kata ile mwanamama amekuwa akifuatilia na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kilosa naye nataka nimtaarifu Mheshimiwa na wananchi wote wa Kata ya Lumuma kwamba, tunatambua changamoto hii na kwa kuwa wapo karibu na Wilaya ya Mpwapwa tumeiagiza *TANESCO*, yapo maeneo tumeamua kuwapa *TANESCO* ili wasambaze umeme vijijini na mpaka sasa zaidi ya maeneo 200 yametwaliwa na *TANESCO* ili isaidie *REA* katika kusambaza umeme vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuahidi mama Mheshimiwa Dkt. Ishengoma tutaambatana katika ziara kwenye kata hii ya Lumuma kuelezea ujumbe huu pamoja na *TANESCO* na *REA* na kwamba watapatiwa umeme katika nyakati za kuanzia mwezi Julai, 2019 na kuendelea. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Susan Kiwanga, swali la nyongeza.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Nimeongea na Waziri mara nyingi na akaniahidi kwamba kwenye mradi wa *REA* ambao sasa hivi upo *field* kwenye Kata ya Idete, Shule ya Sekondari Matundu Hill na Shule ya Sekondari Kamwene ambapo mradi unapita pembeni kidogo anasema maeneo haya ni muhimu kupeleka, lakini mpaka leo hakuna jitihada za Serikali.

Je, ni lini sasa Shule ya Sekondari Matundu Hill Idete na Shule ya Sekondari Kamwene watapatiwa umeme ili wanafunzi wa sekondari waweze kujisomea na kupata ufaulu mzuri? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati. majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nijibu swali la Mheshimiwa Kiwanga Susan kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru kwa swali lake zuri, nami nimewahi kufika Idete; katika Idete pale ikiwemo Gereza la Idete limeunganishiwa umeme kwa kutumia ile umeme wa *low cost design*. Kwa hiyo nataka nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge ahadi ya Mheshimiwa Waziri na hapa nitoe malekezo kwa Shule za Sekondari Kamwene na Matundu Hill Idete nimwagize mkandarasi *State Grid* wa Mkoa wa Morogoro atekeleze maagizo ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, agizo hili sio kwa mkandarasi wa Morogoro peke yake na wakandarasi wote nchi nzima, watekeleze agizo la Serikali la kuhakikisha wanapofikisha umeme katika maeneo mbalimbali kama pana taasisi za umma iwe kituo cha afya, iwe mradi wa maji, iwe sekondari waunganishe. Tuliwaeleza *variation* ya namna hiyo inakubalika na Serikali hii ya Awamu ya Tano haiwezi kushindwa kulipa gharama kama inagharimu mradi mzima wa *REA* awamu ya tatu zaidi ya takribani trioni moja na bilioni mia moja. Kwa hiyo, nawaomba wakandarasi watii maelekezo ya Serikali. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jesephine Genzabuke, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Tarehe 10 Agosti, 2018, Waziri wa Nishati alizindua mradi wa *REA* ///katika Mkoa wa Kigoma katika Kijiji cha Lusesa, Kata ya Lusesa na akaahidi kwamba baada ya mwezi mmoja umeme utawaka katika kata hiyo na viunga vyake vinavyozunguka kata hiyo, lakini mpaka leo umeme haujawaka. Nataka nijue ni lini Serikali itaagiza wanaohusika na umeme waweze kuwasha umeme katika kata hiyo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la dada yangu Mheshimiwa Jesephine Genzabuke kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze kwa kweli kwa kazi kama Mbunge wa Viti Maalum kufuatilia masuala ya sekta ya nishati mkoani kwake. lakini kama ambavyo amesema uzinduzi katika Kata ya Lusesa ulifanyika mwaka 2018 mwezi Agosti, ni wazi kabisa kulikuwa na changamoto ya mkandarasi katika Mkoa ya Kigoma na Katavi na niwashukuru Wabunge wa mkoa hiyo pamoja na wananchi kwa subira yao namna ambavyo waliliridhia. Hata hivyo, nataka niseme mkandarasi huyu wa *CCCE Etern* anaendelea na kazi. Hata hivi karibu Mheshimiwa Waziri amewasha vijiji kama vitatu katika Wilaya ya kibondo.

Kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge amesema katika Kata ya Lusesa ambapo imezinduliwa na ahadi ilitolewa na kwamba mpaka sasa hivi bado vijiji vya Kata hiyo ya Lusesa havijawashwa, naomba nilichukue ili niwasiliane na Meneja wa *TANESCO* wa Mkoa wa Kigoma pamoja na mkandarasi, kwa vile uzinduzi ulifanyika kwa kata hii na ni wazi lazima ilikuwa kazi ifanyike kwa haraka na umeme uwake, pamoja na kwamba mkandarasi hana muda mrefu.

Kwa hiyo nitoe maelekezo kwamba agizo la Mheshimiwa Waziri litekelezwe katika Kata hii ya Lusesa, vijiji hivyo ambavyo vimeanishwa viwashwe na nimwahidi Mheshimiwa Mbunge, baada ya hili Bunge la Bajeti, tutafanya naye ziara katika Mkoa wa Kigoma. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa tuendelee na swali la Mheshimiwa Ally Ungando Seif, Mbunge wa Kibiti.

Na. 233

Kupeleka Nishati Mbadala Kibiti

MHE. ALLY S. UGANDO aliuliza:-

Wananchi wanaoishi katika Jimbo la Kibiti hutumia nishati ya mkaa na kuni kwa matumizi ya nyumbani, shuleni, gerezani na kadhalika, hivyo kusababibisha uharibifu mkubwa wamazingira kwa kukata miti hovy:-

(i) Je, Serikali ina mkakati gani wa kupeleka nishati mbadala?

(ii) Je, ni aina gani ya nishati itakayotumka badala ya kuni na mkaa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

WAZIRI WA WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Seif Ungado, Mbunge wa Kibiti, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Sera ya Taifa ya Nishati ya mwaka 2015 (*The National Energy Policy, 2015*) imetoa mwongozo wakuboresha maisha ya wananchi kwa matumizi bora ya nishati kupitia teknolojia ya kisasa badala ya kuni na mkaa. Aidha, Serikali imekuwa ikichukua jitihada za makusudi kuendeleza vyanzo mbalimbali vya nishati ili kuongeza mchango wa nishati mbadala katika upatikanaji wa nishati nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha muda wa kati kuanzia mwaka 2015 hadi 2020, Serikali inatekeleza miradi ya kuzalisha umeme kupitia vyanzo vya gharama nafuu vya maji na gesi ikiwa ni mkakati ya kuwawezesha wananchi kumudu kutumia nishati vya umeme wa gharama nafuu kwa ajili ya kupika badala ya kuni na mkaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza kutekeleza mradi wa kusambaza gesi asilia katika Miji ya Mtwara, Lindi, Pwani na Dar es Salaam ikiwa ni nishati mbadala ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa. Kwa kuwa sehemu ya kuni na mkaa unaotumika katika Jiji la Dar es Salaam huzalisha katika Wilaya ya Kibiti, hatua ya kuanza kutumia gesi asilia kwa kupikia itapunguza uharibifu mkubwa wa mazingira kupitia ukataji miti hovyoya kwa matumizi ya kuni na mkaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua nyingine tarehe 18 Mei, 2018, Serikali kupitia Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) ilisaini kataba nakampuni ya *Mihan Gas Limited* kwa ajili ya kusambaza vifaa vya kupikia, mitungi ya gesi na majiko kwa kutumia *liquidifies Petroleum Gas* au gesi ya mitungi kwa watumishi wa umma na wananchi wengine. Mpango huo pia unalenga kupunguza matumizi ya mkaa na kuni.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ally Seif Ungando, swali la nyongeza.

MHE. ALLY S. UNGANDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa wananchi wa Kibiti wanategemea sana nishati yao ya mkaa na kuni, je, ni lini sasa wataunganishiwa hii gesi asilia katika Miji ya Kibiti, Bungu na Jaribu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Serikali sasa inajenga mradi mkubwa wa umeme kule Mloka wa *Stiegler's*, je wananchi wa Kibiti ambao kwa kiasi kikubwa wanategemea kukata kuni na mkaa wanaweza wakapatiwa upendeleo wa kupata vibarua?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuruku kwa kunipa nafasi ya kujibu swali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ally Seif Ungando, Mbunge wa Kibiti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeza kwa kazi nzuri anayofanya katika Jimbo la Kibiti, hususan katika sekta hii ya nishati. Maswali yake ya nyongeza kwanza ameuliza ni lini sasa Serikali itasambaza gesi katika Wilaya hii ya Kibiti, katika jibu letu la msingi tumesema katika kipindi hiki cha muda wa kati kati ya mwaka 2010 mpaka 2020 tumekuwa tukutekeleza miradi ya muda wa kati na muda mfupi wa kusambaza gesi katika maeneo mbalimbali. Mpaka sasa Mheshimiwa Waziri wa Nishati wiki mbili zilizopita

amezindua uunganishaji wa gesi nyumba mpya 26. Matarajio yetu mpaka ifikapo Septemba, 2019 kuunganisha nyumba kama 333 katika Mkoa wa Mtwara na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mkoa wa Lindi na Pwani, Serikali kupitia *TPDC* imekuja na mradi mkubwa kabambe wa kusambaza gesi asilia. Mradi huu utafanywa na mashirikiano baina ya sekta binafsi na Serikali na kwa sasa hatua ambao imefikia tumeshampata Mshauri Mwelekezi, anaandaa makabrasha na kufanya *feasibility study* ya mradi mzima, matarajio yetu mwezi wa Tano mwakani kuwapata wakandarasi wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri niwakaribishe sekta binafsi katika maeneo mbalimbali ili kujumuika na Serikali katika mradi mkubwa wa kusambaza gesi asilia kwa matumizi ya majumbani na viwandani na hususan katika Wilaya ya Kibiti kwa kuwa nayo imepitwa na bomba la gesi hususan katika maeneo ambayo ameyataja Jaribu, Kibiti maeneo ya Nyamwimbe, Kata ya Mlanzi, maeneo ya Mangwi, Kata ya Mchukwi na maeneo mengine kama ambavyo anafahamu Mheshimiwa Mbunge, kwa hiyo nimwaidi hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali lake la pili Mheshimiwa Mbunge ameuliza mradi wa *Stiegler's Gorge* Rufiji *Hydro Power* unaotekelezwa katika Kata ya Mwaseni, Kijiji cha Mloka. Ni kweli mradi ule una matarajio makubwa ya kutoa ajira na kwa kuwa maelekezo ya Serikali ya Awamu ya Tano kupitia Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, utekelezaji huu wa miradi hii mikubwa ya mikakati, lengo kubwa ni kuzalisha ajira na katika maeneo ambayo mradi unatekelezwa na kwa Watanzania wote kwa ujumla. Kwa hiyo nimwahidi na hata yeye anafahamu, hata zile kazi za awali za madereva zilizotangazwa, zimetangazwa kupitia Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kibiti na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Rufiji na Wakuu wa Wilaya wa Mkoa wa Morogoro. Kwa hiyo ni wazi kabisa kipaumbele kwa watakaokuwa na sifa wanaostahili, lakini zipo kazi za kawaida za vibarua mbalimbali, watapata wananchi wa Kibiti na wananchi wa

Wilaya ya Rufiji na wa maeneo ya Mkoa wa Morogoro. Kwa hiyo hilo kwa kweli halina mjadala, ndivyo ambavyo tumelipangilia. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kuchauka, swali la nyongeza.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Baada ya Mtwara kupatikana kwa gesi Mheshimiwa Waziri akatangaza kwamba Liwale nao tutapata umeme wa gesi kutoka Mtwara. Wakati ambapo Mheshimiwa Waziri anatangaza nikamwomba nikamwambia kwa umeme ule wa Mtwara nafuu Liwale wakatuachia umeme wetu wa mafuta, lakini jambo hilo halikuteklezwa, matokeo yake sasa Liwale umeme unapatikana kwa shida sana.

Je, Mheshimiwa Waziri anatahidi nini sisi watu wa Liwale shida hii tunayoipata mwisho lini? Maana sasa hivi umeme haupatikani kabisa, unawaka masaa mawili au matano.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuruku kwa kunipa nafasi ya kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Kuchauka Mbunge wa Liwale kupitia Chama cha Mapinduzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kuchauka ameelezea katika swali lake la nyongeza kwamba tulitoa ahadi ya kuunganisha Wilaya ya Liwale katika umeme wa gesi, lakini kwa sasa nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge ni kweli kuwa Wilaya ya Liwale kwa mara ya kwanza imeunganishwa na *grid* ya Taifa kupitia Kituo cha Maumbika, lakini tunatambua changamoto iliyojitokeza katika maeneo mbalimbali ambapo tumeunganisha *grid* ya Taifa lakini inatokana na umbali wa kusafirisha umeme huyo kufikia katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Shirika la *TANESCO* lipo katika hatua ya manunuzi ya kifaa ambacho kitakuwa na uwezo wa kurekebisha hali hiyo ili isiendee. Kwa hiyo niwathibitishie wakazi wa Wilaya ya Liwale, wakazi wa mkoa ya Lindi na Mtwara ambao wameunganishwa kwenye *grid* ya Taifa, wakazi pia wa Mkoa wa Ruvuma na wakazi wa Biharamulo, Ngara kwamba tatizo ni muda na limepatiwa ufumbuzi na kwamba likishashughulikiwa wataona faida ya umeme wa uhakika ambao unatokana na *grid* ya Taifa, kuliko huu ambao ni wa mafuta ambao kwa kweli umelisaikia shirika kuokoa kiasi cha pesa na kuweza kuendelea kuwekeza katika maeneo mengine. Kwa hiyo nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge na kwa kuwa hivi karibuni kwenye tarehe 21 nitafanya ziara katika jimbo lake, nitatoa hayo maelezo. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge muda wetu ni mfupi, hivyo, ukipewa fursa nenda moja kwa moja kwenye swali. Mheshimiwa Cecil Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuumuliza Mheshimiwa Waziri kwamba suala hili la nishati mbadala tuliaminishwa kwa ugunduzi ule wa gesi, basi wananchi wa vijiji wangepikishiwa ile gesi wakaachana kabisa na mambo ya kutumia mkaa ili kuweza sasa kutumia gesi ambayo inapatikana maeneo ya Mtwara. Hata hivyo, mpaka sasa hivi hata Mtwara kwenyewe matumizi ya gesi si makubwa kwa sababu ile miradi ni kama imekuwa *abandoned*, Serikali haiifanyii tena kazi. Sasa nataka kufahamu kutoka kwa Naibu Waziri, je, Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na masuala ya gesi iliyopo Mtwara?

NAIBU SPIKA: Mheshimwa Waziri wa Nishati, majibu kwa kifupi.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nimshuruku sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya msingi ya Waheshimiwa Wabunge. Pia napenda niungane na Mbunge Mwambe kwa matumizi ya gesi kule Mtwara na nimpongeze kwa ufuatiliaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibu mwezi uliopita tumeanza kutekeleza rasmi, mwaka jana tulizindua usambazaji wa gesi Mtwara na katika maeneo 12 ambayo tunaanza nayo vifaa tayari vimepatikana na tarehe 30 mwezi huu ujenzi wa usambazaji gesi Mtwara unaanza. Tunaanza na vituo cha Chuo cha Ufundi pamoja na maeneo yote yanayokwenda mpaka gerezeni na maeneo ya Mtwara Mikindani. Nitake tu kuwapa taarifa na uhakika wananchi wa Mtwara kwamba yataanza sasa mwezi huu tarehe 30 na yatachukua takribani miezi 15 ili wananchi wa Mtwara waweze kupata gesi kama ambavyo tumepanga.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jarome Bwanausi, swali la nyongeza.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi. Tatizo lililopo Kibiti pia lipo katika Jimbo la Lulindi na sisi hatujapitiwa na utaratibu huo wa kupewa umeme mbadala na kutumia gesi kwa ajili ya majumbani. Sasa nataka kumwomba Mheshimiwa Naibu Waziri atueleze maana sisi tunategemea umeme hali ya usambazaji umeme katika jimbo la Lulindi inasikitisha na iko katika kiwango cha chini sana. Je, nini kauli ya Serikali?

NAIBU SPIKA: Mheshimwa Waziri wa Nishati.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nijibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Bwanausi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika baadhi ya maeneo utekelezaji wa kandarasi umesuasua hasa mwanzoni lakini kwa upande wa Mheshimiwa Bwanausi yapo maeneo ambayo yalikuwa mbali sana na mtandao wa umeme, kwa hiyo, imechukua muda mrefu kwa wakandarasi kuyafikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Bwanausi kwa ushirikiano na Waheshimiwa Wabunge wa Mtwara pamoja na mkandarasi, sasa hivi mkandarasi mkandarasi anakamilisha shughuli za kusimika nguzo katika

maeneo 22 ya Mheshimiwa Bwanausi. Ni matarajio yetu katika Jimbo la Bwanausi, maeoneo ya vijiji 22 yatawashwa kabla ya mwezi Septemba, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba tunafanya kila namna kuhakikisha kwamba wakandarasi wanaongeza kasi. Tarehe 22, mimi mwenyewe nitakuwa Mtwara ili kuweka msukumo mkali kwa wakandarasi ili waweze kukamilisha kazi hizo kwa wakati.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tuendeleo na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, Mbunge wa Manonga, sasa aulize swali lake.

Na. 234

Ujenzi wa Barabara za Ziba - Puge na Ziba - Choma

MHE. SEIF K. GULAMALI aliuliza:-

Wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mheshimiwa Rais aliahidi kujenga barabara za Ziba - Puge na Ziba - Choma kwa kiwango cha lami:-

Je, ni lini Serikali itetenga fedha za usanifu wa barabara hizo na hatimaye kuanza ujenzi ili kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, Mbunge wa Manonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Ziba - Puge yenye urefu wa kilometa 83.06 na barabara ya Ziba - Choma yenye urefu wa kilometa 26.6 ni barabara za Mkoa zinazohudumiwa na Wakala wa Barabara *TANROADS*, Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Puge - Ziba na barabara ya Ziba - Choma zitakuwa miongoni mwa barabara zitakazopewa kipaumbele katika kutengewa fedha kwa ajili ya kuzifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa lengo la kujenga barabara hizo kwa kiwango cha lami. Aidha, Serikali kwa kutambua umuhimu wa barabara hizo imekuwa ikizitengea fedha kila mwaka kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ili ziendeleo kupitika majira yote ya mwaka. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, kiasi cha shilingi milioni 712.922 kimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Puge - Ziba na kiasi cha shilingi milioni 170.3 kimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Ziba - Choma.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Seif Gulamali, swali la nyongeza.

MHE. SEIF K. GULAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amasema barabara hizo zitapewa kipaumbele, je, ni vipi atazipa kipaumbele huku tayari bajeti imeshasomwa na pesa hazijatengwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari sasa kwenda kuzungumza na wananchi wa maeneo hayo ili kuwaambia juu ya barabara hizo kujengwa kwa kiwango cha lami? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, Mbunge wa Manonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Seif Gulamali kwa kufuatilia mipango ya ujenzi wa barabara lakini pia maendeleo mbalimbali. Mheshimiwa Gulamali nakumbuka wakati wa ziara ya Makamu wa Rais pia amefuatilia na kuzungumza juu ya barabara hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi sasa hivi tunaendelea na kukamilisha kuunganisha mikoa yetu kwa barabara za lami. Pia kama nilivyosema kwamba tutakapokuwa tumefika hatua nzuri tutaingiza kwenye mpango ujenzi wa barabara hizi muhimu ambazo umezungumza kwa sababu zinahudumia watu wanaokwenda kupata huduma ya matibabu pale Nkinga. Kwa umuhimu huo ndiyo maana katika mwaka 2018/2019 kama nilivyojibu tulitenge fedha nyingi karibu bilioni nzima, zaidi ya shilingi milioni mia nane themanini zilitengwa kwa ajili ya kuboresha maeneo korofi ili wananchi waweze kupita katika maeneo hayo bila shaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna ujenzi wa madaraja Mheshimiwa Gulamali anafahamu kule Mto Manonga, daraja kubwa tunaendelea kujenga lakini pia tunaendelea kuwaunganisha wananchi kutoka Ziba - Choma kwenda Kanawa kule upande wa Shinyanga kwa maana ya Wilaya ya Kishapu. Pia iko miradi mingine kutoka upande mwingine wa Shinyanga tunajenga ili kuweza kuwafanya hawa wananchi wawe kwenye mtandao mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, nitakuwa tayari kwenda kuzungumza na wananchi lakini Mheshimiwa Gulamali kumbuka wakati nikiwa na ziara na Makamu wa Rais pia nilipata nafasi ya kutoa ufafanuzi juu ya mpango kabambe wa kuiboresha barabara hii. Hata hivyo, kwa sababu unahitaji twende nitakwenda nizungumze na

wananchi ili waone mipango mizuri ya Serikali tuliyojipangia kwa ajili ya kuboresha barabara hizi muhimu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Grace Kiwelu, swali la nyongeza.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Barabara ya Same - Kisiwani - Mkomazi ilishafanyiwa usanifu na umekamilika na Mheshimiwa Rais alitoa ahadi barabara hii kujengwa kwa kiwango cha lami. Je, ni lini barabara hii itaanza kujengwa ili kuondoa kero ya muda mrefu kwa wananchi wa Jimbo la Same na majimbo mengine yanayoweza kutumia barabara hiyo? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Grace Kiwelu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba Serikali inayo mpango wa kujenga barabara hii kutoka Same - Kisiwani - Mkomazi lakini pia tutakwenda mpaka kule Mkinga ili iweze kwenda mpaka Tanga. Ni kweli usanifu ulishafanyika, sasa hivi Serikali inafanya mapitio ili tuweze kwenda kwenye hatua ya manunuzi, sasa hivi Mkandarasi Mshauri anaendelea na kazi katika mwaka huu wa fedha ili kufanya *review* ya barabara hii ili tuweze kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge avute subira tukamilishe zoezi hili. Pamoja na hayo tumeweka mpango katika mwaka wa fedha unaokuja kwa maana ya kwamba kidogo kidogo kuna sehemu ambayo tutaanza kujenga kwa kiwango cha lami. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Amina Makilagi, swali la nyongeza.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Mara ni miongoni mwa mikoa ambayo Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeipa miradi mikubwa ya barabara ya kutoka Kisolya mpaka Bunda na barabara ya kutoka Makutano Butiama mpaka Mugumu. Barabara hizi zimekuwa zikijengwa kwa kususua, napenda kujua ni lini ujenzi wa barabara hizi utakamilika maana sasa ni miaka sita (6) tangu ujenzi uanze?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Makilagi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna ujenzi wa barabara unaendelea katika Mkoa wa Mara na Mheshimiwa Mbunge anafahamu na mara nimpongeze tu amekuwa akifuatilia sana hizi barabara. Mradi unaoendelea sasa hivi ni barabara kutoka Bulamba kwenda Kisolya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mbunge anafahamu kwamba Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli alipofanya ziara katika Mkoa wa Mara alitoa maelekezo ili tuweze kujenga barabara hii kutoka Bulamba – Bunda -Nyamuswa kilometa 56. Utaratibu wa hatua ya manunuzi unaendelea na wakati wowote tutapata mkandarasi ili barabara hii ijengwe. Mheshimiwa Mbunge pia anafahamu tunajenga barabara kutoka Makutano – Sanzate, ni kweli kuwa barabara hii na mimi nimeitembelea ilikuwa inasuasua kidogo lakini tumechukua hatua ili kwa haraka hii iweze kukamilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara nyingine ambayo itakuwa inashughulikiwa kwa maana ya kutangaza kupata mzabuni kutoka Sanzate - Nata. Kwenye mpango

huu wa bajeti ambao tumepitishiwa na Waheshimiwa Wabunge juzi tutatoka tena kutoka Nata - Mugumu lakini tutatazama pia kujenga barabara kutoka maeneo ya Mugumu - Tabora B ili tuunganishe kwenda mpaka Loliondo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, iko mipango mizuri tu, nimwombe Mheshimiwa Mbunge avute subira lakini kwa Mkoa wa Mara tumejipanga vizuri yale maeneo ambayo wananachi walikuwa na shida sasa neema inakuja. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Neema Mgaya, swali la nyongeza.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Sisi wananchi wa Mkoa wa Njombe tunaishukuru Serikali kwa hatua za awali ilizofanya katika barabara ya Kibena – Lupembe – Madeke, usanifu yakinifu umeshafanyika na vilevile barabara hii imewekwa kwenye bajeti ya mwaka huu. Nilitaka kujua lini Serikali itaanza kujenga barabara hii ya Kibena – Lupembe - Madeke? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Neema Mgaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu siyo hapa tu Bungeni ameendelea kufuatilia sana barabara za Mkoa wa Njombe.

Naiseme kwamba katika mwaka wa fedha 2018/2019 tunayo bajeti, harakati za kuanza kujenga kilometa 50 kutoka Kibena kwenda Lupembe zinaendelea. Kama hiyo haitoshi tukifika Lupembe, katika mwaka wa fedha unaokuja iko bajeti ambayo tumepitishiwa tutatoka eneo la Lupembe kuelekea Madeke mpakani na Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kuna maboresho makubwa maeneo ambayo yana uzalishaji mkubwa wa matunda, miti, na kadhalika yale maeneo ambayo ni korofi tunaendelea kujenga kwa kiwango cha zege, yale maeneo ambayo yalikuwa na vilima. Harakati hizi zimetusaidia sana kwani sasa hivi wananchi wanaotoka Mlimba wanaweza sasa kuja Lupembe wanakwenda mpaka Makambako kupitia hiyo barabara ambapo awali ilikuwa haipitiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira, tumejipanga vizuri kwa sababu tunaitazama barabara hii kutoka Kibena ili tuweze kuwaunganisha wananchi wa Mikoa ya Njombe na Morogoro.

Ndugu yangu Mheshimiwa Mbunge wa Mlimba alitoa machozi hapa katika eneo lake lakini upo mpango unaoendelea wa kujenga kutoka Ifakara - Kihansi kwa maana ya kujenga kwa kiwango cha lami ili tuunganishe na kile kipande cha kilometa 28 kutoka Kihansi - Mlimba.

Vilevile ile sehemu ya kutoka Mlimba - Madeke nayo tumeiweka kwenye mpango ili mnyororo mzima usafiri ukitoka katika eneo hili la Ifakara tunaunganisha mpaka kwenda Njombe, tumejiweka mipango mizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira na wakati nyingine tuonane ili aone mipango yote kwa maana ya barabara nzima ukitoka Njombe kwenda kwa wenzetu wa Morogoro na utusaidie pia kuzungumza na wananchi waone kwamba Serikali hii imejipanga kuwasaidia wananchi wa maeneo haya.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, sasa aulize swali lake.

Na. 235

Fidia kwa Maeneo Yaliyotwaliwa na JWTZ

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM aliuliza:-

Kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu ya wananchi ambao maeneo yao yametwaliwa na Jeshi la Wananchi (JWTZ) pasipo kulipwa fidia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka kulipa fidia kwa wannachi hao?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, majibu.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Ntambile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika ni kweli yapo maeneo mbalimbali yaliyotwaliwa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa ajili ya utekelezaji wa jukumu la ulinzi wa nchi na mipaka yake. Baadhi ya maeneo hayo yamelipwa fidia na mengine mchakato wa kulipa fidia kwa wamiliki unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali uliopo ni kuendelea na utaratibu wa kulipa fidia stahiki kwa wananchi kadri hali ya fedha itakavyoruhusu na kwa mujibu wa Sheria ya Utwaaji Ardhi kwa ajili ya matumizi ya umma. Kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ilitenga shilingi bilioni 20.9 kwa ajili ya kulipa fidia maeneo yaliyotwaliwa na jeshi. Baada ya uhakiki wa malipo ya fidia tayari kiasi cha shilingi bilioni 3 kimelipwa kama fidia. Aidha, uhakiki wa madai ya fidia unaendelea katika maeneo mengine na mara uhakiki utakapokamilika Serikali kupitia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa italipa fidia hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba wananchi wawe na subira wakati Serikali inakamilisha uhakiki ili kuwalipa stahiki zao.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, swali la nyongeza.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, fedha ambayo Mheshimiwa Waziri ameitaja ya malipo ya shilingi bilioni 3 ni ile ambayo inaenda kulipwa kule Kilwa Masoko, Rasi Mshindo na *Navy Command*. Kuna maeneo yaliyotwaliwa na Jeshi baadhi ya wananchi wameshafariki dunia na Serikali inaendelea kutekeleza miradi mikubwa kwa fedha za ndani ikionyesha kwamba wananchi hawa tayari wamedhulumiwa na hawana chao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali utuambie ni kwa nini basi mmechukua muda mrefu hamtaki kuwalipa wananchi hawa ili hali mnaenda kutekeleza miradi mikubwa ndani ya nchi kwa fedha za ndani? Lini fedha za wananchi hawa zitapatikana?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, taarifa ya utekelezaji wa ahadi za Serikali mwaka 2006 ilieleza wazi kuna maeneo kadhaa ya Jeshi yaliyoorodheshwa ambapo wananchi wanadai fidia na Serikali ikaahidi kwamba itaendelea kulipa. Ukiangalia bajeti iliyopita shilingi bilioni 27 fedha hazikutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atuambie bajeti yake ya kesho anawaambia nini wananchi hawa wanaolalamika kwa muda mrefu, wamekata tama na wengine wameshafariki na lakini hawana mategemeo ya kulipwa fedha zao? Naomba Waziri atuambie waziwazi wananchi hawa ambao wamekata tamaa, wanyonge hawa

na ninyi ndiyo watetezi wa wanyonge watapata lini?
Naomba majibu ya kweli. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, majibu.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:
Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Masoud Abdalah Salim, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba shilingi bilioni 3 zilizotolewa ni kwa ajili ya Rasi Mshindo kule Kilwa. Nimpe tu taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba kati ya fedha tulizoidhinishiwa bajeti iliyopita shilingi bilioni 20.9 ukiacha shilingi bilioni tatu ambazo zimeshalipwa shilingi bilioni 16 zimeshatengwa na kazi inayofanyika sasa hivi ni uhakiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ukichukua zile shilingi bilioni tatu na shilingi bilioni 16 utaona shilingi bilioni 19 zitatolewa katika bajeti hii ambayo tunamalizia. Kwa hiyo, hatuna shaka kwamba baada ya uhakiki maeneo mengi haya yatalipwa.

Kuhusu bajeti ijayo, namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira. Ukweli ni kwamba kama tutafanikisha kulipa shilingi bilioni 19 kati ya shilingi bilioni 20 zilizotengwa katika bajeti tunayomalizia basi bila shaka kwa sehemu kubwa tutakuwa tumetimiza ahadi zetu.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 236

Tatizo la Ubakaji Nchini

MHE. NAJMA MURTAZA GIGA aliuliza:-

Sheria ya Makosa ya Kujamiiiana kwenye suala la ubakaji (*SOSPA*) ya mwaka 1998 na marekebisho yaliyofanywa mwaka 2017 yote yana lengo la kukomesha vitendo vya ubakaji wa watoto chini ya miaka 18 na wanafunzi (kifungo miaka 30) na watoto chini ya miaka 10 (kifungo cha maisha):-

(a) Je, tokea kupitishwa kwa sheria hii (*SOSPA*) na marekebisho yake, ubakaji umepungua au kukoma hapa nchini?

(b) Je, kama bado changamoto ipo Serikali ina mpango mkakati gani mpya katika kupambana kutokomeza ubakaji Tanzania?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Najma Giga, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Makosa ya Kujamiana (*SOSPA*) ya mwaka 1998 na marekebisho yaliyofanyika 2002 imeingiza vifungu vya makosa ya kujamiana kwenye Kanuni za Adhabu ili kukomesha vitendo vya ubakaji kwa watoto ambapo yeyote akipatikana na hatia adhabu yake ni kifungo cha miaka thelathini jela au kifungo cha maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na adhabu hii ambayo ni kubwa ambayo ingeweza kufanya watu waogope kujihusisha na vitendo vya ubakaji lakini vitendo vya ubakaji kwa watoto nchini vimeendelea kuongezeka. Kwa mujibu wa Takwimu ya Hali ya Uhalifu na Matukio ya Usalama Barabarani, matukio ya ubakaji yameongeza kutoka

matukio 394 Desemba 2015 hadi kufikia matukio 2,984 Desemba 2017. Hii ni kutokana na jitihada kubwa ambayo Serikali imefanya na wadau ambalimbali ya kuhamasisha jamii kutoa taarifa ya masuala ya ubakaji pindi yanapotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetekeleza afua mbalimbali katika kukabiliana na ukatili dhidi ya watoto, ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto 10, 988 katika ngazi za Halmashauri, Kata na Vijiji; kuanzisha vikundi vya malezi 1,184 na kuwezesha huduma ya simu kwa watoto ambapo wanaweza kupiga simu namba 116 ili watoto na jamii waweze kutoa taarifa kuhusu ukatili dhidi ya watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto hii, Serikali imeandaa Mpango Kazi wa Taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto 2017/2018 - 2021/2022 ambapo kupitia mpango huu Serikali inatekeleza afua mbalimbali za kutoa elimu bure, kuandaa na kutoa elimu juu ya malezi chanya kupitia vitini vya malezi na makuzi na kuandaa mkakati wa mawasiliano wa kuelimisha wananchi kuachana na mila potofu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, swali la nyongeza.

MHE. NAJMA MURTAZA GIGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nishukuru na kuipongeza sana Serikali kwa jitihada inazozichukua katika kulipoteza hili suala baya katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza, la kwanza, mwaka jana nilizungumza hapa kwamba iwapo elimu tosha itatolewa basi ripoti hizi zitazidi. Kweli Mheshimiwa Waziri amethibitisha, hivyo nawapongeza sana kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachotaka kujua hii idadi kubwa ambayo imeongezeka baada ya wananchi kuhamasika na kutoa ripoti, je, ni wangapi kati ya hao

wameweza kufikishwa kwenye vyombo vya sheria na wangapi wametiwa hatiani na kuchukuliwa hatua zinazostahiki? Siyo lazima mnijibu sasa hivi lakini majibu nayataka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, tunajua kabisa vitendo hivi vinafanywa miongoni mwa jamii tunazoishi, ni miongoni mwa wanaume tunaishi nao wakiwemo babu zetu, baba zetu, waume zetu, wajomba zetu na wengine wanaofanana na hao. Kwa nini Serikali haiji na mpango mbadala wa kutoa ruhusa kwenye jamii ili kuwatambua hawa watu ambao wanajulikana wana vitendo hivi kama ambavyo wanatambuliwa wabakaji, wezi, wavuta unga na wavuta bangi; ili jamii yetu sasa iweze kuwajua na wazazi pamoja na watoto wetu waweze kujitenga na watu hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu kwa maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, matukio haya ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto kwa kiasi kikubwa yanafanywa na watu ambao wako karibu na familia na mara nyingi inakuwa ndani ya familia. Sisi kama Wizara tumeendelea kuelimisha jamii na tunawashukuru sana wenzetu wa Jeshi la Polisi pamoja na Idara ya Mahakama, wamekuwa wanatoa ushirikiano mkubwa sana. Matukio mengi yanashindwa kufika mbali kwa sababu ushirikiano umekuwa ni mdogo ndani ya familia kwenda kutoa ushahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hapa sina takwimu ambazo zinaonesha matukio ni mangapi na kiasi gani yamehukumiwa, lakini kwa taarifa chache ambazo ninazo, ni matuko machache sana ambayo yanafika mwisho kwa sababu tu familia zimekuwa hazitoi ushirikiano kwa Jeshi la Polisi na Idara ya Mahakama ili matukio haya yaweze kufika

mwisho. Kwa hiyo, nitoe rai kwa jamii kutomalizana na haya matukio ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto majumbani na badala yake waruhusu mkondo wa sheria uweze kufika mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala lake la pili, katika nchi ambazo zimeendelea, kuna kitu kinaitwa *Sexual Offender Register*. Wale watu ambao wamehukumwa kutokana na makosa haya ya ukatili wa kijinsia wanatambulika wapi wanakaa, wapi wanafanya kazi na akihamia sehemu mpya watu wote wanaweza wakamfahamu. Kwa hiyo, kwa sasa Serikali hatuna utaratibu huo, lakini ni wazo ambalo tunaweza tukalipokea na kuweza kuliangalia ni jinsi gani ya kulifanya kazi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimwa Wabunge, muda wetu umekwenda, tumalizie maswali yaliyobaki. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Lucy Simon Magereli, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 237

Kuporomoka kwa Elimu Tanzania

MHE. LUCY S. MAGERELI aliuliza:-

Sera ya *cost sharing* ilianzishwa ili kuisaidia Serikali kibajeti katika maeneo ya afya na elimu, hadi leo ni bayana kuwa sera hii imeshindwa na hatimaye Serikali kurejea tena katika kugharamia Elimu ya Msingi na Sekondari:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Elimu ya Tanzania ambayo imeporomoka sana katika shule za Umma inakuwa yenye ubora unaotarajiwa?

(b) Je, Serikali inafanya nini kuhusu madai ya stahiki ya walimu ambazo hazijalipwa kwa muda mrefu sasa?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu,

Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Simon Magereli, Mbunge wa Viti Maalum, kama lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya Tanzania inaendelea kuimarika siku hadi siku katika Shule za Umma na binafsi. Ili kuhakikisha kuwa ubora wa elimu unaendelea kuimarika zaidi, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Mfano, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, zaidi ya shilingi bilioni 56.5 zimetumika katika uboreshaji wa miundombinu katika shule 588. Kati ya hizo Shule za Msingi ni 303 na Sekondari ni 288 yakiwemo madarasa 1,190, mabweni 222 na vyoo 2,141.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali imesambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia vikiwemo vifaa vya maabara na kemikali na vifaa vya kielimu kwa ajili wanafunzi wenye mahitaji maalum katika Shule za Msingi na Sekondari. Pia katika kipindi cha mwaka 2017 hadi Aprili, 2019, Serikali imeajiri jumla ya Walimu 17, 884.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali imeendelea kuimarisha Idara ya Udhhibiti Ubora wa Shule ambapo imenunua na kusambaza magari 45 ya Udhhibiti Ubora wa Shule na pikipiki 2, 897 kwa ajili ya Maafisa Elimu Kata. Pia katika mwaka 2019/2020 Serikali inatarajia kujenga Ofisi 100 za wadhhibiti ubora wa shule na kuongeza idadi ya watumishi ili kuongeza ufanisi katika ufuatiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madai ya stahiki za walimu, Serikali imeendelea kulipa madai hayo yahasuyo mishahara na likizo ambapo kwa kipindi cha Juni hadi Oktoba, 2018 Serikali ililipa zaidi ya shilingi bilioni 16 kwa madai ya malimbikizo ya mishahara. Aidha, hadi kufikia Desemba, 2018 Serikali pia ilipeleka jumla ya shilingi bilioni 5.07 kwenye Halmashauri 184 kwa ajili ya malipo ya likizo za walimu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lucy Simon Magereli, swali la nyongeza.

MHE. LUCY S. MAGERELI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ni kwa bahati mbaya tu kwamba Serikali inatoa majibu na takwimu ambazo haziakisi ukweli. Katika jibu la Mheshimiwa Waziri, hizi takwimu alizozitoa pia nazo haziakisi ukweli kwa sababu ukikokotoa kiasi cha takwimu anazozitoa na ukilinganisha uhitaji ulivyo inaweza kukupa jibu ya kwamba elimu yetu inaporomoka badala ya kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, anaposema Serikali imetoa shilingi bilioni 56.05 katika shule 588, kati ya shule 17,174 maana yake wamehudumia shule 3% tu. Sasa ukiangalia kama hapo takwimu hii inakwamba elimu inakua ama inaporomoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule zetu zina hali mbaya sana na nina mfano halisi ambao uko mita 1,000 kutoka majengo ya Bunge, Shule ya Msingi Medeli, hii shule haina vi... (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lucy, naomba uulize swali tafadhali. Naomba uulize maswali yako.

MHE. LUCY S. MAGERELI: Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala ni *sensitive* kidogo, tafadhali naomba takwimu kidogo.

NAIBU SPIKA: Aaah, sasa siwezi kukupa dakika zako. Swali lako peke yake ni dakika sita. Sasa ukitumia dakika mbili kwenye swali moja la nyongeza maana yake muda wako umekwisha tayari, ndiyo maana nakukumbusha uulize swali.

MHE. LUCY S. MAGERELI: Mheshimiwa Naibu Spika, basi katika takwimu hizo ambazo unazona kwamba 3% tu ndiyo imehudumiwa: Je, mazingira haya duni ambayo yanazikabili shule zetu, elimu itakuwa inakua ama inaporomoka?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Madai ya walimu ni moja kati ya mwarobaini muhimu sana wa kutanzua kuporomoka kwa elimu ya Tanzania. Katika hili naomba nimwombe dua njema mdogo wangu Mwalimu Hilda Galda John Bura aliyefariki tarehe 05 na tukamzika ambaye naye

amefariki akiwa anaidai Serikali madai haya haya ya walimu. Je, kwa takwimu hizi za shilingi bilioni 15.07 alizotoa Mheshimiwa Waziri, ni asilimia ngapi ya madai yote ya waalimu? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu takwimu ninazozitoa kwamba haziakisi hali halisi, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba takwimu hizo nilizotoa ndiyo takwimu rasmi. Pia shule ambazo tumeweza kujenga na kuboresha miundombinu ni katika kipindi fulani. Nimeweza kuainisha kwamba ni kutoka mwaka 2017 mpaka sasa, haimaanishi kwamba huko nyuma hakukuwa na kitu ambacho kimefanyika, lakini haimaanishi kwamba siku za usoni hatutafanya kitu kingine. Kwa hiyo, shule 588 katika kipindi cha miaka mitatu siyo kitu kidogo. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie tu kwamba Serikali itaendelea kuboresha miundombinu kadiri ya upatikanaji wa fedha utakaporuhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuhusu malimbikizo ya madeni ya walimu naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali ya Awamu ya Tano imejitahidi kwa kiasi kikubwa kupunguza madeni hayo. Kwa sasa tunachojaribu kufanya ni kuhakikisha kwamba madeni mapya hayatokei. Tunalipa stahiki za walimu pale zinapohitajika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Nimesimama hapa kuweka msisitizo kwamba Serikali inafanya kazi vizuri sana katika kuhakikisha kwamba inaboresha Sekta ya Elimu. Hii takwimu ambayo imetolewa hapa ni mfano wa Mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo. Haijajumuisha shilingi

bilioni 29 ambazo Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilizitoa kwa ajili ya kukamilisha maboma; haijajumuisha shughuli ambazo Halmashauri zetu katika bajeti zao zinatenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Lucy Magereli kwamba Serikali iko vizuri, mwenye macho haambiwi tazama. Ukienda unaona hata shule kongwe zilivyoboreshwa, zinapendeza, zilikuwa majengo mabovu. Kwa hiyo, watupe muda, Serikali tutaendelea kufanya kazi yetu vizuri. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumalizie swali letu la mwisho. Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Hassan Elias Masala, Mbunge wa Nachingwea, sasa aulize swali lake.

Na. 238

Kuboresha Jengo la Mahakama – Nachingwea

MHE. HASSAN E. MASALA aliuliza:-

Je, nini mpango wa Serikali juu ya kuboresha jengo la Mahakama Wilayani Nachingwea.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Elias Masala, Mbunge wa Nachingwea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama ya Tanzania haipo katika mpango wa maboresho ya majengo ya Mahakama nchini, ambapo pamoja na mambo mengine imekusudia kusogeza haduma ya Mahakama karibu na wananchi. Ili kufikia lengo hilo, Mahakama imeendelea kutatua changamoto kubwa ya uhaba na uchakavu wa majengo kwa kuendelea na kukarabati majengo nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mahakama ya Tanzania inafahamu tatizo la uchakavu wa majengo mengi ya Mahakama nchini, ikiwemo jengo la Mahakama ya Wilaya Nachingwea. Katika kukabiliana na changamoto hii, Mahakama imeweka kipaumbele katika kuboresha na kujenga majengo ya Mahakama nchini kulingana na mpango mkakati wa miaka mitano ambao umeendelea kutekelezwa kwa awamu kutegemea na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge wa Nachingwea kuwa kutokana na uhitaji mkubwa wa rasilimali na rasilimali chache zilizopo, katika mpango mkakati wa miaka mitano, Mahakama iliamua kujipanga upya na kuweka vipaumbele ili kuhakikisha tunaondokana na changamoto hii. Aidha, tayari tathmini ya jengo la Mahakama Nachingwea imeshafanyika. Kimsingi jengo hili linahitaji kujengwa upya na siyo kufanyiwa maboresho. Aidha, baada ya tathmini hiyo kufanyika ujenzi wa jengo hilo umewekwa kwenye mpango wetu wa ujenzi wa Mahakama wa mwaka 2020/2021 kutegemeana na upatikanaji wa fedha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hassan Elias Masala, swali la nyongeza.

MHE. HASSAN E. MASALA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini pamoja na majibu hayo, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri anakiri kabisa kwamba jengo lile halihitaji tu kufanyiwa marekebisho isipokuwa kujengwa; na kuwa pia tathmini imeshafanyika toka mwaka 2017/2018, kuna sababu gani sasa za kutenga fedha au kulipeleka jengo hili kwenye mpango wa kujengwa 2020/2021 badala ya mwaka 2019/2020?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, naomba kujua nini mpango wa Wizara ya Katiba na Sheria katika kuongeza idadi ya watumishi katika Mahakama zetu hasa

Mahakama za Mwanzo? Nachingwea tuna kituo pale kinaitwa Ndomoni, kwa muda mrefu sasa kimefungwa na wananchi hawapati huduma pale. Hivyo, wanalazimika kutembea umbali mrefu kwenda Nachingwea Mjini kufuata huduma ya Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA): Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mpango wa Mahakama wa Miaka Mitano wa Kuboresha Huduma za Mahakama hapa Nchini, imeweka pia vipaumbele vya ujenzi. Baada ya taratibu zote hizo kukamilika, limetengenezwa jedwali ambalo ndiyo linaipelekea Mahakama hii kuanza kujenga hizi Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa pande wa Nachingwea, kwa sababu tathmini ilikuwa inaendelea kufanyika katika jedwali letu, Nachingwea wenyewe ujenzi utanza katika mwaka wa fedha 2020/2021 hasa kutokana na kwamba ilikuwa lazima taarifa hizo zikamilike na tayari kuna baadhi ya Mahakama ilikuwa imeshaingia katika mpango wa ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, ni kweli tunatambua changamoto hiyo lakini kwa sasa kwa sababu Wizara tumeingia makubaliano na Baraza la Ujenzi wa Taifa katika ujenzi wa Mahakama kupitia teknolojia mpya na bei nafuu ya Moladi naamini kabisa kwamba pindi fedha itakapopatikana tutaanza ujenzi wa Mahakama ya Nachingwea ili kuwaondolea usumbufu wananchi wa Wilaya ya Nachingwea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika swali lake la pili la kuhusu watumishi, ni kweli tuna changamoto katika baadhi ya maeneo, lakini nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea kulifanyia kazi kwa maana ya kuajiri

watumishi wengine ambapo tunaenda kupata kibali toka utumishi. Kwa hiyo, pindi ajira hizi zitakapotangazwa na kupatikana, pia Wilaya ya Nachingwea itaangaliwa katika kutatua changamoto hii ya ukosefu wa watumishi katika eneo hilo ili wananchi wa Nachingwea waweze kupata huduma za Mahakama kwa ukaribu lakini na kwa ufanisi zaidi.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali. Nilete kwenu matangazo tuliyonayo asubuhi ya leo. Tutaanza na matangazo yanayohusu wageni waliopo Bungeni leo. Tutaanza na wageni waliopo jukwaa la Mheshimiwa Spika; na hawa ni wageni wa Mheshimiwa Spika wanatoka *Bank of Africa*; wa kwanza ni Ndugu Joseph Iha, ambaye ni *Managing Director* wa *Bank of Africa*; yupo pia ndugu Bruno Ngoo ambaye ni *Head Treasury*, karibu sana. Tunaye pia Ndugu Lomnyaki Saitabau ambaye ni *Head Retail Banking*, karibu sana; tunaye pia Ndugu Asia Mwangonela ambaye ni *Branch Manager* Dodoma. Karibuni sana Viongozi wa *Bank of Africa*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, anao wageni wengine saba ambao ni wahubiri kutoka Kanisa la Kisabato wanaohubiri neno la Mungu na matangazo yao kurushwa katika Redio za Afrika Mashariki na Kati; wa kwanza hapa ni Mch. Dkt. Baraka Muganda, ambaye ni Mtanzania anayeishi Washington; na huyu ndiye Mhubiri Mkuu katika Mikutano ya Wasabato ya Uzoefu wa Nguvu ya Mungu hapa Dodoma. Karibu sana. (Makofi)

Vilevile Dkt. Muganda ameambatana na Ndugu Prince Bahati, Mchungaji Christopher Ungani, Ndugu Gideoni Msambwa, Dkt. Sperence Kilonzo, Ndugu Debora Urrio, Mch. David Mbaga na Ndugu Job Akoko. Karibuni sana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wa Wabunge na mgeni wa kwanza ni Ndugu George Ndimbo ambaye ni mgeni wa Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, ambaye ni Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara na huyu ni Diwani Kata ya Kihagara Wilaya ya Nyasa Mkoani Ruvuma, karibu sana. (Makofi)

Tunao pia wageni 17 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambaye ni Waziri wa Kilimo ambao ni wapigakura wake kutoka Jimbo la Vwawa, Mkoani Songwe wakiongozwa na Ndugu Stephano Simbeye. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 22 wa Mheshimiwa Atashasta Nditije ambaye ni Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano ambao ni Waumini kutoka Kanisa la KKKT Kinondoni Dar es Salaam na Wanajumuiya ya Kinondoni Shamba wakiongozwa na Ndugu Sipe Sito. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu ambaye ni Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii ambao ni wachimbaji wa madini kutoka Mkoa wa Geita; na hawa ni Ndugu Juma Mashimba ambaye ni Mwenyekiti wa Wachimbaji Madini Wilaya ya Geita na Mzee Hosea Katampa ambaye ni Mchimbaji. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Allan Kiula ambao ni Viongozi wa Dini na Viongozi wa CCM kutoka Mkalama Mkoa wa Singida; na hawa ni Mchungaji Nanjota na ndugu Herman Saenda. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Venance Mwamoto ambao ni Madiwani wawili na wageni kutoka nchini Marekani wakiongozwa na Ndugu Risasi Mwaulanga. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 21 wa Mheshimiwa Upendo Peneza ambao ni Wahariri na Watangazaji kutoka Vyombo vya Habari vya Afrika Mashariki wakiongozwa na Ndugu Rebeca Denis. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 11 wa Mheshimiwa Martin Msuha ambao ni marafiki zake kutoka Kisasa, Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Ndugu Alberto Mnyone. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wawili wa Waheshimiwa Wabunge wote wa Wilaya ya Bunda ambaye ni Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Bunda, Ndugu Marycian Sabuni pamoja na mtoto wake Ndugu Peter Godwin. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 11 wa Mheshimiwa Khamis Mtumwa Ali ambao ni Waheshimiwa Madiwani watano na Maafisa sita kutoka Halmashauri ya Kilwa Kaskazini Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Tunao pia wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo na kundi la kwanza ni wanakwaya 31 kutoka kikundi cha kwaya ya Jimbo la Mwakaleli Kanisa la KKKT Dayosisi ya Konde. Nadhani hawakupata fursa ya kuingia hawa. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watatu kutoka Dodoma waliokuja kujifunza namna Bunge linavyofanya shughuli zake wakiongozwa na ndugu Esther Mwita. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni tulionao siku ya leo. Ninalo pia tangazo kutoka Ofisi ya Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu anawaalika Waheshimiwa Wabunge wote mara baada ya shughuli za Bunge kuahirishwa leo kwa ajili ya kushiriki chakula cha jioni yaani futari ama *iftar* katika viwanja vya Bunge. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge tutakapoahirisha shughuli za Bunge mnakaribishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye futari jioni kwenye viwanja vya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo pia tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mtakatifu Thomas Moore hapa Bunge, Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, anawatangazia leo tarehe 15 Mei, 2019 kutakuwa na ibada ya misa kwa Wakristo Wakatoliki mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge saa saba mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa ghorofa ya pili. Waheshimiwa Wabunge, Wakristo wote na wageni mliopo hapa Bungeni mnakaribishwa kushiriki ibada hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo lingine. Kuna Mbunge ambaye alidondosha bahasha yake siku ya Ijumaa iliyopita tarehe 10 Mei, 2019 katika geti la kuingilia Wabunge. Kwa hivyo, Mbunge yeyote aliyepoteza bahasha yake ama aliyedondosha bahasha yake aione Ofisi ya Mheshimiwa Spika na hapa hatuwezi kusema bahasha ilikuwa na nini kwa sababu sasa tusije wote tukaambatana huko. Yule aliyepoteza bahasha aende akieleza kulikuwa na nini basi atakabidhiwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo tutaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mwongozo wa Spika.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Hoja ya kuahirisha Bunge.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

HOJA YA KUAHIRISHA SHUGHULI ZA BUNGE

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 47, kuahirisha shughuli za Bunge na kujadili hoja ya dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyoongea kuna mgomo baridi wa madereva wa mabasi wote nchi nzima wakianza na Morogoro. Madereva wa mabasi kwa nini wanataka kugoma? Sasa hivi barabarani kwenye mabasi yote kwanza yamefungwa ving'amuzi *VTS* na *SUMATRA*, vinakuwa *controlled* na *SUMATRA* Makao Makuu, mtu anapozidisha spidi 85 anapata alama moja kila tendo la kuzidisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kutoka Morogoro hadi Dar es Salaam kuna umbali wa kilometa 193 kuna vibao vya spidi 50 vinavyozidi 22, kuna *zebra* zinazozidi

22. Ukifuata taratibu zote kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro utatumia muda wa masaa sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizidisha 50 unapigwa faini na *traffic*, usiposimama kwenye *zebra* unapigwa faini na *traffic*. Kwa tendo moja la kuzidisha spidi 85 unapopewa alama moja, kwa hiyo jumla alama utakazopata kutoka Morogoro hadi Dar es Salaam unaweza ukafikisha milioni tatu hadi tano kwa safari moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni wizi, ni uonevu, tunataka kwenda nchi yenye uchumi wa kati, lakini kwa mwendo huu hatuwezi kwenda. Kwa hiyo, kutokana na hilo, naomba shughuli za bunge ziahirishwe, tujadili hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Goodluck Mlinga kwa mujibu wa Kanuni ya 47 akitaka kutoa hoja kwamba tuahirishe shughuli zilizopo kwenye orodha ya leo ili tuweze kujadili jambo ambalo ameliita ni la dharura na ametoa maelezo yake kwa kifupi na mimi nimemsikia na wote tumemsikia, sina haja ya kuyarejea maneno hayo. Kwa mujibu wa Kanuni ya 47 inamtaka akishazungumza mimi nikisharidhika kama jambo ni la dharura ndiyo nimpe fursa ili yeye azungumze na ndiyo atoe hoja. Kwa hiyo hakuwa anatoa hoja, alikuwa anatoa maelezo ili mimi nikishalielewa jambo hilo na kuona ni la dharura ndiyo nimpe fursa aweze kutoa maelezo na aweze sasa kutoa hoja yake na kama akiungwa mkono basi Bunge liweze kuchukua hatua.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 47 inafanya kazi kwa pamoja na Kanuni ya 48. Kwa maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Mlinga na kwa mujibu wa Kanuni ya 47(4) na Kanuni ya 48(4) jambo hili linao uwezo wa kushughulikiwa katika utaratibu wa kawaida na kwa sababu baadhi yetu

ndiyo tunalisikia hapa na Serikali iko hapa Bungeni. Serikali ichukue hatua kuona ni mambo gani ambayo yanalalamikiwa na madereva ili nchi iweze kuendelea. Watu wanatakiwa kutoka sehemu moja kwenda nyingine wakati huo huo Waheshimiwa Wabunge, tukijitahadharisha kuhusu ajali mbalimbali zinazotokea.

Kwa hiyo upande wa Serikali ukutane na hawa madereva na wamiliki wa vyombo hivi kuona shida iko wapi ili wote tuweze kwenda kwa pamoja, wakati huo huo wajibu wa Serikali kutulinda dhidi ya ajali uko pale pale. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge, jambo hili litashughulikiwa na Serikali kwa maelezo haya niliyoyatoa kwa utaratibu huo ambao ni wa kawaida kwa mujibu wa Fasili ya 4 ya Kanuni ya 48.

Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninasimama kwa Kanuni ya 68 (70), ninaomba kwa sababu ya muda nisiisome.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilipokuwa nikiomba swali la nyongeza nilipata majibu kutoka kwa Waziri wa Habari na swali hilo lilikuwa ni kwa Waziri wa Mawasiliano na si vibaya Waziri wa Habari kulijibu, lakini naomba Mwongozo wako. Swali langu nilikuwa nikilaumu Televisheni ya Taifa kuonesha kwa upendeleo matangazo mbalimbali hasa nilisema yakihusu Vyama vya Upinzani kwamba habari zetu hazioneshwi kwa usawa na vyama vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri akinijibu alitaka tumletee maudhui kuonesha ni jinsi gani anaweza kutusaidia habari zetu ziweze kutoka. Nataka nikukumbushe kwamba nikichukua *sample* ndogo tu tarehe 9 Mei, Kambi Rasmi ya Upinzani ikitoa habari hapa Bungeni *TBC* Taifa taarifa ya habari ya saa mbili haikuweza kuonesha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani wala michango ya Wapinzani. Kwa muda mrefu sasa *TBC* haijatoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Kiti chako kiweze kufuatilia suala hili na kujihakikishia kwamba tunapotoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani hapa Bungeni iwe michango, iwe hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, *TBC* Taifa ambayo ni Televisheni ya Taifa, inalipia kodi na Watanzania wote itoe usawa katika kuhabarisha Watanzania kinachoendelea katika Bunge lako. Hayo ya nje tutaendelea kupambana kama ikibidi tuone kama tunafaa kwenda Mahakamani. Naomba Mwongozo wako tuone jinsi gani tunapata haki yetu kama Watanzania tunaolipa kodi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa Mwongozo na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 68(7) anaomba Mwongozo kuhusu jambo ambalo limetokea jana kuhusu majibu ya Mheshimiwa Waziri kwa swali lake la nyongeza alilokuwa ameliuliza.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni hiyo inataka jambo liwe limetokea mapema na mapema tulishatoa tafsiri. Kiti hapa kilishatoa tafsiri ya jambo ambalo limetokea mapema maana yake mapema siku hiyo. Kwa hiyo hili jambo limetokea jana na kwa hivyo kanuni ya 68(7) haiwezi kutumika kwenye jambo hili. Hata hivyo, upande wa Serikali umepata ujumbe huu kwa maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo aangalie jambo hili namna linavyofanyiwa kazi.

Pia Waheshimiwa Wabunge, hata mimi huwa naangalia mara moja moja taarifa za habari. Si kila Mbunge anawekwa na ziko nyakati ambazo mimi huwa naangalia taarifa ya habari na wanaweza wakaweka mtu mmoja tu na ni mchangiaji wa Kambi ya Upinzani. Kwa hiyo tuwe tunaangalia...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU SPIKA: Nimesema hata mimi huangalia, kwa hiyo usilete ubishi. Wewe umeangalia na mimi nimeangalia. Kwa hiyo kwa ujumla Serikali imepata ujumbe, lakini

tunapozitazama hizi taarifa tusizitazame kwa siku moja moja lakini kama ni jambo ambalo limejitokeza mara nyingi, upande wa Serikali umepata ujumbe na uangalie namna ya kulifanyia kazi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tutaendelea.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Katibu!

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Viwanda na Biashara

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Ninayo majina hapa ya wachangiaji kwa mujibu wa taratibu zetu. Tutaanza na Mheshimiwa Hassan Elias Masala, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniventura Kiswaga na Mheshimiwa Mashimba Ndaki ajiandae.

MHE. HASSAN E. MASALA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza wa hotuba ya Wizara hii ya Viwanda na Biashara. Ya kwangu nilikuwa naomba nichangie katika maeneo makubwa manne.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza ambalo nilitaka nichangie ni eneo linalohusu Mamlaka ya Biashara - *TANTRADE*. Hawa ukisoma kwa mujibu wa kazi zao ambazo wanazifanya, kazi kubwa mbili za msingi kazi ya kwanza ni kufanya utafiti wa masoko, lakini pia mamlaka hii imepewa kufanya kazi ya intelijensia ya kujua kwa wakati tuliokuwa nao dunia inataka nini katika eneo la bidhaa. Sambamba na hili bado mamlaka hii imekuwa inafanya kazi kwa ajili ya

kutangaza bidhaa zetu kupitia maonesho ambayo yamekuwa yanafanyika pale Sabasaba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hizi zote zinaenda vizuri, lakini bado naomba nijielekeze zaidi katika hizi kazi kubwa mbili. Kwa muda mrefu tumekuwa na wakulima lakini sehemu kubwa Watanzania tumekuwa tunajishughulisha na uzalishaji wa bidhaa mbalimbali ikiwezo hizi bidhaa za mazao. Sasa yako maeneo ambayo kidogo nashangaa kuona namna ambavyo mamlaka hii inavyofanya kazi na namna ambavyo wakati mwingine ilivyoshndwa kusaidia nchi yetu katika kuhakikisha mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitolee mifano katika maeneo makubwa mawili, mimi nina wakulima ambao wanalima zao la mbaazi. Zao hili kwa muda mrefu limelegelega kupata bei na kwa miaka ya karibuni mitatu iliyopita tumeshindwa kabisa kuuza mbaazi zetu, sasa kama mamlaka hii ingekuwa inafanya kazi yake ipasavyo na kama ingekuwa imetekeleza wajibu wake wa kufanya utafiti au uchunguzi juu ya masoko ya zao hili na namna ya kuishauri Serikali nafikiri wakulima wetu leo hii wasingekuwa wanapata changamoto ya wapi wataenda kuuza bidhaa zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo wakulima wetu wako njia panda wanashindwa kujua kama waendeleo kuzalisha mbaazi au wabaki kama ambavyo walikuwa wanafanya zamani kutumia mbaazi kama mboga. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa hebu atueleze mamlaka hii inatekelezwa ipasavyo na kama inatekelezwa kwa nini kwa miaka minne mfululizo tumeshindwa kupata jibu la uhakika juu ya hatma ya zao hili ambalo kwa baadhi ya wakulima wetu wamekuwa wanashiriki kulifanya na hatimaye tumeingia hasara ambayo kimsingi bado tumeshindwa kuwasaidia wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili, mwaka jana kwa maana ya msimu wa korosho nafikiri wewe mwenyewe utakuwa ni shahidi, Mawaziri wetu wamekuwa wanagongana juu ya bei ya korosho. Kama mamlaka hii

ingefanya intelijensia yake ya kuchunguza bei katika soko la dunia, lakini pia kuchunguza uhitaji katika mahitaji ya kidunia, naamini kusingekuwa na mgongano wa bei ambao umesababisha leo hii wakulima wetu wengi washindwe kupata bei ambayo ilikuwa inatazamiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kwa heshima na taadhima basi Mheshimiwa Waziri wa Biashara kaka yangu Mheshimiwa Kakunda aweze kutueleza, hawa watu wa *TANTRADE* ukiondoa kufanya maonesho ya biashara ambayo sasa hivi kwa sehemu kubwa ni kama wanachukua tu wachuuzi hata wauzaji wa mitumba wako pale uwanja wa Sabasaba wanafanya shuguli zao na mambo mengi ambayo yanakwenda pale kufanyika ya kutangaza dawa na vitu vyepesi vyepesi tu, ambavyo kimsingi mimi nilikuwa naona jukumu hili la msingi kama wangezingatia, kama wangewezeshwa basi naamini leo hii sisi tungekuwa tunajua tuzalishe tani ngapi za mbaazi na zitakwenda wapi kwa sababu tayari watakuwa wameshatupa bei na uelekeo wa mazao haya tutayapeleka wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimwombe sana kaka yangu Mheshimiwa Kakunda atakapokuja kuhitimimisha basi atueleze na kama hawajajipanga katika uelekeo huo, basi hebu tuwasaidie na akiwasaidia hawa kuwaweka vizuri maana yake watawasaidia hata watu wa Wizara ya Kilimo ku-*forecast* bei, lakini pia kupanga mipango mizuri ambayo haitaenda kuwaumiza wakulima wetu kama ambavyo sasa hivi inaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo naomba nichangie, ni eneo lingine linalohusu watu wa *SIDO*. Nilikuwa najaribu kupitia hapa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kuna huu Mfuko wa Maendeleo ambao unakopesha wakulima wa *NEDF*. Naomba nimpongeze sana na nilikuwa nafuatilia hapa takwimu za mikopo midogo midogo ambayo imekwenda kwa wajasiriamali. Hata hivyo, *concern* yangu kubwa ambayo nataka tuweze kushauriana vizuri ni tuone namna gani mfuko huu wa *SIDO* unavyochangia na

unavyosambaa kuwafikia wale wanyonge walioko maeneo ya mbali kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napitia takwimu nyuma za hiki kitabu nione katika Mkoa wa Lindi mathalani, Wilaya ya Nachingwea, ni wajasiriamali wangapi wadogo wadogo ambao wamenufaika na Mfuko huu wa *SIDO*, lakini ni kiasi gani cha fedha ambacho ndani ya miaka hii miwili, mitatu kimeenda kwa wakulima. Niwapongeze kwa sababu fedha nyingi zimekwenda, lakini uwiano wa namna ambavyo tumewafikia wajasiriamali wadogo wadogo kidogo unanitia mashaka. Sasa naomba kipaumbele chetu kijielekeze kwa kadri ya uzalishaji tunaoufanya na namna ya kuwezesha wajasiriamali wadogo kwa shughuli za uzalishaji wanazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao mamalisha lakini pia tunao watu wadogo ambao wanafanya kazi ya ubanguaji wa korosho kule kwetu. Haya makundi yote kama tungeweka utaratibu mzuri wa kugawa hizi fedha naamini tungeweza kuwafikia wanyonge wengi sana walioko kule chini badala ya kukopesha tu katika maeneo makubwa au maeneo ya mijini ambako hawa ndiyo wamekuwa wanajua fursa na wamejua kuzichangamkia na kuacha wakulima wetu wadogo wadogo amabo wako katika maeneo yale ya mikoani na wilayani kule chini. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri naomba sana watakapokuja kuhitimisha watuwekee utaratibu mzuri ambao utapelekea hata wale wakulima na wajasiriamali wadogo wadogo walioko chini wapate kunufaika na Mfuko huu wa Maendeleo kwa ajili ya kukopesheka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ambalo nataka nichangie ni eneo la mradi wa matrekta ya *URSUS*. Naomba nipongeze mradi huu wa matrekta ya *URSUS* ambao uko pale Kibaha. Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara yake tunatambua jitihada kubwa ambazo wamekuwa wanazifanya, lakini bado naomba tuone namna ambavyo mradi huu unavyoweza kuwafikia pia walengwa ambao ni wakulima walioko katika maeneo ya pembezoni. Kibaha ni

center, mkulima anayetoka Mtwara, Ruvuma, Lindi ni nadra sana kufahamu fursa inayoweza kupatikana kupitia mradi huu wa matrekta. Matrekta haya ni bora na tulitamani sana yangewafikia wakulima wetu ili waweze kuzalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ukienda kwenye baadhi ya maeneo trekta ni ya kugombaniana. Wakulima hawana *access* ya kupata vyombo hivi kwa ajili ya kulima kilimo cha kisasa. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri ikimpendeza hebu tuone utaratibu wa kufungua *center* katika baadhi ya maeneo. Kwa mfano tunaweza tukaweka *center* ya Kusini ambayo itajumuisha mikoa mitatu ya Lindi, Mtwara, Ruvuma kule *at least* wakaweka *sample* ya matrekta na utaratibu wa namna ambavyo wakulima wetu wanavyoweza kukopa au kuweza kuyapata haya matrekta kwa gharama nafuu zaidi, tofauti na ilivyo sasa hivi mtu wa kutoka kule mbali aweze kuyafuata haya matrekta Kibaha au maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi mradi mkubwa ambao tunategemea kukopa matrekta ni wa *SUMA JKT* ambao bado haufanyi vizuri sana. Hata hivyo, kupitia mradi huu naamini Serikali kama mtaweka mazingira mazuri, basi wakulima wetu wengi watapata *access* ya kufikia na kuweza kuchukua matrekta ambayo yatawasaidia katika uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwisho ambalo nilitaka...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, kengele ilishagonga.

MHE. HASSAN E. MASALA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Boniventura Kiswaga atafuatiwa na Mheshimiwa Mashimba Ndaki, Mheshimiwa Antony Komu ajiandae.

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba niipongeze Serikali kwa namna ambavyo inaendelea na jitihada zake za kuhakikisha kwamba wawekezaji kwenye nchi hii wanapatikana. Japo zipo kasoro ndogondogo ambazo tunapaswa sisi Wabunge tushauri na tusikilizwe na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwona Mheshimiwa Rais anapokuwa na mahangaiko makubwa sana moyoni mwake, kadri ambavyo anachukizwa na mwenendo ambao unazuia uwekezaji wa haraka kwenye nchi hii kwenye viwanda vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na viwanda vingi ambavyo tulivibinafsisha, ningeshauri Serikali iweze kuvipitia upya tuone kama vinafanya vizuri kazi iliyokusudiwa. Kwa sababu inaonekana kuna viwanda vingi havifanyi vizuri na viwanda hivi kama vikifanya vizuri tutaondoa kabisa tatizo kubwa la ajira lililoko nchini mwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda ambavyo vilikuwa vikileta uchumi kwa nchi hii, bado havijatazamwa vizuri. Tulikuwa na Kiwanda cha Zana za Kilimo kule Mbeya, tulikuwa na viwanda vya nguo mpaka leo havifanyi vizuri, tulikuwa na viwanda vya kapeti, vimeshakufa, tulikuwa na viwanda vya kutengeneza vifaa vya umeme nchini, vimeshakufa.

Namshauri sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, aweze kuvipitia upya viwanda hivi ili tuweze kuona kama vinaweza kuendelea kuzalisha kama vilivyokuwa vinazalisha zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapowekeza kwenye viwanda, tunaongeza ajira kubwa, tukiongeza ajira, watumishi wale wanalipa kodi, kwa maana ya *PAYE, SDL* pamoja na *WCF*. Kwa hiyo, huo ni mkusanyiko mkubwa

ambao unaweza kuchochoe uchumi kwenye nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko kasoro nyingi ambazo wawekezaji wanazipata kupitia taasisi zetu nyingi ambazo wengine jana walichangia, ziko taasisi kwenye viwanda na uwekezaji wa jumla karibu 27 na kuendelea. Tungeshauri, taasisi hizi za Serikali ziunganishwe ziwe mlango mmoja, zipunguze *bureaucracy* ili wawekezaji waweze kuwekeza kwa haraka zaidi. Bila hivyo, tutakuwa tunaimba wimbo uleule bila mabadiliko kwenye nchi hii. Niishauri sana Serikali isikilize ushauri wa Wabunge wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende pia kwenye *service levy*. Wakati sheria hii ya *service levy* inatungwa ilikuwa imejielekeza kwenye viwanda, wala haikujielekeza kwenye maduka ya jumla ya rejareja lakini leo biashara hizi zinakufa kwa sababu ya kutoangalia upana wa sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wanatunga sheria hii, kwa mfano, *Breweries*, ikiwa pale Mwanza llemela, *distributor* wa Shinyanga, Geita, Singida na Tabora, akiuza bia yake watu wa Tabora, Singida, Shinyanga wana-*claim* madai yake *Breweries* llemela. Leo *distributor* wa llemela na Shinyanga, ukichukua bia pale kwa *distributor* wa llemela, ukapeleka Misungwi, unadaiwa *service levy*, hata yule mwenye *bar* ya kawaida naye anadaiwa *service levy*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mwenye biashara kwa mfano mfuko wa sukari, gharama yake ni shilingi 108,000, faida yake ni Sh.500, akitozwa *service levy* ni shilingi 324.

Kwa hiyo, anabakiza kama shilingi 170. *Service levy* inatozwa kwa mauzo, mfanyabishara hawezi ku-*declare* kodi yote kwa sababu inachukua gharama kubwa kuliko ingetozwa kwa faida. Kwa nini tusibadilishe sharia ya *service levy* tukatoza kwa faida, tukiwa tumeondoa gharama za

uendeshaji kama ambavyo tunatozo *corporate tax*. Tukifanya hivyo, tutawaondolea adha wafanyabiashara hawa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba ukae na wafanyabiashara, kama ambavyo Waziri Mkuu alikaa na wafanyabiashara kule Kariakoo, alibaini mambo mengi. Niombe pia Mawaziri mnaohusika, Rais alipokaa na wafanyabiashara na wachimbaji wa madini akaleta mapendekezo ya sheria hapa, leo tunaona ambavyo madini yetu yanalipa zaidi ya kile kilichokuwa kinalipwa, wakwepaji kodi wanaondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokaa na wafanyabiashara, wana manung'uniko mengi ambayo kwa kweli tukiwasikiliza na kuleta hapa marekebicho ya sheria, tunaweza kusaidia biashara nchini. La sivyo, hatutakuwa tumesaidia biashara nchini, tukiendelea kuwa na kodi nyingi ambazo hazina faida. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inashindikana *service levy* kutozwa kwa faida, basi ipungue iwe 0.1% badala ya 0.3%. Kwa sababu hata benki wamepewa waraka na Katibu Mkuu, Wizara ya TAMISEMI, wawe wanachajiwa 0.1%, kwa nini wafanyabiashara wengine nao wasipate huo mwanya wa kuweza kutozwa kwa asilimia hiyo? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, *OSHA* ina msaada gani kwa biashara? Tulikuwa tunajua *OSHA* inasimamia usalama wa watumishi kazini lakini leo wamekuwa watozaji wa kodi, watu wenye viwanda, *petrol station* na hoteli, wanalalamika, kwa sababu badala ya tozo zile zingine za kawaida (*WCF*) ambapo ni mchango ambao unasaidia wakati mtumishi anapata tatizo, labda la ajali kama fidia wanatoza kwa mwaka, kati ya milioni moja mpaka milioni tano, wafanyabiashara hawa wanalalamika sana. Tuangalie tozo ambazo haziwezi kusaidia kwenda mbele...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, muda wako umekwisha, ahsante sana.

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, atafuatiwa na Mheshimiwa Antony Komu, Mheshimiwa Katani Ahmed Katani ajiandae.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi pia niweze kuchangia Wizara hii ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, kwa kuwa na ndoto kubwa ya Tanzania ya Viwanda ifikapo 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niwapongeze Mheshimiwa Makamu wa Rais pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutafsiri ndoto hii vizuri kwa watendaji wa Serikali walioko chini yao. Kwa kweli, mambo yakienda hivi, tunaweza kufikia ndoto hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumze mambo machache tu ambayo Serikali lazima iyaangalie tunapotaka kufikia ndoto hii ya Tanzania ya Viwanda ifikapo mwaka 2025. Hatuwezi kuwa na viwanda imara ikiwa hatuwezi kuvilinda. Viwanda vinavyoanzishwa kwenye nchi yetu lazima vilindwe. Hakuna nchi ambayo imetamani kuwa nchi ya uchumi wa viwanda, halafu ikaviacha viwanda vyake bila kuvilinda kwa sababu vingeweza kufa. Hivyo hivyo, nasi kama nchi, lazima tuwe na juhudi za makusudi kulinda viwanda vyetu ili viweze kusimama, kukua na kuimarika. Vinginevyo tusipovilinda, itakuwa ngumu kufikia ndoto ya Mheshimiwa Rais ya Tanzania ya Viwanda mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba tunaweza kuvilinda viwanda vyetu kwa njia za kikodi na

utawala. Tusipofanya hivyo, nimesema Tanzania ya Viwanda hatuwezi kuipata haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vyetu vingi vimeanzishwa lakini havifanyi kazi kwa uwezo wake kamili. Tulikuwa na viwanda vya nguo 33 mwaka 1992 lakini leo tuna viwanda vitano vinavyofanya kazi lakini navyo kwa chini ya kiwango. Ni kwa sababu viwanda hivi vimeachwa wazi vishindane na mabwana wakubwa walioanzisha viwanda vya nguo muda mrefu kama India, China, Uturuki na nchi zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kulinda viwanda vyetu vya nguo itakuwa ni ngumu, lakini tukivilinda viwanda hivi, vinaweza vikatupatia ajira kwa wakulima wetu, ajira kwa watu wetu, kwa maana ya wafanyakazi viwandani lakini pia vinaweza vikaongeza kipato kwa ajili ya taifa letu kwa maana ya kulipa kodi. Tusipofanya hivyo hatutafanikiwa kabisa *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kuona namna alivyotoa hotuba yake Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, sijaona kama kuna sera makusudi ya kulinda viwanda vyetu ili viweze kukua. Kwa namna vilivyo sasa hivi, viko kwenye kiwango cha chini sana, ni viwanda ambavyo tunaweza kuviita ni vichanga. Sasa tukivi-expose kwenye mashindano haya makubwa, havitaweza kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hotuba ya Waziri, amesema viwanda vyetu vya chuma vina uwezo wa kuzalisha tano milioni moja, lakini vinazalisha tani laki mbili na arobaini, mwisho hapo. Sasa tatizo ni nini? Tatizo ni kwamba vinashindanishwa na viwanda vya chuma vilivyostawi na kuimarika muda mrefu vya Wachina.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda hivi visipolindwa, haviwezi kukua na vikiendelea kufanya kazi kwa uwezo wa chini namna hii, gharama zake ni kubwa, matokeo yake wananchi wetu wanaendelea kununua nondo na vifaa vingine vya chuma kwa bei ya juu. Lazima tulinde viwanda

vyetu, lazima tuvilinde viwanda vya nguo, chuma na viwanda vinavyoinukia sasa hivi. Tusipofanya hivyo, kuwa na Tanzania ya Viwanda, itakuwa ni ndoto 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pia vivutio vya uwekezaji kwenye viwanda. Vivutio hivi vya uwekezaji kwa viwanda, lazima vile vinatabirika. Mwaka jana tulipitisha sheria kuvilinda viwanda vinavyozalisha madawa, ni jambo zuri sana, lakini tusiishie kulinda viwanda vinavyozalisha madawa tu lazima twende pia kwenye viwanda vingine. Lazima tuweke vivutio vinavyoeleweka, vinavyotabirika, vitakavyokuwa vya muda mrefu ili hawa wawekezaji watakapokuja hapa ndani, wawe na uhakika ya kwamba vivutio hivi vitakuwa ni vya kudumu na hivyo wanaweza wakafanya biashara hapa ndani vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala la Mradi wa Mchuchuma na Liganga. Mradi huu wa Mchuchuma na Liganga ni wa muda mrefu sana. Kwa kweli niungane na wengine wote waliosema kwamba imechukua muda mrefu na inabidi sasa juhudi za makusudi zifanyike ili tuwe na mradi huu mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka kutoa tahadhari...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, kengele ya pili imeshagonga.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, muda ni mdogo sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na, Mheshimiwa Antony Komu, atafuatiwa na Mheshimiwa Mheshimiwa Katani Ahmed Katani, Mheshimiwa Shukuru Kawambwa ajiandae.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii ambayo ni muhimu sana katika ustawi wa taifa letu kwa sababu tukiwa na tukiweza kufanya biashara vizuri, tunaweza tukafanya mambo mengine mengi ya kijamii na tukaweza kwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze alikoishia ndugu yangu Mheshimiwa Mashimba Ndaki, ambaye tumesoma darasa moja kwamba ili tulinde viwanda vyetu, ni lazima tuwe na mazingira yanayotabirika. Katika nchi yetu, tuna tatizo kubwa sana la mazingira ya biashara yasiyotabirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi huu uliopita tu, *TRA* walitoa tangazo la kupiga marufuku vinywaji vyote ambavyo havina stika ya kieletroniki kwamba ikifika tarehe 30 ya mwezi uliopita, hivyo vinywaji vyote vitakuwa vimekoma na havitakuwa na thamani tena. Hiyo marufuku inavyofanyika sijui walizingatia nini kwa sababu hivyo vinywaji vilinunuliwa katika utaratibu wa kisheria na vina stika ambazo zinatambulika na vimeshasambazwa katika nchi nzima. Maana yake vinywaji hivi vinapatikana Dar es Salaam, vinakwenda kwenye jimbo fulani, labda la ndugu yangu Mlimba kule Ifakara, sasa unavyowaambia unawapa siku chini ya 30 kwamba wavirejeshe vyote viweze kupata stika nyingine na wasipofanya hivyo, hiyo biashara itakuwa imekoma, kwa kweli ni kitu cha ajabu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Naibu Waziri nilimweleza na amelifanyia kazi. Katika hali ya namna hiyo, inatupa shida na ndiyo maana biashara inasinyaa kila kukicha katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, kuna masuala haya ya kurejesha *VAT*. Tumeambiwa hapa kuna *burden* ya zaidi ya shilingi bilioni 45, sasa ni nani anakuja kuwekeza hapa wakati hana uhakika wa kuridishiwa kile ambacho kiko kwenye mkataba? Kwa hiyo, katika hali kama hii, inatupa shida sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira ya kufanya biashara ni magumu sana. Ndugu yangu Mheshimiwa Bashe alisema jana kuhusu habari ya kuanzisha kiwanda cha kusindika maziwa. Leo tunavyozungumza, nchi yetu inazalisha maziwa lita bilioni 2.4 kwa mwaka lakini maziwa tunayosindika ni lita kama milioni 37 tu. Hii ni kwa sababu ya mlolongo wa kodi ambazo zipo, jana Mheshimiwa Bashe alisema ni 26, mimi ninalo andishi hapa, ni tozo na kodi 28. Taasisi au mamlaka ambazo zinakwenda kushughulika na wewe siku ukiamua kuanzisha kiwanda cha kusindika maziwa ni 11 na taasisi moja inaweza ikarudi hata mara nne kwenye hiyo biashara yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wa Kenya, leo wanazalisha maziwa lita bilioni tano kwa mwaka, wanasindika zaidi ya lita bilioni tano kwa mwaka. Leo Uganda wanazalisha lita bilioni 2.4, wanasindika zaidi ya lita laki tano kwa siku, sisi tuko kwenye laki moja na elfu hamsini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ndugu zangu ili uanzishe kiwanda cha kusindika hapa Tanzania, unapashwa ulipe zaidi ya shilingi milioni 33 ndiyo kiwanda kianze kuzalisha. Sasa tunang'ang'ania milioni 33 lakini tunapoteza ajira na kodi ambazo tunaweza tukazipata kwa kuwepo na viwanda vingi, tunapoteza mapato ambayo yanatokana na bidhaa zinazotokana na maziwa ambazo ziko zaidi ya 20. Sasa jamani, hii ni akili gani? Tumelogwa na nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa hiyo hatutumii fursa ambazo tunazo ambazo tumepewa na Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye hoja ya tatu, nayo ni sakata la korosho. Nasi kwenye ukurasa wa 42 kwenye kitabu chetu cha Maoni ya Kambi ya Upinzani Rasmi Bungeni, tumesema watu wawajibike. Hapa nataka niwe *very specific*; na niliombe sana Bunge hili linisikilize na lichukue hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliingia mkataba na kampuni inaitwa *INDO Power* ya Kenya. Siku tulivyoenda kuingia mkataba Serikali ilikwenda pale, Mawaziri kadhaa

walikwenda pale akiwepo Waziri wa wakati huo wa Katiba na Sheria, Profesa Palamagamba Kabudi na Gavana wa Benki Kuu alikuwepo pale. Katika watu waliozungumza, Kabudi alizungumza, akasema Kampuni hii ina weledi, ina uzoefu, ina uwezo wa kifedha na hata huyo mmiliki wa kampuni hiyo alikuja kwa ndege binafsi ya kukodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Gavana wa Benki Kuu akasema alifanya *due diligence* kuona kwamba kampuni hiyo ina weledi wa kutosha na uwezo wa kutosha wa kufanya hiyo biashara. Baada ya miezi minne, ile biashara, kama Watanzania walivyosema na Mheshimiwa Rais alisema, Watanzania siyo wajinga. Walisema hii kampuni ni ya kitapeli, haina uwezo huo. Waliandika kwenye mitandao. Baada ya miezi minne imeonekana kampuni ile haina uwezo, imeshindikana na ile biashara imekufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli Bunge hili linakubali Mheshimiwa Kabudi aendelee kubaki na Uwaziri wake, mtu ambaye kila kukicha anamdanganya na kumfanya Mheshimiwa Rais aendelee kupotoka hivi! Hapa duniani Rais wa nchi akilalamika, Rais wa nchi akilia, kinachoweza kumsaidia ni Bunge la nchi. Kama Bunge la nchi likishindwa, basi tunamuachia Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri tusifike hapo ndugu zangu, Bunge lako Tukufu lichukue hatua ili hawa watu wawajibike. Kabudi; na ningefurahi sana angekuwepo hapa; Kabudi, mnakumbuka masuala...*(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Komu, ni Mheshimiwa.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Profesa Kabudi, nafurahi kama angekuwepo hapa, kwa sababu mnakumbuka *issue* ya makinikia, mnakumbuka *issue* ya Sheria ya PPP, mnakumbuka *issue* ya sheria ya kulinda rasilimali za nchi hii, mnakumbuka *issue* ya Sheria ya Takwimu; haya mambo yana utata. Kwa hiyo, naliomba Bunge hili lichukue hatua dhidi ya Kabudi, awajibike. Hawa wengine ndugu zangu hapa akina Kakunda,

Mheshimiwa Japhet Hasunga, hawa ni watu ambao wako kwenye basi tu, lakini anayeendesha hili basi, ni Kabudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana, tusije tukamfanya Rais wetu aonekane kwamba ni mtu tu ambaye analialia jambo ambalo siyo heshima kwa Bunge hili na siyo heshima kwa Watanzania walio...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Katani Ahmad Katani, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa na Mheshimiwa Maulid Mtulia ajiandae.

Wachangiaji wa Chama cha Wananchi CUF mtachangia kwa dakika tano tano, ninayo majina manne hapa. Naambiwa Mheshimiwa Maftaha hatachangia, kwa hiyo, Mheshimiwa Katani Katani atachangia kwa dakika kumi. *(Makofi)*

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi, lakini nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuweza kuchangia katika Wizara hii. Mimi nianze kidogo kuweka sawa baadhi ya mambo ambayo yapo kwenye Wizara hii ya Viwanda na Biashara. Nitaendelea kuunganisha pale alipochangia ndugu yangu Mheshimiwa Antony Komu suala la wasaidizi wa Mheshimiwa Rais kumpotosha kwa mambo mengi sana. Kwenye korosho, hili limetokea, watu wamempotosha sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Mheshimiwa Rais akiwa Arusha alizungumzia suala la kangomba ambalo nataka nikwambie, kwa sisi Waislam hiyo biashara inayoitwa

kangomba siyo dhambi, kwa sisi Waislam. Kwa sababu ipo hadithi sahihi kabisa inatoka kwa Ibn Abbas Radhiya Allahu-Anhu, Ibn Abbas anasimulia, alikuta Mtume amefika Madina na alipofika Madina akakuta watu wanafanya biashara ya matunda kwa makubaliano, kwa uwiano wanaokubaliana wenyewe. Mtume alipokuta biashara ile inakwenda, akasema hii biashara siyo haramu. Hadithi hii imepokelewa vizuri kabisa na wapokeaji wazuri kwa sisi Waislam ambao ni Bohari pamoja na Muslim. Kwa hiyo, kangomba siyo haramu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Waziri wa Biashara ambaye upo hapa, kwenye korosho tunajua watu hawajapata fedha mpaka leo; wapo waliopata fedha na upo utaratibu ambao umetumika labda hujui, nikukumbushe tu kwamba mwezi wa Nne zimetoka fedha, mtu anadai shilingi milioni 59 ili ku-*rescue situation* ionekane wakulima wamelipwa fedha, anaingiziwa shilingi milioni tisa anadai shilingi milioni 41. Hicho ndicho kichokuwepo kwenye korosho. Ukitaka ushahidi, mimi ninayo simu hapa, nimeingiziwa fedha mwenyewe. Nadai shilingi milioni 48, nimeingiziwa shilingi milioni nane, nyingine naendelea kudai na hili unalijua vizuri, unalifahamu vizuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo wakulima wa korosho wameanza kufanya palizi, hawana fedha. Kama hawana fedha, wanatafuta watu wanaingia makubaliano, mtu anampa shilingi 100,000/= wanakubaliana wenyewe kwamba atampa gunia moja la korosho. Mnakaa mnamshauri Mheshimiwa Rais kwamba aliyefanya vile ni kangomba. Hii ni biashara halali kwa sisi Waislam. Kwa hiyo, kangomba siyo haramu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya msingi ya biashara hii ni kwamba Serikali hamjajipanga. Leo Serikali imezungumza kwamba inachukua fedha kuwalipa wakulima, lakini mpaka wakulima wanadai fedha za korosho. Je, mkulima asilime korosho? Anapatikana mtu ambaye amekubaliana naye mwenyewe kwa hiari yake anampa fedha, mwingine anachukua trekta anaenda kulima shamba

la mikorosho. Akishalima ekari moja kwa makubaliano kwamba atampa korosho kilo 50, lakini mkikaa mnamwambia Mheshimiwa Rais kwamba wale watu ni kangomba. Wale siyo kangomba. Kwa hiyo, jambo hili lazima Mheshimiwa Waziri alijue vizuri sana ili akitokea, isije mwakani tena watu mkakurupuka mkamshauri Mheshimiwa Rais ndivyo sivyo kwenye korosho.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Katani, ongea nami ujumbe wako uwafikie. Kwa sababu ukiongea nao moja kwa moja sasa, hakuna namna wao wataupata. Wewe ongea na kiti ili wao waupate.

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwa hiyo, naomba sana suala hili wakati wanamshauri Mheshimiwa Rais waende kufanya *research* kwanza, wajue matatizo ya wakulima yakoje? Mwaka huu tutakuwa na tatizo la dawa. Kuna tatizo la wakulima, kulima korosho yenyewe. Leo ukienda Mtwara, mikorosho watu wanawekeza. Shamba lenye ekari 10 mtu anawekeza kwa shilingi 500,000/= tu. Yule aliyewekezwa shamba, akivuna gunia 50 kwa sababu amewekeza na hana shamba, kesho kutwa anataka akuoneshe hati ya shamba, maana yamefanyika mwaka huu. Mtu alikuwa hatakiwi kulipwa fedha, mpaka alipokwenda Mheshimiwa Rais juzi, akasema watu wote walipwe. Huu ni ushauri ambao wasaidizi wa Mheshimiwa Rais wanamshauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwenye hili, naomba sana Bunge lifahamu vizuri, kwamba kwenye biashara hizo za mazao na siyo kwenye korosho tu, hata kwenye mpunga. Mimi nina trekta Ifakara pale, nalimisha mashamba, mwisho wa siku wananilipa magunia ya mpunga. Ukija kutafuta shamba langu, mimi sina shamba Ifakara.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA): Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, nadhani ninatoa fursa mwishoni kwa wachangiaji kwa

sababu ya muda wetu. Kwa hiyo, tuwe... (*Kicheko/Makofi/Vigelegele*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hebu tusikilizane. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Naibu Waziri mtapata fursa ya kufafanua jambo hili. kwa sababu muda wetu ni mfupi, watu wamalize kuchangia halafu ninyi mtapewa muda wa kutoa maelezo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, ni taarifa zote. Maana msije kuwa mnapiga makofi kwamba mtu ataruhusiwa taarifa. Kitakachoruhusiwa ni utaratibu na siyo taarifa. Mheshimiwa Katani. (*Makofi*)

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nataka niombe sasa Mheshimiwa Waziri ajaribu kutueleza kama alivyokuwa anazungumza ndugu yangu Mheshimiwa Komu; ile kampuni, baada ya kampuni kushindwa sasa kuilipa Serikali zile tani 100,000 za korosho walizokuwa wameingia makubaliano ya kisheria, watuambie hao *INDO Power* wanatufidiaje kwa kutudanganya? Maana wamelidanyanga Taifa. Ni lazima tuone *INDO Power* moja wanashtakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili watulipe fidia kwa sababu Watanzania walikuwa na matumaini kwamba korosho tani 100,000 zimepata mnunuzi, kumbe ni matapeli, Wakenya wamekuja kututapeli na wametudhalilisha wakulima wa korosho ambao mpaka leo hatujapata fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala la viwanda. Kule Kusini tulikuwa na viwanda vya kubangua korosho takribani 12. Vile viwanda vimeuzwa. Waliouziwa vile viwanda, maelezo yalikuwa waendeleze vile viwanda kwa ajili ya kubangua korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anajua, vipo viwanda leo ni maghala ya kutunzia korosho, siyo viwanda vya kubangua korosho. Wakati ana *windup* atuambie Serikali ina mpango gani kwa wale walionunua viwanda kwa dhamira ya kubangua korosho kwa kubinafsishwa wana mpango gani kuhakikisha wale walioshindwa wana mpango gani kuhakikisha wale walioshindwa kupangua korosho viwanda vinataifishwa, virudi kwa watu ambao wanaweza kupangua korosho ili tuweze kuendelea na tasnia ya viwanda Tanzania? Atusaidie na bahati nzuri alikuwepo kwenye ziara ya Mheshimiwa Rais na haya ameyasikia mwenyewe na mengine amejionea mwenyewe kwa macho, ajaribu kutusaidia kujua viwanda vile vya korosho mambo yake yanakuaje? *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU SPIKA: Mimi sina kengele hapa juu Waheshimiwa Wabunge, muda unaangaliwa hapo na kengele mbili zimeshagonga. Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Maulid Mtulia na Mheshimiwa Gibson Meiseyeki ajijandae.

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia katika hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Viwanda na Biashara. Nichukue fursa hii kumpongeza sana yeye Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa pongezi sana kwa Serikali kwa mkakati huu wa ujenzi wa viwanda; ni mkakati mzuri, mkakati wenye tija sana na ni mkakati ambao

utapelekea nchi yetu kuweza kufika katika hadhi ya nchi ya uchumi wa kati. Mkakati huu wa ujenzi wa viwanda nchini naomba nimpe pongezi sana Mheshimiwa Rais kwa kuusimamia mkakati huu kwa nguvu zake zote. Ni mkakati ambao una tija sana na ni mkakati ambao ni ukombozi kwa vijana wa kike na wakiume Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukombozi mkubwa kwa sababu katika mambo ambayo yanawaathiri vijana sana hivi sasa na tatizo hili linaendelea, ni ajira. Vijana hawana ajira; waliosoma wasiosoma, wenye vyeti vya Chuo Kikuu, nakadhalika, ajira imekuwa mtihani mkubwa. Viwanda vitatuletea ajira. Kwa hiyo, Mheshimiwa suala hili la viwanda lisimamie kwa dhamira nzuri ili ilete ukombozi kwa wananchi wetu na hususan vijana wa kiume na wa kike katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Serikali kwamba katika ujenzi wa viwanda hivi, basi msisitizo uwe katika viwanda ambavyo vinatumia malighafi ya hapa ndani nchini kwetu. Malighafi ya hapa nchini kwetu ndiyo maana miradi kama Mchuchuma, Liganga ni miradi migumu sana kwa sababu inatumia moja kwa moja malighafi ya nchi yetu, lakini viwanda vya saruji, viwanda vya vigae, viwanda vya kuchakata minofu ya samaki, viwanda vya kuchaka muhogo na kadhalika, hivi ni viwanda muhimu sana, kwa sababu kule tunapata faida mara dufu; tunapata ajira viwandani, tunapata pia kazi katika uzalishaji wa zile malighafi ambazo zinaenda kwenye viwanda hivi. Kwa maana hiyo, tunakuza zaidi wigo ule wa ajira kwa vijana wetu wa Kitanzania ambao tunahitaji sana waweze kupata kazi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda hivi vinajengwa ardhini. Kwa hiyo, ni muhimu sana Serikali ikafanya juhudi kubwa kuhakikisha kwamba inatoa maeneo ya kujengea viwanda mapema; na kwa maana hiyo pia kuyalipia fidia kwa wale wananchi ambao wana maeneo hayo. Nalisema hili kwa uchungu sana kwa sababu katika juhudi hii ya kutwaa maeneo, katika Jimbo la Bagamoyo kuna wananchi sasa ni miaka 11. Huu ni mwaka wa 11 wametwaliwa maeneo yao

chini ya *EPZ I* na *EPZ II* na mpaka leo mwaka wa 11 hawajalipwa fidia hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1971 Mheshimiwa Marehemu Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere mwaka aliwaita Waingereza kuja kuwaonesha maendeleo makubwa ambayo tumepiga ndani ya kipindi cha miaka kumi. Miaka kumi ni muda mrefu. Sasa huu ni mwaka wa 11, wengine wamefariki, wengine wamepata vilema, wengine yaani wamekata tamaa. Wananchi hawa ni wananchi maskini kabisa, hawana uwezo mkubwa. Kimfaacho mtu chake, wamekaa mwaka wa kwanza, wa pili, wa tatu, wa 10 na wa 11 hawajapata fidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Bagamoyo *EPZ* imechukua maeneo mara mbili; *EPZ I* imechukua eneo jumla ya hekta 5,742, halafu tena *EPZ II* hekta 3,338 kwa maana ya jumla ya hekta 9,080 katika hao wafidiwa ni 2,180, mpaka leo kuna wafidiwa 1,025 ambao bado hawajalipwa, miaka 11 baadaye wafidiwa 25,000. Jumla ya fedha ni shilingi bilioni 51 tu ndizo wanazodaiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi bilioni 51 zimesubiriwa kwa miaka 11. katika bajeti ya shilingi trilioni 32, shilingi bilioni 51 ni tone tu katika bahari; na wananchi hawa ndiyo kila kitu, maana yake wanategemea kila kitu. Wengine akina mama wajane wameachiwa watoto, wajukuu na kadhalika, kupata hela hii ndiyo ukombozi wa kila jambo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali yangu adhimu, Tukufu iweze kuwalipa fidia wananchi hawa mapema iwezekanavyo, wamesubiri sana. Katika kusubiri kwao maana yake watakapokuwa wamelipwa tu, ardhi hii iko *free* sasa kuweza kutumika kwa ajili ya viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo mwaka 2018 katika bajeti ni liliongelea, naiomba tena Serikali yangu Tukufu mwaka huu, *EPZ II* imehusisha maeneo yenye makazi makubwa ya wananchi jumla ya hekta 3,338; Ziha

kwa Awadhi, Ziha kwa Mtoro, Mlingotini, Kondo na Kiromo, vijiji vyote hivi vina wakazi wengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na tahadhima, naiomba Serikali yangu Tukufu iondoe maeneo haya ya makazi makubwa ya wananchi katika mradi wa *EPZ* ili wananchi hawa waendeleo kuishi kwa amani na utulivu. Wameshatoa zaidi ya hekta 5,700 kwa ajili ya hii *EPZ* na nadhani inatoshia kabisa na hawajalipwa kwa miaka 11, wala hawana mahali pa kwenda na hawana nguvu za kuhamia mahali pengine. Naiomba Serikali yangu adhimu iwaache wananchi waendeleo kuishi katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi...*(Makofi)*

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda umeshaisha Mheshimiwa. Kengele ya pili imeshagonga.

MHE.DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Naibu Spika, muda umekuwa mfupi. Nakushukuru sana kwa kunipa fursa. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza mchangiaji Mheshimiwa Katani alikuwa anatakiwa kuchangia dakika kumi, lakini naomba radhi kwa sababu meza ilimwekea dakika saba badala ya dakika kumi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Katani tunaomba radhi, lakini wachangiaji wa *CUF* watakaofuata watapewa zile dakika tatu zako zilizobaki ili muda wa Chama cha Wananchi *CUF* uwe umezingatiwa. Ahsante sana.

Kwa hiyo, tutaendelea na Mheshimiwa Maulid Mtulia, atafuatiwa na Mheshimiwa Gibson Ole-Meiseyeki na Mheshimiwa Ali Salim ajiandae.

MHE. MAULID S. MTULIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa fursa hii adhimu nami kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu lakini vilevile nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na salama. Pia nitoe pongezi zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wka kazi kubwa na juhudi yake na hasa kutuelekeza katika Tanzania ya viwanda. Hakika Tanzania ya viwanda inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waswahili tuna msemu wetu “mzigo mzito mpe Mnyamwezi” na sina shaka Waziri wa Wizara hii ni Mnyamwezi. Namwomba kila la heri afanye kazi hii tukimtegemea kwamba atatua hapa tulipo. Ushauri tu; Mheshimiwa Waziri Wabunge wenzangu wengi wamesema akae na wadau, lakini naanza kusema Mzee wangu akae na wafanyakazi wake, Wakuu wake wa Idara. Kuna tatizo limetokea wakati mwingine mabwana wakubwa hawatoi nafasi za kutosha kwa wataalam wetu kutoa ushauri. Sasa haya yote yaliyosemwa na Wabunge ni vizuri wakaenda wakakaa na wataalam, naamini wataalam wana njia ya kututoa hapa tulipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuja hapa na kilio chetu cha watu wa Dar es Salaam. Dar es Salaam kilikuwa ni kitovu chetu cha biashara, lakini leo iko wapi Dar es Salaam yetu ya biashara? Iko wapi Kariakoo yetu? Namtaka Mheshimiwa Waziri aturejeshee Kariakoo yetu ya Wanyarwanda, ya Warundi, ya Waganda na Wakongo. Kariakoo ambayo tulikuwa tunafanya biashara na mimi kama Mbunhge wa Kinondoni nanufaika sana na biashara inapochangamka katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakuwaje na biashara katika Jiji la Dar es Salaam kama hatuna miundombinu inayoweza kutuwezesha kufanya biashara? Nichukue fursa hii kuwapa pole Wanadar es Salaam wote kwa mafuriko yaliyotokea kutokana na mvua kubwa iliyonyesha. Dar es Salaam barabara zetu zinapitika kiangazi tu. Juzi tu hapo barabara ya Jangwani imefungwa kwa sababu ya mafuriko, barabara ya Mkwajuni imefungwa kwa sababu ya mafuriko

na niseme kwamba tunawaomba sana wenzetu wa Wizara ya Fedha, ule mpango wa *DMDP* waliokubali kutuongezea Dola milioni 100 kwa ajili ya kufanya mabadiliko, kujenga daraja vizuri pale, kufanya Dar es Salaam ipitike mpango ule ufanyike, kwa sababu haya ndiyo yanayoiua Dar es Salaam yetu na haya ndiyo yanayoiua Kariakoo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kariakoo ilikuwa ni kitovu cha uchumi, ilikuwa ndiyo Dubai yetu, lakini leo wapi haipo tena. Kwa hiyo namtaka Mheshimiwa Waziri asiulize tufanyeje kwa sababu ni jambo lililokuwa wazi kwamba Kariakoo imedorora, milango iko wazi, *frame* hazina wapangaji, biashara haifanyiki, Watanzania wanakwenda kuchukua mzigo kutoka Uganda, *it is shameful*. Unatoka hapa unakwenda kufuata mzigo Uganda watu ambao hawana bahari, kwa nini? Kwa sababu bandari yetu inasemekana kodi kubwa, watu wanapita Mombasa, wanapeleka mzigo Uganda. Sasa mambo haya mengine maana yake ni lazima tuyafanyie kazi. Haiwezekani Kariakoo inakufa ndani ya mikono yetu, haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nataka nizungumzie watu wangu wa sanaa (*COSOTA*); *COSOTA* wanasimamia hati miliki na hati shiriki, leo vijana wangu wacheza filamu, vijana wangu waimba muziki, vijana wangu wafanya sanaa kazi zao zinafilisiwa, kazi zao zinaporwa, zinadhulumiwa, wameingizwa mikataba ya *Chief* Mangungu. Msanii anakwenda kwa mtu ambaye anamtazama kama *sponsor*, anamwambia kazi hii bwana kwa vile umeileta kwangu unataka nikudhamini, sasa hii kazi itakuwa ya kwangu na wewe utakuwa msimamizi, hiyo ndiyo mikataba walioingia vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kazi zao zote zinasomeka ni kazi za mtu mmoja haiwezekani na Sheria ilikuwepo ya mwaka 1999. Ifike mahali Serikali iwatetee hawa watoto wa kimaskini, kazi zao zirejeshwe kwao wenyewe. Haiwezekani kama mtu ameingizwa mkataba wa kitapeli unasema aliuza mwenyewe, aliuza akiwa na uelewa? Aliuza kwa usahihi? Kama ameuzi, ana mkataba wa kuuza?

Hakuna. Mkataba uliokuwepo ni kwamba yeye, msimamizi na mjanja mmoja anajiita yeye ndiyo mmiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ifike mahali Serikali yetu iwe na uwezo wa kutoa maamuzi na hasa tunapowatetea vijana wetu wanyonge. Haiwezekani vijana wanyonge wanafanya kazi zao kwa jasho lao, halafu hawapati matunda ya kazi zao, haiwezekani. Lazima ifike mahali vijana wetu wapate matunda kutokana na jasho lao, siyo kurubuniwa rubuniwa. Hili jambo mimi kwa kweli nina *appeal* kwa Mheshimiwa Waziri na *COSOTA* lazima ifanye jambo ambalo vijana watahisi kwamba Serikali ipo pamoja nao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema biashara; biashara lazima iwe na miundombinu. Hivi sisi leo tuna biashara za viwanda, viwanda lazima uze. Leo nimeona kwenye kitabu saruji zinakwenda nje, lakini sijaona nondo. Hivi kweli Congo, Nchi za nje zinachukua saruji zinashindwa kuchukua nondo, lakini tunawezaje kupeleka nondo Congo kama hatujatengeneza miundombinu ya kutoka hapa Tanzania kwenda Congo? Tunawezaje kulitumia soko la Congo? Tunapokuwa sisi hatutengenezi miundombinu kwenda kulifuata soko, nilitegemea viwanda vyetu vinavyozalisha *cementile cement* ipite iende mahali ikafanye biashara. Mimi nategemea Wachina wanaingiza nondo Tanzania siyo kwa ajili ya soko la Tanzania, iwe ni *transit*, ipite kwa ajili ya kwenda kwenye masoko mengine na haiwezi kwenda kwenye masoko haya mengine lazima sisi tutengeneze miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo miundombinu ya kwenda Congo ni muhimu sana kwa sababu kuna soko kubwa, soko ambalo linaweza likawa ni suluhisho la biadhaa zetu za nondo, biadhaa zetu za *cement*, mahindi yetu, mchele wetu na bidhaa zote zinazozalishwa. Sasa tunapokosa kutengeneza hii miundombinu na kutengeneza kwamba vitu vinavyoingia viwe vinapita vitajaa hapa na vikijaa hapa badala yake vinaleta mzigo mkubwa kwa viwanda vyetu vya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nimengalia kwenye kitabu hapa kuna watu tunafanya biashara India, sijaona biashara Uturuki kitabu hiki hakijasema na Watanzania wengi sasa hivi wanachukua biashara Uturuki, lakini kitabu hiki hakijaeleza kwamba biashara ya Tanzania na Uturuki ikoje...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mtulia kengele ya pili imeshagonga, ahsante sana.

MHE. MAULID S. A. MTULIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Gibson Ole Meiseyeki utachangia kwa dakika tano, Mheshimiwa Ally Salim atachangia kwa dakika saba watafuatiwa na Mheshimiwa Salim Turkey.

MHE. GIBSON B. MEISEYEKI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii. Nianze kwa kusema kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati hiyo ya viwanda na biashara lakini pia mimi ni mjasiriamali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye vikao vyetu hivyo vya Kamati wakati mwingine tunapatwa na bumbuwazi kwa jinsi ambavyo kero hizi ambazo wafanya biashara na wawekezaji wanazipata katika nchi yetu. Kwa kweli hali ni mbaya ya kibiashara sasa hivi nchini na sisi humu ndani tumezidi kulia. Tumekuwa kama watu wa kulia tu na narudia kusema kwa sababu nimeshasema hivyo kipindi cha nyuma, ifike mahali tuisaidie Serikali na tuisaidie nchi yetu humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wamechangia kwa masikitiko sana humu ndani ya Wizara hii, sasa ufike wakati baadaye wakati tunapitisha hapa tumsaidie Waziri, baadhi ya kero hizi ambazo wafanyabiashara wamekuwa wakilia zitatuliwe humu humu ndani, tusiipitishie hii Bajeti leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara wanalalamikia sana, kwa mfano, suala la *ETS* hizi *electronic stamp*, ni kazi ya *TRA* lakini wanaogharamia ni wazalishaji, kwa nini msilipe wenyewe? Kwa sababu hizo *stamp* ni kwa faida yenu nyie kujua *production* za viwandani. Wanalalamika kwamba hizi fedha ni nyingi zinasababisha wanashindwa kukuza mitaji yao. Leo Waziri na Serikali humu ndani ifute hiyo ili tuweze kusonga mbele. Wengine wanasema hata matangazo ya biashara zao wanaweka mabango barabarani, *TRA* wanakusanya kama ni maeneo ya *TARURA* na wenyewe wanakuja wanakusanya fedha, sasa hawa watu watakuza mitaji yao lini? Kama inawezekana achaji mmoja mwingine abaki, kwa sababu *TRA* na *TARURA* ni *organ* ambazo zinaweza kufanya kazi pamoja kwa nini wanadaidai wafanyabiashara? Hivi viwanda vyetu vya ndani visipotangaza biashara zao watapataje masoko? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Komu hapa, kama siyo yeye ni nafikiri ni Mheshimiwa Japhary alisema ng'ombe ili aweze kupata maziwa lazima umlishe, lakini sisi hapa hatuwasaidii wafanyabiashara, tunawakwamisha na *in fact* na hali ya nchi yetu sasa hivi Kimataifa siyo nzuri kwa maana ya uwekezaji, *is not good*. Sasa tunaongea, tunalia halafu tukiondoka, mwakani tena tunaendelea hivyo hivyo. Nashauri kwamba Bunge hili leo liisaidie Serikali, tuwasaidie wananchi wetu, tuna vijana wengi wanamaliza Vyuo Vikuu kama wenzangu walivyotangulia kusema, hatujui wakitoka hapo wanakwenda wapi. Uwekezaji tunau-*discourage* badala ya kuu-*promote*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba kwamba leo tumsaidie, maana najua alikuwepo hapo Mheshimiwa Charles sasa hivi tunaye Kakunda, kuna wakati unaongea anakuangalia tu. Kuna namna hawawezi, wanashindwa, hawana cha kufanya. Kuna wakati umefika hapa tukafikiria pengine na wafanyabiashara wa nchi hii tuwakutanishe na Rais ili baadhi ya kero wazimalize pale pale *on the spot* maana yake hapa ndani tunaona tunazungusha tu, muda unakwenda, hakuna uwekezaji, tunaendelea kuzalisha vijana, hawapati ajira, sasa naona sisi kama Wabunge tuna

nafasi yetu hapa badala ya kulialia tu tunaweza tukahitimisha haya mambo humu humu ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hapa Waziri wa Fedha atuambie *ETS* wanaifanya vipi, habari ya mabango na kero nyingine hizo za kodi ambazo zimetamkwa hapa ndani, hizo kodi tu-*harmonize* akina *OSHA* na nashukuru Rais alivyokuwa kusini mwa nchi hii alishangaa nay hii *OSHA* maana yake ni nini. Anatoka *OSHA*, anaingia sijui mtu wa *levy*, msururu wa watu, kila siku wapo maofisini kwa watu. Wawekezaji tullionao hapa nchini kama hawatuzungumzii vizuri hatutapata wawekezaji wanya. Ni lazima tuhakikishe hawa tullionao tunawa-*contain* vizuri ili wanapoulizwa kuhusu uwekezaji Tanzania waweze kutu-*advertise*, waweze kuitangaza Tanzania kama ni sehemu nzuri ya kuwekeza, lakini sasa hivi tunapata *negative comments* kwamba Tanzania siyo sehemu nzuri ya kuwekeza. Sasa tutakwenda wapi na watoto ambao tunawazaa?

Mheshimiwa Naibu Spika, bidhaa zetu za ndani; najaribu kupata picha hivi watu wote humu ndani tungekuwa Wamasai tukawa tunavaa yale mashuka ya Kimasai ni viwanda vingapi vingekuwepo sasa hivi Tanzania vingekuwa vinajaribu kutuvalisha hizo nguo? Humu ndani tumevaa masuti tu hizi siyo *products* za Tanzania. Ifike mahali tuwe na utashi wa kisiasa na tuanzia humu Bungeni. Hebu tuondoeni haya matai tai na masuti ambayo ni ya kuagiza tuvaeni nguo za kwetu... (*Makofi*)

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Nilikuwa nimemwita Mheshimiwa Ally Salim kwamba atachangia dakika saba atafuatiwa na Mheshimiwa Salim Turkey, Mheshimiwa Josephine Genzabuke ajiandae.

MHE. ALI SALIM KHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa

kutujaalia siku hi ya leo kuwa na afya njema na kusaidia kutoa michango yetu kwa ajili ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ulio wazi kwamba suala la biashara limeingia katika matatizo makubwa na mimi nina mambo kama matatu tu hivi ambayo nitayazungumzia leo. La kwanza; kuonesha kwamba biashara ina utata ni kwamba nchi imetengeneza dheria hata bidhaa zake zinazotoka ndani ya nchi nazo zinalipiwa ushuru kama bidhaa ambazo zinatoka nchi za nje, kwa kweli hili ni jambo la ajabu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kule Zanzibar tuna Kiwanda cha Maziwa kikubwa tu ambacho kinazalisha maziwa ya kutosha, lakini leo maziwa yale yakitoka Zanzibar kuja bara yanatakiwa yalipe ushuru kama maziwa ambayo yametoka nchi za nje, hili ni jambo la aibu sana na la ajabu sana. Kibaya zaidi, *TRA* inaonekana kwamba kuna jambo maalum hapa linaendelea kuhusu Zanzibar kwa sababu baada ya Wazanzibari kulalamikia huu ushuru, *TRA* imempa fursa mwekezaji Said Salim Bakhresa kumwondolea *VAT* ya asilimia 87 ili kiwanda kile kihame kutoka Zanzibar na kije kijengwe bara ili aweze kufanya biashara zake. Hili kwa kweli ni jambo la aibu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atuambie shida hapa hasa ni nini. Maana yake ikiwa leo anajiwekea vikwazo yeye mwenyewe ndani ya nchi, atashindanaje na Rwanda, Kenya na Burundi, atashindana nao vipi, ikiwa ndani ya nchi yake mwenyewe amejiwekea vikwazo yaani biashara zisiende, hawa walioko nje ya nchi hii anashindana nao vipi? Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri akija hapa atuambie kuhusu jambo hili linakaakaaje na matatizo haya yanaondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, Mheshimiwa Waziri ni shahidi; mimi na Mheshimiwa Waziri Kakunda tulikwenda kwenye semina moja na semina hiyo inahusiana na masuala ya wajasiriamali pamoja na wafanyabiashara. Mwenyewe alikiri katika semina ile kwamba wafanyabiashara

kwa mfano walioko mpakani baina ya Tanzania na Uganda wamehama wale wenye biashara zao kutoka Tanzania wote wamehamia Uganda, kwa sababu Uganda akishakata leseni yake ya kufanyia biashara hana bughudha nyingine anafanya biashara zake kwa utulivu, bila shida yoyote. Sasa leo ikiwa imefika mahali Watanzania wanaacha nchi yao wanakwenda kufanya biashara sehemu nyingine kutokana tu na vikwazo vya biashara ndani ya nchi hii, kwa kweli hili ni jambo la kusikitisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano mmoja; leo ukitaka kwenda kuwekeza *UAE*, *UAE* sharti lao kubwa ambalo wanalo lazima upate raia wa ile nchi akudhamini ndiyo uweze kufungua kampuni au kuanzisha biashara. Ukishafanya hivyo, basi wewe *process* zake hata wiki haifiki, umesajili ampuni yako, unafanya biashara zako na inakupa *citizenship* ya watu watatu ambao umetokanao ulikotoka ili wasimamie shughuli zako kufanya kazi zao katika nchi ya *UAE*. Leo ndani ya nchi yetu hii tumeporomoka mpaka tumefika watu wa 147 katika nchi 190. Hivi sasa Mheshimiwa Waziri nimwambie tu kwamba sasa hivi baadhi ya wawekezaji wanaangalia fursa kufanya biashara zao ama uwekezaji wao katika nchi ya Burundi, nchi ambayo inaonekana kwamba haiko tulivu katika masuala ya kisiasa, leo wawekezaji wanafikiria wakawekeze huko Burundi kulikoni kuja kuwekeza Tanzania hapa! Kwa kweli hili ni jambo la aibu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri akija hapa atuambie shida hasa ni nini? Tumsaidie kitu gani ili haya matatizo yatatuke?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, kule Kilwa Masoko waliambiwa wananchi wa kule kwamba watayarisheneo ili waweze kujenga Kiwanda cha Mbolea. Eneo tayari limetayarishwa lakini mpaka leo hii hakuna jambo lolote ambalo limefanyika na watu wameondolewa katika maeneo yao kusubiri ili kiwanda cha mbolea kijengwe ili kuimarisha uchumi huo wa viwanda kupitia wakulima wetu ambao wanalima kule katika eneo la Kusini, sasa shida ni nini? Mheshimiwa Waziri akija hapa atuambie tatizo ni nini hasa ambalo mpaka leo linakwaza mambo haya? Kila kona ya nchi hii kuna shida ya suala la biashara na viwanda. Hebu

akija hapa Mheshimiwa Waziri atuambie jambo ambalo linamkwaza ambalo mpaka hivi leo linamfanya asifanye kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, kwa nini Mheshimiwa Waziri mpaka toka alipoteuliwa kuwa Waziri hajawaita wafanyabiashara akakaa nao akawasikiliza, shida iko wapi ili akaona kwamba ni taasisi gani ambayo inakwamisha au kuna ugumu mahali gani halafu tukatafuta njia ya kutokea hapa, lakini leo anakuja analeta bajeti hii ili ikishapitishwa hapa ndiyo imetoka matatizo ya nchi yanabaki kama yalivyo. Sasa Mheshimiwa Waziri akija hapa naomba atupatie ufumbuzi wa masuala haya ili Bunge lione ni namna gani bora kusadia nchi hii iweze kutoka katika masuala haya yenye mkwamo huu wa biashara pamoja na viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli sasa hivi ukija kwenye suala la biashara, hii dhana ya biashara kule Zanzibar yaani kama kuna njama za makusudi hivi kuiua biashara Zanzibar isifanyike. Sasa tunaomba Mheshimiwa Waziri ndiyo maana hapa kunaingia masuala mengi ya kuona kuna matatizo gani katika masuala ya Muungano ili yaweze kutatuliwa haya biashara zifanyike kwa uhuru...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

MHE. ALI SALIM KHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeshamwita Mheshimiwa Salim Turkey, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Yosepher Komba ajiandae.

MHE. SALIM HASSAN ABDULLAH TURKY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Napenda

niendelee kuwapongeza Waumini wote wa Kiislam kwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, Ramadhani zao ziwe njema tufunge kwa raha mustarehe na wale wanaotusindikiza tushirikiane vizuri zaidi.

MHE. SALIM HASSAN ABDULLAH TURKY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Napenda niendeleo kuwapongeza waumini wote wa Kiislam kwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, Ramadhani zao ziwe njema, tufunge kwa raha mustarehe na wale wanaotusindikiza, tushirikiane vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuchangia, nataka ni-*declare interest* mimi ni mfanyabishara mwenye viwanda. Napenda ku-*declare interest* kwa sababu hata kule Jimboni kwangu nilipogombania watu walinipa kura nyingi sana kwa sababu waliamini ni mfanyabiashara na mwenye viwanda. Kwa hivyo, leo nikisimama hapa naomba sana watu wasinitafsiri kwamba natetea viwanda vyangu, natetea viwanda vya Tanzania kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme katika kukubali kauli ya Mheshimiwa Rais wetu, kampuni zetu sisi tumewekeza baada ya kuona Mheshimiwa Rais yupo tayari kupokea viwanda. Hivi sasa tumejenga kiwanda kikubwa sana *East Africa* nzima kiwanda cha kukoboa mpunga ambacho kiko Morogoro, kinakoboa tani 280 kwa siku na watu wa Morogoro wapo watakuwa mashahidi na baada ya miaka miwili kiwanda hicho kitakuwa kinakoboa tani 560. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hilo halitoshi, Mheshimiwa Rais alikuwa anatuhimiza sana kiwanda cha dripu, nacho kiko tayari tukijaliwa mwezi Oktoba tutamwalika rasmi aje akifungue. Kama hilo halitoshi, hapa Dodoma tunawekeza kiwanda kikubwa kabisa cha *sunflower* kwa Afrika hii na tumepata hekari 90 Zuzu, tunategemea mwanzo wa mwaka ujenzi utanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baada ya kumuamini Mheshimiwa Rais katika viwanda tunapata changamoto kubwa sana ambapo tunaamini kwamba kuna watu wanadumaza maendeleo ya viwanda vyetu. Kuna mfano halisi, sasa hivi kuna mafuta yako bandarini ya kampuni karibu tatu au nne ikiwemo na ya Burundi, mafuta haya yalipofika nchini na kawaida ya nchi yetu mafuta yakifika bandarini yanakaguliwa na *TBS*, *TBS* walipoyakagua walisema mafuta haya ni *crude*, tena mabaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara wale walipopeleka *documents* zao *TRA*, la kushangaza sana Kamishna anazungumza pale kwamba mafuta haya ni mabaya tunayataifisha. Neno taifisha sasa hivi katika juhudi za Mheshimiwa Rais wetu jamani linatoka wapi, litatutisha wafanyabiashara. Ikiwa mfanyabiashara mwenye kiwanda mafuta yake yanataifishwa Wamachinga mitaani wanaopiga kelele wana hali gani? Wanapopiga kelele kwamba *TRA* wanawasumbua, hili lina ukweli wake. Kwa hiyo, naomba Wizara husika waangalie suala hili wanali-*control* vipi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mafuta haya baada ya yeye kuyakataa yasitoke *association* ya wenye viwanda wakapeleka maombi Ofisi ya Waziri Mkuu, Waziri Mkuu kwa utaratibu wao wenyewe wakapeleka mafuta haya yakachunguzwe na Mkemia Mkuu. Mkemia Mkuu amesema mafuta haya ni *crude*. Sasa wametoka watu wameenda tena *TRA*, Kamishna anasema mafuta haya siyo *crude* ni *semi-finished*. Yale mafuta ambayo yalikuwa yanasemwa hayafai kuliwa na binadamu, watakufa, hayawezi yakaingia nchini, sasa anasema ni mazuri yaliwe na watu hawa, hapo ndipo tulipofika sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumkamata hapo akadai sasa vifaa ambavyo anataka uwe navyo mafuta yakingia nchini. Anakudai wewe *export originally document* na *documents* zote *originally* zinatokea nchi ile. Sisi wanunuzi hata wasafirishaji wa korosho wa nchi hii, unapotengeneza *export certificate* hiyo ni mali ya *exporter*

siyo ya *importer*, sisi tunazoletewa ni *copy*. Hiyo sheria alianza mwaka jana *copy* zilikuwa zinakubaliwa lakini kwa mzigo huu sasa anakwambia lete *original*, tunazitoa wapi huu mwezi wa saba?

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaambieni hili jambo sisi wenye viwanda vya mafuta bahati nzuri asilimia 90 ni Watanzania wazalendo, tunatokaje hapa? Hizi *documents* anazozidai kwa kweli hatuwezi tukazipata hata siku moja kwa sababu ni mali yao na sisi hapa tayari tumeshaleta *copy certified* ambazo ndizo zilikuwa zikitolea mzigo miaka yote hiyo, leo unaambiwa ulete *originally* tunatoa wapi *originally*? Kwa hiyo, mkae mkijua hili jambo linadumaza maendeleo ya viwanda vyetu. Leo viwanda vitano vya *refinery* vimefungwa, watu 280 wamekosa ajira kwa sababu ...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Turkey, kengele imeshagonga, ahsante sana.

MHE. SALIM HASSAN ABDULLAH TURKY: Mheshimiwa Naibu Spika, dakika 10 madam.

NAIBU SPIKA: Hakuna Mbunge wa CCM yeyote anayepewa dakika 10, kwa sababu humu ndani CCM ndio wengi kwa idadi kwa hiyo na wachangiaji ni wengi vilevile.

MHE. SALIM HASSAN ABDULLAH TURKY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Josephine Genzabuke atafuatiwa na Mheshimiwa Yosepher Komba, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika ajiandae.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba niunge mkono hoja. Nawapongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Naibu wake, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuhamasisha viwanda. Viwanda ni ajira, kwa sababu viwanda vikifanya kazi vitatumia malighafi inayotokana na wakulima kwa maana hiyo wanawake, vijana wataweza kupata kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili viwanda viweze kufanya kazi ni lazima malighafi nyingine itokane na kilimo. Kwa maana hiyo basi, nashauri kwa sababu viwanda vinahitaji malighafi kutoka katika sekta mbalimbali kwenye kilimo, uvuvi na mifugo, ni vizuri Serikali ikaweza kushirikiana ili sekta ya viwanda pamoja na kilimo vyote vikaenda kwa pamoja. Mfano, ili viwanda vya nguo viweze kufanya kazi ni lazima pamba ipatikane, wakulima waweze kulima pamba na pamba iweze kupelekwa viwandani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwenye viwanda vya viatu tunapata mabegi, viatu, kwa hiyo, ngozi itatokana na wagufaji wa ng'ombe na kadhalika. Pia kwenye uvuvi tunapata viwanda vya samaki, kwa mfano, vile viwanda vilivyoko Mwanza vinatokana na uvuvi. Kwa maana hiyo, viwanda pamoja na sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi ni vitu ambavyo vinatakiwa viende sambamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, katika viwanda vya mafuta ni lazima tuwekeze kwenye kilimo cha mchikichi, alizeti na kadhalika. Katika ujenzi wa viwanda ni muhimu sekta ya kilimo nchini ikazingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanikisha mambo haya yote tukiwahasisha wananchi wakaweza kulima kilimo cha mchikichi na Serikali ikawasaidia wananchi kuwapelekea pembejeo na miche naamini tutaweza kufanya vizuri katika zao hili na viwanda vya mafuta vitaweza kufanya kazi kutokana na malighafi tunayoizalisha sisi

wenyewe kupitia kwa wakulima wetu. Kwa mfano, katika Mkoa wa Kigoma, naomba Serikali iwasaidie wananchi wa Kigoma kupata miche ya michikichi na pembejeo ili waweze kulima kilimo chenye tija katika zao la mchikichi na baadaye tuweze kupata viwanda vinavyoweza kutengeneza mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo yote niendeleo kuomba Serikali iweze kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje kwenda kuwekeza viwanda Kigoma ili wananchi wakilima watapata sehemu ya kuuzia lakini pia ajira zitaweza kuongezeka. Naomba Serikali iweze kuongeza bajeti ya Wizara ya Biashara na Wizara ya Kilimo kufikia malengo tuliyojiwekea ya ujenzi wa viwanda. Bajeti ya Wizara ya Viwanda kwa kweli ni ndogo.

Kwa hiyo, naomba Wizara ya Viwanda na Biashara iweze kuongezewa bajeti ili iweze kufanya vizuri katika dhana ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna moja nililotaka kulizungumzia kuhusu *OSHA*. Naomba Serikali iandae mpango wa *blue print* ili tuweze kufanya vizuri katika nyanza hii kwa sababu malalamiko yamekuwa ni mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu *SDL* wanayokatwa wafanyabiashara na wenye viwanda yote inapelekwa kwenye ujuzi. Naomba kiasi hiki kinachokatwa kiweze kurudishwa kipelekwe Wizara ya Viwanda na Biashara kwenda kuwasaidia watu wa *SIDO* na *TIRDO* ili kuongeza uwezo katika taasisi hizi. Kwa maana hiyo, naomba kabisa hayo yote niliyoyasema yaweze kuzingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa naomba...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Yosepher Komba dakika tano, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika na atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Michael Mmasi.

MHE. YOSEPHER F. KOMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Kwa sababu dakika ni tano nianze kwa kusema, suala la korosho tunamuomba Mheshimiwa Waziri alichukulie *serious*. Kama ambavyo Kambi ya Upinzani imeshauri wale wote ambao wamehusika, tumeona manyanyaso makubwa waliyoyapata watu wanaoitwa kangomba ambao walikuwa tayari kuwasaidia wakulima wetu lakini kumbe Serikali hii iko tayari kumkumbatia kangomba wa Kenya kuliko kangomba wa Tanzania. Kwa hiyo, naomba wale wote ambao wanahusika wawajibike, Waziri wa Sheria, Fedha na Viwanda na Biashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia kitabu cha Mheshimiwa Waziri, nimeangalia kwenye suala la makusanyo ya Mafungu 44 na 60 na nimeangalia miradi ya maendeleo. Kwenye makusanyo mwaka 2018/2019 mlikuwa mmeweka makadirio ya shilingi milioni 20 *point* lakini 2019/2020 kwa maana ya mwaka huu ambao mnauanza mmeweka makadirio ya shilingi milioni tano. Sasa sielewi Wizara ambayo ndiyo kauli mbiu ya nchi, Serikali ya Viwanda, mmetoka kukusanya shilingi milioni 20 mmepeanga kukusanya shilingi milioni tano. Nitaomba maelezo Mheshimiwa Waziri kwamba sasa mmeshaacha kufanya shughuli za kutengeneza miundombinu ya biashara na uwekezaji? Kwa nini makusanyo mmeshuka kwa kiasi hiki? Mnataka kupewa fedha nyingi lakini nyie hamko tayari kukusanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kwenye miradi ya maendeleo, fedha za ndani zilikuwa shilingi bilioni 100 kwa mwaka wa fedha huu tunaoumaliza. Hata hivyo, kwenye Fungu 44 kati ya shilingi bilioni 90 mmepelekewa shilingi bilioni 6.47 sawa na asilimia 6.5 kutoka Serikalini. Kwenye Fungu 60 kati ya shilingi bilioni 7 ambazo militakiwa mpewe Hazina mpaka leo haijatoa hata shilingi, hiyo ndiyo Serikali ya Viwanda mnayoihubiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakati unaweza ukasema hii Wizara haipo labda kwa matendo yake, hakuna mchango wowote kwenye nchi hii kwenye Wizara hii unaoonekana kwa macho. Mmekuwa watu wa kupiga kelele na propaganda, sijui ukiwa na brenda tatu una kiwanda, ukiwa na cherehani ni kiwanda, lakini kwenye uhalisia hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natoka Mkoa wa Tanga ambao ulikuwa na viwanda vingi sana miaka ya 80 na 90. Naomba nikutajie baadhi ya viwanda ambavyo Mheshimiwa Waziri utakuja kuniambia hapa vilikuwa vya Serikali mmeshindwa kuvifufua, hamjabinafsisha, vimekufa. Mje mniambie hapa tangu Serikali ya Awamu ya Tano imengia katika viwanda hivi ni vingapi vinafanya kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na Kiwanda cha Mbolea (*Tanzania Fertilizer Company*), Kiwanda cha Nondo (*Steel Rolling Mills*), Kiwanda cha Blanketi, Kiwanda cha Amboni Plastiki, Karakana ya *Railway*, *Sao Mill*, Kiwanda cha Foma (*detergent*), Kiwanda cha *Cheap board* pale Mkumbara, Kiwanda cha Ngano, pembe imekufa na tulikuwa tunazalisha mpira Muheza. Naomba Mheshimiwa Waziri ukija hapa utuambie kwa Mkoa wetu wa Tanga ni viwanda vingapi vimefufuliwa tangu Awamu ya Tano imeingia madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina suala la Wilaya yangu ya Muheza ninakotoka. Tulikuwa tunalia usiku na mchana na Mheshimiwa Mwijage ni shahidi nilikuwa namuambia kila siku napokutana naye, wakulima wakubwa wa machungwa na matunda nchi hii wanatoka Mkoa wa Tanga, labda na Iringa na mikoa mingine. Tunalima sana machungwa lakini sasa hivi wakulima wa Tanga na Muheza machungwa yamekuwa ni sehemu ya mbolea ya mashamba yao, machungwa hayana bei. Kipindi cha Awamu ya Nne chungwa lilikuwa linauzwa shilingi 100 mpaka shilingi 200 kwa mkulima anachuma anauza kwa bei hiyo, sasa hivi ni shilingi 15 mpaka shilingi 25, Serikali ya Viwanda hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wanapata shida, wanafanya mengi. Nimeomba Kiwanda cha Machungwa Wilayani Muheza, tunapata shida, machungwa yanaoza na yanatupwa. Mheshimiwa Waziri uje uniambie hapa ni lini ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Michael Mmasi, Mheshimiwa Lucy Mayenga ajiandae.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii. Pia nawatakia kheri Waislamu wote wanaofunga Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitakwenda kwenye viwanda, kweli Serikali ya Awamu ya Tano imejenga viwanda vingi lakini viwanda hivi kama havikuangaliwa vizuri basi vitakufa haraka sana. Ni lazima viwe na watu wenye ujuzi wa kuviendesha viwanda hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wawe na viwanda vya malighafi kwa sababu malighafi nyingi inaagiziwa kutoka nje ya nchi na kuleta hasara kwa Taifa. Kwa hivyo, ni lazima viwanda vijengwe hapa ili kupunguza gharama na kuipatia mapato Serikali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Mwenyezi Mungu katika nchi yetu ametujalia utajiri mkubwa yakiwemo maziwa na bahari. Katika nchi yetu tunazungukwa na bahari katika ukanda wa Pwani wa Dar es Salaam, Tanga, Lindi, Zanzibar, Pemba na sehemu nyingine lakini hakuna viwanda vya kuchakata samaki, tunakosesha Tanzania kupata mapato. Kwa hivyo, Serikali ijipange kujenga viwanda vya minofu ya samaki. Tunawaachia Wachina wanakuja na meli zao,

wanavua samaki wanaondoka nao sisi tupo tunaangalia. Kwa hivyo, Serikali ijipange kujenga viwanda hivyo hata Zanzibar na Pemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaambiwa kuwa Zanzibar siyo nchi, Tanzania ni Taifa moja lakini kinachosikitisha bidhaa zinazotoka Zanzibar kuja Tanzania Bara hawapewi vibali. Tuna sukari, maji ya *drip* na maziwa lakini haviruhusiwi kuingia Tanzania Bara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kushangaza Tanzania Bara inaleta vitu Zanzibar mfano bia, sigara, soda na vitu vinginevyo, kwa nini na wakati ni nchi moja? Kwa nini na sisi hatufaidiki? Nchi moja itakuwa tukiwa Zanzibar lakini tukiwa Bara ni nchi mbili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, mfano wa magari. Gari linapotoka Tanzania Bara tunalipa ushuru, lakini linapoingia Zanzibar unalipa tena ushuru mara mbili. Ni kwa nini ilipe ushuru mara mbili? Hili ni tatizo.

MBUNGE FULANI: Na ni nchi moja.

MHE. MGENI JADI KADIKA: ...na ni nchi moja. Kwa nini tufanye hivyo? Kuna nini? Naomba basi, kama ni nchi moja, basi isiwe tunalipishana ushuru mara mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu wafanyabiashara. Kwa kweli, Wafanyabiashara tunawarudisha nyuma au Serikali inawarudisha nyuma kwa sababu kodi inayotozwa ni kubwa mno. Mfanyabiashara anapewa mahesabu anaambiwa miaka mitatu hujalipa; sijui hivi, kuna hili, kuna hili, inapigwa thamani ya kupewa mfanyabiashara wakati ile biashara yake aliyonayo kwenye duka haitoshi. Ile biashara yake yote ikipigiwa thamani haitoshi, tunampeleka wapi mfanyabiashara huyu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana wafanyabisahara wengi wamefunga maduka yao, wafanyabiashara wengi wanarudisha leseni. Je, tunakwenda

wapi? Tunakwenda wapi? Serikali hii hatuko masikini, tuna utajiri wa kutosha, kwa nini tuwabane wafanyabiashara wao tu? (*Makofi*)

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa, kengele imeshagonga. Mheshimiwa Ester Michael Mmasi, atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Mahmoud Mjimwa ajjandae.

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia kwa dakika hizi chache ambazo umenipatia. Nina heshima ya pekee kabisa na ninasimama kwa unyenyekevu mkubwa nikiwapongeza Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii husika, lakini pia na kwa taarifa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitapenda kukita mchango wangu kwenye vipengele viwili. Kama ambavyo imewasilishwa, kuongelewa na kujadiliwa na Wabunge wengi hapa ndani suala la Liganga na Mchuchuma, nami nitapenda nijielekeze huko kwa maslahi mapana ya ajira kwa vijana wetu wa Kitanzania. Pia nataka kuongelea ushiriki wa vijana mathalan *graduates* wa nchi hii katika muktadha mzima wa masuala ya biashara na ujenzi wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nimesimama nimeshika kitabu kilichoandikwa na Wizara ambayo wamewasilisha hapo mbele. Nitapenda nirejee ukurasa wa 15. Ninaongea haya kwa masikitiko makubwa na sijui; ninaongea kwa sababu kaka yangu Mheshimiwa Kakunda wewe ni Mheshimiwa Waziri ambaye ni mmoja wa wajumbe ambao nimekuwa nikizunguka na ninyi kwenye programu zangu za vijana. Kwa hiyo, unafahamu fika maneno waliyokuwa wanakwambia vijana wale. Nimezunguka na wewe miko mingi tu na umeniahidi tutazunguka miko mingi ukasikilize changamoto za wanafunzi wa Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana mama yangu, Mheshimiwa Ndalichako ambaye ni mlezi wa wazo langu hili pamoja na kaka yangu Mheshimiwa Olenasha, nawashukuruni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ninaongea ikiwa hii ni sauti ya wanafunzi wa Vyuo Vikuu. Nikiangalia ukurasa wa 15 pale *Section No. 29*, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa ninaomba Mheshimiwa Waziri ikibidi ondoa huu utata hapa. Naongea hivi nikiwaomba hata wasaidizi wenu wanisikilize na waamini kwamba Wabunge tunasoma. Waamini hata taarifa zilizotolewa na Mheshimiwa Spika kwamba, hili ni moja ya Bunge mahiri ambalo vijana na Wabunge wote tunajituma katika kusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitapenda urejee hapa, nawe ni Mwanasheria, utanisaidia na utaniongoza pamoja na Kiti chako hapo mbele. Hapa tunaambiwa moja ya changamoto iliyosababisha mkwamo wa *project* hii ya Liganga na Mchuchuma ni pamoja na pale ambapo mwekezaji yule alitokea kudai *additional incentives*, yaani vivutio vya ziada. Hii ilisababisha kukwama kwa mradi huu kwa maana ya kwamba, baada ya kupitishwa na Bunge lako hili Tukufu sheria zile mbili za kulinda na kuhifadhi maliasili ya nchi hii (*Natural Wealth Resources Permanent Sovereign Act* na *Natural Wealth Resources Renegotiation of Unconscionable Terms 2017*) ndiyo ilisababisha kukwama kwa mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasikitika kusema huu ni uwongo mkubwa na sijui kwa nini tunaandikiana vitu kama hivi, kwa sababu moja. Hapa wanasema, kwenye *section 29* kwamba, wakati majadiliano yanaendelea kuhusu vivutio hivyo vya ziada, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya kupitisha sheria hizi mbili na ili kukidhi matakwa ya lbara ya 27 ya Azimio la Umoja wa Mataifa ya sheria hizi mbili, mikataba yote ya nyuma ya aina hiyo, yaani ya Liganga na Mchuchuma pamoja na Liganga, yaani zile sheria mbili za kulinda na kuhifadhi maliasili ya nchi hii zilisababisha kuwa ni

sharti la kimkataba kwamba Mradi wa Liganga na Mchuchuma ukapitiwe vipengele vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe masharti ya sheria zote hizi mbili ni pale ambapo tunaona mikataba hii ilikuwa na masharti hasi. Haikuwahi kuandikwa mahali popote kwamba baada ya kupitisha sheria zile, basi Liganga na Mchuchuma ilitakiwa lende ikapitiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutapitia Liganga na Mchuchuma kama pale ambapo tumeona kulikuwa na masharti hasi. Pengine upande wa Wizara unafahamu masharti hayo hasi yako wapi, lakini hii sidhani kama ni kweli. Nasema hivi kwa sababu, wanasema pia ati mchakato wa kupitia upya mkataba huo unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimrudishe Mheshimiwa Waziri na nirejee haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sheria zile ikumbukwe tunaambiwa katika *Part Two*, Ibara ya 4(1) inasema, *“For effective performance of the oversight and advisory functions stipulated under article 63(2) of the Constitution, The National Assembly may review any arrangement or agreement made by the Government relating to natural resources.”*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye *Article 5*, ukienda kwenye *section 5* ya Sheria ile ya *Renegotiation for Unconscionable Terms* inasema, *“Where the National Assembly consider that certain terms of arrangements and/or agreement of the natural wealth and resources of the entirely arrangement or agreement of natural resources made before the coming into force of this Act and for the interest of the people of The United Rublic of Tanzania, the reason of Unconscionable terms it may by resolution advise the Government to initiate renegotiation.”*

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani inamaanisha hivi, pale ambapo itabainika kuna masharti hasi, ni Bunge hili litapeleka, litapitisha azimio (*resolution*). Likishapitisha azimio

Wizara husika ndani ya siku 30 itaenda kwa mwekezaji na kumpa matakwa ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema huu ni uwongo kwa sababu hakuna azimio lolote lililowahi kupitishwa na Bunge lako hili Tukufu kupitia Mkataba wa Liganga na Mchuchuma, hakuna mahali popote. Tunachukia sana, nami binafsi sipendi kuandikiwa taarifa ambayo nikiisoma ninaona huu ni upotoshaji. *(Makofi)*

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninadiriki kusema kwamba ninafikiri Wizara ijipange kutuambia pale kuna kufidia. Kuna fidio lile ambalo mlifanya tathmini mwaka 2017, pengine hizi ndiyo tuziite masharti hasi. Siamini kwamba eti sheria hizi mbili zimesababisha kwamba Liganga na Mchuchuma isimame kwa sababu tu sheria hii ina matakwa hayo ya kisheria. Bunge hili halijawahi kupitisha azimio mahali popote. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ester Michael Mmasi. Kengele ilishagonga, nilikupa muda ili umalize hoja yako. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Lucy Mayenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa na Mheshimiwa Daimu Mpakate, ajiandae.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii angalau nami niweze kuchangia kwenye Wizara hii, ingawa bahati mbaya dakika hizi tano ni chache sana, lakini sina budi kutumia muda huo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisimama hapa mara ya mwisho wakati nikizungumza kwenye Wizara hii ya Viwanda

na Biashara nikatoa wazo kwamba Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla iweze kuihamisha *TIC* kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara na kuihamishia aidha kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu au Ofisi ya Rais. Ninaomba kwa heshima na taadhima nithibitische kwamba, Mheshimiwa Rais ni msikivu, ninafahamu kwamba vyombo vyake vimesikia na wamepima wameona kwamba, wazo hilo lilikuwa ni zuri. Ninajua kwamba vyombo vyake vitakuwa vilishafanyia kazi kabla hata sijazungumza na ndiyo maana *TIC* imehamishwa. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo *TIC* imehamishwa, bado Wizara inatakiwa sasa ifanye haraka na kwa mkakati maalum kuweza kuleta Sheria ya *TIC* mpya hapa Bungeni. Sheria Namba 26 ya Mwaka 1997 imepitwa na wakati. Yaani miaka imekuwa ni mingi mno kiasi kwamba mabadiliko yanayoendelea sasa hivi duniani hayaendani na hii sheria. Hata hivyo, sheria hiyo ikiwepo itasaidia kurekebisha vitu vingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vitu vingi ambavyo vimezungumzwa na Wabunge kwenye Bunge hili kwamba kuna masuala ya tozo, masuala sijui ya taasisi mbalimbali ambazo zinashughulikia biashara pamoja na uwekezaji. Sheria hii endapo kama ikiletwa, itaweza kurekebisha mambo haya; mambo ya *OSHA* watu wanalalamika, mambo ya sijui *NEMC* na kadhalika, kwa hiyo, mambo mengi yataweza kurekebishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile uratibu wa masuala mazima ya uwekezaji angalau yataweza kufanywa na chombo kimoja, maana sasa hivi ni vile kila mtu mkubwa. Kila taasisi inajiona kwamba kubwa. Kila mtu, leo anakuja anasimama anasema hivi, mwingine kesho anakuja anasimama anasema hivi. Kwa hiyo, sheria hii ikiletwa, itaweza kusaidia ili mambo yakae sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile mara ya mwisho nilizungumzia kuhusu habari ya vibali vya kazi pamoja na ukaazi. Mheshimiwa Waziri, yapo masuala mengine

hayatakiwi labda mpaka mtu mkae mtafute mwezi mzima muweze kuyafanyia kazi. Hili suala la vibali vya kazi halijakaa sawa sawa katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani sheria hiyo hiyo ya mwaka 1997 inasema kwamba, mwekezaji akija, kwenye sheria imeandikwa kwamba anaruhusiwa kupewa watu watano. Kwa hiyo, huku sheria inasema aruhusiwe kupewa watu watano, lakini akishafika wale watu watano hapewi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala tunaonekana hatuwezi kuaminika. Huu ni uwekezaji, lazima ifike wakati tuone kwamba sisi kama nchi ndiyo tuna shida na wawekezaji na siyo kwamba wawekezaji wana shida na sisi. Tukiwa na mtazamo wa kusema kwamba wawekezaji wana shida na sisi, hatuwezi kufika. Nami nilikuwa naomba Wizara ya Uwekezaji, Wizara ya Viwanda na Biashara inabidi mkimbie maana sasa hivi naona bado mnatembea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nizungumzie kuhusu suala zima la wafanyabiashara. Baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa wakisimama hapa wanazungumzia kwa mfano, kuna hoja ambayo inasemwa na wafanyabiashara sitaki kusema ni wapi; kwamba, kuna mafuta yamekamatwa, yamewekwa huko, meli zimekaa miezi saba. Kama unaulizwa *document*, *TRA* kosa lake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, tusije tukaja tukakaa mara nyingi tukawa tunaweka mzungo mkubwa sana kwa *TRA*. Hakuna mfanyabiashara na wala hakuna mkusanya kodi ambaye anapendwa, lazima na sisi tuweze kujiangalia tumekosea wapi? Kama unaambiwa lete kibali *original*, hamna mfanyabiashara ambaye unaleta mzungo unakosa kibali *original*, haipo.

MHE. MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee. La mwisho, naomba kumpongeza sana

sana Mheshimiwa Rais wangu. Naomba kumwambia maneno yafuatayo: Miradi yoyote ile ambayo inaletwa katika nchi yetu kama haina maslahi au haina tija, naomba kusema kwamba waizuie huko huko wala hata isiendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu gani? Tuna imani kubwa, tunaomuunga mkono katika nchi hii na katika Bunge hili tuko wengi. Kwa hiyo, miradi kama inaonekana kwamba ina hitilafu, kwa msimamo aliouonesha Rais wetu; kwanza cha kwanza kabisa hakuna mtu mwenye *information* katika hii nchi kama Rais wetu. Rais ndio mtu wa kwanza mwenye *information* za uhakika kuliko mtu mwingine yeyote. Kwa hiyo, akikaa akasema kwamba suala hili haliko sawa sawa, mjue kwamba haliko sawa sawa. Sasa tukikaa tena hapa mtu akasimama akasema unajua suala hili sijui limekaa hivi, mwisho tutakuja kuvunjiana heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Lucy Mayenga, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Mahmoud Mjimwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Daimu Mpakate, Mheshimiwa Joseph Mhagama ajiandae.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu kwanza nitajielekeza kwa mtindo wa maswali. La kwanza nilitaka kumwuliza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, nini *role* la *NDC* hapa nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wa *NDC* tumewapa majukumu mengi sana, lakini ukiangalia hakuna hata jukumu moja katika yale tuliyowapa mpaka leo lililotekelezwa. Tukianza na suala la Mchuchuma na Liganga,

Mchuchuma na Liganga iko chini ya *NDC*. Mwaka 2012 tulisaini mkataba na Wachina hapa kuendeleza maeneo ya Liganga na Mchuchuma, lakini mpaka leo hakuna jambo lolote lililofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili yanapatikana *material* ya uhakika kwa ajili ya viwanda vyetu kwa maana ya chuma pamoja na makaa ya mawe. Kwenye makaa ya mawe tulikuwa tunaweza kupata umeme wa uhakika ambao tungeweza kupata umeme wa Megawati 50, lakini mpaka leo hakuna jambo lolote linalofanyika. Sasa nataka Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anakuja hapa aje kutuambia sababu zipi zilizosababisha mpaka leo hii mradi ule haujaanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa namwomba ndugu yangu Mheshimiwa Mheshimiwa Rashid angetoka pale amwache Mheshimiwa Waziri atusikilize tunachokisema, kwa sababu atakuwa anamchanganya.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo nilitaka kuchangia ni suala la umeme, kwa maana ya umeme wa upepo. *NDC* walituhakikishia kwamba tungepata umeme wa upepo maeneo ya Makambako na Singida, lakini mpaka leo hatujaona juhudi zozote zilizofanyika katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ni suala la *Arusha General Tyre*. Hiki kimekuwa kilio cha miaka mingi, lakini mpaka leo hakuna chochote tunachoambiwa kuhusu suala la *General Tyre*.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa tunataka atupe majibu ya maeneo haya manne, kwa nini hayafanyiki? Kama hakuna majibu ya kutosha, hatuna sababu ya kuendelea kuwa na *NDC* kwa sababu, tutakuwa tuna watu ambao tunawalipa mishahara, lakini kazi zao hatuzioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo nilitaka kulichangia ni suala la *Kurasini Logistic Centre/Kurasini Logistic*

Hub. Eneo hili ni *sensitive*. Serikali ya Tanzania tumelipa shilingi bilioni 90 kwa ajili watu waondoke kwenye maeneo yale, lakini huu ni mwaka wa saba hakuna jambo lolote la maana lililofanyika pale. Ule ni mradi mkubwa ambao ulikuwa unagombewa na nchi zaidi ya kumi, lakini kwa namna ya kipekee Wachina walitufanyia upendeleo kutupa ule mradi, lakini hakuna jambo lolote la maana linalofanyika katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kusikitisha kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri, hakuna hata sehemu moja ambayo amezungumzia *Kurasini Logistic Centre*. Kwa hiyo, nataka atuambie kwamba zile shilingi bilioni 90 zimepotea au zimekwenda wapi? Kama ingekuwa hatuzihitaji kuzitumia kwenye maeneo haya, bora tungezipeleka kwenye maeneo mengine. Mheshimiwa Waziri kanyamaza kimya, kitabu kizima hakuna hata sehemu imezungumzia habari ya *Kurasini Logistic Centre*. Kwa hiyo, shilingi bilioni 90 zinapotea bila utaratibu wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine nataka kuzungumzia ni utekelezaji wa Mradi wa *Bagamoyo SEZ*. Pale napo tumelipa zaidi ya shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kuwalipa watu fidia. Sasa kwa utaratibu ambao siyo wa kawaida, hela zitakuwa zinapotea kwa utaratibu huu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atuambie, sababu zipo zinasababisha hii miradi mikubwa ambayo ingeweza kuinua uchumi mkubwa wa nchi hii inapotea bila utaratibu?

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwisho nililotaka kuchangia ni suala la viwanda vinvavyobinafsishwa. Ifike wakati sasa, *Dar es Salaam Stock Exchange* ivisajili viwanda vyote vinvavyobinafsishwa. Hii itasaidia ku-*control tax evasion*. Kwa hiyo, huyu *regulator (CMSE)* ni vyema akaleta sheria hapa Bungeni kwamba viwanda vyote vilivyobinafsishwa visajiliwe kusudi tuweze kuvi-*control* kwenye soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Daimu Mpakate, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mhagama na Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene ajiandae.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuchangia mchana huu. Kwanza kabia naomba niweke *record* sawa. Naona kuna baadhi ya wenzetu hawaelewi hii *certificate of original* inatolewaje? Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, *cerifcate of original* anapewa *exporter*. Akishapewa *exporter*, yeye anaweza akawa anapeleka sehemu tatu tofauti. Kwa hiyo, sehemu zinazokwenda, zinaenda nakala, *certificate of original* anabakinayo *exporter*. Kwa hiyo, ninaungana mkono na wenzangu waliotangulia, hasa Mheshimiwa Turkey kwamba, siyo sahihi *TRA* kudai *certificate of original* kwa sababu *certificate of original* ni mali ya *exporter*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo nilikuwa napenda nichangie sehemu mbili ambazo nilikuwa nimejipanga nichangie. Suala la kwanza ni suala la wakala wa vipimo. Wote tunajua tatizo la vipimo lilivyo. Kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba anategemea kuajiri watu 153. Katika kero ambayo inaendelea katika maeneo mengi hasa ya nchi yetu ni suala la vipimo. Vipimo vinatumika kwa wakulima, madukani na kila mahali, hata barabarani magari yanapimwa kwa kutumia vipimo. Vile vipimo vimetengenezwa na vyuma na ofisi za vipimo ziko mikoani tu. Kwa hiyo, wanakagua maeneo mengi hivyo vipimo kwa mwaka mara moja. Kwa hiyo, utakuta mara nyingi wanaotumia vipimo wanakuwa wanawapunja wateja wao kwa ajili ya vipimo ambavyo wanavitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana Wizara mjipange kufungua ofisi kwenye wilaya ili wale watumishi wa vipimo upande wa wilayani waende kukagua mizani ile mara kwa mara. Kwa sasa watu wanaotumia vipimo wanapata tabu sana, wakitaka huduma ya watumishi wa vipimo lazima mtu aende mikoani, hasa watu wa mafuta shida hiyo wanayo, mizani mingi shida hiyo wanayo ndiyo

maana wakulima wengi wanalalamika kwamba wanapunjwa katika vipimo vyao ambavyo wanavitumia wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo napenda nilichangie ni suala la mfumo wa stakabadhi ghalani. Mfumo huu upo kwa mujibu wa sharia, lakini kanuni zimeleta matatizo mengi ambayo yamesababisha watumiaji wa mfumo ule kuwa tofauti. Kwa mfano, sasa hivi limezuka janga, hawa wanaotumia mfumo wa stakabadhi ghalani hasa wakulima na vyama vya ushirika kupunjwa mazao yao yanapopotea kwenye maghala makuu, lakini hatua yoyote inayochukuliwa kutoka kwenye Serikali au kwa mfumo wa stakabadhi ghalani. Kwa hiyo, naomba Sheria ya mfumo wa Stakabadhi Ghalani irekebishwe ili kuhakikisha kwamba inaweza kumlinda mkulima au mtumiaji wa mfumo wa stakabadhi ghalani aweze kupata haki yake ya mapunjo ambayo yanatokana na matumizi ya mfumo wa stakabadhi ghalani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia mfano halisi uliopo kwenye Sekta ya Korosho, sasa hivi korosho zipo maghalani na tunategemea kwenye mazao mengine tutumie mfumo wa stakabadhi ghalani, sehemu ya kuhifadhi yale mazao hakuna. Naomba, nadhani Serikali jambo la kwanza kulitilia maanani lingekuwa ni suala la kuongeza maghala katika maeneo yetu ambayo yanazalisha mazao, bila kuwa na maghala, mfumo wa stakabadhi ghalani hauwezi kufanya kazi kama wanavyosema wenyewe mfumo wa stakabadhi ghalani. Kwa hiyo, naomba sana Serikali kwa ku-*rescue situation* iliyopo sasa kwa upande wa maeneo ya kusini, basi ichukue hatua za haraka ili kuongeza maghala katika maeneo mbalimbali ili korosho au mazao yaweze kuhifadhiwa kama yanavyotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hiyo, kuna *risk* kubwa kwa upande wa ma-*warehouse operator* ambao wanafanya shughuli zile, wanaingiliwa sana na Serikali tofauti na sheria inavyohitaji kuhusu huu mfumo wa stakabadhi ghalani. Sasa hivi wengi ma-*warehouse operator* wanaogopa

kufanya kazi ile kwa sababu muda/wakati wowote wanaweza kuwekwa ndani bila ya utaratibu, jambo ambalo linakatisha tamaa watumiaji wa mfumo wa stakabadhi ghalani. Hii inapoteza haki yao ya msingi ambayo ipo katika mfumo wa stakabadhi ghalani. Naomba sana Serikali iangalie hii sheria, iangalie upungufu wote uliopo kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani urekebishwe ili wadau wa mfumo wa stakabadhi ghalani uweze kupata haki yao kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo nilikuwa napenda nichangie. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel na Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba ajiandae.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba hii. Naomba nianze moja kwa moja kwa sababu ya muda, katika kuzungumzia masuala mawili muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni suala zima la uwezeshwaji au mazingira bora ya uwekezaji pamoja na kufanya biashara. Haya maeneo ni muhimu sana na ndiyo hasa yanabeba uzito mzima wa jinsi ambavyo maendeleo ya biashara au viwanda nchini kwetu yatakwenda. Kwa bahati mbaya sana, Wizara yenyewe inapata bajeti ndogo mno kiasi kwamba hata ile kazi ya kuandaa ule uwezeshwaji inakuwa siyo rahisi kiasi hicho. Tumejionea jinsi ambavyo bajeti iliyopangwa na bajeti iliyotolewa ni ndogo sana katika matumizi ya kawaida na hata ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, kuna suala zima la kuweka mazingira bora ya uwekezaji katika viwanda vyetu. Nataka kukumbusha Serikali kuwa mwaka 2010 *task force* iliundwa ya Wizara nane kwa ajili ya kutengeneza *roadmap* ya kuweka utaratibu ambao utarahisisha uwekezaji na vilevile kufanya biashara. *Task force*

ile ilikuja na mapendekezo mazuri sana na chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kulikuwa kuna uratibu sasa wa jinsi gani ya kutekeleza yale mapendekezo yaliyotokana na ile *roadmap* ya kwanza ambayo ilikuwa inalenga ku-*improve uncompetitiveness* ya uendheshaji wa shughuli zetu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sielewi ile ilifikia wapi kwa sababu mwaka jana tena tulikuja na *blue print* na vyote vinatokana na taarifa zinazotoka nje kuonyesha kuwa sisi *ranking* yetu inazidi kudorora. Sasa hii *blue print* haikuwa tofauti sana na ile *roadmap* ya kwanza lakini pamoja na hayo yote bado hatuoni jinsi gani ambavyo tuna mwelekeo unaotutoa hapa tulipo ambapo bado hatujakuwa na mwelekeo mzuri wa jinsi ya kuanzisha viwanda na kuviimarisha. Tunaona kabisa na ni ukweli usiopingika kuwa biashara zinadorora na nyingine zinafungwa, wawekezaji hawana amani kwa kifupi naweza kusema hivyo, wawekezaji waliopo na wale ambao wanataka kuja bado hawajakuwa na amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu inasemekana ni ya amani na utulivu lakini kiuchumi na kibiashara hakuna huo utulivu wala amani. Nasema hivyo kwa sababu ya jinsi ambavyo shughuli zinaendeshwa; kwanza maamuzi yanachelewa sana kufanyika na hii tunazungumzia tangu vibali vinapoombwa mpaka *proposal* zinapoletwa na wawekezaji wanaotaka kuja kuwekeza mpaka inapofikia kuwa sasa wanaanza kufanya shughuli zao au wanaamua kuondoka. Huu muda ni mrefu mno kwa mtu ambaye anataka kuja kufanya biashara. Tunajua kabisa katika biashara muda mali, hawezi mwekezaji kuja kukaa miezi mitatu hotelini hapa anangojea *decisions* na wakati tumesema tuna *TIC* ambayo ni *one stop center*; hiyo *one stop center* kwa nini ichukue miezi mitatu kuamua jambo la mwekezaji anapokuja nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, kuna mambo madogo madogo mengi ambayo yanaleta tatizo; yamezungumzwa humu ndani masuala ya *permit*, ajira na hata mikopo kwa ajili ya wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie suala ambayo yamejitokeza katika *ranking* ya hivi karibuni ambayo ilipata kwa ajili ya Serikali yetu. tumefanya vibaya sana kwenye masuala ya *cross border trade* ambayo sisi tuna *advantage* kubwa sana; tuna fursa kubwa sana katika biashara ya mipakani kwa sababu tuna mipaka mingi sana Tanzania na wazalishaji wadogo wadogo wengi na hasa wakiwa akinamama ndiyo wenye nafasi kubwa sana ya kufanya hiyo, lakini tumefanya vibaya. Tuna fursa kubwa ya kufanya biashara sisi na nchi nyingi zinazotzunguka pamoja na Afrika ya Kati, lakini tumekwama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna matatizo vilevile ya masuala ya kodi na hii inaletwa na biashara kuwa siyo nzuri sana kwa hiyo hata kodi kukusanya inakuwa vigumu. Tunajikuta tunazunguka katika *vicious circle* ya kutokuwa na mikakati mizuri kwa sababu tu ya jinsi ambavyo tunaendesha hizi shughuli zetu sisi wenyewe. Matatizo yote tuliyanayo ni...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele ilishagonga Mheshimiwa Janeth Mbene, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nilikuwa nimeshamwita Dkt. Godwin Mollel, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba, Mheshimiwa Ashatu Kijaji ajiandae.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutambua na kuelewa vizuri ni namna gani ambavyo tunaweza tukaifikia Tanzania ya viwanda, lakini bila kusahau viongozi wa Wizara.

Hata hivyo, napenda kuwakumbusha kwamba pamoja na kwamba kuna juhudi nzuri sana ambazo Wizara inafanya, lakini Rais anafanya tusipuuze sana malalamiko haya ambayo yanasemwa na Wabunge, lakini kuna mambo

yanayotokea chini kwa watendaji ambayo tunatakiwa kukiri na kujaribu kuyafanyia kazi kama ambavyo Wizara ya Maji imekiri na ipo tayari kufuata chini ili kuweka mambo sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kusema kwamba tunajua kwamba ukisema unatengeneza kiwanda, huna namna ya kuwa na kiwanda wakati bei ya umeme ipo juu. Leo katika Tanzania hii umeme tunanunua *unit* kwa maana ya dola senti 10, lakini Uingereza ni 0.12 ya senti, maana yake huwezi ukajenga kiwanda cha nguo hapa Tanzania kwa umeme wa namna hiyo kwa *standard* ya nguo iliyotengenezwa Uingereza ukauza soko la nje. Kwa maana hiyo, hakuna namna yoyote mtu anaweza akawekeza kwenye kiwanda cha nguo ndani ya Tanzania. Rais wetu amelijua hilo, amewekeza kwenye *Stiegler's Gorge*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, utaona na watu wanasema Wizara hii ni Wizara mtambuka; uwekezaji unaofanyika kwenye Wizara ya Miundombinu, Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu, yote mwisho wa siku unaenda kuonekana kwenye kuboresha hii Sera ya Viwanda na kuboresha kwenye eneo la viwanda. Kwa mfano, ukienda kwenye afya tunaposema tunaboresha afya na kupeleka hela kwenye afya, maana yake tunaenda kuboresha siyo afya tu kwa maana ya watu kutibiwa lakini tunaenda kuwaboresha huduma akinamama na mwisho wa siku watazaliwa watoto wazuri tutafanya lishe, tutaendelea na tutapata watoto wenye akili nzuri kwa sababu kwenye viwanda siyo tu suala linalosaidia viwanda ni kwamba kuleta teknolojia kutoka nje, *innovation* na ugunduzi ni vitu ambavyo vinasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utakuta leo *SIDO* yetu wana-*copy* vitu kutoka nje lakini hawawezi kwenda zaidi ya hiyo ku-*copy* kutoka nje. Rais anapowekeza kwenye eneo la afya maana yake *generation* inayokuja mbele tutaweza pamoja na ku-*copy* lakini na sisi tutaweza kugundua na tutaweza ku-*compete* kwenye soko la uwekezaji na ugunduzi na hasa viwanda sasa vitaanza kuonekana vina tija kwenye Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwenye elimu; leo kwenye elimu tunawekeza kwenye VETA. Leo tumeambiwa tunajenga Vyuo vya VETA zaidi ya 26 mwaka huu, hii maana yake ni *input* ya Serikali kwenye kuwekeza kwenye viwanda, mwisho wa siku zile pesa zilizokwenda kule zinarudi kuingia kwenye viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile utaona watu wanazungumzia bandari; mimi niseme kwamba Rais Kikwete yupo vizuri sana, alianza huo mradi lakini akaona kidogo kuna shida akasema Morogoro walisema mimi ni mpole mpole lakini naenda kuwaletea chuma, mkali zaidi na mzalendo. Ametuletea mwisho wa siku akamkabidhi faili akamwambia hebu chunguza vizuri hata *Stiegler's Gorge* akamkabidhi yote. Rais akaangalia akahakikisha uwekezaji utakaowekezwa kwenye *Stiegler's* una manufaa kwa Taifa akaupitisha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, akaenda Bagamoyo akaangalia akasema hatuna bandari ambayo tunaiuza Tanzania, tuna bandari ambayo tunataka kuwekeza. Akapiga breki yule mzalendo akasema ngoja nitulie niweke na wakati huo akichukua ushauri kutoka Spika na watu wengine namna nzuri ambayo tutawekeza kwenye bandari zetu zote kuanzia Mtwara mpaka Bagamoyo na tutaelekea mpaka Tanga na hatutaki mtu atakayekuja ku-*dictate terms* hapa ni namna gani tunaendesha hili Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilihama nikaja upande huu na kauli mbiu yangu ya kwanza nilisema naenda kuungana na wazalendo ambao watalinda rasilimali za Taifa hili. Tumekuja kuungana na mtu ambaye ningekuwa ni profesa wa chuo kikuu, Rais Dkt. John Pombe Magufuli ningempa *Ph.D* ya heshima ya sheria ya kuwa profesa wa uchumi na uongozi. Amezisha mambo mengi, wengi walikuja hapa wakifikiri haiwezekani, imethibitika inawezekana; Dodoma leo tupo hapa na jiji linakua. Amezisha *Stiegler's*, watu waliogopa na inaenda, na amesoma *chemistry* lakini amefanya mambo ya uchumi ya kustaajibisha, ndiyo maana mimi leo nasema nashukuru. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ukiangalia China, China ambayo leo imeendelea vizuri, kabla ya kufungua mipaka kuingia kwenye *foreign direct investment* walifunga mipaka wakajihakikishia kwamba wana nguvu ya kutosha ya *negotiation* na wana nguvu ya ndani, ndipo sasa wakafungua mipaka na wanaenda kizalendo na ndiyo maana leo Marekani na China wanabishiana kwenye masuala ya biashara na... (Makofi)

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha. Waheshimiwa Wabunge nilishamwita Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Mheshimiwa Omary Mgumba ajiandae.

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia Wizara hii nyeti, Wizara iliyobeba msingi mkubwa kabisa wa Ilani ya Uchaguzi ya 2015/2020 chini ya Rais wetu na Mwenyekiti wetu wa CCM wa Tanzania ya viwanda ambao Mheshimiwa Rais ameusema na ameanza kuitekeleza kwa kiwango kikubwa tangu ameingia madarakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatofautina katika maeneo mengi sana tunapotazama jambo hili la viwanda, wapo wanaoona kazi haijafanyika, lakini na wapo wanaofanya uchunguzi wa kina kwenye mahitaji makubwa ya viwanda tunaona kwamba kuna kazi kubwa sana imefanyika. Matatizo ya sekta hii ya viwanda na biashara yapo mengi lakini nitataja yaliyokuwepo kwenye ngazi nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, ngazi ya kwanza ilikuwa katika mazingira ya uzalishaji na mazingira ya kufanya biashara. Katika mazingira ya kufanya biashara, Serikali ilishatambua jambo hili na kuna kazi kubwa ambayo imeshafanya na jambo hilo ni kuandaa dira (*blue print*)

ambayo imebainisha matatizo na imeweka mapendekezo ya namna ya kutatua matatizo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu kwa Wizara ni kwamba, kama ambavyo Serikali iliweza kuleta sheria tukarekebisha kwenye upande wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, ilete sheria ambayo itafanya *merging* ya zile taasisi zote ambazo ndiyo zinaleta *multiplicity* ya *duties* pamoja tozo ambayo inaleta matatizo katika mazingira haya ya ufanyaji wa biashara katika nchi yetu. Hatutaweza kuondoa tu vile vitu ambavyo vinafanya wananchi wetu wananyanyasika na mazingira ya ufanyaji wa biashara yanakuwa mabaya kama hatutaanza kwanza kwa kuziunganisha taasisi hizo ambazo kuishi kwake zinategemea tozo zinazotolewa na wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, kwa sababu dira ile ilikuwa imebainisha maeneo ya taasisi ambazo majukumu yake yanafanana, ilete sheria ile ambayo itaunganisha taasisi hizo zote na tukiunganisha taasisi hizo, zile tozo zinazoenda sambamba ambazo zinaleta matatizo kwa wananchi wetu, zitakuwa zimefutika. Hatutaweza kuzifuta tozo peke yake kwa sababu taasisi nyingi hizo zinaishi kwa kutegemea tozo hizo ambazo wananchi wetu wanatozwa na zinasababisha matatizo katika biashara za watu wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakuwa tumeshatatua tatizo pia la muda mwingi kutumika kwa wananchi kusubiri vibali vya taasisi nyingi ambazo zina-*justify* kutoza tozo hizo kwa kujifanya kwamba zina majukumu japo majukumu yale yanafanana na yangeweza kufanywa na taasisi moja na ikaondoa gharama na muda ambao unatumika kwa watu wanaoshughulika na biashara kwenda katika madirisha mengi.

Kwa hiyo, jambo hili kwa sababu Serikali tayari ilishatengeneza *blue print* ile, tunaweza kusema kwamba kuna hatua kubwa ambayo imeshafanyika sasa tufanye ile ya umaliziaji ili tatizo hilo liweze kuondoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo lilikuwa tatizo na lilikuwa kigezo ambacho Serikali imeshalifanyia kazi kwa kiwango kikubwa na Waheshimiwa Wabunge wengine wameshaongelea ni suala la umeme. Suala hili la umeme ni jambo muhimu na kigezo muhimu sana kwenda kwenye viwanda *serious* katika nchi yoyote inayoenda kwenye viwanda vikubwa ambavyo vinaweza vikachukua vijana wengi wakapata ajira katika maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili wengi tunaweza tusitambue faida yake na kwa nini tunalisemea kwa kiwango kikubwa na kwa nini Rais aliamua kufanya uamuzi wa kijasiri kuweza kuhakikisha kwamba tunakuwa na uzalishaji mkubwa wa umeme ambao unaweza ukaendesha viwanda. Kwa umeme tuliokuwa nao, mtakumbuka hata matumizi ya majumbani tu tulikuwa na mgao wa umeme; tusingeweza kuwa na viwanda vingi *serious* kwa kiwango kile cha umeme tulichokuwa tunakuwa nacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo limesalia ambapo Serikali na Wizara inatakiwa ilifanyie kazi ni kwenye ngazi ya uzalishaji. Kwa malighafi tulizonazo tukiweza kutengeneza viwanda vikubwa ambavyo vinatakiwa vitumie umeme mkubwa huu tunaotengeneza na picha kubwa aliyokuwa nayo Mheshimiwa Rais ya kutengeneza viwanda, tunahitaji tutengeneze *zoning* katika nchi yetu ili kuweza kutengeneza mazingira (*mechanization*) kwenye uzalishaji ili tuweze kuzalisha malighafi ambazo zinaweza zikatosha kuwa na viwanda vikubwa ambavyo vinaweza vikatufanya katika sekta ambazo tutakuwa tumezitaja tuweze kuwa wazalishaji wakubwa duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele ilishagonga Mheshimiwa Mwigulu, ahsante sana.

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na kazi kubwa inayofanywa na Rais na Wizara hii. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, kufanya ziara/kongamano la wawekezaji na wafanyabiashara Mafinga. Wakati tunaelekea uchumi wa viwanda, Mafinga tumepiga hatua kubwa hasa katika suala zima la mazao ya misitu. Hata hivyo, tuna changamoto nyingi sana kuanzia masuala ya *Regulatory Authorities* lakini pia kuna fursa kutoka *TIB, TADB* na kadhalika. Nimeomba mwaka wa nne sasa Serikali (Wizara) kwa kushirikiana na Serikali ya Mkoa, Wilaya na Halmashauri tufanye kongamano Mafinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *PVOC*, binafsi baada ya kuhudhuria semina ya *TANTRADE* ambapo *TBS* na *WMA* walitoa mada kati ya hizo niliuliza suala la *PVOC* ambalo kwangu mimi naona ni kuwanufaisha watu kati (*the so called agents*). Maana kazi kubwa inafanywa na *TBS* za nchi husika, mfano ukitoa mzigo China lazima pawepo *TBS* ya kule itoe *certificate* lakini tena mtu analipa dola 800 ili upate *COC*, inapotea bure. Afadhali ingelipwa hapa, kwa sababu pamoja na yote hayo bidhaa ambazo ni *fake* na *substandard* zinaingia nchini. Makusudio yangu ni kushika shilingi hasa ikiwa hapatatolewa maelezo ya kutosha.

MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, niombe kutamka kuwa naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. Napenda Waziri wa Viwanda na Biashara Mheshimiwa Joseph Kakunda (Mbunge) anipe ufafanuzi katika maeneo yafuatayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala imeleta waraka wa kununua mazao ya ufuta, soya, alizeti na choroko kwa mfumo wa stakabadhi ghalani katika kipindi cha uvunaji wa mazao hayo hususan zao la ufuta katika Wilaya ya Namtumbo bila maandalizi yoyote. Hakuna maghala yaliyoandaliwa wala Vyama vya

Msingi vya Ushirika havina maandalizi yoyote. Kwani suala hili ni la dharura au ni njama za Bodi hiyo kuwagombanisha wananchi na Serikali yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyama vya Msingi vilivyopo Namtumbo vinajihusisha na zao la kimkakati la tumbaku na wananchi wana uzoefu mbaya wa kuibiwa mauzo ya tumbaku yao na hivyo wana uoga ulio dhahiri wa kupeleka ufuta wao kwa Vyama hivyo vya Msingi bila kulipwa fedha zao kutokana na walivyodhulumiwa siku za nyuma. Tunalazimisha na matokeo yake sisi viongozi wao wa kuchaguliwa tunachukiwa. Naomba Waziri mwenye dhamana na biashara usitumie nguvu ya sheria kijeshi, badala yake wasiliana mapema na Waziri mwenzako mwenye dhamana ya ushirika na kilimo mpange na kufanya maandalizi ya utekelezaji wa sheria yoyote ile ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wakulima kabla ya msimu wa mavuno kuwadia.

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara ya korosho kwa msimu huu unaomalizika haijaisha vizuri pamoja na uamuzi wa Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli wa Serikali kununua korosho kwa bei nzuri ya Sh.3,300 kwa kilo moja. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais lakini Mawaziri mnaohusika na biashara hiyo mmetuangusha. Mpaka leo hii wananchi 76 wa Tarafa ya Sasawala, Wilaya ya Namtumbo hawajalipwa jumla ya Sh. 344,800,500/=. Wananchi hao ni wakulima waliozalisha na kuuza zaidi ya kilogramu 1,500 kwa kila mkulima. Dhana ya “kakumba” iliyotumika kuchelewesha malipo kwa wakulima hao imesababisha mateso makali kwa wakulima hao na kwa msimu huu wamenyimwa fursa ya kupalilia na kupuliza viualitifu katika mikorosho yao kwa kukosa uwezo. Tafadhali wakulima hao walipwe ili wajikimu na kuendeleza kilimo cha korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, wana Namtumbo kupitia Chama Kikuu cha Ushirika (SONAMCU) tumefanikiwa kumpata mnunuzi wa tumbaku, lakini kuna changamoto mbili kubwa Serikali isaidie kutatua. Moja, soko la tumbaku yetu ya Moshi (DFC) liko zaidi nchi za kiarabu kupitia mlango wa

nchi ya Misri. Kwa kutokuwa wanachama wa COMESA, tumbaku yetu inaingia Misri kwa bei kubwa kutokana na ushuru unaotozwa na hivyo kushindana na washindani wetu ambao ni wakulima wa tumbaku hiyo na ni wanachama wa COMESA, ambao huingiza tumbaku yao bila kutozwa ushuru. Pendekezo, Serikali iingie *“bilateral agreement”* na Misri ili tumbaku yetu iingizwe nchini Misri bila ushuru kama ilivyo kwa nchi za COMESA vinginevyo turudi kuwa wanachama wa COMESA.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, mnunuzi wetu kampuni ya *Premier Active Tanzania Ltd.* wanaidai Serikali shilingi bilioni 12 zilizohakikiwa kama marejesho ya VAT. Hawarudishiwi, hivyo uwezo wa kampuni wa kuendelea kununua tumbaku ya wakulima wetu unapungua na nia yake ya kufufua kiwanda cha kuchakata tumbaku cha Mjini Songea haitekelezeki na hivyo kutunyima fursa za ajira na soko la uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni biashara, hivyo Waziri shirikiana na Waziri wa Kilimo na Waziri wa Fedha na Mipango haki ya kampuni ya kulipwa marejesho ya VAT yaliyohakikiwa ipatikane ili nasi wakulima wa tumbaku tuendelee kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na za kutukuka anazozifanya. Namtumbo tumeshuhudia maendeleo makubwa katika nyanja mbalimbali ikiwemo na upatikanaji wa soko la tumbaku na soya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsanteni sana. Naunga mkono hoja kwa asilimia 100. Nawasilisha.

MHE. MARIA N. KANGOYE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia fursa ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayofanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais kusimamia Wizara kwa uaminifu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Wizara ya Viwanda na Biashara imekaa vyema na imeelezea mikakati mizuri ya Serikali ya kuhakikisha tunaijenga Tanzania ya Viwanda. Pamoja na mipango hiyo, bado ipo haja ya Wizara kuhakikisha inakaa na wadau wengine wa viwanda kama Wizara ya Kilimo, Wizara ya Fedha na Taasisi mbalimbali kama *NDC, OSHA, NEMC, TFDA, TBS, TRA* na nyingine ili kuhakikisha dhamira na mipango mikakati iliyoainisha ndani ya hotuba hii inafanikiwa, kwani kwa asilimia kubwa taasisi hizi kwa namna moja ama nyingine zinakwamisha jitihada za kujenga Tanzania ya Viwanda kwa kodi na tozo nyingi pamoja na urasimu mrefu wa kupata vibali vya biashara bila kusahau Wizara ya Fedha inayotoa bajeti ndogo ama kiasi kidogo cha fedha kwa ajili ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila leo tunakumbushana kuhusu kilimo kuwa uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania lakini mara zote tumekuwa tukijisahau kuimarisha biashara ya kilimo ambayo inatuingizia mapato makubwa na kuongeza ajira kwa Watanzania tena kwa uhakika. Nasema hivyo kwa kumekuwa na changamoto ya wafanyabiashara wa bidhaa za kilimo, wanaouza bidhaa nje ya Bara la Afrika kwa kulazimika kwenda Nairobi ama Holland kupeleka bidhaa zao kwa ajili ya kuthibitishiwa ubora katika maabara zinazokidhi vigezo vya Kimataifa. Pamoja na yote, Tanzania bado haijawa na maabara ya kupima ubora wa bidhaa kama mbogamboga na maua zilizothibitishwa Kimataifa. Ombi langu ni kuwa Serikali iwekeze katika maabara za aina hiyo ili kupunguza adha za wafanyabiashara hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ukosefu wa maabara hizo, bado kuna changamoto za ukosefu wa ndege za kutosha kwa ajili ya usafirishaji wa mboga mboga na maua ambapo wafanyabiashara wengi wamelazimika kusafirisha bidhaa zao kupitia *Jomo Kenyatta Airport*. Naomba Serikali

ihakikishe inaweka mipango ya kuhakikisha kwamba inaweka mazingira ya ndege za aina hiyo kutua nchini kwa wingi kwa ajili ya bidhaa zetu kusafirishwa kwenda katika masoko ya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana naunga mkono hoja.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, leo naomba nianze mchango wangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kutoa mchango wangu kwa njia hii ya maandishi. Pia nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa dhamira yake ya kupeleka Tanzania kuwa na uchumi wa kati na nchi ya viwanda na dhamira hii tunaiona kwenye matendo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza pia Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kufanya kazi kwa bidii katika kusimamia Wizara hii, pamoja na watendaji wote katika Wizara hii. Hata hivyo, ninayo mambo ya kushauri katika kutimiza kauli mbiu hii ya Tanzania ya Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachowavutia wawekezaji kuja kuwekeza ni utulivu, amani na usalama uliopo lakini mara wanapoonisha nia ya kuwekeza wanakumbana na vikwazo vingi sana ikiwa ni pamoja na utitiri wa taasisi za usimamizi kama vile *TBS, OSHA, NEMC, TFDA, FIRE* na nyingine kama hizi ambazo kwa uhalisia zote zinafanya kazi zinazofanana. Vilevile urasimu wa njoo kesho, njoo kesho imekuwa ni kikwazo kingine. Kazi ya wiki moja inachukua miezi mitatu hata mwaka mzima. Pia taasisi hizi bado zimegubikwa na rushwa kubwa kubwa na ndogo ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado bidhaa zinazozalishwa nchini zina bei kubwa kuliko zinazozalishwa nje. Hii inachangiwa kwa kiasi kikubwa na gharama za uzalishaji nchini kuwa kubwa, kunakochangiwa na wingi wa kodi, nishati ya umeme na mafuta lakini hili la urasimu linagharimu sana nchi yetu. Watu wanaogopa kufanya maamuzi pale

wanapohitajika kufanya hivyo, aidha ni kwa kutaka rushwa au kwa kushindwa kuwajibika. Kazi ya kwanza ya Wizara hii ingekuwa ya kulea wafanyabiashara na wawekezaji wa viwanda lakini kinyume chake sasa imekuwa ni maadui wakubwa kwani mfanyabiashara anapokuja Wizarani anaonekana kama msumbufu, badala ya mdau wa maendeleo mwenye kiwanda ni adui wa taasisi zilizo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufungaji wa maduka ya wafanyabiashara na ufungaji wa viwanda haulingani na ufunguaji wa maduka na viwanda vipya. Hii maana yake ni kuwa mazingira ya kufanya biashara nchini ni magumu sana. Ipo haja ya Serikali kukaa pamoja na wafanyabiashara wenye viwanda kuangalia namna nzuri ya kufanya biashara nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufungamanisha kilimo na viwanda ni jambo muhimu sana lakini utekelezaji wa jambo hilo siyo mzuri sana. Uchakataji wa mazao yetu ya kilimo bado ni wa kiwango cha chini sana. Bado wakulima wengi wakubwa na wadogo hawana masoko ya uhakika wa mazao yao. Hii ni kutokana na ukosefu wa viwanda vya kutosha vya kuchakata mazao hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa naishauri Serikali kama kweli ina nia ya kutekeleza sera hii ni lazima kupunguza masharti na urasimu kwa watu wanaoonesha nia ya kuanzisha viwanda vya kuchakata mazao yetu ya kilimo, uvuvi na ufugaji. Huwezi kufungamanisha kilimo na viwanda kama hakuna viwanda vya kutosha vya kuongeza thamani ya mazao yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya wafanyakazi wa kigeni kwa mwekezaji wa nje bado halijakaa sawa, kuna malalamiko mengi sana kwenye sekta hii. Wako wawekezaji walio waajiri wageni bila ya kuwa na sababu maalum tena bila kufuata sheria. Viko viwanda hata madereva, vibarua, fundi saidia na wengine kama hao ni wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia vipo viwanda au wawekezaji wanakataliwa kuajiri watu hao (wageni) hata wale walioko ndani ya sheria. Jambo hili limekuwa likihamasisha rushwa makazini. Serikali ifanye ukaguzi wa mara kwa mara viwandani ili kusimamia sheria hii kwani ajira nyingi zinakwenda kwa wageni, hivi sasa jambo hili limekuwa ni la kwaida sana Watanzania wazawa viwandani wamebaki kuwa vibarua wasiokuwa bali ajira ya mikataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Waziri wa Viwanda na Biashara awe mlezi wa wafanyabiashara na wenye viwanda na kusikiliza changamoto wanazopata. Si kweli kwamba wafanyabiashara wote ni wakwepa kodi na ni wezi, je kwa nini watu hawa wanakwepa kodi? Lazima Serikali ije na utafiti kwa nini wafanyabiashara wanakwepa kodi. Kulipa kodi kabla ya kuanza biashara si jambo jema, *TRA* waangalie vyema jambo hili. Kama ni sheria basi sheria hii iko kinyume na maelekezo wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa naishauri Serikali lazima tufanye mabadiliko makubwa ya kisera juu ya namna ya kufanya biashara na uwekezaji nchini kwani kuzilaumu taasisi zinazosimamia sheria hatuzitendei haki. Kama zinaonekana ni kikwazo basi ni bora sheria za kuanzishwa taasisi hizi zikaletwa hapa Bungeni tuzifanyie marekebisho ili kuondoa utitiri wa taasisi hizo maana wote tunakubaliana kuwa taasisi hizi ni kikwazo kikubwa kwa wawekezaji na wafanyabiashara.

MHE. NURU A. BAFADHILI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mungu kwa kupata nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mbeje yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara wengi wanalalamikia suala zima la ushuru. Wafanyabiashara wanapofikia mpakani kibali cha kuingiza bidhaa nchini imekuwa ni kero. Kuna kulipia ushuru wa *TFDA*, *VAT* na tozo nyingine nyingi. Mfano unaingiza pipi, biskuti, tende na kadhalika unatakiwa ulipie Sh.800,000 kwa kila bidhaa, mfano hizo bidhaa tatu itabidi ulipie Sh.2,400,000 kwa miaka mitano.

Je, mfanyabiashara ambaye mtaji wake ni mdogo Serikali haioni kuwa inamkandamiza mfanyabiashara huyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, utakuta magari ya mizigo, mfano Kenya kuja Tanzania ni mengi kuliko Tanzania kwenda Kenya kwa vile kuingiza bidhaa Kenya kuna unafuu wa ushuru. Nashauri kama itawezekana masharti yalegezwe *TFDA* angalau mzigo utozwe kodi 1% kila mzigo unapoingizwa. Pia Soko la Afrika Mashariki wawe na kituo kimoja cha *Bureau of Standards* ambapo bidhaa zao zinalipwa ushuru baada ya kupimwa badala ya kazi hii kufanywa na *TFDA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna magari maalum ya kubeba kemikali lakini magari haya yanawaumiza wafanyabiashara wadogo kutokana na tozo ilivyo kubwa. Mfano, kuna wafanyabiashara wadogowadogo ambao wanaingiza nchini *office glue*, inabidi mfanyabiashara awe na gari maalum lililosajiliwa hata kama ana *carton 50* za *office glue* inahesabika kuwa ni kemikali, huwezi kubeba *carton 50* katika gari la tani 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri uwepo utaratibu wa kusajili magari hata kuanzia tani moja. Hii ya kusajili tani 10 imelenga kwa wafanyabiashara wakubwa na kuwaacha wafanyabiashara wadogo kuendelea kubaki maskini. Naiomba Serikali iangalie suala hili la magari ya kubeba kemikali.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia katika hoja hii kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kuchangia kuhusu matatizo ya wafanyabiashara. Watu wengi wamefunga biashara zao kutokana na manyanyaso wanayoyapata kutoka kwa watu wa *TRA*. Wafanyabiashara wengi kabla ya kuanza biashara anapitia hatua nyingi ambazo zote ni za tozo mbalimbali. Kabla mtu hajaanza kuuza biashara yake anaanza kutoa fedha za kodi na wakati huo makadirio ya *TRA* yanakuwa makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishauri Serikali kwamba watu wanapofungua biashara wasikadiriwe tozo hadi wafanye biashara zao kwanza waone mapato wanayoyapata ndipo waanze kutozwa kodi. Ndiyo maana watu wanafungua biashara kwa kodi hiyo kubwa, mwisho wa siku wanaona ni gharama wanaamua kufunga biashara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, *SIDO*. Naomba viwanda vidogovidogo viimarishwe kwani ni muhimu sana. Vimekuwa vikiwasaidia wajasiriamali wadogowadogo lakini *SIDO* haichukuliwi kama ni muhimu. *SIDO* inaweza kuajiri wanawake na vijana wengi nchini lakini hata bajeti ya kutosha haitengwi. Naitaka Serikali ilichukue suala hili la *SIDO* kwa umakini na kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya *SIDO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Liganga na Mchuchuma. Sijui ni kwa nini mradi wa Liganga na Mchuchuma unasuasua wakati sisi kama Wabunge wa Mkoa wa Njombe tumehamasisha wananchi kufanya maandalizi ya mradi huo kwa kilimo cha mazao mbalimbali yakiwemo matunda na mbogamboga. Wananchi wamefanya bidii kulima lakini mazao yao hayana soko kwa kuwa walikuwa wanategemea mradi wa Liganga na Mchuchuma. Niitake Serikali iharakishe mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. SONIA J. MAGOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuwapongeza watendaji wote wa Wizara kwa jitihada kubwa wanazozifanya kuendeleza sekta hii ya viwanda na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, niionbe sana Wizara iingalie Tanga kwa jicho la huruma kabisa. Mkoa wetu unazalisha matunda kwa kiwango kikubwa sana tena mengine ambayo huwezi kuyapata mahali pengine popote tatizo hatuna kiwanda. Matunda yanaoza sana na kusababisha hasara kubwa kwa wananchi, hivyo Serikali

iwasaidie wananchi hawa kuondokana na tatizo hili na kukuza wigo wa biashara na uchumi kwa Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tunaomba tupatiwe kiwanda kwa ajili ya nafaka kama mahindi, mihogo, ambayo inalimwa kwa kiasi kikubwa sana katika Mkoa wa Tanga. Kuna viwanda vinasuasua sana kama cha chuma, kamba hakiko vizuri kabisa kwa sasa. Pia tungeomba turejeshewe viwanda vya mbolea na *plastic* ambavyo vililhamishwa hivyo kudororesha kwa kiasi kikubwa uchumi wa Mkoa wa Tanga.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya Mkoa wa Kilimanjaro vilivyobinafsishwa bado havijaanza kufanya kazi kama ambavyo Serikali imekuwa ikiagiza. Mji wa Moshi katika miaka ya 70 hadi mwanzoni mwa miaka ya 90 ulikuwa una viwanda vikubwa zaidi ya 12 ikiwa ni pamoja na viwanda vya watu binafsi. Viwanda hivyo ni pamoja na viwanda vya magunia, ngozi, mbao, nguo, pipi, vibiriti, karatasi na kadhalika. Hali ilivyo sasa ni tofauti kabisa kwa vile viwanda vyote hivyo vimekufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali ipitie upya kanzidata ya viwanda katika Mkoa wa Kilimanjaro ili ione ni namna gani inaweza kufufua viwanda vilivyokufa katika Mji wa Moshi na Mkoa wa Kilimanjaro kwa ujumla. Kufufuliwa kwa viwanda hivyo kutachochea ukuaji wa uchumi wa Mkoa wa Kilimanjaro na Taifa kwa ujumla. Pia, kutaongeza ajira na mambo mengine kama hayo. Aidha, ni vizuri Wizara ikawatafuta wawekezaji binafsi ambao viwanda vyao vimekufa ili kuona ni jinsi gani wanaweza kushirikishana namna bora ya kuvifufua.

Mheshimiwa Naibu Spika, uimarishaji wa soko la ndani. Dhamira ya Serikali ya kujenga Tanzania ya Viwanda itafikiwa iwapo tutaimarisha soko la ndani. Soko la ndani ndilo litakalohakikisha mauzo ya bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya ndani. Wajibu wa Wizara ya Viwanda na Biashara ni kutoa msukumo na motisha kwa wafanyabiashara wa Tanzania ili biashara zao ziimarike ambapo wataweza

kuajiri wafanyakazi wengi sana, hivyo kuongeza kipato cha Watanzania na kwa maana hiyo kuongeza nguvu ya soko (*purchasing power*).

Mheshimiwa Naibu Spika, soko la ndani ndilo linaweza kufanya wawekezaji wa kiwango cha kati na cha chini kuimarika na baadaye kuwa wawekezaji wakubwa watakaouza nje. Soko la ndani ndilo linaweza kukuza kidogokidogo viwango vya bidhaa zetu zinazozalishwa na kuziingiza kwenye ushindani wa soko la nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kodi ya Huduma (*Service Levy*). Sheria ya Kodi hii ya Huduma lazima ibadilishwe ili iweze kulipika. Utaratibu wa sasa ambapo kodi hii inalipwa kwa kigezo cha mauzo ghafi siyo utaratibu wenye tija kwa wafanyabiashara na kwa Taifa kwa ujumla. Utaratibu huu unaweza ukafilisi wafanyabiashara kama ukitekelezwa kama ulivyo. Hivyo, ushauri wangu ni kwamba kodi hii itozwe katika faida na kama haifai kutozwa katika faida itozwe kwa viwango kulingana na madaraja ya biashara.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia bajeti hii ambayo kimsingi imebeba dhana ya Serikali ya Viwanda, naomba kuikumbusha Serikali mchakato wa viwanda 100 kila mkoa. Mkoa wa Katavi kutokana na kuendelea kuwa na changamoto za maji na umeme pamoja na masoko kutokana na miundombinu ya barabara kuwa kero kwa usafirishaji, naomba utekelezaji kwa kutatua kero hizi ili viwanda vilivyoanzishwa na vikundi mbalimbali ikiwemo viwanda vya alizeti, Manispaa ya Mpanda; viwanda vya mazao, mpunga na mahindi; viwanda vya maziwa (makanyagio); viwanda vya nyama, ukizingatia Mkoa wa Katavi kuna ufugaji wa kutosha viweze kuendelea. Hivyo, ni rai yangu kuomba Serikali hii kufungamanisha sekta ya ufugaji na viwanda ili dhana ya viwanda ifanikiwe.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuweza kutoa mchango wangu katika hotuba hii. Pia nawatakia Waislamu duniani kote Ramadhan Kareem.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imejipanga uchumi wa viwanda na ni ukweli usiofichika viwanda vingi vimejengwa. Hata hivyo, kama viwanda havitakuwa na usimamizi mzuri na wataalam wenye ujuzi mkubwa vitakufa na kukosekana kwa matarajio ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima Serikali iweze kuhimiza kujenga viwanda vya kuzalisha malighafi ili kupunguza kupoteza fedha nyingi kuagiza malighafi kutoka nje na kuisababishia Serikali hasara. Mungu ametupa utajiri mkubwa katika nchi hii ikiwemo maziwa na bahari lakini nitazungumzia bahari, tunazo bahari zetu kama Dar es Salaam, Mafia, Tanga, Lindi, Zanzibar lakini bahati mbaya hatuna viwanda vya kuchakata samaki, hii inapelekea kuwakosesha vijana ajira na kupoteza pato kubwa la Taifa.

Pia inapelekea leo kuwaachia Wachina kuuza samaki wetu na kuondoka nao. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga viwanda hivi katika Miji niliyoitaja ili tupate maendeleo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema Tanzania ni nchi moja na Taifa moja lakini la kushangaza bidhaa zinatoka Zanzibar mfano sukari, maziwa ya Azam, maji ya Drop hayaruhusiwi na hawapewi kibali kuingia Tanzania Bara lakini Zanzibar zinaingia mfano condom, sigara, bia na kadhalika. Nitoe mfano mwingine magari yanayotoka Tanzania Bara ni lazima ulipe ushuru wa bandari *TRA* na magari yale yale yanapofika Zanzibar yanalipa tena ushuru na *TRA*. Je, hiyo ni haki? Tunaomba changamoto hii itatuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu huo, naomba kuwasilisha.

MHE. JANETH M. MASABURI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe pongezi kwa Waziri na wasaidizi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vikwazo ambavyo vinazuia maeneo yote *EPZ* kutoanzisha viwanda hapa nchini

vitatuliwe. Mfano, eneo la *EPZ* Morogoro hatua za haraka zichukuliwe kwa kushirikisha Wizara ya Ardhi na TAMISEMI na kutoa maamuzi kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vidogovidogo, *SIDO* ipewe uwezo mkubwa zaidi kwa kutengewa fedha za mafunzo kwa vitendo na kuwakopesha vijana mitambo midogo na ya kati na kuanzisha viwanda vidogovidogo kwa vijana kwa wilaya zote hapa nchini. Hii itasaidia kupunguza tatizo la ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Dodoma uwekezwe kwa viwanda vingi vya mvinyo kutokana na zabibu ya Dodoma kukubalika katika soko la dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa 100%.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja na nampongeza Waziri wa Viwanda na Biashara pamoja na Naibu wake na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi sina, naomba nimpongeze Rais wangu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya kuhamasisha ujenzi wa uchumi wa kati wa viwanda. Miradi mikubwa ya ujenzi wa miundombinu inayoendelea ikijumuisha njia za reli, umeme, barabara, viwanja vya ndege na bandari ni ishara tosha kuonyesha dhamira njema ya Rais ya kujenga uchumi wa viwanda inakwenda kutekelezwa kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huu, nashauri sasa Serikali iwekeze juhudi za dhati za kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji wa viwanda vya aina mbalimbali nchini kwa kuondoa au kupunguza kodi zisizo za lazima, kuharakisha utoaji wa vibali na kutangaza fursa mbalimbali za uwekezaji zilizopo katika nchi yetu. Hizi fursa ni pamoja na kuanzisha na kufufua viwanda vya mazao ya kilimo, mifugo, madini na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe hoja kuhusu mradi wa Magadi Soda Engaruka. Mradi huu umezungumziwa katika kitabu cha hotuba ya Waziri ukurasa wa 17. Pamoja na utafiti wa kina ambao umeanza kufanyika kubaini upatikanaji wa rasilimali ya magadi, maji safi, athari za mazingira na kijamii, naomba nitoe angalizo kuhusu masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ingawa eneo kubwa la mradi wa magadi liko katika Wilaya ya Monduli, vilevile kuna sehemu ya ardhi iliyopimwa ambayo imeingia ndani ya eneo la Wilaya jirani ya Longido (Kijiji cha Sokon). Hivi sasa tunavyojadili bajeti ya Wizara hii, wananchi wa Kijiji cha Sokon wanaoishi katika eneo ambalo limeingia ndani ya ardhi iliyopimwa na kufanywa sehemu ya viwanda wameshapewa notisi ya kuhama ndani ya wiki mbili na huku bado hawajafidiwa. Nashauri wananchi wasibughudhiwe mpaka wafidiwe kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, faida za mradi kwa wananchi ama Wilaya husika. Kwa kuwa mradi huu wa magadi umetwaa vipande vya ardhi vilivyoko ndani ya Wilaya ya Monduli na Longido, ni vyema Wizara itambue hilo na ibainishe kuwa kiko katika wilaya zote mbili ili jamii zote wapate faida na kuepusha migogoro isiyo ya lazima ya kugombania rasilimali husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, miundombinu. Kwa kuwa eneo la mradi ni mbali (*remote area*) na lenye mazingira magumu na lisilo na barabara inayopitika, nashauri Serikali iwekeze kwanza katika kufungua barabara za kufikia eneo la mradi. Kuna njia mbili za kufika katika eneo la mradi: Barabara ya kutoka Mto wa Mbu (km 70); na barabara ya kuunga barabara ya moram inayotoka Longido – Oldonyo Lengai (km 14).

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, umuhimu wa kuanzisha kiwanda cha kuchakata nyama. Kwa kuwa eneo la Bonde la Engaruka na maeneo yote yanayopakana nalo ni ya wafugaji ikijumuisha Tarafa nzima ya Ketumbaine, Wilayani

Longido, Engaresero, Wilayani Ngorongoro na Tarafa ya Ngorongoro, Wilayani Monduli. Napenda kuishauri Serikali kuwa kijengwe kiwanda katika eneo hili cha kuchakata nyama. Eneo hili ni tajiri kwa mifugo na lina nyanda pana za malisho kasoro maji safi na kwa kuwajengea wafugaji kiwanda cha kuchakata nyama na mazao mengine ya mifugo itakuwa ni faida ya ziada ya kufunguliwa uchumi wa viwanda katika Bonde la Engaruka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba kuhitimisha kwa kutamka tena kuwa naunga mkono hoja.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Naibu Spika, ubinafsishaji viwanda vya Serikali ambavyo havifanyi kazi hususani viwanda vya Mkoa wa Morogoro mfano Asante Moproco, Canvace, Morogoro Shoes Tanaries na kadhalika, iko haja Serikali kuangalia upya uwekezaji huo kwani kwa sasa kuna malalamiko kuwa wawekezaji wameuza vipuri mfano, Morogoro Canvas vipuri havipo Serikali ifuatilie. Hivi ilikuwa ni uwekezaji, ubinafsishaji au ufilishaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Tumbaku Morogoro kilichokuwa na uwezo mkubwa wa uzalishaji na kutoa ajira, sasa hivi kimepunguza uzalishaji na ajira na kinadai Serikali *tax returns* za zaidi ya bilioni 25. Serikali irudishe fedha hizo viwanda viweze kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, *importation* ya bidhaa zinazozalishwa nchini kwa wingi mfano maziwa hatuna sababu ya kuendelea kuruhusu uingizaji wa maziwa ya nje na yanauzwa bei ndogo ikilinganishwa na maziwa yanayozalishwa nchini. Hatuwezi kukuza uchumi kama Serikali haiweki mazingira rafiki kwa viwanda vyetu vya ndani kwa kuvilinda ili viweze kukabiliana na ushindani. Vilevile, *returns* za *tax* kwa viwanda vingi hapa nchini hazirudi hii inaweza kushusha fursa za uwekezaji kwa viwanda vingi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara nyingi zinafungwa kutokana na mazingira magumu ya biashara Kariakoo na

katika mikoa mingi. Juzi Mtwara tumeona kwenye TV wafanyabiashara wamerudisha leseni za biashara, hii siyo sawa. Kuna mzigo mkubwa wa kodi mfano OSHA, leseni, *tax leavy*, Manispaa na kadhalika. Mzigo huu mkubwa wa kodi siyo afya na biashara nyingi zinakufa. Serikali iangalie jinsi ya ku-*harmonize* hali hii kwani uchumi wa nchi yoyote unategemea mapato yanayotokana na wafanyabiashara wadogo ambao wapo wengi nchini.

MHE. ROSE C. TWEVE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi ili niweze kutoa maoni yangu kwenye Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa mchango mkubwa wanaoutoa kwenye Wizara hii. Wizara ya Viwanda na Biashara ndiyo yenye jukumu la kusimamia Sera ya Viwanda na Biashara nchini na Wizara nyingine ndiyo watekelezaji. Kwa hali ya kawaida, Wizara ya Kilimo ndiyo tulitegemea ichangie sana au zaidi kwenye maendeleo ya viwanda hapa nchini. *So far* Wizara ya Viwanda haina *direct link* na Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Taifa tunategemea kuingiza mafuta ya kula kutoka nje. Sasa Wizara ya Viwanda inge-*link* na Wizara ya Kilimo tungehakikisha tunakuwa na mbegu bora na kuweza kuzalisha mafuta ya kula hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2018 tulizindua mradi wa *ASDP II* na mradi huu una pesa nyingi sana. Tungekuwa na *link* na Wizara ya Kilimo ingetusaidia sisi kama nchi kuweka mkakati mzuri wa kuzalisha *products* zetu badala ya kutegemea bidhaa kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati umefika sasa kuhakikisha tunatengeneza soko la ndani. Lazima taasisi za kiserikali wapewe tamko rasmi kuhakikisha vitu vyote ambavyo vinatumiwa na hizi taasisi za kiserikali watumie bidhaa ambazo zimezalishwa hapa nchini. Tanzania ya

Wiwanda inawezekana kwani lazima tujipange vizuri na *sector* zote nchini lazima zishirikiane.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwatakie kheri Mheshimiwa Waziri na watendaji wote katika utekelezaji wa bajeti yao. Naunga mkono hoja.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Urambo na Kaliua ni Wilaya zinazoongoza hapa nchini kwa kilimo cha tumbaku. Pamoja na Wilaya hizi kuongoza kwa kilimo hiki, Mkoani Tabora bado hakuna kiwanda cha kusindika tumbaku pamoja na uwepo wa miundombinu ya reli na hata barabara inayojengwa. Je, ni lini Serikali itajenga kiwanda cha kusindika tumbaku Wilayani Urambo?

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri. Pia nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa utekelezaji wa mkakati wa ujenzi viwanda ili Tanzania ifikie hadhi ya nchi ya uchumi wa kati 2025. Huu ni mkakati wenye tija kubwa sana kwa nchi yetu. Mkakati wa viwanda ni ukombozi kwa vijana wa Tanzania, tatizo kubwa sana la vijana leo ni ajira, viwanda vitaondosha tatizo hili kubwa kwa vijana. Naiomba Serikali iweke msisitizo katika ujenzi wa viwanda vinavyotumia malighafi ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetenga katika Jimbo la Bagamoyo eneo la viwanda kwa awamu mbili, EPZ I (hekta 5,7420 na EPZ II (hekta 3,338). Jumla ni hekta 9,080. Vijiji vitano (5) vimehusika: Zinga, Kondo, Mlingotini, Pande na Kiromo. Maeneo ya EPZ I yamethaminiwa mwaka 2008 ikiwa na jumla ya wafidiwa 2,180. Cha kusikitisha ni kwamba miaka 11 leo wafidiwa 1,025 hawajalipwa fidia yao. Naiomba Serikali yangu Tukufu iwalipe fidia wananchi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, EPZ II (hekta 3,338) inajumuisha maeneo yenye makazi ya wananchi wengi, zikiwemo Zinga kwa Awadhi, Zinga kwa Mtoro, Kondo, Mlingotini na Kiromo. Vijiji hivi vina jumla ya kaya 3,381 (sensa 2012) zenye watu 12,797. Wananchi hawaridhii kuhamishwa maeneo yao. Naiomba Serikali yangu Tukufu kuwaachia wananchi maeneo yao ya makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo na pia kupata fursa kuchangia. Niipongeze Serikali kwa kazi kubwa na nzuri inayofanya na pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara hii, tumeona mabadiliko makubwa ya mtazamo na fikra (*mind set change*). Nipoongeze na kumshukuru Mheshimiwa Rais kuanzisha Wizara ya Uwekezaji na kazi yao kubwa ni kufanya uratibu baina ya Wizara zote kuhakikisha kunakuwa na mazingira wezeshi na bora katika uwekezaji ambayo ni muhimu kwa suala la biashara na pia viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri katika maeneo machache; kwanza Serikali iharakishe kutekeleza *Blue Print*. Jambo hili linahitaji uratibu wa Wizara zote na utafanya gharama za uzalishaji zipungue bila kuathiri ubora na viwango. Nashauri Serikali iunganishe Taasisi za Udhibiti kuwa mbili, muundo wa juu na muundo wa chini. (*Upper Stream Regulatory Authority* na *Lower Stream Regulatory Authority*) na taasisi hizo zifanye majukumu yao ya udhibiti na zisiwe taasisi za kuwa chanzo cha mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii taasisi hizi ndizo kikwazo kubwa cha kufanya urahisi wa kufanya biashara (*Ease of doing business*) na pia (*cost of doing business*) kupunguza gharama za uzalishaji. Pia tunashauri Maafisa Biashara ngazi ya Taifa, ngazi ya Mkoa, ngazi ya Wilaya ndio wawe sehemu ya kutoa leseni na ushauri wote unaohitajika kufanya biashara yoyote (*one stop center*). Pia pawe na

kanuni ya kubana utoaji wa adhabu (*fine*) ili kwanza mtu apewe fursa ya kurekebisha kabla ya tozo ya adhabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali iwekeze katika kuelimisha kupitia taasisi zetu za elimu ya ufundi, *SIDO*, *TEMDO* na pia katika Taasisi ya Utafiti - *TIRDO*. Bila utafiti hatutaweza kuwa na mafaniko. Tunaomba *SDL*, fedha zote asilimia nne na nusu 4.5% ziende katika kuboresha taaluma ya ujuzi kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu Serikali tuwekeze katika Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ili kukuza ajira, biashara na kupatikana kwa malighafi ya viwanda vyetu. Muhimu kupata utafiti wa bidhaa tunazoagiza kutoka nje ambazo tunaweza kuzalisha ndani ya nchi ili tuweze kuzalisha ndani ya nchi badala ya kuagiza nje. Leo hii Serikali itaona sekta isiyokuwa rasmi inakua kwa kasi kubwa na sekta rasmi kushuka kwa sababu ya kutokuwa na mazingira na usawa wa kufanya biashara. Napongeza na kushukuru jitihada zote za Wizara na wataalam wote. Siku zote changamoto ndogo ndogo zitakuwepo na ni kuangalia namna ya kuboresha na kuondoa hizo changamoto.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia katika Wizara hii. Pili napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Biashara pamoja na watendaji wake wote kwa kuandika na kuiwasilisha kwa umakini wa ufasaha na hali ya juu. Katika kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Biashara na Viwanda napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Matrekta aina ya *Ursus*. Napenda kuipongeza Serikali kwa azma yake ya kuendeleza mradi huu wa matrekta, kama inavyojulikana kwa dhana ya kuelekea kwenye sera ya viwanda haiwezi kufanikiwa bila ya kuimarisha kilimo cha kisasa. Vitendea kazi katika kilimo moja katika hivyo ni matrekta. Hata hivyo, ni vyema Serikali ikatilia mkazo mradi huu. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 10 imeeleza idadi ya matrekta

na idadi ya hekari zilizokwishalimwa uwiano wake ni heka 214.1 limelimwa kwa kila trekta moja. Hii ni idadi ndogo sana kwa nchi inayoelekea kwenye kuimarisha viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu katika jambo hili ni kwamba Serikali ipunguze bei ya matrekta na kuondosha vikwazo vilivopo ili wananchi wengi waweze kumudu kununua matrekta hayo. Inaonekana kuwa bado bei ya matrekta sio rafiki kwa wakulima wetu. Tanzania ya viwanda itawezekana ikiwa miundombinu ya kuboresha kilimo ambayo ni pamoja na kupunguza bei za matrekta ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ambayo ni muhimu kwa uchumi wa nchi yetu kwa kuzingatia mambo muhimu ili kufikia uchumi wa kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa kiwanda cha mbolea; kulingana na umuhimu wa kilimo katika kukuza viwanda au uchumi ni vyema kutazama hitaji kubwa la bei kubwa ya mbolea; ili kumaliza tatizo hilo tujenge kiwanda cha *urea*.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wafanyabiashara kufunga biashara zao; kumekuwa na mabadiliko makubwa kutoka kwa wafanyabiashara badala ya kuongeza wafanyabiashara inakuwa kinyume chake. Nashauri Serikali kufuatilia suala hili ili kuendelea kuinua uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maafisa wapewe elimu pamoja na malalamiko mengi ya wafanyabiashara wengi nchini kwenye halmashauri zetu, lakini huko kuna Maafisa Biashara inaonekana wafanyabiashara sasa hawaoni umuhimu wa Maafisa hawa kwani miongoni mwa majukumu ni pamoja na kutoa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya sukari kuendelea kupanda; Wizara ina mkakati gani wa kuweza kudhibiti bei ya sukari kwani suala hili linaathiri kwa kiasi kikubwa wananchi wa hali ya chini. Pia nataka kujua kununua sukari nje ya nchi kunapunguza bei ya sukari au inaongeza bei kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi ya huduma; suala hili limekuwa na changamoto kubwa kwa wafanyabiashara pia lina wafanya wafanyabiashara wetu kukata tamaa na wengine kuhama. Nashauri Serikali kuleta marekebisho ya sheria hiyo ndani ya Bunge letu ili ifanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira ya biashara yasiyotabirika; kumekuwa na shida kubwa kwa taasisi mbalimbali zinazohusiana na mambo ya biashara, matamko ya mabadiliko ya kila wakati kuhusiana na biashara nchini. Nashauri Serikali kupitia upya kauli zake ili kabla haijatoa tamko lolote izingatie mazingira halisi ya wafanyabiashara wetu nchini.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha *MUTEX* Musoma kilichokuwa kinazalisha kanga na vitenge, kilitoa ajira 1,000, lakini tangu kibinafsishwe kiwanda hiki hakifanyi kazi hivyo kufifisha uchumi kwa Mkoa wa Mara na Taifa kwa ujumla. Kiwanda hiki kwa sasa kimekosesha ajira kwa Wanamara na hasa wanawake walikuwa wakifanya kazi kwenye kiwanda hiki. Je, ni lini kiwanda hiki kitarudishwa Serikalini au kutafuta muwekezaji mwingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia zipo taarifa kwamba mashine mpya zilizokuwepo katika kiwanda hiki kwa sasa hazipo tena na ziling'olewa. Je, Serikali wanazo taarifa za kiwanda hiki kuharibiwa miundombinu yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, taulo za wanawake, watoto wa kike zinazuzwa bei ghali hivyo wanawake na watoto wa kike wenye kipato cha chini kushindwa kumudu gharama na hata kuhudhuria masomo yao kikamilifu. Katika bajeti ya mwaka 2018/2019, Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana

alifuta kodi kwenye malighafi zilizotumika kutengenezea taulo za kike. Je, tangu tumeondoa kodi hizo ni viwanda vingapi vimejengwa hapa ndani kwa ajili ya kutengeneza taulo hizi? Kwa sasa bei imeshuka kwa kiasi gani ili kuleta unafuu kwa wanawake na wasichana?

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya kutengeneza madawa hapa nchini; Tanzania tunatumia pesa nyingi katika kuagiza madawa kutoka nje ya nchi. Ningependa kujua ni viwanda vingapi vimejengwa mpaka kufikia sasa? Serikali ina mpango gani wa kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje ili kuwekeza hapa nchini badala ya kutegemea viwanda vya nje?

MHE. JOYCE J. MUKYA: Mheshimiwa Naibu Spika, kuna uhusiano mkubwa kati ya sekta ya kilimo na ukuaji wa uchumi wa viwanda. Kama inavyoeleweka *vision* ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuendeleza viwanda nchini na kukuza uchumi wa kati kupita viwanda hivyo, lakini ili viwanda viweze kuzalisha kwa kiwango ambacho kitazalisha vizuri na kukuza uchumi wa kati, tunahitaji *material, human resource* na haya kwangu ni mambo muhimu zaidi kwa viwanda vya ndani. Sasa kama tunavyofahamu kilimo sasa hivi hapa Tanzania hakipovizuri kutokana na hali ya uchumi wa wananchi kuwa chini kwa kushindwa kuhudumia mazao yao ipasavyo kutokana na huduma za pembejeo, mbegu, kuwa juu na vilevile hali ya hewa kwa sasa siyo nzuri sana kwa wastani wa mazao ya wakulima kilimo kinachangia takribani 65% ya malighafi zote za viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Serikali ihakikishe inaboresha kwanza kilimo na kuelekeza katika viwanda ambavyo vitaongeza thamani katika uzalishaji wa mazao mbalimbali. Mfano ya mifugo kama ngozi, maziwa, kwato, pembe, damu, ambavyo vyote hivi vinasaidia katika kutengeneza bidhaa mbalimbali kwenye viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, manyanyaso ya wafanyabiashara mbalimbali tokea Awamu ya Tano imeingia madarakani; kumekuwa na matatizo makubwa kwa

wafanyabiashara nchini kama vile hawana uhalali wa kufanya biashara au kutafuta njia mbadala ya kujikimu katika maisha kama sekta nyingine zinavyofanya. Wafanyabiashara ndiyo walipakodi wakubwa katika nchi hii, lakini wamekuwa hawatendewi haki kabisa na biashara sasa hivi imekuwa ni kama kansa katika nchi yetu. Kodi zimekuwa nyingi zaidi ya 25 ili tu kuanzisha kampuni yoyote ya kibiashara nchini. Hili linafukuza hata *investors* ambao wanataka kuja nchini kuwekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishauri Serikali kuwasaidia wafanyabiashara katika kuhakikisha wanakua na mazingira mazuri ya kufanya biashara na kuisaidia Serikali pia hata kufanikiwa katika kupata kodi kupitia biashara wanayofanya, lakini pia wafanyabiashara wanasaidia sana katika kuendeleza uchumi wa kati kupitia viwanda ambavyo ni *vision* ya Serikali ya Awamu ya Tano.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii. Nianze kwa kumpongeza Mtoa Hoja Mheshimiwa Waziri Joseph Kakunda kwa wasilisho zuri asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kisiwa cha Mafia kimejaaliwa hazina kubwa ya rasilimali za bahari na aina mbalimbali ya samaki. Kwa sasa kuna kiwanda kimoja tu cha kusindika samaki, naishauri Serikali yangu makini kuangalia uwezekano wa kujenga kiwanda kikubwa cha kusindika samaki katika Wilaya ya Mafia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kiwanda cha kusindika nazi; Tanzania inaongoza katika Afrika katika kulima nazi na inashika nafasi za juu katika dunia. Kisiwa cha Mafia kinalima zao hili kwa wingi lakini hadi sasa hakuna kiwanda hata kimoja cha kusindika nazi na mazao yanayotokana na nazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni utendaji kazi wa Shirika la Viwango (*TBS*);ni ukweli usio na shaka *TBS*

inakabiliwa na changamoto kubwa ya vifaa vya kupima ubora ili iendane na kasi ya ukuaji wa viwanda nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni mfumo wa malipo ya ushuru wa bidhaa kwa kielektroniki yaani *ETS*; ni ukweli usio na shaka mfumo huu umesaidia kuongeza mapato ya Serikali, ni ushauri wangu sasa Serikali iongeze wigo wa bidhaa zinazotumia mfumo huu katika vinywaji na sigara kwenda kwenye bidhaa nyingine kama *cement*, nondo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja.

MHE. ZAINAB M. AMIRI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nitoe shukrani kwa Wizara ya Viwanda na Biashara, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara pamoja na Naibu Waziri pamoja na watendaji wote kwa kazi wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali itoe *tax period* kwa wafanyabiashara wanaotaka kuanzisha biashara zao, ndipo walipe/wakadiriwe mapato. Tatizo watu wanalipa kabla ya kuanzisha biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iunde Tume Maalum ya kufuatilia viwanda vilivyobinafsishwa na kuona utendaji wake na kuisaidia Serikali kufikia Tanzania ya Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zinazotolewa na Hazina ni chache na hazifiki kwa wakati, naishauri Serikali itoe fedha kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa masoko kwa mazao yetu nje ya nchi ufanywe kwa umakini na kuwe na mikataba maalumu ndipo uhamasishaji wa kulima zao husika uanze, kuepuka usumbufu kama ulivyotokea katika zao la mbaazi kukosa soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara wenye viwanda vinavyotumia sukari ya viwandani wanaidai Serikali bilioni 43.2. Hadi sasa ni shilingi bilioni 13 tu ndizo zilizolipwa, hivyo Serikali iwalipe wafanyabiashara hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ijaze nafasi ambazo watendaji wake wanakaimu ili kuweza kuwa na maamuzi katika masuala mbalimbali ya kiutendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vitumie malighafi zinazopatikana nchini mwetu ili kukuza kilimo chetu, pia kusaidia bidhaa kuwa na bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ipunguze utitiri wa kodi kwa watu wanaotaka kuanzisha viwanda ili kuweza kuwapa fursa na wawekezaji wengine kuvutiwa na uwekezaji hapa nchini mwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nawaombea afya njema na umri mrefu Mheshimiwa Waziri Joseph G. Kakunda ili kuweza kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kuleta hotuba nzuri. Nampongeza pia Mwenyekiti mpya wa Bodi ya *TANTRADE* aliyechukua nafasi niliyoiacha wazi baada ya kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Buyungu. Kipekee nampongeza *Director General* wa *TANTRADE*, Ndugu Edwin Rutagezuka kwa utendaji wake mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo nipende kuchangia na kushauri katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya vitambulisho vya Taifa katika kurasimisha biashara; kwa mujibu wa Wizara ya Mambo ya Ndani, hadi sasa, vitambulisho vya *NIDA* vilivyopatikana ni takribani milioni 16 tu katika nchi nzima. Sharti la kutumia vitambulisho hivyo katika kurasimisha biashara lililowekwa na *BRELA* limezuia malalamiko kutoka

wajasiriamali wengi ambao wanashindwa kusajiri na kurasimisha biashara zao kwa kutokuwa na vitambulisho hivyo. Ushauri wangu ni kwamba, *BRELA* iendelee kutumia vitambulisho mbadala hadi hapo Serikali itakapokuwa imewapa Watanzania wote vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafutaji wa masoko ya mazao ya kilimo; masoko ya mazao ya kilimobado ni changaoto kubwa ukizingatia kwamba bei za mazao zinatawaliwa na uzalishaji katika nchi zinazotuzunguka na mahitaji yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri *TANTRADE* ijikite katika kufuatilia ubora wa mazao ya kilimo kwa matumizi ya chakula na viwanda kutafuta masoko ya mazao ya chakula, ni vema *TANTRADE* ishirikiane na Mashirika ya Kilimo na Chakula ya Kimataifa kama *FAO* na *WFP* ili kuwa na takwimu halisi za mahitaji ya mazao na kuwaelekeza wafanyabiashara kutafuta masoko hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ni muhimu *TANTRADE* ishirikiane na Wizara nyingine kama vile Wizara za Mambo ya Nje na Kilimo ili kubaini vikwazo vya usafirishaji wa bidhaa (mazao) kutoka Tanzania kwenda katika nchi nyingine ili kuviondoa. Mifano iliyopo ni pamoja na vikwazo vya kusafirisha mazao ya chakula kwenda katika nchi za Sudan Kusini kupita Uganda, Kenya, Burundi, Rwanda na *Congo DRC*. Kipekee napenda kujua *status* ya soko la muhogo la China.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzisha vituo vya kuunganisha zana za kilimo. Inakadiriwa kuwa Tanzania ina eneo la hekta milioni 44 zinazofaa kwa kilimo ambapo eneo linalolimwa hadi sasa ni kama hekta milioni 10.1 tu (*I stand to be corrected*). Hata hivyo, eneo linalolimwa kwa kutumia zana (*very roughly*) ni kama ifuatavyo:-

Eneo linalolimwa kwa jembe la mkono 70%, eneo linalolimwa na wanyamakazi 20% na eneo linalolimwa kwa matrika 10%, jumla 100%

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri, kwa kuwa ni vigumu kwa kila mkulima kumiliki trekta, ni vema Serikali ianzishe vituo vya kuunganisha, kukodisha na kuhudumia (*servicing*) vituo vya zana za kilimo, yaani *Tractor Assembling, Hiring and Service Centers*) ambavyo vinatoa huduma kwa wakulima wetu ili walime maeneo makubwa zaidi. Vituo hivyo vitasaidia pia kutoa ajira za mafundi mbalimbali watakaoandaliwa na vyuo vya ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishaji wa *Saturday Bonanza*; wakati nikiwa Mwenyekiti wa *TANTRADE*, tulikuwa na mawazo ya kuanzisha magulio wa ajili ya kuwaelimisha wafanyabiashara wasio rasmi (Almaarufu-Machinga) ili waweze kutumia viwanja vya maonesho (SABASABA-Mwalimu Nyerere) Dar es Salaam. Je, mchakato huo umefikia wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwa kutumia mfumo huo, tungeweza kuwasaidia Wamachinga na kujua wenye bidhaa wanazozuza na kuiwezesha Serikali kupata ushuru unaostahili kuliko hali ilivyo sasa mitaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kuchukua nafasi hii kuchangia Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna eneo la ardhi ya wananchi ambao wametoa ardhi yao kwa *EPZ* ambao wamechukua eneo la Kata ya Mwengemshindo katika Manispaa ya Songea, lakini wananchi hao hawajalipwa fedha zao za fidia mpaka sasa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wananchi hawa ambao wamekuwa wakisubiri kwa muda mrefu bila kulipwa fedha, walipwe ili waweze kuendeleza shughuli zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Usindikaji wa Tumbaku (*SONAMCU*) kilichopo katika Manispaa ya Songea,

mwaka jana mwezi Mei niliuliza ni lini Kiwanda cha *SONAMCU* kitaanza, majibu yalikuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshapata mwekezaji ambaye tayari ameshasaini mkataba wa kuendesha kiwanda hicho na kwamba kiwanda hicho kitaanza kufanya kazi Mwezi Agosti, 2018, lakini mpaka sasa kiwanda hiki hakijaanza; tatizo ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, tangawizi; katika Wilaya ya Songea Vijijini katika Kata ya Mkongotema, Wino, Madaba na Maweso wanalima sana zao la tangawizi ambalo limekuwa linatumika kama chakula, dawa na kadhalika. Kwa kuwa zao hili ni muhimu sana na linazalishwa kwa wingi katika maeneo niliyoyataja, Wizara hii ingetafuta namna ya kufanya au kuwasaidia wakulima hao kupata wawekezaji wa kiwanda ili waweze kuongeza thamani ya zao hili na tija kwa maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iangalie namna ya kuwawezesha wakulima wa zao la mahindi kwa kutafuta wawekezaji wa viwanda vya uchakataji wa zao la mahindi. Ni matumaini yangu kuwa Wizara ikijipanga vizuri haya yote yanawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mchango wangu huu wote uingie kwenye *Hansard*.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata fursa ya kuchangia Hotuba ya Wizara hii ya Viwanda na Biashara. Napongeza hotuba hii na naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tuna dhamira ya kweli ya kujenga uchumi wa viwanda na biashara, ni lazima tuoneshe kwa vitendo. Kwa kuanzia na mkakati wa makusudi wa kutenga bajeti kubwa na ya kutosha kukidhi mahitaji ya kujenga mazingira yote wezeshi ya uwekezaji kwenye viwanda na biashara. Bajeti inayotengwa ni ndogo na inayotolewa ni ndogo zaidi, 30% kwenye matumizi ya

kawaida na 6% maendeleo, ni ndogo mno kwa sekta muhimu kama hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujenga mazingira mazuri ya uwekezaji bado hii ni changamoto kubwa. Mwaka 2010 Serikali iliunda *task force* ya kutengeneza *roadmap* ya kuboresha mazingira ya uwekezaji baada ya kupata *rank* mbaya toka *survey* za kimataifa. Kwa hiyo Wizara nane kama Fedha, Viwanda, Kilimo, Uwekezaji, Nishati, Miundombinu, Ardhi na Maji wakapitisha *roadmap* iliyozingatia mambo yafuatayo:-

- (i) Kurahisisha utoaji wa vibali vya ujenzi;
- (ii) Ukaguzi wa maeneo ya biashara;
- (iii) Ku-*streamline* malipo ya kodi mara mbilimbili kupitia taasisi mbalimbali;
- (iv) Kuweka wathamini wa Serikali wa kikanda; na
- (v) Kupitia sheria zinazoruhusu mlolongo wa *roadblocks*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hii *taskforce*, Ofisi ya Waziri Mkuu iliratibu pamoja na wadau utayarishwaji wa mpango wa utekelezaji. Uliendelea na utekelezwaji wa maeneo yenye *quick wins*, kutengeneza mpango wa ufuatiliaji na tathmini na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, hiyo *roadmap* imefikia wapi katika kuboresha mazingira ya biashara? Sasa mwaka uliopita tukaja na *blue print* na yenyewe inatokana na *ranking* yetu kwenye *doing business* imeshuka, sasa vimefikia wapi? *Win wins* ziko wapi, mbona hali imezidi kuwa mbaya?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kurasini *Logistics Park*, huko nyuma ililenga kutumia eneo ambalo lingekuwa kitovu cha biashara kati ya China, Tanzania na nchi zote za jirani yetu hadi Afrika ya Kati, chini ya ubia wa Tanzania (*EPZA*) na

kampuni ya China. Tanzania ilikuwa kati ya nchi nne Afrika zilizoteuliwa kufaidika na uwekezaji huo na kuboresha biashara kati ya China na Tanzania. Sasa kwa nini tunabadilisha matumizi na kuingiza suala la kuunganisha magari?

Mheshimiwa Naibu Spika, majadiliano na maamuzi yanachukua muda mrefu sana, hii inakatisha tamaa wawekezaji na kuongeza gharama na kujenga mazingira ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu inayoenda kwenye viwanda vingi nchini na hata katika maeneo ambayo yamelengwa uwekezaji mkubwa mfano Mradi wa Liganga, Engaruka, viwanda vya *Coca-Cola*, *TBL*, Mbeya, Kilimanjaro na viwanda vingi vya Dar es Salaam, Chang'ombe na Keko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia katika hotuba hii. Tunapozungumzia biashara tunazungumzia uwekezaji wa ndani na wa nje, hivyo, kama ambavyo Serikali inasema kuwa inahitaji nchi hii iwe nchi ya viwanda, lazima ifahamu kuwa viwanda ni biashara na kama mazingira ya kufanyia biashara siyo rafiki, basi hata viwanda havitaweza kuwepo. Ni vizuri Serikali ikaelewa kuwa kama wafanyabiashara wa kawaida wanashindwa kufanya biashara basi tusitegemee wafanyabiashara kutoka nje kuja kuwekeza katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ifahamike kuwa biashara ni mawasiliano, kila kinachofanyika hapa kwetu kinajulikana karibu dunia nzima, hivyo, kama tumeshindwa kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji wa ndani tusitegemee kupata wawekezaji toka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema kuwa biashara zinafungwa lazima Serikali itafute namna ya kuondoa tatizo na siyo kuendelea kukomaa bila kuondoa changamoto

zilizosababisha biashara kufungwa kila mahali hapa nchini na kama tukiendelea hivyo basi tutegemee kukosa kukusanya kodi kama tunavyokuwa tunategemea siku zijazo. Hata hivyo, kibaya zaidi wafanyabiashara wengi wametimkia katika nchi jirani na kusajili biashara zao huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni Taifa gani ambalo linaweza kuendelea na kufikia uchumi wa kati kama wananchi wake hawana uwezo wa kulipa kodi na kodi zinalipwa kutoka kwenye faida? Pia kodi zinalipwa kulingana na ukubwa wa biashara, sasa kila wakati tunaishauri Serikali kuwa irekebishe baadhi ya sheria za kodi na tozo mbalimbali ili kufanya urahisi wa kufanya biashara ili mitaji ya watu ikue na kutoa nafasi kwa wafanyabiashara kuchangia pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hii haioneshi dhamira ya kuwa nchi ya viwanda, kama tunaweza kuidhinisha pesa ya maendeleo, shilingi bilioni 100 lakini pesa iliyotoka mpaka sasa ni bilioni 12 halafu unasema tuko tayari kuwa nchi ya viwanda, huo utakuwa uongo mchana kweupe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Benki ya Dunia kuhusu urahisi wa kufanya biashara duniani, Tanzania sasa ni ya 137 kati ya nchi 190 duniani na changamoto zilizotajwa ni pamoja na kodi ambazo siyo rafiki kufanya biashara na ugumu wa kuanzisha biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali hii tangu imeingia madarakani imekuwa haiwaamini tena wafanyabiashara, imewapa majina mengi sana kama wizi, mara wapiga dili, yote hayo yanaonesha kuwa Serikali haitambui kuwa wafanyabiashara ni wadau muhimu kabisa katika Taifa hili na kama mpaka leo Watanzania wamewapa madaraka haya haitambui hilo, basi Taifa hili ni haki linavyoangamia kwa wafanyabiashara kuitwa majina haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo matukio ambayo yametokea hivi karibuni kwa wafanyabiashara wa maduka ya kubadilishia pesa za kigeni kufungwa na pia kuondoka

na pesa pamoja na vitendeakazi, Watanzania wanataka kujua je, ni kwa nini Serikali ilifunga maduka hayo na kuchukua pesa zilizokuwa katika maduka hayo na je hiyo ndiyo elimu kwa walipakodi hao?

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitegemea taarifa kutoka Serikalini sababu ya kufunga maduka hayo ambayo yameanzishwa kwa mujibu wa sheria ya nchi na kama kulikuwa na tatizo Serikali inawasaidiaje hawa wafanyabiashara? Pia taarifa ilitoka kuwa Serikali kwa sasa imeelekeza wapi huduma ya kubadilishia pesa itatolewa? Je, katika nchi hii hakuna tena mtu kufungua duka la kubadilishana pesa za kigeni? Kama ndivyo katazo hilo liko kwa mujibu wa sheria ipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo yote ni mambo yanayoiweka nchi yetu katika mtazamo mbaya wa kuonesha jinsi Tanzania isivyokuwa nchi salama katika kufanya biashara. Pia kama kuna pesa zilizochukuliwa kutoka katika maduka hayo ya kubadilishana pesa ni shilingi ngapi? Je, ni wafanyabiashara wangapi wanafikishwa mahakamani na kwa kosa gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashuhudia pia wafanyabiashara mbalimbali wakisota mahabusu kwa muda sasa, je, Serikali inajua kuwaweka ndani wafanyabiashara bila taarifa yoyote kwa umma ni kuendelea kuongeza hofu kwa wafanyabiashara mfano Yusuph Manji, Lugemalira na wengine wengi bila taarifa rasmi za wazi kwa umma ili umma ujifunze na kujua kinachoendelea juu ya wafanyabiashara hao? Je, Serikali inaweza kutufahamisha ni wafanyabiashara wangapi wako rumande kwa kosa la kutakatisha fedha? Je, Serikali imepata faida gani katika kuwakweka rumande wafanyabiashara hao?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali isiyo ya kawaida bado Serikali haikubali kuwa sasa Tanzania siyo sehemu salama kwa kufanya biashara, ukienda Kariakoo sasa utaona vyumba vimefungwa na vimebandikwa matangazo chumba kinapangishwa. Jambo hilo hapo awali halikuwepo kabisa

na ni kwa sababu wafanyabiashara wameshindwa kufanya biashara. Kuna kikosi kimeanzishwa kinaitwa *task force*, hiki kinakaa nje ya maduka na kukamata mtu anayetoka kununua mzigo katika maduka na kuuliza risiti, baadaye huwanyang'anya mizigo na kuutaifisha na kumtoza mwenye duka faini ya milioni tatu au zaidi na muda mwingine hupokea rushwa ya kati ya milioni moja au milioni moja na nusu na kumalizana na mfanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo faini ya milioni tatu imeongeza rushwa kwa hiyo *task force*, lakini pia imepelekea wageni kunyang'anywa mizigo na sasa stoo za *TRA* Dar es Salaam zimejaa mizigo ya wafanyabiashara hao wageni na baada ya muda *TRA* huipiga mnada mizigo hiyo. Kitendo hiki kimesababisha wafanyabiashara kutoka Congo, Zambia na kadhalika kuacha kuja Dar es Salaam kununua.

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Naibu, nashukuru sana nami nichangie katika Wizara hii muhimu ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, COSOTA; kwanza kabisa ningependa kuishauri Serikali ihamishe *COSOTA* kutoka kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara na kuipeleka kwenye Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Hii itasaidia sana kuifanya kuwa kwenye Wizara inayohusiana kabisa na masuala yao ya sanaa ambayo ni Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, changamoto inayowakabili wasanii wa nchi hii ni wizi wa kazi za wasanii na sheria inayolinda kazi za wasanii Sheria Na.7 ya mwaka 1999 imepitwa na wakati na kwa kweli imekosa meno kabisa na imeshindwa kabisa kuwalinda na kuwasaidia wasanii wa Tanzania ambao kila kukicha kazi zao zinaibwa na kuuzwa kiholela na hakuna sheria inayowabana wezi wa kazi za wasanii. Naiomba sana Serikali kama kweli inataka kuwasaidia wasanii wa Tanzania basi iilete hapa Bungeni Sheria ya Hati Miliki na Haki Shiriki Na.7 ya mwaka 1999 tuifanye marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vidogo vidogo vya kuchakata mazao ya kilimo na vya kuchakata mazao ya mifugo; Jimbo la Mikumi linalima sana mazao mbalimbali, lakini tuna tatizo kubwa sana la viwanda vidogo vidogo vya kuchakata mazao hayo ambayo yangeweza sana kutoa nafasi kwa wananchi wa Mikumi kuweza kupandisha thamani ya mazao yao kwa kuyachakata kwenye viwanda hivyo. Naiomba sana Serikali iweze kulitilia mkazo hili ili tuweze kuwasaidia wakulima wetu ambao wanalima kwa bidii zote, lakini masoko yamekuwa ni kitendawili kikubwa sana kwao, hasa kwenye Kata za Tindiga, Kilangali, Kisanga, Uleling'ombe, Mhenda, Ulaya, Masanze, Zombo, Vidunda, Ruhembe, Mikumi, Kidodi, Mabwerekwere na Kata ya Malolo. Hivyo tunaomba sana Serikali iangalie suala hili muhimu kwa kutusaidia tupate viwanda vidogo vya kuchakata mazao ya kilimo na viwanda vya mazao ya mifugo kama viwanda vya nyama, ngozi, maziwa na kadhalika ili tuweze kuwasaidia wakulima na wafugaji wa Jimbo la Mikumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Naibu Spika, *service levy* imekuwa kero kwa wafanyabiashara iondoshwe haraka, hakuna mkakati mkubwa wa kusaidia kilimo kwa lengo la kufungamanisha uchumi wa viwanda na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya umeme inaendelea kuwepo kwani, kuna kupungua na kuongezeka umeme hasa eneo la Ukanda wa Pwani kiasi cha kuathiri viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, chuma cha Liganga na Mchuchuma, ndiyo namna pekee ya kuendeleza mradi wa *SGR*, vinginevyo tutapoteza fedha nyingi kununua chuma, kutoka Japan, Serikali iangalie na kuufanya mradi huu wa kipaumbele kati ya vipaumbele vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutekelezwa Mradi wa Bagamoyo wa *SEZ*; Serikali lazima ije na kauli moja juu ya

hatma ya Mradi wa Bandari ya Bagamoyo, Serikali lazima ione *economic impact* ya kuanzisha mradi huu mkubwa kwa Taifa. Ni rai yangu Serikali ijifunze na kupembua ni ipi miradi ya mkakati na ianze nayo badala ya miradi mingine, ambayo tija yake inategemea miradi mingine, mfano *SGR*, inategemea ufanisi wa bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya korosho ni rai yetu kuwa wakulima wote watahendewa haki katika kwa malipo stahiki ya mazao yao. Aidha, natoa rai kwa Serikali kuendelea na kuhakikisha mambo haya hayajitokezi tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Nchi ya Uchumi wa Viwanda; haiko *clear*, ni rai yangu Wizara itakamilisha suala hili haraka. Sera hii ijibu masuala ya *PPP* mazingira ya kufanyia biashara, elimu za biashara na kadhalika.

148 -**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, kwanza kabisa kuipongeza Wizara husika kwa juhudi zao katika kuinua Tanzania ya viwanda na hata kueneza falsafa ya Tanzania ya Viwanda. Hili ni jambo ambalo mimi binafsi naona ni vyema kupongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujikita kwenye maeneo mawili. Mosi, utekelezaji wa mradi wa makaa ya mawe Liganga na Mchuchuma, pamoja na ushiriki wa vijana kwenye uchumi wa viwanda na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapofanya mapitio ya *report* ya Wizara, *page* ya 15 sura ya 28, 29 na 30, nadiriki kusema Wizara ya Viwanda na Biashara pengine iridhie kuendesha sehemu ya sentensi inayosomeka kwenye sura namba 29 ambayo kwangu naona ni upotoshaji mkubwa kwa Taifa, hasa tunapofanya marejeo ya Ilani ya Chama Tawala sambamba na utungwaji wa sheria mbili za ulinzi wa maliasili za nchi (*Natural wealth Resources Permanent Sovereignty Act, 2017*) pamoja na Sheria ya *Natural Wealth and Resources Contract Review Renegotiation of Unconscionable Terms 2017*).

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema ama naishauri Wizara kufuta kipengele hiki chote kwa sababu moja; sababu za mkandarasi kuomba vivutio vya ziada hauna nafasi kwenye sheria zote mbili, kwa sababu sheria hizi mbili au hususan Sheria inayohusu mapitio ya mikataba yenye masharti hasi, hakuna mahali popote inapo-*deal* na maombi ambayo yako nje ya mkataba. Ikumbukwe na kama ilivyoandikwa na Wizara ukurasa wa 15, ombi la mwekezaji la kuomba vivutio vya ziada havikuwepo kwenye *terms* za mkataba, kwani hii ni *addition incentives* na siyo sehemu ya mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inapotosha kwa kueleza Umma na Watanzania kwamba mkataba wa Liganga na Mchuchuma umekwama kwa sababu moja ya matakwa ya sheria zote hizi mbili; ni pamoja na kufanya mapitio ya mkataba kati ya *NDC* na Sichuan Hangda *Group* na kwamba baada ya Mkandarasi kutaka vivutio vya ziada hii imesababisha Wizara kufanya mapitio ya mkataba. Huu ni uwongo kwa sababu tunapofanya *Part III* inayoeleza *procedure on how to deal with the Review Renegotiation of Unconscionable Terms*, imeweka bayana utaratibu wa kisheria utakaotumika kufanya mapitio haya ya mikataba yote iliyoonekana kuwa na masharti hasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, najjuliza, inakuwaje leo Wizara inatuambia kutokana na masharti hasi ya mkataba wa Liganga na Mchuchuma, basi mchakato wa kufanya mapitio unaendelea na angali jukumu hilo ni la Bunge? Naishauri Wizara irejee sheria ya masharti hasi Ibara ya 4(1) – (5), inasema bayana kwamba jukumu la kufanya mapitio ya mikataba hasi ni la Bunge. Rejea pia Katiba ya Nchi Ibara 63(2), hii ni kwa kuwa mradi wa Liganga na Mchuchuma hauna unyeti wowote (*sensitivity*) kama ambayo ingekuwa ni mradi wa chini ya Taasisi ya Idara za Usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wizara husika imetuambia kuwa mchakato wa mapitio ya mkataba wa Liganga na Mchuchuma unaendelea: Je, ni lini Bunge lako Tukufu liliwahi kutoa azimio la mapitio ya mkataba wa

Liganga na Mchuchuma? Kwani ukirejea mkataba wa masharti hasi, ni lazima Bunge lako litoe azimio la kufanya mapitio ya Liganga na Mchuchuma, kitu ambacho hakikuwahi kutokea. Sasa ni kwa nini tunaambiwa mchakato unaendelea? Rejea *Part II 5(3) of this Act*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaongelea umuhimu wa kuendelezwa kwa mradi wa Liganga na Mchuchuma kwa sababu vijana wetu hawana ajira na pia ukiangalia pamoja na chuma kinachozalishwa nchini, Tanzania ni asilimia 80 na asilimia 20 tu ndiyo inayoagizwa nje ya nchi, lakini bado ajira hailindwi. Kati ya ajira 23,150,000, ajira 20,000,000 zote ni ajira za muda ambapo ajira za muda mrefu ni 3,150 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye mchango wangu wa ushiriki wa vijana kwenye Sekta ya Biashara na Viwanda, ikumbukwe Bunge lako hili Tukufu lilipitisha kusudio la kushirikisha vijana kwenye zabuni (*tenders*) ambapo vijana walionekana wenye kuwapa nafasi/dirisha maalum ili waweze kushiriki rasmi kwenye michakato ya zabuni, lakini swali langu kwa Wizara: Je, ni kwa nini kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri hakuna taarifa yoyote inayohusu ushiriki wa vijana kwenye Sekta ya Viwanda na Biashara?

Mheshimiwa Naibu Spika, nchini Kenya upo mfuko maalum *Youth Enterprises Development Fund* ambapo vijana wenye umri kati ya miaka 18 - 35 walihusishwa kikamilifu. Haitoshi, pia nchi ya Kenya imekuwa ikitenga kiasi cha fedha kwenye kila Bajeti yao ya mwaka wa fedha ambapo *five years back* mfuko huu ulikuwa na *USD 940,000*. Malengo ya mfuko huu ni pamoja na kutoa *startup capital, create Mark space and incubators for young graduates and dropout students*.

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika nchi yetu ya Tanzania chini ya Wizara hii imekuwa na Mfuko wa Maendeleo ya Wajasiliamali Wachanga (*NEDF*) ambapo *last financial year* ilitengwa shilingi bilioni 15 ambayo haikuwahi kutoka hata senti moja. Ushauri wangu kwa Serikali, iweze kutoa fedha angalau asilimia 50 ya fedha ya maendeleo.

Last financial years kati ya shilingi bilioni 100 ilitoka shilingi bilioni 12, fedha za maendeleo. Serikali ikiweza kutoa *at least* asilimia 50 ya fedha za maendeleo, basi Mfuko wa *NEDF* uongezewe fedha hata kufika shilingi bilion 50 - 100 ili vijana wengi zaidi waweze kupata *start up capital* na hata suala la uhaba wa ajira uondoke.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja na kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza kwa kazi nzuri Mheshimiwa Waziri, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la shamba la mpira Muheza na Kiwanda cha *General Tyre*, Arusha. Napongeza kwa kuonekana kwa dalili za kupatikana kwa mwekezaji za kupatikana kwa mwekezaji wa kiwanda cha matairi. Nimefika na Kamati ya Bajeti na kuona kiwanda hicho, kwa kweli hakuna kiwanda pale, maana mwekezaji mwenyewe anapaswa kutoa mashine zote za zamani na atapaswa kuweka mashine nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kushauri kwamba kutokana na Muheza kuwa na shamba kubwa la mpira ambalo hapo awali lilikuwa linalisha kiwanda hicho bora, kiwanda hicho kijengwe kwenye maeneo hayo hayo ya shamba husika. Tutakuwa tayari kutoa eneo kubwa kwa ujenzi wa kiwanda hicho. Naomba wazo hili lipewe uzito wake au atafutwe mwekezaji mwingine atakayewekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu biashara. Hivi karibuni Kamati ya Bajeti ilikuwa Kampala, Uganda. Kule tulikuwa wafanyabiashara wengi wa Kariakoo na wengine wa nchi jirani, wakinunua vitu mbalimbali na kuvirudisha nchini au nchini mwao. Wafanyabiashara wote hao walikuwa na biashara zao Kariakoo na sasa wamehamia Kampala.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba Wizara ijaribu kuchunguza kuona ni jambo gani lililowafanya wafanyabiashara hao kuhama? Vile vile iangalie uwezekano wa kuwarudisha.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwa kuunga mkono maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na nishauri Serikali ipitie hotuba hiyo kwa umakini, kwa umuhimu na kuchukua yale ambayo yatasadia Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni miaka mingi sasa Serikali imekaa kimya na haitoi suluhisho la ubinafsishaji viwanda nchini hasa Mkoani Morogoro. Mfano, Kiwanda cha Mazulia Kilosa, Kiwanda cha *Spare Parts* Mang'ula, Kiwanda cha Moprocco na viwanda vingi ambavyo vilipewa wawekezaji na kuviondolea mashine na kubadilisha matumizi ya viwanda hivyo. Hii inaondoa ajira kwa Watanzania, inakosesha soko la mazao ambayo yangetumika viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, napenda kupata majibu ya Serikali, ni viwanda vingapi vilivyobinafsishwa na kushindwa kuviendeleza/kubadilishiwa matumizi na hatua zilizochukuliwa Mkoani Morogoro?

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara nchini Tanzania imekuwa ni maumivu makubwa kwa wafanyabiashara ndogo na kubwa. Mtu akitaka kuanzisha biashara anatakiwa kulipa kwanza kodi inayokadiriwa kwa mtaji alionao. Hata kama biashara imepata hasara au haikupata faida, lazima kodi aliyokadiriwa ilipwe. Je, kwa nini kodi isilipwe kutokana na faida?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna vyo vya biashara (*CBE*) na kwa kuwa kuna wahitimu wanaohitimu: Je, Serikali haina haja ya kuwaunganisha wahitimu hao na wafanyabiashara wakubwa nchini ili nao wawe wafanyabiashara na kuliingizia Taifa kipato? Je, ni lini Wizara itawafikia wanyabiashara wakubwa na wadogo ngazi za

wilaya na mikoa ili kupata changamoto zao na namna ya kuzitatua?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara ichukue hatua ya kukaa na Wizara ya Fedha ione namna bora ya utozaji kodi mbalimbali ili kukuza biashara nchini na kuepusha ufungaji wa biashara nyingi hasa za watu wa kati. Ahsante.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuwapongeza viongozi wa Wizara hii. Mheshimiwa Kakunda Waziri wa viwanda na Biashara na Naibu wake Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utahusu maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni tozo ya usafirishaji kwa wafanyabiashara. Kuna malalamiko ya wafanyabiashara kuwa na tozo nyingi na taasisi nyingi za udhibiti. *SUMATRA*, Zimamoto, *TFDA*, *OSHA*, *TRA*, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, *WCF* na zinazofanana na hizo. Tozo zifuatazo; *Corporate Tax*, *Service Levy*, *OSHA*, *TFDA*, *TBS*, tozo ya ukaguzi wa Zimamoto, nashauri kuwe na kituo kimoja cha ulipaji tozo hizo na taasisi zipunguzwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri viwanda vya korosho vilivyobinafsishwa vifufufuliwe na vifanye kazi ya kubangua korosho. Wanunuzi wengine wanafanya maghala, nashauri wanyang'anywe. Tuwe na mkakati mahsusi wa muda mfupi wa kuuza nje korosho zilizobanguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SIDO* ni taasisi ambayo inaweza kuwakomboa wakulima na wajasiriamali wengine katika kutoa teknolojia mpya katika uzalishaji. Naomba taasisi hii ipewe fedha za kutosha ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi. Pia maonyesho ya *SIDO* yaboreshwe na teknolojia zinazotumika ziwe za kisasa. Aidha, kuwe na utaratibu wa kuwasilisha teknolojia hiyo kwa wakulima au wajasiriamali wa vijijini.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa shukrani na sifa kwa Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii kuweza kuchangia kwa maandishi katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa hongera na pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Morogoro miaka ya nyuma ulikuwa mkoa wa viwanda. Hivi ninavyochangia sasa hivi, viwanda vingi vya zamani vilivyokuwa vinafanya kazi, vimekufa, havifanyi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hoja yake, wananchi wote hususan wa Mkoa wa Morogoro atueleze hatima ya viwanda hivi ambavyo vimekufa na havifanyi kazi tena kama Kiwanda cha Ngozi, *Ceramics* na Magunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Serikali kwa kuanza ujenzi wa viwanda nchini Tanzania. Pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa mkakati mkubwa wa ujenzi wa viwanda. Tanzania ya viwanda inawezekana. Viwanda vingi na hasa vidogo na vya kati vimeanza kujengwa katika mikoa yetu yote ya Tanzania. Naamini hata tatizo la soko la mikunde ikiwepo mbaazi, litapatikana hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi hizi kwa Serikali, kwani kiwanda cha mikunde/mbazi kimepewa kipaumbele, kimejengwa kiwanda cha kununua na kuchakata mikunde. Kiwanda hiki kimejengwa na wawekezaji kutoka India. Kimejengwa Kata ya Mtego wa Simba, Wilayani Morogoro Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu Mradi wa Mchuchuma na chuma cha Liganga. Mradi huu una manufaa sana kwa nchi yetu. Umechukua muda mrefu. Ni miaka wingi sana tangu mradi huu umeanza, mpaka sasa

hivi Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake anasema, mchakato wa kupitia upya mkataba kati ya *NDC* na *Sichuan Hongda Group* unaendelea. Sasa ni muda muafaka mradi huu ufike mwisho, kusudi uweze kuianufaisha nchi yetu, waanze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, fursa za masoko kwa wajasiliamali wadogo na wa kati, akina mama/wanawake wengi wamejikita sana katika biashara ya usindikaji, nguo na kazi za mikono.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo wanalokumbana nalo ni upatikanaji wa soko/masoko ya uhakika. Mheshimiwa Waziri mkakati wa kuwatafutia masoko kwa uwazi na uhakika ni muhimu ili kuinua uchumi wa familia zao na nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri jambo hili uliangalie sana ili kuwasidia wananchi wanaojishughulisha wakiwa na nia moja ya kuinua uchumi wa familia zao na uchumi wa nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. MARY D. MURO: Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali juu ya mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara ni ndogo jambo linalosababisha mazingira magumu ya utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishauri Serikali juu ya Mradi wa *Bagamoyo Special Economic Zone*. Mradi huu umeingiza hasara kwa kutokutekelezwa mpaka sasa. Tukumbuke kuwa fidia kubwa imelipwa ikiwa ni fedha za

walipa kodi na ni muda mrefu. Je, hiyo fedha ingeingizwa kwenye mradi mwingine, tungekuwa wapi sasa hivi? Fedha nyingi zimetumika kwenye kuhakikisha kuwa mradi huu unalitoa Taifa letu hapa lilipo kuelekea uchumi wa kati kwa kuifanya reli kupokea mzigo mkubwa toka bandarini kubeba na reli zetu kuelekea kwenye nchi nyingi zisizo na bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Bagamoyo na Mkoa wa Pwani walitoa maeneo yao wakijua kuwa nao vipato vyao vitaongezeka kwa bandari hiyo kujengwa, kwani wangepata ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, tozo za *TFDA* zinatozwa kwa fedha za kigeni na kwa kila *product* inayotengenezwa nembo yake na kwa gharama kubwa. Hivyo, tunawavunja moyo wajasiriamali wadogo ambao ndio kwanza wanajikusanya kwa mitaji midogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni *TRA*. Naomba kuishauri Serikali kuacha kutoza kodi *on capital basis* kwani unamkadiriaje mteja anayeanzisha biashara wakati hajaanza biashara? Hii imefanya watu wengi kushindwa kuendeleza biashara zao, kwani mitaji yao inakuwa imemezwa kwenye kodi kabla ya biashara kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni ufungaji biashara. *TRA* badala ya kujadili na wafanyabiashara ndipo wafunge au wapewe muda wa kulipa kidogo kidogo wanafunga biashara. Hii ni kuipa hasara Serikali.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuwepo Bungeni leo na kuchangia Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuiomba Serikali yetu sikivu kutoa msamaha (*exemption*) au kuruhusu taasisi ambazo wameagiza tende kama chakula kwa kutoa msaada kwa watu masikini wenye mahitaji. Naamini ombi langu litakubaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie biashara katika Tanzania. Wafanyabiashara nchini Tanzania ni sawa na wale wanaofanya biashara katika nchi nyingine; na kazi ya biashara ni kununua na kuuza, pamoja na kulipa kodi katika idara husika, mfano *TRA*. Wafanyabiashara wa Tanzania wamekuwa kila mara wakilalamikia mifumo ya kodi ambayo siyo rafiki kwa wafanyabiashara wenyewe na biashara zao. Tanzania kuna utitiri wa kodi. Utitiri huu wa kodi unasababisha wafanyabiashara kujiona wanaifanyia kazi Serikali kwa kuwa katika mapato. sehemu kubwa ya mapato inabidi kulipia kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe wafanyabiashara kote duniani wanafanya biashara ili wapate faida baada ya kulipia gharama za uendeshaji kama mishahara ya wafanya kazi, gharama za umeme na maji, kodi na tozo mbalimbali (Serikali Kuu na Halmashauri), michango mbalimbali katika taasisi, fremu ya biashara ilipo biashara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mfanyabiashara kuona hana anachopata katika biashara, anachobaki nacho anaona bora afunge biashara kwa kuandika barua ya kufunga biashara kwenda *TRA* ili wasiendeele kutozwa kodi. kufuatia jambo hili, mapato ya Serikali yanapungua na hatimaye wafanyabiashara wanahamia nchi jirani ambapo wanaona kuna masharti nafuu ya kufanya biashara. Mfano wafanyabiashara ya nguo, wanaona ni nafuu kufanya biashara nchini Uganda, wanaanzisha maduka ya jumla na rejareja kisha wafanyabiashara wadogo wanakwenda kufuata nguo Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni bidhaa kutoka Zanzibar kuja Tanzania Bara. Pamekuwepo na sintofahamu ya hali ya juu kwa bidhaa kutoka Zanzibar kwa kulipiwa kodi mara mbili. Kwa mfano, ukinunua sukari Kiwanda cha Mahonda ukija nayo Tanzania Bara unatakiwa uilipie tena kodi. Swali; je, nikinunua sukari *Mtibwa Sugar*, Kilombero, *Kagera Sugar* au Kilimanjaro *TPC*, kwa nini hailipiwi ushuru? Au tatizo ni kuvuka bahari?

Mheshimiwa Naibu Spika, bidhaa zinazotoka Zanzibar zinasaidia kupunguza ukali wa mfumuko wa bei na pia bei rahisi na hupunguza baadhi ya kero ya upungufu kwa baadhi ya bidhaa. Hivyo, bidhaa za Zanzibar ziwe huru. Hata sera ya kulinda viwanda vya ndani bado itafanya vizuri na haitaathirika kwa bidhaa toka Zanzibar. Ni ajabu hata redio na TV moja pia inabidi ilipiwe kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanga ulikuwa ni Mji wa viwanda tokea katika zaa za ukoloni, lakini hata katika miaka ya 1970 mwanzoni mwa uhuru hadi miaka ya 1993 ndipo mambo yalipoanza kuharibika, hususan baada ya kuanza kubinafsisha (*privatization*) mashirika na makampuni ya Serikali. Tanga kulikuwa na viwanda vifuatavyo: *Steel Rolling Mill* (chuma), *Foma Detergent*, *Amboni Plastic*, *Sikh Saw Mills*, *Tanganyika Blanket*, *Mkumbara Cheapboard*, *TIP Soap Company*, *Tanga Dairy*, Kiwanda cha Kamba Ngomeni, *Tanzania Fertilizer Company*, *Tanga Nicolln* (*coconut oil production*) na *CIC Textiles*.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vyote hivi vimekufa, vimeuliwa kwa kuwauzia wafanyabiashara ambao hawana uwezo wa kuviendesha. Tujjulize, viwanda hivi vilijiri Watanzania wengi mno, leo Watanzania (wafanyakazi) wako wapi? Kutofanya kazi kwa viwanda hivi ni dhahiri mzunguko wa fedha, ajira na maisha ya watu wa Tanga yameathirika sana. Nataka kujua, Serikali (Wizara) imejipangaje kufufua viwanda hivi au kuvichukua kwa wawekezaji walioshindwa kuviendeleza viwanda hivi?

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni upatikanaji wa vibali/leseni. Ni rahisi kwa ngamia kupenya kwenye tundu la sindano kuliko kuanzisha viwanda Tanzania, kwa sababu kuna vikwazo na vipingamizi na visingizo vingi unapotaka kuanzisha kiwanda Tanzania. *OSHA*, *TBS*, *TFDA*, *NSSF*, *EWURA*, *NEMC* na *SUMATRA*, hivi vyote ni vingi vinavyowaudhi/kusumbua wafanyabiashara wanaotaka kuanzisha viwanda Tanzania. Nashauri, hebu viondolewe na zibaki taasisi mbili tu badala ya utitiri wote huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni biashara ya usafirishaji mabasi. Jana, tarehe 14 Mei, 2019 wasafirishaji wa mabasi na madereva wameandaa mgomo wa kutosafirisha abiria nchi nzima kupitia vyama vyao kuwa kuanzia leo, tarehe 15 Mei, 2019 hawatafanya safari kwa mabasi yao na madereva hawataendesha mabasi. Hii ni kutokana na kero ya *Traffic Police* kuwatoza faini zaidi ya mara tatu kwa safari moja ya Tanga – DSM, Tanga – Arusha na mikoa mingine nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wito wangu ni kwamba Serikali itambue kuwa wenzetu hawa (wasafirishaji) wanaisaidia Serikali kuwahudumia Watanzania, hivyo waondoe faini/vikwazo visivyo na ulazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara ya boda boda nayo ni miongoni mwa biashara zinazotoa huduma kwa Watanzania katika Sekta ya Usafirishaji. Ni moja ya sehemu ambapo imeweza kuondoa kero maeneo ya mijini na hasa vijijini. Changamoto ya biashara hii nayo inawekewa vikwazo na vikorombwezo vingi kama zilivyo biashara nyingine na kufanya mazingira ya biashara kuwa mabaya. Wamewekewa *SUMATRA*, *TRA* (mapato), Halmashauri na *traffic sticker*. Vyote hivi inabidi bodaboda alipie kodi na tozo. Ukiangalia kwa kina, nayo inaonekana ni usumbufu. Ingetakiwa walipe sehemu moja tu kama *SUMATRA* au *TRA* tu na kuondoa ukiritimba uliopo.

MHE. SUZANA C. MGONUKULIMA: Mheshimiwa Naibu Spika,, Mradi wa Liganga ni miongoni mwa miradi ya kimkakati na ulianzishwa kwa lengo la kujenga kiwanda cha kufua chuma. Utekelezaji wa mradi huu umechukua muda mrefu, takribani miaka nane bado haujaanza. Kamati ilijulishwa na Wizara juu ya tathmini waliyoifanya katika bidhaa za chuma na kubaini kuwa vinakumbana na changamoto ya upatikanaji wa malighafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nia ya Serikali ya nchi yetu ya Tanzania ni kuwa nchi ya viwanda, kuna kila sababu kwa Serikali kuhakikisha inajipanga kukamilisha mradi

huu wa Liganga ili chuma kinachopatikana iwe malighafi ya viwanda vyetu hapa nchini. Kwa kufanya hivyo, mapato yataongezeka na hivyo basi, tutakuza uchumi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tufikie malengo ya nchi yetu ya viwanda, Sekta ya Kilimo lazima iboreshwe. Hakuna viwanda bila kilimo. Hadi sasa Sekta ya Kilimo imesahaulika kabisa, pembejeo hazipunguzwi ruzuku ili wakulima wote wapate pembejeo na kwa kuwa asilimia 75 ya Watanzania ni wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na utoaji wa vitambulisho kwa wajasiriamali kwa utaratibu mpya, Serikali inapoteza mapato. Mjasiriamali ambaye alikuwa analipa ada/ushuru wa shilingi 500/= kwa siku kulingana na biashara yake, itamlazimu kwa mwezi kulipa shilingi 15/= ukizidisha kwa miezi 12 sawasawa na mwaka mmoja mjasiriamali huyu atalipa jumla ya shilingi 180,000/=. Kitambulisho hiki kinatozwa shilingi 20,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hesabu ya kawaida $180,000 - 20,000 = 160,000$. Ukichukua wafanyabiashara wadogo wadogo, wapo wengi sana hivyo kwa kutumia njia hiyo Serikali inapoteza mapato makubwa sana. Serikali ijitathmini kuendelea na mpango huu au kubadilisha ili Serikali iendelee kupata mapato kutokana na tozo za mauzo ya ujasiriamali.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wake wa dhati wa kutekeleza Sera ya Tanzania ya Viwanda. Mara baada ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 viwanda nchini vimeendelea kuongezeka kwa kasi kubwa na vya zamani vimeendelea kufufuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara na Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanazozifanya usiku na mchana. Mwenyezi

Mungu aendelee kuwajalia afya njema katika kusimamia utekelezaji wa Sera ya Tanzania ya Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya Waziri na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara ni kutengeneza mazingira ya watu wanaotaka kuwekeza kwenye viwanda na biashara nchini. Kazi hiyo inaendelea vizuri na kwa weledi mkubwa. Wawekezaji wengi wa nje na ndani ya nchi wanapenda sana kuwekeza nchini lakini kuna shida ya usumbufu wa kupata vibali mbalimbali vya kuanzisha viwanda na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara ione umuhimu wa kuunganisha baadhi ya vibali au kodi. Pia vibali au kodi hizo zilipwe kupitia ofisi moja. Mfano wa kodi au vibali hivyo ni kama vile *TFDA*, *NEMC*, *OSHA* na kadhalika. Mwekezaji anapoenda kutafuta vibali hivi avipate kwenye ofisi moja. Tuwe na jengo moja la uwekezaji na biashara. Hali iliyopo sasa imewakatisha tamaa wawekezaji na wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Ubinafsishaji nchini ilitekelezwa kwa shinikizo la Mataifa ya kibepari. Hivyo Tanzania ilitekeleza sera hiyo bila kuwa na uzoefu wa kutosha. Zoezi zima la ubinafsishaji halikufanyika kwa umakini na usahihi uliohitajika. Matokeo yake kuna mali za Vyama vya Ushirika ziliuzwa kwa wafanyabiashara bila hata kushirikisha Wanaushirika. Pia kuna maeneo viongozi wachache waliuza mali hizo bila ya vielelezo. Mfano fedha zilizopatikana hazijulikani zillirejea kwenye akaunti ipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri ni Kiwanda cha Chai cha Lupembe. Kiwanda hiki kilikuwa ni kiwanda chenye umiliki wa asilimia 100 ya wakulima wa chai kupitia ushirika wao wa *MVYUULU*. Baadaye miaka ya 1970 Serikali ilipewa kuendesha kiwanda hiki lakini baadaye Serikali ambayo ilipewa jukumu la kukiendesha tu, ikamwuzia mwekezaji bila kufuata taratibu na kusababisha mgogoro ambao una miaka 12. Ushauri wangu ni kwamba ni vizuri Serikali ikatatue migogoro kama hii mapema ili viwanda hivi viendelee kuzalisha kwa tija kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Liganga na Mchuchuma ni muhimu sana kwa maendeleo ya viwanda nchini. Mradi wa Liganga ukikamilika tutatatua tatizo la kuagiza chuma nje ya nchi. Tutapata fedha za kigeni na chuma tutapata kwa bei rahisi. Nchi ya Ujerumani ilifanya mapinduzi makubwa ya viwanda miaka ya 1870 baada ya kuanza kuzalisha chuma na makaa ya mawe. Pia uwepo wa makaa ya mawe Mchuchuma utasaidia kupata nishati ya kutosha na ya bei nafuu. Hivyo mradi huu ni wa muhimu kwa maendeleo ya viwanda nchini. Ni vizuri Serikali ikaona umuhimu wa kuutengea fedha za kutosha na uweze kuanza mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Bagamoyo *SEZ* kama ilivyoielezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ni wa muhimu katika kufungua fursa za kiuchumi. Pamoja na umuhimu wake, ni muhimu sana kupitia mikataba tutakayoifunga na mwekezaji isije ikatokea kama ilivyo kwenye nchi za Zambia, Sri Lanka, Eritrea na Namibia. Hivi sasa nchi hizo zimejikuta ardhi yao inamilikiwa na China. Mikataba mibovu itatuingiza kwenye Ukoloni Mamboleo. Naishauri Serikali tuendeele kupitia kwa umakini mikataba tunayotarajia kuifunga na wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vidogo vidogo (*SIDO*). Viwanda hivi ni vya muhimu sana kwa maendeleo ya viwanda na ukuaji wa uchumi wa nchi. Viwanda hivi ndivyo vinavyoajiri watu wengi nchini. Serikali ione umuhimu wa kuongeza bajeti. Nchi zote zilizoendelea duniani zilianza na kuimarisha viwanda vidogo vidogo. Naishauri Serikali iweke utaratibu wa kutoa mikopo kwa watu au vikundi vyenye nia ya kuanzisha viwanda vidogo vidogo ili mazao yanayozalishwa yaweze kuongeza thamani kupitia viwanda hivi vya *SIDO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuunga mkono hoja.

MHE. GIMBI D. MASABA: Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 27 Kamati ya Viwanda ilikutana na

wafanyabiashara wa makampuni kama zaidi ya 23. Katika kikao hicho, changamoto za mlundikano wa kodi zilitawala sana ila naomba nibebe haya machache kuhusiana na viwanda vya ndani vya kuyeyusha chuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji wa viwanda 16 vya chuma nchini ni dola milioni 170.3 ambayo ni takribani shilingi bilioni 392 na vinatoa ajira kwa Watanzania 25,913. Uwezo wa viwanda hivi kuzalisha kwa mwaka ni tani 1,082,700. Uzalishaji wa sasa ni tani 240,336 sawa na 22% tu na shida kubwa imeelezwa ni uhaba wa chuma nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, akiba ya chuma tuliyonayo kama nchi ni tani milioni 126 ambazo zinaweza kuchimbwa *metric ton* milioni tatu kwa zaidi ya miaka 100 ambapo uhitaji wa chuma wa Taifa ni *metric ton* 440,336 ukiondoa chuma kwa ajili ya *SGR* ambapo hata nati moja inatoka Uturuki ambapo Afrika Mashariki pekee kwa mwaka inaingiza chuma chenye thamani ya dola bilioni 1.5 sawa na trilioni 3.3 thamani ya kiwanda cha makaa ya mawe na chuma cha Liganga na Mchuchuma ni dola bilioni 2.9 sawa na shilingi trilioni 6.38 fedha ambayo tunairudisha kwa miaka miwili tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania kwa mwaka inaingiza chuma zaidi ya *metric ton* 200,000 sawa na 45% tu mahitaji ya chuma. Tena chuma hiki kinaingizwa kwa kodi kidogo au bila kodi kabisa huku tukijua tunadhoofisha sana viwanda vingi kujiandaa kufungwa. Hivyo, naomba kodi ya dola 400 kwa *metric ton* iongezwe ili kufidia *gap* kwa wafanyabiashara wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mambo matatu kwa Waziri wa Viwanda na Biashara. Naomba chuma kinachotoka nje kiongezwe ushuru hadi kufikia dola 400 kwa *metric ton* ili kulinda viwanda vya ndani. Kwa nini tunashindwa kuanzisha kiwanda chetu kwa ajili ya kuyeyusha chuma hapa nchini ili hata *SGR* ijengwe kwa chuma chetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ile kampuni *SHGL* iliyokuwa inataka kununua migodi ya Liganga na Mchuchuma kwa

miaka 100 ili wao wachukuwe 80% na Tanzania 20% makubaliano yamefikia wapi? Naomba kufahamu kuhusu wafanyabiashara kumi wa mji wa Kahama ambao walikamatwa toka mwezi wa 10 mwaka 2018 mpaka leo wana miezi saba wako ndani na hawajui hatima yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri afike katika Gereza la Shinyanga Mjini kujua hatima ya wafanyabiashara hao. Nini hatima yao? Naomba kama wamebainika na kosa wapigwe faini na waachwe waendeleo na biashara zao. Ili kuweza kufikia uchumi wa viwanda ni lazima wafanyabiashara wetu tuwaone kwa jicho la huruma zaidi, kwani ndio nguzo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kuhusu miradi ya Kimkakati ya Mchuchuma na chuma na Liganga.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ieleze Umma kama ni kweli katika sehemu hii ya Liganga kuna aina ya madini (*products*) zinazojulikana kama *Vanadium Pentioxide* na *Titanium* ambayo vinatumika katika kutengeneza ndege kwa kuwa ni vyepesi (*light*) na hivyo kuwa na thamani kubwa ukilinganisha na Chuma? Pia, je, baada ya ku-*extract* madini haya, chuma kinaweza kuchukuliwa kama *by product*? Ni vyema jambo hili likaangaliwa kwa ukaribu zaidi ili nchi isije ikapoteza mali nyingi zinazotoka ardhini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Same, kuna madini mengi sana ya Jasi (*Gypsum*), maeneo ya Makanya na Bendera. Jasi huwa inatumika kutengenezea "*POP*" (*Plaster of Paris*), kutengenezea mabomba ya majitaka, *ceiling boards*, mbolea na sehemu nyingine inatumika kwenye Viwanda vya Saruji.

Mheshimiwa Naibu Spika, "*Deposits*" zilizoko maeneo tajwa hapo juu ni mengi kiasi kwamba kungeweza

kuanzishwa viwanda takribani vinne hivi. Naishauri Wizara hii ya Viwanda, isaidie kutuma wataalamu maeneo haya ili kufanya uchunguzi juu ya *deposits* hizi za *gypsum* na uwezekano wa kuanzishwa viwanda hivyo kwa kushirikiana na Wizara ya Uwekezaji. Lengo ni kutekeleza Azma ya kuifanya Tanzania Nchi ya Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, atafuatiwa na Mheshimiwa Omary Mgumba na Mheshimiwa Angellah Kairuki ajiandae.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii. Naomba nianze kwa pongezi kwa Waziri, Mheshimiwa Kakunda na Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya kwa kazi kubwa wanayoifanya kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie machache sana katika Wizara hii, mambo mawili au matatu. La kwanza, nianze na alilolisema Mheshimiwa Dkt. Chegeni jana kwamba mimi Naibu Waziri wa Fedha mwaka jana nililidanganya Bunge kwa kutoa takwimu ambazo siyo sahihi kwa biashara zinazofungwa na zinazofunguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuliambia Bunge lako Tukufu, sina sababu ya kudanganya kwa sababu niko *field*, mimi nafahamu kinachotokea, biashara zinazofungwa tunazijua, biashara zinazofunguliwa tunazijua. Nimpe tu taarifa Mheshimiwa Dkt. Chegeni kwamba kwa mwaka huu kuanzia Julai, 2018 hadi Aprili, 2019 biashara zilizofungwa nchi nzima ni 16,252 lakini biashara zilizofunguliwa ambazo ni mpya ni 147,818. (*Makofi*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndiyo ukweli, huo ndiyo uhalisia. Kama

biashara zingekuwa zimefungwa bila kufunguliwa nyingine tungewezaje kukusanya kodi inayokusanya Mamlaka ya Mapato Tanzania?

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, hili lazima tulielewe, kwa sababu sehemu ambako biashara inafungwa tu hiyo wachumi tunaita *it is a dormant economy, Tanzania is not a dormant economy* na hatujawahi kufika huko, tunaendelea kuisitiza. Kwa hili, nimpongeze sana Dkt. John Pombe Magufuli, Watanzania halali wamemuelewa na wanaendelea kufanya biashara halali. *(Makofi)*

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wanaendelea kufanya biashara...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mtulie, kwani wakati mnaongea si tulikuwepo.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane na kuna wengine mkianza kutajwa majina huwa mnajisikia vibaya sana. Kwa hiyo, tusifanye fujo ambazo ukitajwa hapa mbele unaanza kujisikia vibaya, tumuache Mheshimiwa anachangia kama wewe ulivyopata fursa ya kuchangia, muache atoe ufafanuzi amalize.

Mheshimiwa Naibu Waziri, zungumza na mimi tu wala hawa wasikupe taabu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba niendeleo kusema uchumi wetu uko imara na makini, tunaendelea kutenda kwa ajili ya Watanzania. Hili ni jambo la msingi sana na ndiyo maana hatujawahi kushuka kwenye makusanyo tangu ameingia Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli madarakani chini ya triloni moja kukusanya kila mwezi. Huu ndiyo uhalisia na ndiyo tunayoyajua ambao tuko *field*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala la pili ambalo napenda kuchangia, nalo ni hili ambalo limesemwa hapa kwamba kwa nini waagizaji wa mizigo kutoka nje wanaombwa *original documents*. Sheria inasema nini? Kifungu cha 234 cha Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki kinamtaaka mteja kuleta nyaraka halisi za uingizaji wa mizigo, sheria inatuelekeza hivyo. Kwa mujibu wa sheria hii mzigo wa kuthibitisha muamala wowote ule upo kwa muingizaji wa muamala huo hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria inatuambia *a burden of proof of any import transaction rests on the shoulder of the importer or the authorities of the exporting country*. Tunachokifanya kwa sasa, nimesema Watanzania halali wanafanya biashara halali wamemuelewa Dkt. John Pombe Magufuli na hii lazima tuelewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mwaka jana tu kipindi kama hiki ombwe kama hili la mafuta lilitokea, tujulize swali la kwanza, kwa nini huwa wana-*target* kipindi kama hiki cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani? Lazima tuelewe *scenario* nzima kabla hatujasimama kuwatetea, kwa nini wana-*target* kipindi kama hiki? Sheria inasema hivyo, hiki ni chakula, unapotuletea tuoneshe umeitoa nchi gani kwa *original document*, hiki ni chakula. Sisi tuliopewa mamlaka haya ya kusimamia tunataka Watanzania walindwe kwa kila hali na lazima tulisimamie jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niyasemee mafuta haya. Mafuta yaliyopo bandarini yalikuja *metric tons* 14,400. Katika mafuta haya yapo ambayo hawajafanya *declaration*

mpaka leo, yako bandarini lakini hawajafanya *declaration*, kipi kinafichwa kwenye hilo? Lazima tujiulize ndugu zangu Watanzania. Waheshimiwa Wabunge tuelewe dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano ni njema sana. Kwa hiyo, lazima kabla hatujabebwa tu tuelewe nini kilichopo kwenye mzigo huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hawaja-*declare* mpaka leo, yapo mengine wame-*declare* ndiyo hayo ambayo hawajaleta *original documents* na sisi hatutotoa bila kuleta *original documents*...

MBUNGE FULANI: Sawasawa.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kutoa mpaka tuweze kutekeleza sheria. *Original documents* ziletwe tujiridhishe ni *crude oil* au siyo *crude oil* kwa sababu *crude oil* inalipiwa kodi kutoka kwenye *country of origin*. Kama imelipiwa kule watuletee tujue thamani yake ili tuweze kuwapelekea Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mafuta hayohayo yapo mengine yameondolewa. Mwanzo walisema yanatumika ndani ya nchi lakini wameyaondoa wameyapeleka nchi jirani, lipi linafichwa hapo?

(*Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Kijaji, muda umekwisha lakini inavyoonekana una hoja nyingi sana za kujibu hapo, maliza hoja zako ndani ya dakika moja ninayokuongezea.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nimalizie kwa kusema tunaendelea kusisitiza Watanzania waendeleo kumuelewa Dkt. John Pombe Magufuli, biashara halali ziendeleo kufanyika na tunaendelea kulinda afya ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Omary Mgumba, tutamalizia na Mheshimiwa Angella Kairuki.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nitoe mchango wangu kwenye Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, ndugu yangu, Mheshimiwa Kakunda; Naibu Waziri; Katibu Mkuu; Naibu Makatibu Wakuu, kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya, ndani ya muda mfupi wa miaka mitatu matokeo tumeyaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi kumsifia tu bila kutaja hata viwanda vichache ambavyo vinaonekana kwa kila mmoja. Niseme kwenye mambo ambayo ni ya msingi, tukianza kwenye viwanda vya matunda, Wizara hii imefanikisha kufungua viwanda vikubwa viwili, kuna Alvin kule Bagamoyo lakini kingine kiko pale Chalinze Mboga. Ni viwanda vikubwa saizi moja na Bakhresa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda kwenye viwanda vya mpunga, kuna viwanda vingi vinajengwa lakini kikubwa kuliko vyote Afrika Mashariki na kati kinajengwa pale Morogoro Mjini, Kihonda. Wengi mkipita pale Njiapanda ya Viwandani mkono wa kulia mtakuona, ambacho kitakuwa kiwanda kikubwa kuliko vyote Afrika Mashariki na Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kahawa viwanda vitatu; kipo cha AMIMZA kule Bukoba Mjini, *KADERES* pale Karagwe na OLAM pale Misenyi. Vyote hivi ni matunda ambayo yamekuja ndani ya muda mfupi katika kipindi cha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, twende kwenye chai pale *Unilever*. Juzi tu Mheshimiwa Rais alienda kukizindia kiwanda kikubwa ambacho kinatoa ajira na uhakika wa masoko ya mazao yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mpaka sasa tuna maombi chungu nzima ya walioonesha nia ya kuja kuwekeza kwenye viwanda vya korosho. Tuna matarajio makubwa mwaka huu tutaanza kubangua korosho kwa kiasi kikubwa ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawapongeza kwa kazi hiyo. Nimetaja vichache, viko vingi, naamini nikianza kuvitaja muda wangu utakwisha hata mchango wangu nisitoe sehemu zingine, kwa hiyo, nawapongeza sana kwa hayo makubwa mnayoyafanya kuibea Serikali hii na kuwatumika wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja nyingi hapa zimetolewa za Wabunge, hatuwezi kuzijibu zote kutokana na muda lakini naamini kabisa Wizara au Serikali italeta kwa maandishi majibu ya Wabunge wote mliochangia na michango yenu tunaithamini sana, mtapata majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ya kulinda viwanda vyetu vya ndani, hoja ni ya msingi kwa sababu viwanda hivi tunagombeana na wenzetu, vinakuja, lazima tuweke mazingira mazuri ya kuvilinda. Waheshimiwa Wabunge, tumewasikia, tunavifahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitolee mfano tu kwamba kuna viwanda hivyo kama vya alizeti, sio vyote vinafungwa kwa sababu ya mipango mibovu ya Serikali, hapana. Nitolee mfano viwanda viwili vya alizeti vilivyofungwa pale Singida, vimefungwa kwa sababu ya upungufu wa malighafi nchini. Kwa hiyo, tusichukulie hiyo kama ni changamoto, tuichukue kama ni fursa ya kwenda kuongeza uzalishaji wa alizeti ili viwanda vyetu vipate *raw material* ya kutosha. Ndiyo maana hata viwanda vingine vya alizeti vinachakata mbegu za alizeti kwa muda mfupi sana, miezi mitatu baada ya hapo mbegu nchini hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, siyo kila kiwanda kinachofungwa ni kwa sababu kuna mazingira mabaya, hapana, vingine vinafungwa kutokana na kwamba kama

Watanzania hatujatumia vizuri fursa ya kuongeza uzalishaji kwa ajili ya ku-*feed* hivyo viwanda vyote kwa *raw material*. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, tuchukue hii kama ni fursa tukawaambie wapigakura wetu tuongeze uzalishaji kwa sababu soko la uhakika lipo kwa viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujasiriamali umezungumzwa sana hapa katika suala la kangomba, mimi sipendi sana kuita kangomba, mimi nataka niwaite wajasiriamali. Mtoto wako usimfatafutie majina mabaya, hawa wajasiriamali ni Watanzania, ni watoto wetu na ndugu zetu na Serikali tumewasikia. Kinachogomba ni sheria ambayo Bunge hili ndiyo tulipitisha, kwa mfano, Sheria ile ya Korosho Na. 12 na Na. 15, ukikutwa na korosho kama huna kibali cha Bodi ya Korosho unatakiwa ukamatwe, yaani hata haya tunayoyafanya ni huruma na ubinadamu kwa Watanzania. Tukifuata sheria inavyosema basi hata wale wakulima wote ilipaswa tuwaweke ndani. Sasa hivi tuko kwenye mchakato kama Serikali kuipitia Sera ya Kilimo ya mwaka 2013 ili tuangalie mapungufu yote hayo na tuje na sera na sheria ambayo inakidhi mahitaji ya sasa na hali ya sasa ya masoko yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wakati mwingine haya tunayoyafanya ni kwa mujibu wa sheria ambazo zimetungwa na Bunge hili. Niwaombe ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, tukileta sheria hiyo kuondoa hao mnaoita kangomba (wajasiriamali) wafahamike basi muweze kuipitisha ili sisi kwa wajibu wetu wa Serikali kwenye kusimamia sheria uwe sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hilo pia wanasema kwamba labda hatujalipa, tumewatesa wakulima, hapana. Ni kweli tunakiri kuna wakulima mpaka sasa bado hawajalipwa, tunadaiwa zaidi ya shilingi bilioni 102 kati ya shilingi bilioni 724. Mpaka sasa tumeshalipa zaidi ya shilingi bilioni 622. Sasa hivi Serikali tunaweka mazingira mazuri ili kuwezesha Benki hii ya Maendeleo ya Kilimo kupata hizi shilingi bilioni 102 haraka iwezekanavyo ili kwenda kuwamalizia wakulima wachache hawa waliobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye soko la mbaazi, kwanza ni kweli miaka mitatu iliyopita soko la mbaazi lilikuwa siyo zuri. Sababu kubwa ni kwamba hatukuwa tumeingia mkataba maalum na walaji na soko kubwa la mbaazi katika nchi ya India. Baada ya kuona mapungufu hayo, Serikali tuko kwenye mchakato wa kuingia makubaliano maalum na watumiaji au wanunuzi wakubwa wa mbaazi duniani; India na nchi nyingine, ili tuwe na uhakika wa mbaazi zetu tukizalisha tunakwenda kuuza wapi, kwa bei gani na kwa nani ili haya mabalaa yote yaliyotukuta yasitokee.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini cha mwisho, bado tumeimarisha...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Omary Mgumba, muda wako umekwisha, ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Angella Kairuki, Waziri wa Uwekezaji.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI): Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Niungane na wenzangu kwa kuwapongeza sana Waziri wa Viwanda na Biashara, Naibu Waziri pamoja na Makatibu Wakuu na wengine wote katika Wizara hii, kwanza kwa namna ambavyo wanachochea uwekezaji katika viwanda lakini pia kwa namna ambavyo wanasimamia kuhakikisha kwamba biashara zinashamiri tukitambua kwamba biashara na sekta binafsi ndiyo injini ya ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zimejitokeza hoja mbalimbali, ntajitahidi kwa ufinyu wa muda kujibu baadhi, hususani nipende kuingia katika hoja ya wingi wa taasisi za udhibiti nikiunganisha pamoja na mazingira bora ya uwekezaji

na biashara. Kama ambavyo tumekuwa tukisema, lakini pia hata katika hotuba ya Waziri wa Viwanda na Biashara imejitokeza, Serikali katika nyakati mbalimbali kuanzia wakati wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara wakati wa *BEST Programme* mwaka 2003 lakini pia mwaka 2010 ulipoundwa Mpango Kazi au Mwelekeo wa *Roadmap*, pia mwaka 2017/2018 ambapo Serikali ilikuja na mpango wa kuangalia mifumo mbalimbali ya taasisi za kiudhibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari kama Serikali, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara imekuwa ikiliangalia suala hili kwa kina na hasa kuangalia changamoto ambazo zimekuwa ndiyo vikwazo katika kuhakikisha kwamba kunakuwa na uwekezaji mkubwa lakini pia biashara kuweza kukua. Napenda tu kusema kwamba tayari Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara nyingine katika sekta mbalimbali, tumeshachukua hatua kupitia mapendekezo yote ambayo yametolewa katika *roadmap* pamoja na *blueprint*, tumeendelea kuandaa mpangokazi wa *blueprint* pamoja na ile *comprehensive action plan*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini si hilo tu, Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe kwa kutambua kwamba yeye ndiye mratibu na msimamizi wa shughuli mbalimbali za Serikali, tayari alishaitisha kikao tarehe 17 Aprili, lakini pia tarehe 18 Jumamosi hii tena tutakua na kikao na Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Wizara mbalimbali ili kuweza kupitia kwa kina changamoto na vikwazo vyote ambavyo vimekuwa vikichangia kutokua kwa biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda tu kuwatoa hofu Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwamba tayari Serikali inaendelea kuyafanyia kazi. Kwa kutambua hili, tayari ziko tozo ambazo zimependekezwa kuondolewa. Naamini kwa kuwa tumeshaziwasilisha Wizara ya Fedha kupitia ile *Task Force* ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ya kuangalia maboresho ya kodi, katika Muswada wa Fedha ambao utaletwa mwezi Juni nyingi mtaweza kujionea mabadiliko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo tozo ambazo Mheshimiwa Waziri wa Afya amezipendekeza kupitia *TFDA*, zipo ambazo zitafutwa kabisa, lakini tunaamini zipo ambazo zitapunguzwa. Pia katika Bodi yetu ya Maziwa, Bodi yetu ya Nyama pamoja na taasisi nyingine za Kiserikali, *TBS* na nyinginezo, yapo mapendekezo mengi tu ambayo Wizara mbalimbali zimeweza kuyawasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niendeleo tu kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba suala zima la mifumo ya udhibiti tunaliangalia ili kuhakikisha kwamba wafanyabiashara wetu pamoja na wawekezaji wanafanya biashara zao na wanakuwa na uwekezaji ambao unashamiri bila kuwa na vikwazo vya aina yoyote. Naamini tutaweza kujionea mabadiliko makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya Mheshimiwa Lucy Mayenga ya kuleta mabadiliko ya Sheria ya Uwekezaji. Kwanza, nimshukuru kwa kuleta hoja hii, ni hoja ambayo pia kama Serikali tumeiona tukitambua kwamba Sheria yetu ya Uwekezaji ni ya muda mrefu, ni takribani miaka 22 na ukiangalia mambo ambayo yaliasisiwa na kuakisiwa wakati huo, mwaka 1997, inawezekana kabisa hayaendani na mazingira ya sasa ya mwaka 2019 na baadaye. Pia kuangalia suala zima la ushindani baina yetu na nchi nyingine Afrika pamoja na nchi nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijahitimisha endapo muda utaniruhusu, wapo wengi sana ambao wamezungumzia masuala ya kuomba viwanda Muheza, wengine wamezungumzia masuala ya kuwa na viwanda mbalimbali katika uchakataji wa mifugo, kilimo, uvuvi na mengineyo. Napenda tu kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba katika azma yetu ya uwekezaji suala zima la kilimo, mifugo na uvuvi ni eneo ambalo limepewa kipaumbele kikubwa na ni moja ya vipaumbele namba moja katika kuvutia uwekezaji. Tunafanya hivi kwa kutambua kwamba zaidi ya asilimia 65.5 ya Watanzania wameajiriwa katika kilimo na tunafanya hivi kwa kutambua kwamba unapowekeza katika kilimo, mifugo na uvuvi kwa kiasi

kikubwa, tija yake ni kubwa na wananchi wanapata athari kubwa katika uwekezaji wa aina hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho tumekifanya hivi sasa kwa kushirikiana na Mheshimiwa Jenista na Mawaziri wengine ambao wanasimamia kilimo, mifugo na uvuvi; tunaandaa programu maalum ya uwekezaji mahsusi katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi kuangalia vikwazo zaidi ni nini kupitia Mradi wetu wa *ASDP II*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari tumeshaanza mashauriano na Taasisi Isiyokuwa ya Kiserikali au Mdau wa Maendeleo *AGRA* ili kuja na programu jumuishi kabisa ambayo itasaidia kuangalia sekta binafsi katika kilimo, mifugo na uvuvi ni nini hasa imekuwa ni kikwazo, tunafanyaje kuwekeza katika mbegu, tunafanyaje katika masuala mazima ya trekta, teknolojia, pembejeo, mitaji na mambo mengine kwa ujumla wake ili tuangalie mnyororo mzima wa uzalishaji na uchumi katika sekta nzima ya kilimo, mifugo na uvuvi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini kwa kufanya hivi tutaweza kupiga hatua kubwa na na Watanzania na Waheshimiwa Wabunge wataweza kujionea mabadiliko makubwa. Hatufanyi tu katika kilimo, mifugo na uvuvi, tutaendelea pia kuangalia sekta zingine ambazo tunaamini zitaweza kuwa na tija na athari kubwa katika uchumi na uwekezaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha kwanza kwa siku ya leo. Nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi kamili jioni leo.

(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae. Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na mpaka siku ya leo tupo hapa. Kwa namna ya pekee napenda pia nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Viongozi wote Wakuu wanaomsaidia kwa kuwa na imani nasi na hivyo kuendelea kutuamini katika kuongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wameweza kuchangia katika hii bajeti yetu kwa azma ya kuifanya Wizara yetu iweze kutekeleza majukumu yake vizuri na pia kuzisaidia sekta ambazo zinapewa huduma na Wizara yetu ya Viwanda na Biashara; na hivyo chini ya uongozi madhubuti wa Waziri wetu Mheshimiwa Joseph Kakunda tunawaahidi kwamba michango yote ambayo imetolewa, yenye tija na nia ya kuisaidia nchi yetu, tunaichukulia kwa umakini mkubwa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi michango imetolewa katika sura mbalimbali; na unapopewa ushauri lazima utafakari, ushauri huu unapewa na nani? Napewa kwa sababu gani na una malengo yapi? Una manufaa gani? Kwa hiyo, tumeweza kuchambua ushauri karibu wote ambao umetolewa na tumeona asilimia kubwa ya ushauri huu ni mzuri na unalenga kujenga na kuimarisha nchi yetu. Kwa hiyo, tuko pamoja na tutafanyia kazi kadiri inavyowezekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi Wizara ya viwanda na Biashara kwa kushirikiana na Wizara nyingine imejizatiti katika kuhakikisha Tanzania inakuwa na viwanda na biashara endelevu zinazoakisi rasilimali nyingi ambazo zipo Tanzania; na Tanzania kwa kweli wote tunafahamu imejaliwa rasilimali nyingi sana. Ni dhahiri kuwa sekta binafsi iliyo imara ndiyo itakayowezesha kuchakata na kuongeza dhamani ya

rasilimali hizi, halikadhalika kuzitumia bidhaa hizo na ziada yake kwenda kuziua ndani na nje ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa misingi hiyo, tunategemea kwamba kwa kuwa na sekta binafsi ambayo inaweza kuhimili ushindani, ndipo tutakapoweza kupata manufaa makubwa ya rasilimali zetu. Niseme tu kwamba ni ukweli usiopingika, pamoja na jitihada kubwa ambayo Serikali imefanya katika kuimarisha shughuli za sekta binafsi nchini ambayo ndiyo chimbuko na chanzo cha mapato ya nchi, kwa sababu hata tukisema kwamba mfanyakazi analipa kodi, lakini chimbuko la fedha ni pale inapokuwa imetengenezwa kupitia viwanda au hao hao wafanyabiashara ndio hao sasa kodi zao zinawalipa watumishi fedha na hizo fedha nazo zinarudi tena kuchangia katika mfumo wa kikodi. Kwa hiyo, sekta hii ni muhimu sana. Kimsingi ndiyo moyo wa nchi katika kulifanya Taifa letu liweze kuwa imara na liweze kuchakata hizi mali nyingi tulizojaliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, tunakubali kabisa zipo changamoto ambazo bado zinawakabili wanaviwanda wetu na wajasiriamali au wafanyabiashara kwa ujumla. Kwa kutambua hilo, ndiyo maana Serikali baada ya kukaa na wadau mbalimbali, iliona iko haja ya kusema kwamba sasa tufikie mwisho tutambue, tuainishe changamoto hizi na tuzifanyie kazi. Kwa sababu hizo changamoto zimekuwa karibu katika kila sekta, kwa sababu wafanyabiashara au wachakataji wako katika kila sekta, ilibidi lazima tuangalie kila Wizara, kila mdau ni namna gani anapata tatizo au changamoto kupitia mazingira na mfumo uliopo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa misingi hiyo, tulikaa tukatengeneza hii *Blue Print*, yawezekana wengine kati yetu bado hawajaiona, lakini wengine wameshaona. Kwa hiyo, niseme tu kwamba Wizara itajitahidi kusambaza kwa wadau wengi zaidi ili tuweze kuona nini lilichopo kwenye *Blue Print*. Hilo andiko ni hili hapa, lina kurasa nyingi ambalo linataja kila sekta. Kimsingi mambo mengi yaliyokuwa yanachangiwa

humu ndani kama changamoto, tayari yalishaainishwa humu, lakini kutokana na teknolojia na namna ambavyo tunaendelea kupata ushindani na hali ya kinfumo wa kibiashara, tunaamini kwamba bado *Blue Print* haitakuwa ni mwarobaini, bali itakuwa ni kazi endelevu ya kuendelea kuiboresha kwa kadri ambavyo changamoto zinavyojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hiyo iko katika maeneo ya ngozi, tumesikia hapo, pia iko katika maeneo ya taasisi za udhibiti kama *OSHA*, *Workers Compensation Fund* na taasisi nyingine kama *TFDA*, wote kila mmoja amechambuliwa humu. Hali tuliyofikia sasa ni kuhakikisha kwamba tunatengeneza mpango mkakati wa utekelezaji, nini kifanyike wakati gani na watu gani washiriki?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunayo furaha kuliarifu Bunge letu Tukufu kwamba tayari kuna wadau wameshajitokeza wenye nia ya kusaidia utekelezaji wa mpango huu wa *Blue Print*. Kwa hiyo, naamini kwa dhamira na nia njema ya Serikali, huo upungufu au changamoto zilizojitokeza zitafanyiwa kazi na tunaahidi kufikia mwezi wa Saba tayari huo mpango mkakati wa utekelezaji utakuwa tayari na hivyo *Blue Print* kuanza kufanyiwa kazi na zile sheria ambazo zinazoonekana kuwa ni za kikwazo, zitaletwa humu Bungeni ili ziweze kufanyiwa kazi. Tunaamini kwamba, baada ya kuanza kufanyia kazi hii *Blue Print* hatutegemei tena kwamba sisi wenyewe tutaendelea kutunga zile sheria au kanuni kinzani zitakazokwenda tena kinyume na hii *Blue Print*. Kwa misingi hiyo, labda kutakuwa na kamati maalum ambayo itaweza kuangalia ni nini kinaletwa Bungeni ili kisitengeneze tena tatizo juu ya tatizo kwa nia njema na dhamira ambayo tayari nchi imeshaiweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu hoja pia iliyotolewa na Waheshimiwa Kambi ya Upinzani kuhusu korosho. Niseme tu kwamba kwanza hoja hiyo sisi tumeipokea na tumeiona ni nzuri kwa sababu inatusaidia kufafanua zaidi kwa wananchi nini kilichotokea katika suala la korosho. Korosho kama wote tunavyofahamu, ni zao muhimu na linawasaidia wananchi wengi hususan katika Mkoa wa

Mtwara, Lindi, Ruvuma, Tanga na mikoa mingine ambayo sasa hivi inajizatiti katika kilimo cha korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ambayo ilikuwa inatolewa na wanunuzi wa korosho kwa kipindi cha nyuma ilikuwa ni mbaya sana. Kwa mtu yeyote mwenye nia njema na nchi yake, mwenye nia njema na wakulima, kwa vyovyote vile hawezi kukubali kuona hali kama hiyo iendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa misingi hiyo, tunao wajibu na heshima kumpa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli ambaye hakuiangalia tu faida ya kupata hiyo hela ndogo wanayoileta wafanyabiashara kwa gharama ya kuwatesa wakulima kwa ile bei ndogo, ndipo aliposema kama nchi ibebe huo mzigo. Tukaona kwamba korosho zinunuliwe kwa shilingi 3,300/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ni maamuzi makubwa sana ambayo katika nchi yetu nasema kwamba kwa upande wa wakulima pengine haijawahi kutokea. Kwa hiyo, kwa maamuzi hayo, yamefanya kwamba ule mzigo ambao wangeubeba wakulima urudi sasa kwa Serikali ambayo ina vyanzo vingi vya mapato ukilinganisha na huyu mkulima. Kwa hiyo, sisi tunaendelea na niwapongeza sana Wizara ya Kilimo ambao tayari wameshalipa sehemu kubwa ya fedha na hiyo nyingine tunaamini itaendelea kulipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kampuni ya *INDO Power* ambayo ilikuwa inunue korosho, jamani kampuni ile nashangaa tunaizungumza sana. Yule ni mdau ambaye alitaka kununua korosho sawa na wadau wengine wowote. Mnapokuwa na makubaliano kwamba nataka labda nichukue mali yako hii, tuchukulie kama ingekuwa ni nguo dukani kwako, tunapeana muda; kufikiana muda fulani utakuwa umetekeleza, umelipa. Kama hajalipa, sisi tunamchukulia ni sawa na mfanyabiashara mwingine yeyote ambaye alikuwa hana uwezo, hatuwezi kuendelea kuitunza korosho eti tunamwekea mtu ambaye hana uwezo wa kulipa kwa wakati huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ingekuwa imepata hasara kama tungekuwa tumechukua hizo korosho tukampa yeye, halafu tukamwambia baada ya muda utatulipa. Tulikuwa hatujampa, tulichukuwa *precautions* zote na hayo ndiyo mambo makubwa aliyofanya Mheshimwia Prof. Kabudi, kuhakikisha kwamba mambo yote ya msingi kwa kushirikiana na Wizara yetu na wadau wote muhimu tunayalinda.

Kwa hiyo, hata kama akiwa amepata fedha sasa, anataka kuja kununua, kama hatujamaliza kuuza, sisi tutampa tu, lakini kama hajafika, tunaendelea na wanunuzi wengine. Kwa hiyo, Serikali au nchi haijapata hasara. Sisi tumefanya biashara zetu kwa umakini tukizingatia kwamba hakuna hata senti tano au mali ya Tanzania inayoweza kuliwa na mtu mjanja mjanja, hilo hatukubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nichukue nafasi hii kuwashawishi lakini pia kuwaonya, sisi wenyewe Watanzania tunapokuwa na jambo zito kama hili, siyo suala la kufanya la mzaha mzaha, tunapochukua maamuzi mazito, siyo masuala ya kimzaha mzaha, ni masuala ambayo yanagusa mustakabali wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wengine unaweza kukuta wanazunguka zunguka tena wanamfuata mnunuzi, anamwambia unajua hapa bwana, ungefanya hivi, ufanye hivi. Wewe ni Mtanzania? Kwa nini ufanye hivyo? Kwa faida ya nani? Nilitegemea wote tutashirikiana, tutaungana na tena hasa kwa Wabunge wanatoka Mkoa wa Mtwara na Lindi na Ruvuma kwa sababu waadhirika wakubwa walikuwa wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme tu kwamba Serikali inaendelea na mikakati, korosho ambayo ilitakiwa kubanguliwa kwa muda mrefu ilikuwa viwanda vingine vimefungwa, havibagui korosho, sasa hivi tunabangua, tumefungasha tunazo katonni zaidi ya 17,427 tayari kwa kuuza na zimekuwa-*tested*, zipo katika hali nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hiyo korosho ambayo bado haijabanguliwa, tumei-*test* katika maabara yetu ya Tanzania, lakini na maabara nyingine za nje zimedhibitishwa kuwa na ubora wa kiwango cha juu. Kwa hiyo, bado tuko katika hali nzuri. Anayetaka kuja kununua kwa tija, karibu; anayetaka kuja kununua kwa kutuibia au kutufanya sisi manamba, kwaheri. Tanzania siyo jalala, Tanzania ni nchi inayojitambua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine ambalo limejitokeza kuhusiana na bajeti ya Wizara yetu kuwa ni ndogo. Kwanza niseme kwamba tunapokea kwa kiasi fulani *concern* za Waheshimiwa Wabunge. Kama ambavyo inaeleweka kwamba kupanga ni kuchagua, nasi Wizara yetu kimsingi ni Wizara ambayo ni *coordinator*, yaani inashawishi Wizara nyingine ziweze kuweka miundombinu rafiki kwa ajili ya hawa wazalishaji wetu na wafanyabiashara kwa ujumla. Ndiyo maana bajeti nyingine unaona haziji moja kwa moja kwenye Wizara yetu, zinajitokeza katika Wizara nyingine. Mfano mzuri ni kama ambavyo ilielezwa hapo awali na Mheshimiwa Mollel kuhusiana na ujenzi wa umeme, *Stiegler's Gorge* kuhusiana na mradi mkakati wa *SGR*. Nye mnakumbuka, reli hii ya kati ni ya toka mwaka 1905, mpaka leo ilikuwa haijakarabatiwa kadri ya kiwango kinachohitajika kuweza kubeba mzigo unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, tunazo meli kama Liemba ya mwaka huo huo 1905, lakini mpaka leo haijaweza kupata huo ufadhili. Huyo mjomba tunayemsubiri kila siku atufanyie kazi, yuko wapi? Hayupo. Lazima tujifunge mikanda. Katika kujifunga mikanda, kuna maeneo yatakuwa yanaathirika kwa muda, kwa sababu nguvu zote zinakuwa zimeelekezwa huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, Serikali kimsingi inasikiliza ushauri wa Waheshimiwa Wabunge. Naamini michango iliyotolewa haiwezi ikaishia hewani tu, lazima Serikali itafanya kitu katika kuangalia maeneo yale yenye umuhimu na ambayo yanakusudiwa kwa ajili ya kuleta tija kwa haraka ikiwemo na maeneo ya miradi mikubwa ya

kimkakati yatazidi kuangaliwa na kutengewa fedha inayotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi niseme tu kwamba dhamira iliyopo ya Serikali ni kubwa sana katika kuhakikisha kwamba tunajitoa katika wimbi hili la kuitwa sisi ni masikini Tanzania wakati tuna rasilimali nyingi nyingi, nyingi. Hapana, muda umefika wa sisi kufanya maamuzi ya liyo sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu baadhi ya viwanda ambavyo havifanyi vizuri kutokana na bidhaa mbalimbali ambazo zinaingizwa kutoka nchi za nje. Kweli suala hilo tunalitafakari, lakini unakuta katika baadhi ya viwanda vyenyewe vinatumia rasilimali (*raw materials*) kutoka nje. Pia tunataka tujiridhishe hivi viwanda vyetu ambavyo tunasema havina uwezo wa kushindana katika hali iliyopo, kule wanapochukuwa malighafi, wanapata kwa bei halali au pengine kuna mazingira ya urafiki yanayofanya pengine huko wanapochukulia mali ghafi yaongezwe bei kiasi kwamba inapofika hapa hizo mali ghafi zisiweze kuzalisasha kwa tija? Kwa hiyo, tutaangalia pande zote mbili, kwa sababu sisi tusingependa kuishi kama nchi ambayo inajiangalia tu yenyewe bila kuwa na washindani wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba viwanda vya ndani vinalindwa. Kwa misingi hiyo niseme tu kwamba Wizara tumejizatiti, tumejipanga, kuhakikisha kwamba viwanda vyetu vya ndani vinapewa msaada unaohitajika ikiwemo kupunguziwa kodi katika bidhaa maalum au pengine kupewa msamaha au ruzuku katika baadhi ya malighafi na vile vile kuweza kuweka tozo zaidi kwa bidhaa ambazo zinatoka nje ya nchi wakati kuna utoshelezi ndani ya nchi. Tumefanya hiyo katika maeneo mengine. Kwa mfano, *cement* sasa hivi hatuagizi kutoka nje, tunajitosheleza. Hizo nondo, tumo katika mkakati huo na kwa kweli sasa hivi Tanzania inafanya vizuri sana katika viwanda vyake. Ni vile tu kwamba tulizoea kuviona baadhi ya viwanda vilivyokuwa vinajionesha vyenyewe ndiyo vyenye nguvu, tukavidharau vile vingine vidogo vidogo ambavyo vinaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo wawekezaji ambao wako tayari, akina *Kilua Integrated Group* wako hapo, ni Watanzania. Sio hao tu, tunao wengi ambao wanakuja. Vile vile tumefanikisha kuvutia viwanda vingi ambavyo sasa vimeanzishwa nchini, mfano kiwanda cha *Cassava (starch)*, yaani wanga wa unga wa mihogo ambacho kiko kule Lindi. Juzi juzi hapa Mheshimiwa Rais amezindua tena Kiwanda cha Unga pale Mlale, Kiwanda cha Maparachichi pale Rungwe, Tukuyu na vile vile tumeona hata *Unilever* pale Njombe; na viwanda vingi vinaendelea kufunguliwa. Tatito labda hatujapata fursa ya kutembelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba sana Watanzania tupende bidhaa zetu za Tanzania, tupende kutumia bidhaa zetu na tujivunie, vile vile kwa wafanyabiashara na wajasiriamali wote kwa ujumla. Sasa hivi kitambulisho cha ujasiriamali kimeshushwa ni shilingi 20,000/= tu, huhitaji hata sasa utengeneze mahesabu, sijui ufanye nini; kwa mtu mwenye mtaji wa chini ya shilingi milioni nne, huyu akishakuwa na kitambulisho chake cha shilingi 20,000/= tu cha ujasiriamali, habughudhiwi, anaendelea na shughuli zake popote pale. Hayo ndiyo mambo ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli katika kuwasaidia wanyonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba katika masuala haya ya undelezaji wa biashara, hayawezi kufanyika na mtu mmoja. Hata sisi wenyewe tuwe na *positive thinking*, tuwe na hali ya kusemea vizuri nchi yetu. Ukishaulizwa swali tu, eh mazingira ya biashara nchini kwako yakoje? Unaanza; unajua tuna taabu nyingi sana, unajua kuna *OSHA*, kuna nini. Sasa unajiuza hasi wewe mwenyewe, ukishajiuza hasi na yule anayeandika atasema mazingira yako ni magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani changamoto iliyopo siyo tozo tu, ni kuweka mazingira ambayo yatawafanya wafanyabiashara watengeneze faida ili waweze kumudu kulipa hizo tozo, kwa sababu baadhi ya tozo ndiyo chanzo cha uchumi, chanzo cha kuwezesha kuendeleza miundombinu mbalimbali ikiwemo ya afya, maji na mengine. Hata juzi ilikuwa bahati nzuri Mheshimiwa Dkt.

Mpango alipokataa, ilikuwa tuongeze tozo nyingine kwenye mafuta, tulishasahau kwamba tunawadunga tena hao hao wafanyabiashara. Kwa bahati nzuri suala hilo tulliona kwa mapana, halikuweza kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme kwamba Wizara yetu imejipanga na tutaendelea kutumia ushauri wenu Waheshimiwa Wabunge na wadau wengine na kuhakikisha kwamba taasisi zetu zote zinafanya kazi kijasiriamali, siyo bora uko kazini. Mimi nimefika kazini, nimewaundumia akina nani na kwa namna gani? Hilo ndilo tunalitaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee niwashukuru wadau ambao huwa wanaturudishia mrejesho wa kupongeza jitihada ambazo tunazifanya. Mfano tu kiwanda cha karatasi Mgololo, walikuwa na changamoto tulipowatembelea, lakini tukamwona Waziri wa Maliasili changamoto zikaondolewa, wakatushukuru. Halikadhalika kulikuwa na wadau waliokuwa na shida ya kupata ardhi, kama hao wa *cassava* kule Lindi, tayari wanafanya shughuli zao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wapo wengi wenye shida kama hizo, tunasema kwamba ofisi yetu Wizara ya Viwanda na Biashara iko wazi na sisi wenyewe tuko ndani, siyo kwamba tu ipo wazi halafu hatuko ndani, tuko tayari kuwasikiliza msihangaika peke yenu, hakuna mkubwa kwenye ofisi yetu, sisi wote ni sawa mfalme ni wewe mteja, mfalme ni wewe mwenye kiwanda, mfalme ni wewe mfanyabiashara ambaye mwisho wa yote unachakata uchumi wetu na kulifanya Taifa letu liwe na uchumi imara na tuweze kulipia mahitaji yetu ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya, nashukuru sana na niwaombe Waheshimiwa Wabunge kutuunga mkono katika hoja yetu hii na naunga mkono mimi mwenyewe hoja yetu ya Bajeti ya Viwanda na Biashara. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Sasa nimwite mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Kakunda.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kukupongeza kwa dhati wewe mwenyewe pamoja na Mheshimiwa Najma Giga ambaye alikuwa Mwenyekiti jana kwa jinsi mliyotuongoza tangu nilipowasilisha hotuba yangu jana, mliyosimamia mjadala na hadi kufikia muda huu nawapongeza sana na kuwashukuru sana.

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge 40 ambao wamechangia kwa maandishi na Waheshimiwa Wabunge 37 ambao wamechangia kwa kusema moja kwa moja hapa Bungeni. Kwa ajili ya muda naomba majina ya Wabunge wote waliotoa ushauri, maoni, na mapendekezo yawe kwenye orodha ya *hansard* kwa ajili ya kumbukumbu, nawashukuru sana.

Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Naibu Mawaziri na Mawaziri waliopata nafasi ya kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali yaliyojadiliwa. Kwa namna ya kipekee namshukuru sana Naibu Waziri wangu Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya kwa jinsi alivyotoa ufafanuzi aliyotoa hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikiri kwamba Wabunge wote waliochangia kwenye hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara wameipatia Serikali ushauri na maoni mazuri ambayo mengi tutayafanyia kazi na kutoa taarifa kupitia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ufafanuzi wangu ninaotoa ni kwa maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa upande wa Kamati ni maeneo mawili tu ya kuzungumza. La kwanza niahidi kwamba mapendekezo ya Kamati tutayafanyia kazi, ingawa kuna baadhi ya mapendekezo yanagusa mikataba, kwa hiyo baadhi ya mapendekezo ambayo yanagusa

mikataba itabidi yaingizwe kwenye mfumo wa majadiliano yanayoendelea. Kamati itapewa taarifa rasmi kupitia utaratibu wa ratiba zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kutopendwa sokoni kwa bidhaa zinazozalishwa nchini na ushauri wa Kamati wa kuhamasisha Watanzania kupenda kununua na kutumia bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya Tanzania. Tumeupokea ushauri huo kwa mikono miwili na moyo mkunjufu, kwa sababu mtu asiyependa chake ni sawa na kutojithamini mwenyewe. Viwanda vyetu vinazalisha vitenge vizuri sana, lakini vikiandikwa *made in* Tanzania baadhi ya Watanzania hawanunui mpaka baadhi ya viwanda vya nguo vinalazimika kuandika *made in* Nigeria ndiyo vipate soko. Sasa hii ni tatizo ambalo naomba Waheshimiwa Wabunge wote tushirikiane kuliondoa katika nyoyo za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ushauri huo wa Kamati ya Bunge letu tuanzie na Bunge, lionyeshe mfano kwa kupendekeza manunuzi ya bidhaa za Tanzania kwenye ofisi zote za umma, Ofisi za Bunge na hata Bunge hili likubali kubadilisha kanuni za mavazi ya Wabunge hasa Wabunge wanaume ikiwezekana waruhusiwe kuingia Bungeni wakiwa wamevaa mashati nadhifu ya vitenge vikiwa vya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hotuba ya Upinzani niseme tu kwamba, mwaka wa fedha 2018/2019 haujakwisha, randama aliyoinukuu Mheshimiwa Waziri Kivuli ilikuwa na takwimu za hadi mwezi wa Tatu 2019, bado miezi minne hadi mwezi wa Nne takwimu zimebadilika na hadi wiki ijayo ninazo taarifa kwamba takwimu hazitakuwa zile zilizonukuliwa. Kwa maana hiyo kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sawa, siyo sahihi kabisa na haitokuwa sahihi kabisa kusema kwamba eti bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ilikuwa ni bajeti hewa, isipokuwa kilicho sahihi ni kusema kwamba Serikali huwa ina umakini mkubwa katika kutoa fedha za utekelezaji hadi pale inapojiridhisha kwamba hatua stahiki za maandalizi ya utekelezaji zitakuwa

zimekamilika. Mfano, baadhi ya maeneo yanayoendelea na ratiba ya mapitio ya mikataba na baadhi ya maeneo yanahitaji tafiti kwanza zifanyike na kukamilika kabla ya utekelezaji kuanza lazima fedha zake zitasubiri kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Viwanda na Biashara ina imani kwamba kwa maeneo na miradi ambayo taratibu za maandalizi zimekamilika mfano wa ulipaji wa fidia kwenye mradi wa Mchuchuma na Liganga fedha zitatolewa kabla ya kwisha kwa mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili katika hotuba ya Upinzani, ni lawama na kubeza utekelezaji wa miradi mikubwa ya ujenzi wa reli ya kati kwa viwango vya Kimataifa na mradi mkubwa wa kufufua umeme wa *Stiegler's*. Napenda nisisitize pongezi zangu kwa Mheshimiwa Rais kwa maamuzi ya kihistoria aliyoyafanya kujenga miradi hiyo. Kwa mujibu wa Maazimio ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Dunia uliofanyika Rio de Janeiro, Brazil mwaka 1991, uchumi maana yake ni ardhi na anga kwa maana ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta za uchumi ambazo ni kilimo, mifugo, uvuvi, maji chini na juu ya ardhi, maliasili ikiwemo uoto wa asili na wanyamapori, madini na ujenzi kwa ujumla na sekta za uchumi anga ambazo ni pamoja na nguvu jua, mwanga, hewa na mvua ni sekta muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yoyote ile ikiwemo Tanzania. Hata hivyo uzalishaji ghafi kwenye sekta hizo hauwezi kuwa na faida kubwa kiuchumi kama sekta ya viwanda haitachakata malighafi zinazozalishwa ili kupata bidhaa zenye thamani kubwa ambazo zitafikishwa kwenye maeneo mbalimbali zinakohitajika kwa matumizi ya binadamu na viumbe wengine kupitia mifumo wa biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Sekta ya Viwanda na Biashara itimize jukumu lake hilo vizuri, inahitaji mazingira wezeshi yanayopunguza gharama za uzalishaji, gharama za hifadhi, gharama za usafiri na gharama za usafirishaji. Kwa maana rahisi mazingira wezeshi ni bandari inayofanya kazi vizuri, barabara nzuri za lami, madaraja makubwa, mfano,

madaraja ya Mkapa, Kikwete na Magufuli, viwanja vya ndege, reli ya viwango vya Kimataifa, mradi mkubwa wa kufufua umeme wa uhakika kama *Stiegler's* ambao utazalisha megawati 2,100 kuwa na uhakika wa kuhudumia viwanda. Miundombinu hiyo ndiyo chachu kubwa ya uwekezaji kwenye viwanda na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii itakapokamilisha miradi hiyo na miradi mingine ukiwemo ule ambao utatekelezwa baadaye wa reli ya Mtwara hadi Mbambabay, ambao baadaye itajengwa reli kupita kwenye maeneo ya miradi ya chuma ya makaa ya mawe ya Liganga na Mchuchuma itachochea kwa kasi ya aina yake maendeleo ya ujenzi wa viwanda na biashara nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili limezungumzwa sana ni eneo la *software* kwenye biashara. Hoja hii imejitokeza kwa kuchangiwa na Wabunge wengi sana na ilionekana kama ndiyo pekee ambayo pengine inakwamisha maendeleo ya viwanda na biashara nchini. Serikali imedhamiria kutekeleza mapendekezo yaliyomo kwenye mfumo wa kuweka mazingira rafiki ya ufanyaji biashara, uwekezaji na ufanyaji biashara nchini ambao utaboresha na kupunguza gharama za uwekezaji na ufanyaji biashara. Mfumo huo ambao ndiyo *blue print* utakaoanza kutekelezwa mwezi Julai ndiyo ambao utakuwa ni mwarobaini wa kuondoa malalamiko mengi sana ya sekta binafsi, sekta ya viwanda na sekta ya biashara hapa nchini. Tumejizatiti na naamini chini ya uratibu na usimamizi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, mambo mengi yatakaa vizuri na kuanzia mwaka ujao wa fedha malalamiko yatakuwa yamepungua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, yamezungumzwa mengi sana na Waheshimiwa Wabunge kuhusu miradi ya kimkakati. Labda nikianza na Mradi wa Mchuchuma na Liganga, niseme tu kwamba Serikali imedhamiria kuanza uchimbaji wa makaa ya mawe ya Mchuchuma na chuma cha Liganga. Uendelezaji wa mradi huu utaanza mara tu baada ya mambo kadhaa kukamilika ikiwemo mchakato wa kurekebisha vipengele katika hati ya makubaliano kulingana

na sheria mpya ya ulinzi wa maliasili, kulipa fidia ya ardhi kwa wananchi watakaopisha utekelezaji wa mradi, kujenga miundombinu wezeshi kwenye eneo la mradi, hasa barabara, reli na njia ya msongo wa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la kurekebisha vipengele vya mkataba ni kulinda maslahi ya nchi kufuatia Sheria mpya za Madini za mwaka 2017 na Sheria za kulinda maliasili zetu. Kwa hiyo majadiliano ya kina ni lazima yafanyike upya kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, vivutio vingi vilivyooombwa na mwekezaji vinapingana na sheria za nchi hivyo kufanya utekelezaji wake kuwa mgumu. Pili, mkataba uliosainiwa baina ya mwekezaji na Serikali una vipengele vingi vinavyomnufaisha zaidi mwekezaji kuliko Serikali. Tatu, kufanya tathmini upya juu ya kiwango na ubora wa madini ya chuma *titanium, vanadium na aluminium* katika mgodi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakumbuka kwamba wakati wa mkataba ule wa awali kilichokuwa kinatajwa ilikuwa ni chuma na makaa ya mawe peke yake ilidhaniwa kwamba *titanium, vanadium na aluminium* kwamba hiyo itakuwa na viwango kidogo sana ambavyo havitakuwa na maana katika mapato, kumbe hiyo tulikuwa tunaingizwa katika mkenge ambao Taifa hili kama mkataba ule ungesainiwa kama ulivyokuwa, inawezekana aliyesaini angebatizwa jina la Mangungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafanya jitihada za dhati kupunguza muda wa majadiliano ili kuhakikisha kwamba tunamaliza majadiliano ndani ya muda mfupi. Aidha, katika mradi huo Serikali inaangalia uwezekano wa kutenganisha mradi wa makaa ya mawe na ule wa kuzalisha umeme ili kurahisisha utekelezaji wake. Lengo ni kuwa na vyanzo vingi vya kuzalisha umeme wa uhakika ukiwepo uzalishaji wa umeme wa makaa ya mawe utakaotumika viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, klatika mradi wa Liganga madhumuni ni kuchenjua na kuzalisha bidhaa mbalimbali za chuma ikiwemo *vanadium* na *titanium* ili kukidhi soko la ndani na nje ya nchi badala ya kuuza chuma ghafi. Kwa hiyo, kuuza bidhaa za chuma cha Liganga kwa wenye viwanda nchini ndiyo nia ya Serikali ili kuongeza mnyororo wa thamani na hivyo kukuza sekta ya chuma nchini. Azma hiyo itatekelezwa mara tu Mradi wa Liganga utakapoanza uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mwelekeo wa Serikali ni kutenganisha Mradi wa Chuma cha Liganga na ule wa Makaa ya Mawe wa Mchuchuma. Hata hivyo suala hili linahitaji majadiliano na wadau mbalimbali kwa kuwa mkataba wa awali ulikuwa unganishi kwa lengo la kuzalisha chuma na umeme kwa kutegemeana ambapo umeme unaotokana na makaa ya mawe ungetumika kuyeyusha chuma cha Liganga ili kupata bidhaa mbalimbali zitokanazo na chuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tungetekeleza nina takwimu hapa, ule mkataba wa awali kama ungesainiwa ulivyokuwa, Serikali ingepoteza dola za Kimarekani bilioni kumi na tisa laki nane na milioni mia nane sitini kwa chuma na vile vile tungepoteza dola 23,342,200,000 kwa *aluminium* na dola milioni 450 kwa *titanium*. Hii ingekuwa ni hasara kubwa kwa Taifa na mikataba ya aina hii iliwahi kusainiwa huko nyuma na Bunge liliwahi kutangaza kwamba mikataba ile ilikuwa mibovu. Kwa hiyo, kwa sasa hivi tuko makini kuhakikisha kwamba tunalinda maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa *Soda Ash* Engaruka; madhumuni ya Serikali katika Mradi wa Magadi soda wa Engaruka ambao utazalisha magadi soda kama msingi wa viwanda vya kemikali nchini yako wazi. Kwa sasa Serikali imetoa fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu ambao inaitwa *tekno economic study* kama nilivyosema kwenye hotuba. Lengo la *study* hiyo ni kubaini faida na namna bora ya kutekeleza mradi huu. Kwa hiyo, upembuzi huu yakinifu utakapokamilika ndiyo utakaotushauri tutekeleze vipi mradi huu. Namwomba sana Mheshimiwa Mbunge

Kalanga tushirikiane katika hili kwa sababu huwezi kuanza kujenga barabara ya lami leo kwenda kwenye eneo la mradi wakati upembuzi yakinifu haujatushauri je, tutajenga mabomba au tutajenga barabara ya lami au tutajenga barabara ya changarawe. Kwa hiyo naomba tuwe na subira, wananchi wawe na subira mradi huu utatekelezwa na tutakuwa na faida kubwa sana kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Matairi cha Arusha, napenda nirejee kama nilivyosema kwenye hotuba yangu Serikali imedhamiria kufufua kiwanda hiki, kile kiwanda cha Kenya wameshakifunga hakizalishi tena kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanasema hapa tunazidiwa na Kenya. Kenya watategemea matairi kutoka kwenye Kiwanda cha Matairi cha Arusha tutakapoanza uzalishaji. Kwa hiyo, hiyo ni fursa ambayo tutaitumia na hii kampuni ambayo tunaendelea na majadiliano nayo, majadiliano haya tutayakamilisha kwa haraka iwezekanavyo kama ambavyo Wabunge wameonesha ili tuhakikishe kwamba kiwanda kinaanza uzalishaji wa matairi. Tunawatafutia eneo lingine ili kuongeza eneo maana yake eneo hilo la Arusha limeonekana ni dogo, kwa hiyo tutawatafutia eneo la hekta 100 nje ya Arusha na litakapopatikana tu tayari tutaingia kwenye makubaliano rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kiwanda cha *Tabotex* cha Tabora ni kweli kwamba kiwanda hiki hakifanyi kazi tumeshamwonya mwekezaji mara nyingi, ameandika barua kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu tangu mwezi wa 12 akiomba muda wa kufikiriwa kwa sababu alikuwa anatafuta mkopo *TIB*. Sasa mkopo wa *TIB* wa shilingi bilioni tano sisi hatujajua kama ameupata, lakini muda wake alioomba umepita. Kwa hiyo itakapofika tarehe 31 sawasawa na ambavyo tumezungumza kwenye viwanda vingine, kiwanda hiki itabidi kirejeshwe Serikalini kama hatakuja na *concrete plan* ya kuendeleza kiwanda hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kuhusu miradi ya mikakati, ni miradi ya *EPZA*. Miradi ambayo ni ya kujivunia

sana hapa nchini ni miradi ya *EPZA* ingawa kuna changamoto katika baadhi ya maeneo machache, eneo la Tanga na maeneo mengine kwa ajili ya fidia, lakini miradi ambayo tayari inafanya kazi, inafanya kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Riziki Lulida alizungumzia mradi wa *EPZA* wa utengenezaji wa nguo pale Ubungo, akisema kwamba wafanyakazi pale ni kama vile wananyonywa, lakini nikwambie tu ukweli kwamba wafanyakazi walioajiriwa pale kiwandani kwenye kiwanda cha *Took Garment Limited* ni wafanyakazi 2,600 na idadi hii itaongezeka kufikia wafanyakazi 4,000 miezi michache ijayo. Wafanyakazi ukiwatembelea pale, nimetembelea pale nimeongea nao, wanaridhika na hali ya ajira kwenye kiwanda hicho na si kweli kwamba wanalipwa sh.100,000 au chini ya hapo, wafanyakazi wengi wanalipwa mishahara ambayo wamekubaliana. Kwa hiyo kazi inayoendelea pale inaendelea vizuri na kuna amani na utulivu na hakuna mgogoro wowote na endapo kutakuwa na mgogoro mimi nitakuwa wa kwanza kuusikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Indo Power* nataka nirudie tena Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumza, ile Kampuni ni Kampuni genuine kabisa iko Kenya imefanyiwa *due diligence* vizuri kabisa na Balozi wetu wa Tanzania nchini Kenya na Balozi wa Kenya nchini Tanzania, tumepata taarifa za kutosha linafanya biashara hapo Kenya na ni Kampuni ambayo inastahili kufanya biashara ndani ya Kenya, Afrika Mashariki na Duniani kwa ujumla. Sasa mkataba ambao tuliingia na kampuni hiyo mkataba ule ulikuwa halali na ulikuwa na vipengele vya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa bahati mbaya kampuni ile imechelewa kutekeleza baadhi ya vipengele, kiasi ambacho kikafikia tukaanza sasa kupata matatizo, baadhi ya watu wengine wa Tanzania hapa, kama benki inataka kulipa labda mtu fulani anataka kununua korosho Tanzania, wakaanza kupeleka taarifa kwamba mnalipa korosho, zimeshanunuliwa na kampuni fulani. Kwa hiyo ndiyo maana tumetangaza kwamba ile kampuni tumeamua

kuachana nayo ili kusudi tuweze kuuza korosho na hizi korosho tutaziua hivi karibuni tofauti na watu ambao wanafikiri kwamba hatutauza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kulinda viwanda vya ndani, naomba tushirikiane Bunge zima, Serikali nzima na wananchi tushirikiane kuhusu suala la kulinda viwanda vya ndani. Hatua ya kwanza ya kulinda viwanda vya ndani ni kuhakikisha kwamba wanapata *raw materials* kwenye viwanda. Kama kiwanda kinajengwa halafu hakipati *raw materials* kitakufa, kwa hiyo tusije kukamata koti la Mheshimiwa Kakunda, kwamba Kakunda hajasimamia vizuri viwanda vimekufa kama vimekosa *raw materials* itabidi wote tusimame tuulizane. Kwa hiyo jambo la kwanza ni kuhakikisha kwamba, viwanda vinapata *raw materials*.

Mheshimimiwa Naibu Spika, mimi na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo tumeshazungumza tumekubaliana viwanda, kwa mfano, viwanda vya korosho tumekubaliana vitapata *raw materials*. Hata wale wanaotaka ku-*invest* kwenye viwanda vya korosho Tanzania tunawapa mkataba maalum kuwahakikishia watapata *raw materials* ili viwanda visife wala kuhamishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ngozi Serikali haijazui kuuza ngozi ghafi nje. Hadi sasa ngozi zinauzwa kwa wingi katika nchi za Ghana na Nigeria na vibali vinaendelea kutolewa kwa wale wanaohitaji. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 kilo za ngozi ghafi 3,636,700 za ng'ombe zenye thamani ya shilingi trilioni 4.6 na kilo 274,000 za mbuzi zenye thamani ya shilingi 320 zilisafirishwa nchi ya nje. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba tumezuia kusafirisha ngozi nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu miradi ya maendeleo kutumia vifaa vinavyopatikana nchini. Hili limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge, mambo mengine yanahusu mikataba, tunaendelea kuzungumza na Wizara ya Fedha na wadau wengine kuhakikisha kwamba sehemu kubwa ya matumizi kwenye miradi mikubwa ya maendeleo kwa mfano ujenzi wa barabara, reli na madaraja

wanatumia vifaa ambavyo vinazalishwa ndani ya nchi ikiwemo bidhaa za chuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani nitakuwa nimegusa maeneo maeneo muhimu sana ambayo yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge na mengine yote ambayo yamezungumzwa tumeyachukua na tutayatolewa taarifa wakati utakapofika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha, ahsante sana.

WABUNGE FULANI: Toa hoja.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa tutaendelea na utaratibu wetu, Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU - KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae, Katibu.

Fungu 44 - Viwanda

Kif. 1001 – *Administration and Human Resources Management*.....Sh.12,929,375,000/=

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki ndicho chenye Mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Kwa mujibu wa Kanuni zetu tumeletewa majina ya Wabunge ambao wanahitaji kupata ufafanuzi wa jambo mahsusni kwenye eneo hili. Tutaanza na Mheshimiwa Mwanne Mchemba.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kumwomba Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi kwa yale ambayo nilikuwa nimechangia jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kunipa majibu hapa sasa hivi, kwanza nimshukuru kwa sababu kuna baadhi ya majibu nimeridhika nayo. Pia amesema mwekezaji wa Kiwanda cha Nyuzi amepeleka maombi ya mkopo (barua) kwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, ndiyo kusema yeye mwenyewe tayari hajitoshелеzi. Pia amesema mwisho ni tarehe 30 ya mwezi huu. Uzuri na bahati, kwa kuwa nami nitakuwepo tarehe 30 ili kupata jibu sahihi ambalo litatusaidia sasa kujua kweli huyu mwekezaji yupo *serious* na hiki kiwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hilo tu, kabla huyo mwekezaji hajapata mkopo na kabla Mheshimiwa Waziri Mkuu hajajibu ile barua ya kuridhia kupata mkopo huo wa shilingi bilioni 5, nimwombe Mheshimiwa Waziri waende wakague kiwanda kile ameondoa mitambo yote, kwa sasa haipo kwenye kiwanda hicho. Kwa hiyo, nimwombe anipe ufafanuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine la Kiwanda cha Tumbaku...

NAIBU SPIKA: Ni jambo moja tu Mheshimiwa. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo amezungumza Mheshimiwa Mwanne Mchemba labda nifafanue kwamba mwekezaji aliomba mkopo *TIB*. Baada ya kuwa ameomba mkopo *TIB* ndiyo akandika barua ya kumuarifu Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba nimeomba mkopo *TIB*, kwa hiyo, naomba Serikali inivumilie. Hayo ndiyo yalikuwa maudhui ya barua aliyoundika kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu aliandika mwezi Desemba na mpaka leo mwezi huu Mei hatuoni

kinachoendelea, ndio maana tumeweka ukomo kwamba mwisho tarehe 31 kama atakuwa hajaleta maelezo ya kutosheleza basi kiwanda kile tutakirudisha Serikalini. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwanne Mchemba, kabla hajasimama.

Waheshimwa Wabunge, tuzitembelee Kanuni zetu tena, mambo yanayohojiwa sasa hivi siyo hoja ya kitu kimoja. Tunaposema jambo mahsusi fulani ni jambo la kisera ni jambo la siyo jambo la sehemu moja kwa sababu unamtaka Mheshimiwa aanze kufanya kipindi cha maswali na majibu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, mnaoomba ufafanuzi usiombe ufafanuzi kuhusu kitu kimoja tu mahsusi, hapana, ni jambo mahsusi lakini la jumla na la kisera. Kwa hiyo, tuzitembelee Kanuni zetu.

Waheshimiwa Wabunge, tuendeleo na Mheshimiwa Ester Michael Mmasi.

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru kwa nafasi hii. Napenda nijikite moja kwa moja kwenye maelezo ya Mheshimiwa Waziri ambapo nitapenda sasa nipate kauli ya Serikali ya mwisho kabisa kabla sijaweka kusudio la kushika shilingi. Kama sitapata maelezo ya kuniridhisha nina *intention* ya kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo bado pale pale kwenye suala Liganga na Mchuchuma. Wakati nasikiliza majibu ya Mheshimiwa Waziri ametamka vikwazo vya mradi huu kama vikwazo viwili. Alizungumzia suala la vivutio ambapo amesema vivutio vilivyotolewa na mwekezaji vimeonekana kukiuka sheria za nchi na akarejea zile sheria mbili za kulinda maliasili ya nchi yetu. Akasema pamoja na vivutio hivyo lakini pia kuna masuala ya tathmini kwamba tathmini ya chuma haijafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata tabu, kwa sababu Mheshimiwa Waziri atakumbuka mkataba huu ulisainiwa mwaka 2014 lakini vitutio vya ziada vimeombwa mwaka 2017 na huyu mwekezaji. Kwa hiyo, vipo nje vya masharti ya zile sheria mbili, kwa sababu ile ni *addition incentive*, ilikuja kama *addendum* haikuwa ndani ya mkataba ule ambao tunasema tunaorudia kuupitia kwa sababu una masharti hasi. Naomba Mheshimiwa Waziri ajiridhishe na eneo hilo vinginevyo natangaza kushika shilingi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini unaposema tathimini ya kujua ubora wa chuma, mimi nikipewa ruhusa ya kuwachukua *TBS* kuwapeleka Liganga na Mchuchuma kesho saa 11.00 jioni nitakuwa Liganga na Mchuchuma pamoja na timu ya *TBS*. Ni kitu gani kinachokawiza mradi huu mkubwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wote tuliongea wote tunaona Liganga na Mchuchuma ni ajira kwa sababu hata sasa chuma inayovunwa Tanzania ni 80%, 20% tuna-*import* kutoka nje lakini tazama ajira, ajira 23,150 zinazotokana na uvunwaji wa chuma hiki 20,000 ni vibarua. Mwekezaji yeyote hawezi kufanya kazi ambayo haina malipo lakini ingekuwa ni Serikali badala ya kuwa na wafanyakazi *permanent* 3,150 leo hii tungekuwa tunaongelea *permanent staff* ni wale 20,000 ambapo kwa hili Liganga na Mchuchuma leo hii tunaona ni vibarua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapongelea Liganga na Mchuchuma, ni umeme, makaa ya mawe na ajira kwa vijana wetu, tuseme nini tena? Tunaomba majibu ya kuturidhisha Mheshimiwa Waziri kwenye hili, mimi bado sijaridhika, naomba kupata majibu ya Serikali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, ufafanuzi.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napata *concern* ya Mheshimiwa Mbunge juu ya uchungu kuhusiana na kuendelezwa kwa Mradi wa Liganga na Mchuchuma. Tunaita

Liganga na Mchuchuma kwa sababu hizo ndiyo *main components*, kama ambavyo tumeweka kwenye kitabu chetu ukurasa wa 125 unaweza kuangalia hata ile picha inavyoonyesha ule mradi au kile chuma kipo kiasi gani na ni baraka kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua Watanzania Mwenyezi Mungu ametujalia kuwa na aibu na heshima sana. Mtu anapotuletea mkataba au mapendekezo ambayo yamekaa ndivyo sivyo wakati mwingine tunamuangilia lakini roho zetu zinaumia. Tunasema kwa nini ameamua kutufanya wajinga, kwa nini ameamua kuona nchi hii labda ni ya wendawazimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika mkataba huu pamoja na sheria ambazo tumezungumzia kuna mambo ambayo tumeona hayajakaa vizuri, hatuwezi tukauza rasilimali kubwa ya Watanzania eti kwa sababu ili mradi tuwe na furaha kuna mwekezaji umekuja hata kama huo uwekezaji hauna tija katika nchi. Ndiyo maana kwa heshima ile ile tunasema turudi mezani tukae vizuri, sisi wenzio tulivyopita upya tumegundua hili na hili mwenzetu unasemaje? Akiridhika sawa, hajaridhika kwa kitu ambacho hakina tija kwa kweli kabisa aende na sisi tutaendelea kutafuta mwekezaji ambaye ataleta tija katika nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo hali halisi na katika hilo hatuna mchezo. Mwekezaji yeyote anayekuja aje akijua kwamba Watanzania siyo wajinga, wana akili zao. Sasa hivi tunaendelea kusomesha Watanzania wengi katika maeneo hayo ya kimkakati ili kuhakikisha kwamba kila mkataba tunaoingia unakuwa ni wenye tija. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimwa Mmasi, nakuona umesimama lakini tunarudi palepale kwenye Kanuni yetu ya 103 na mwongozo ulishatolewa kuhusu matumizi yake ni kwamba unataka ufafanuzi kwenye mshahara wa Waziri kwa jambo ambalo hujaridhika na utekelezaji wake lakini jambo la jumla na kisera. Sasa hapa ni mradi mahsus, tukiushikia

shilingi hapo tutakuwa tunakosea sisi wenyewe miongozo ambayo tumejiwekea.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ndiyo utaratibu ambao tumekuwa tukiutumia. Kwa hiyo, tutaendelea na Mheshimiwa Antony Komu.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mimi nimekusudia kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri kama sitapata maelezo ya kuridhisha kuhusu utekelezaji wa sera na sasa kuna sheria ya PPP kwa sababu kwa maoni yangu pamoja na umuhimu wa sera hiyo sioni ikifanya kazi inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera hii ingetokelezwa tungekuwa na unafuu mkubwa sana katika uendeshaji wa nchi yetu lakini leo Serikali inalazimika kufanya kila kitu yenyewe, kutengeneza miradi mikubwa ya kibiashara yenyewe wakati tuna sera hii ambayo ingetusaidia ili Serikali ikaweza kwenda kufanya mambo mengine hasa ya kutoa huduma za jamii.

Kwa mfano sasa tuna *crisis* ya mishahara ya watumishi na Rais amesema kabisa kwamba jamani tuvumilie tufanikishe haya mambo makubwa tunayoyafanya, mambo ambayo yangeweza yakatekelezwa kama sera hii ingekuwa inafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nipate maelezo kutoka kwa Waziri tatizo ni nini, ni mazingira au ni *political willingness* ya watu walioko madaraka ama ni sheria zetu zilizoko? Napenda nione *commitment* ya Mheshimiwa Waziri labda watafute *independent consultant* atakayeweza kutupa ufumbuzi wa tatizo hili ili sera hii ifanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sitapata maelezo ya kuridhisha kwenye suala hilo, nitaomba nitoe hoja ili Bunge liniunge mkono tuijadili. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Komu amekosea shabaha kwa sababu amenipiga risasi mimi wala sihusiki. Kwa hiyo, amenionea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimamizi wa sera ya *PPP* na sheria na kanuni zake ni Mheshimiwa wa Waziri wa Fedha. Kwa hiyo, angesubiri muda wa Wizara Fedha utakapofika, ndiyo aulize hilo swali. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Komu.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka majibu ya Serikali na Serikali ni moja na kila mmoja kwenye Serikali yupo hapa lakini *specifically* kwenye biashara tuna matatizo. Leo tumenunua ndege kwa fedha taslimu, tuna mazungumzo hapa ya Liganga na Mchuchuma hayaishi, tuna mambo ya Bagamoyo hayaishi, tuna masuala ya LG upande wa gesi kule hayaishi, yapo chini yako Mheshimiwa Waziri. Tunataka majibu ni kwa nini hii *PPP* haitekelezeki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe hoja...

MWENYEKITI: Usitoe hoja, ngoja tuelewane vizuri, wewe kaa tu tuelewane vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, mshahara unaokamatwa hapa ni wa Waziri wa Viwanda na Biashara, ndiyo mshahara wake unaoshikwa hapa. Kwa hiyo, jambo mahsusi ambalo halitekelezwi sawasawa chini yake yeye siyo chini ya mshahara wa Waziri mwingine. Kwa hiyo, Wizara ya Fedha nadhani itakuwa inajitayarisha kuja na maelezo hayo wakati wao utakapofika. (*Makofi*)

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Komu, tumemaliza hilo la kwako, kwa hiyo, inabidi tuelekee kwa mtu mwingine.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Ali Salim Khamis.

MHE. ALI SALIM KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kutoka Mheshimiwa Waziri kwamba katika masuala ya kibiashara katika mchango wangu nilisema kwamba kuna bidhaa ambazo zinatoka Zanzibar kuja Tanzania Bara au ambazo zinakuja hapa Tanzania Bora kwa ajili ya kwenda Zanzibar lakini biashara hizi zikifika hapa zinalipishwa ushuru kama vile ni biashara zinazotoka nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, leo ukiangalia bidhaa za mafuta ya *petrol* na *diesel* nchi za nchi za *East Africa* zinalipishwa dola tatu kwa pipa (*port charge*) lakini mafuta ya Zanzibar yanalipishwa dola kumi. Pia maziwa ambayo yanatengenezwa Zanzibar kuja Bara yanaambiwa yalipe ushuru kama bidhaa ambayo inatoka nchi za nje wakati mwekezaji huyu ambaye amewekeza biashara hii ni mzawa na kiwanda kipo Zanzibar lakini kuna vikwazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefikia mahali *TRA* wamempa *offer* Said Salim Bakhresa kwamba ahamishe kile kiwanda chake cha maziwa kutoka kule Zanzibar kije Bara ili wampe *discount* ya asilimia 87 ya *VAT* ili kiwanda kije hapa. Sasa nilikuwa naomba ufafanuzi wa Waziri, shida hapa ni nini? Kama sikuridhika na majibu ya Waziri...

MWENYEKITI: Ngoja Mheshimiwa ili twende vizuri. Hoja yako inayotaka ufafanuzi ni nini? Kwa dakika moja. Hoja yako ni ipi unayotaka ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri?

MHE. ALI SALIM KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni biashara baina ya Zanzibar na Bara, ndiyo nataka ufafanuzi hapo kwenye masuala ya kibiashara.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Biashara. Biashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimhakikshie Mheshimiwa Ali kwamba tunazo sheria mbili pale katika Wizara yetu ambazo ni za Muungano. Kuna sheria ya Usajili na Leseni za Viwanda ni ya Muungano kwa ajili ya usajili na leseni, lakini usimamizi wa viwanda siyo wa Muungano. Usimamizi wa viwanda vya Zanzibar unafanywa na Wizara ya Viwanda na Biashara ya Zanzibar na usimamizi wa viwanda kwa upande wa Bara unasimamiwa na mimi moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kuna Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (*TANTRADE*), nayo ni ya Muungano, ndiyo maana unakuta kwamba Naibu Mkurugenzi Mkuu wa *TANTRADE* anatoka Zanzibar wakati Mkurugenzi Mkuu wa *TANTRADE* anatoka Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, masuala haya yamekuwa yanazungumzwa katika maeneo mengi na mpaka sasa hivi mazungumzo yako vizuri. Kikao cha mwisho cha Serikali ambacho kilifanyika hivi karibuni kimezungumza masuala hayo na mengi ambayo yamezungumzwa yameonekana kwamba hakuna matatizo, isipokuwa tu yale ambayo yanakiuka masharti ya mikataba ya Kimataifa. Kwa mfano, kama mtu anaagiza malighafi kutoka nje ya nchi, halafu akaileta Dar es Salaam, hapo sijataja Zanzibar, akatengeneza kwa malighafi ile, pengine ile malighafi haijatozwa ushuru inavyotakiwa kutoka kule ambako alileta. Huyu akivuka kwa mfano akauza Kenya, atalipishwa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa mwulizaji kwamba mazungumzo yaliyopo kati ya *TRA* na *Board* ya Mapato ya Zanzibar ni mazuri tu. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha yuko hapa, anaweza akadhibitisha kuhusu namna ya kumaliza changamoto zilizopo ambazo nyingine zilikuwa zinakiuka masharti ya biashara ya Kimataifa. Naibu Waziri labda angeruhusiwa akaelezea. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, leo kuna changamoto hapa. Nadhani Mheshimiwa Kakunda sijui amefunga, kwa hiyo, hataki kabisa leo hoja zake zijadiliwe hapa.

Waheshimiwa Wabunge, tunapozungumzia mshahara wa siku ya leo, tukiweka mambo ambayo hayahusiki ambayo hayatajwa kwenye hii orodha ya nyongeza ya kwanza humu; ukisema biashara kati ya Tanzania Bara na Zanzibar uwe unazungumzia yale mambo ambayo yako humu. Ambayo hayako humu, maana yake ni kwamba ni utawala binafsi. Ndiyo maana yake.

Kwa sababu hiyo, jambo ambalo tunaweza kulihoji hapa kati ya Zanzibar na Tanzania Bara ni lile ambalo linahusika kwa mujibu wa Katiba hii. Kwa sababu Waziri wa kule naye ana utaratibu, Waziri wa huku ana utaratibu kwa mujibu wa Katiba yetu.

Sasa hapa kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri, yaani kama anatoa muda, maana yake nitoe muda, mifano anayoitoa iwe ni ile ambayo biashara zilizoanzishwa ambazo zipo chini ya Idara ya Forordha. Ndiyo inavyotaja Katiba yetu hapa. Nje ya hapo, Mheshimiwa Kakunda hawezi kujibu hata kama tunazungumzia biashara. Kwa sababu yako ya biashara ambayo ni ya Tanzania Bara na yako ya biashara ambayo ni ya Zanzibar.

Kwa hiyo sasa...

MHE. ALI SALIM KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani kidogo. Mheshimiwa Waziri amekiri...

MWENYEKITI: Nakupa dakika moja.

MHE. ALI SALIM KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba kuna shida ya jambo ambalo mimi nimelizungumza na mazungumzo yanaendelea, lakini na yamekaa vizuri, lakini hajatufafanulia mazungumzo haya yanazungumzwa vipi? Kwa hiyo, hoja hii

ninayoizungumza Mheshimiwa Waziri ameelewa; na ukiangalia kwenye nyongeza ya hiyo ya mambo ya Muungano ipo, naye ametamka, amenukuu huko kwamba masuala ya leseni ni masuala ya Muungano. Kwa hiyo, swali langu ninalouliza, tunataka ufumbuzi wa jambo hili kwa sababu raia wa nchi hizi mbili wanapata shida katika masuala ya biashara, lakini leo ukichukulia mfano mmoja...

MWENYEKITI: Tuelewane vizuri, sasa hivi unasema leseni, lakini ulizungumzia ushuru. Mheshimiwa Ally Salim, twende vizuri, ulizungumzia ushuru, sasa hivi unasema leseni kwa kuwa Mheshimiwa Waziri kasema leseni ni jambo la Muungano; na ndiyo maana akampeleka kule kwa Waziri wa Fedha kwa sababu wale ndio wanaoshughulika, maana hapa umetaja mambo mengi; ukaingia na *TRA*, mradi umehama umeelekea huku na mambo kama hayo.

Sasa unayo nakala ya Katiba hapo ili nikusaidie kusoma ni kipi ambacho ni cha Muungano?

MHE. ALI SALIM KHAMIS: Ninayo.

MWENYEKITI: Kama unayo hebu tusomee nyongeza ya kwanza kwenye hiyo orodha, namba 10 hapo inaongelea biashara zinazozungumzia Idara ya Forodha. Nje ya hapo, haihusiki.

MBUNGE FULANI: Anayo.

MWENYEKITI: Eeh, atasoma. Kwa hiyo, nimeshamwelezea iko wapi. Kwa hiyo, atasoma. Tunaendelea na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi kuhusu masuala ya viwanda ambavyo vimekufa na vimeshindwa kufufuliwa kutokana na sera au ubinafsishaji ambao ulikuwa hauna tija kwa Taifa. Wawekezaji hao wameshindwa kuviendeleza hivyo viwanda. Kwa hiyo, napenda nipate ufafanuzi katika viwanda vifuatavyo:

TANCUT Iringa, Kiwanda cha Mbolea cha Tanga, Kiwanda cha Chuma Tanga, Kiwanda cha Sonamko Songea, Kiwanda cha Morogoro *Canvas*, Kiwanda cha *General Tyre* Arusha na Kiwanda cha ZZK Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini viwanda hivi vimebinafsishwa lakini mpaka sasa hivi ukiangalia hivi viwanda vingi vimegeuzwa kuwa ni sehemu ya kufugia wanyama na vimegeuzwa kuwa ni magodauni ya kuhifadhia chakula. Naomba pia ifahamike kwamba tuko katika misingi ya Sera ya Viwanda, sera ambayo tukijipanga vizuri tutakuwa tunaweza kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kupata ufafanuzi katika maeneo hayo; ni kwa nini viwanda hivi vimekufa na havina mkakati wowote wa kufufuliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti,...

MWENYEKITI: Moja tu Mheshimiwa.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Nilikuwa nataka nipate ufafanuzi...

MWENYEKITI: Utapewa fursa Mheshimiwa Jacqueline Msongozi. Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Jacqueline Msongozi kwamba tuko makini sana Serikalini na kuhusu viwanda vyote 156 ambavyo vilibinafsishwa tulivifanyia tathmini na taarifa ambayo tunayo Serikalini tangu mwaka 2018 imetupa ufafanuzi mzuri kuhusu namna ya kufufua viwanda ambavyo havifanyi kazi hadi sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa yangu na katika hotuba yangu nimesema kwamba kati ya viwanda 68 ambavyo havifanyi kazi, viwanda 20 vimefutwa kwenye

orodha ya viwanda kwa sababu viliuzwa kama mali moja moja. Mtu mwingine ananunua kiti, anaondoka; mtu mwingine ananunua labda meza, anaondoka; mtu mwingine ananunua jengo hili, anaondoka; mtu mwingine ananunua kiwanja, anaondoka. Kwa hiyo, hivyo siyo viwanda na hivyo ni pamoja na baadhi ya alivyotaja kama kile cha Iringa cha *TANCUTA* Almasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vingine alivyotaja kama cha *General Tyre*, mazungumzo yanaendelea vizuri na hivi karibuni kitafufuliwa. Viwanda vingine vilivyobaki, kile kiwanda cha ZZK Mbeya tayari tumeshapata ufumbuzi wake na tayari uzalishaji utanza hivi karibuni. Viwanda vingine alivyosema ni viwanda ambavyo vimekuwa vikipewa *notice* tangu mwaka 2018 na *Treasurer Register* mwezi wa Saba, *notice* ya mwisho ni ile ya Waziri wa Viwanda na Biashara ambapo tumsema ifikapo tarehe 31 Mei, kama hawataleta maelezo yanayojitosheleza kuhusu ufufuaji wa hivyo viwanda, vitarejea Serikalini ili vitafutiwe wawekezaji wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo maelezo sahihi. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msongozi.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kimsingi mimi sijaridhishwa na majibu ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2018 mwezi wa Tano...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msongozi, kwa ajili ya muda, kama hujaridhika, unataka hoja yako ijadiliwe, toa hoja kama Waheshimiwa Wabunge watakuunga mkono ili ijadiliwe, halafu utapewa fursa ya kuhitimisha hoja yako.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa sababu ya hoja hii mahsusi ya kuchochea uchumi katika nchi yetu, naomba sasa nitoe hoja ili Waheshimiwa Wabunge wenzangu waniunge mkono na tuweze kuichangia. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Hoja haijaungwa mkono. *(Kicheko)*

Haya, Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Augustino Vuma. *(Kicheko)*

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. AUGUSTINO V. HOLLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme tu kwamba nategemea kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri kama hatanipa majibu ya kutosha. Hoja yangu ni kwamba ustawi wa Sekta ya Viwanda na Biashara hapa kwetu ni ukweli usiopingika kwamba inategemeana na mazingira rahisi ya kufanya biashara katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, mazingira ya kuanzisha na kufanya biashara katika nchi yetu yamekuwa na changamoto kubwa na ukiritimba mkubwa mpaka kufikia sehemu Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amezionya taasisi mbalimbali ambazo zinahusika na uanzishwaji na uendeshaji wa biashara kwa kuleta urasimu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuthibitisha hilo, kwenye ripoti ya mwaka 2018 ya urahisi wa kufanya biashara duniani Tanzania imekuwa ya 144 kati ya nchi 190 ukilinganisha na mwaka 2017 ambapo tulikuwa wa 134. Kwa hiyo, naomba *commitment* ya Serikali, uko mkakati gani wa kuhakikisha kwamba ukiritimba huu katika kuanzisha na kufanya biashara unapungua na hatimaye mazingira yanakuwa ni mazuri kwa ajili ya kuvutia wawekezaji kwenye viwanda na kwenye biashara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatanipa maelezo mazuri, nitashika shilingi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, ufafanuzi.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nimwombe

sana Mheshimiwa Mbunge na Ramadhani hii aturudishie tu shilingi hiyo, naomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi kama ambavyo tulieleza hapo awali, ni kwamba Serikali imekuwa ikijitahidi kuweka mazingira wezeshi. Kwa mfano, kwa sasa hivi hata usajili wa biashara unasajilia popote nchini ulipo. Ni kweli kuna changamoto ndogo ndogo kwa mfano za kiujuzi namna ya kusajili biashara au pengine mtandao unaweza ukawa umecheza kidogo, akapata shida kidogo ya kiusajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa kushirikiana na Halmashauri zetu, wananchi wamekuwa wakisaidiwa na sasa hivi usajili umekuwa ukiendelea vizuri na pia umewezesha hata Watanzania wengi zaidi kupata Vitambulisho vya Taifa, kwa sababu anaposajili pia anatakiwa kupata na Kitambulisho cha Taifa. Vyote vimekuwa vikifanyika kwa pamoja na ndani ya siku tatu mtu amekuwa akipata namba yake ya usajili ambayo inaunganishwa moja kwa moja na TRA. Hayo ni mambo machache ya kuyazungumza

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kama tulivyosema, niombe tu kwa ridhaa yako, baadaye labda tukupe hii *Blue Print* upitia uchambue kila eneo, vyote vimeainishwa humu. Changamoto zote zimeainishwa humu. Sisi tunaamini kabisa, baada ya kuanza utekelezaji wa hii *Blue Print* ambayo ni Julai tu, kesho kutwa inakuja, naamini kabisa hali itakuwa ni nzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba wananchi hata hivyo kwa muda huu ambao tunaendelea, waendeleo kupitia katika ofisi zetu za Serikali kupata msaada wa kuondoa changamoto ambazo zinawezekana kuondolewa bila hata ya kutumika kwa hii *Blue Print*. Kwa ujumla wake pia changamoto nyingine zinatokana na utumishi, yaani za kiutawala. Kwa hizo, kwa upande wa Serikali, nawaomba sana Watumishi wa Serikali wachukue wajibu wao kuhakikisha kwamba wanawasaidia wafanyabiashara na wanaowekeza ili kuhakikisha kwamba wanapata huduma inayostahili kwa wakati. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, kabla hujakaa, *Blue Print* inaainisha changamoto au *Blue Print* ndiyo mkakati wenyewe; ili ajue kama amepata majibu au hajapata? Kwa sababu ana lengo la kushika shilingi, hajashika bado. *Blue Print* ni changamoto au ndiyo mkakati wenyewe?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Blue Print* kwanza inaainisha hali halisi ya changamoto zilizopo katika sekta husika na eneo lipi? Hata kama ni taasisi ya kiudhibiti, ina *issues* zipi? Kama ni tozo, ziko ngapi kufuatana na sekta fulani? Utatuzi wake unatakiwa uweje? Kwa hiyo, vyote vimeainishwa. Sasa kuna vingine utatuzi unahitaji mpaka mabadiliko ya sheria, lakini kuna vingine vinaweza kuanza kutekelezwa hata bila ya kubadilika kwa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sasa tumeshaanza katika baadhi ya maeneo. Kwa mfano, katika eneo la udhibiti wa bidhaa za chakula, *TBS* alikuwa anakagua na *TFDA* alikuwa anakagua. Kwa hiyo, tayari tumeshaingia makubaliano ya kukubali taarifa za baadhi ya taasisi ambazo zinakuwa zimefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Sawa. Kwa hiyo, *Blue Print* inao mkakati humo ndani. Ndiyo au hapana?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Ndiyo. Mheshimiwa Augustino Holle Vuma.

MHE. AUGUSTINO V. HOLLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli sijaridhishwa na majibu, naomba nitoe hoja sasa ili Bunge waweze kuniunga mkono na tujadili hoja hii.

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Hoja haijaungwa mkono. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa wabaki wamesimama wanaotaka kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Vuma. Mheshimiwa Mwigulu, Mheshimiwa Hawa Ghasia sijaelewa, umesimama kwenye hoja hii au una jambo lingine? Aah! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Ghasia, Mheshimiwa Shangazi, Waheshimiwa Mawaziri nimeshawaona, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Mheshimiwa Mtulia, Mheshimiwa Salome Makamba, Mheshimiwa Anatropia, Mheshimiwa Mwijage.

Mheshimiwa Mwigulu Nchemba.

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kizuri katika jambo hili tunaloliongelea ni kwamba tayari Mheshimiwa Rais kashatolea maelekezo mara kadhaa kwamba tatizo hili lilishajulikana na amezelekeza taasisi zilizo chini yake kuweza kuhakikisha kwamba wanatekeleza mambo ya aina hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili tayari *Blue Print* ilishatengenezwa ambayo imebainisha changamoto na tayari hatua nyingine zimeshaanza kuchukuliwa ambazo zinaenda kumaliza tatizo hili. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ni mpya, sio mpya sana lakini ni mpya kwenye Wizara, namwomba mdogo wangu aendelee kumpa muda kwa sababu ndiyo bajeti yake ya kwanza ili akakae na wataalamu wake walimalize tatizo hili kwa sababu tayari lilishabainishwa na Mkuu wa Serikali kashatoa maelekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungeweza kubishana hapa na kushinikiza kama Serikali ingekuwa bado haijaona tatizo la aina hii na ingekuwa bado haijatengeneza mkakati wa namna ya kuweza kutekeleza. Kwa kuwa haya yote yameshafanyika na ndiyo tunapitisha bajeti ili Mheshimiwa Waziri akatekeleze mambo haya, namwomba mdogo wangu ampe fursa Mheshimiwa Waziri pamoja na Wasaidizi wake na wataalam wake wakayafanyie kazi mambo haya na kwa kuzingatia kwamba kuna kazi kubwa sana ambayo imeshafanyika katika Wizara hii ambayo inatupa dira mpya

kwenye upande wa ufanyaji kazi wa Wizara pamoja na mazingira bora ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo halikuwa tu kwenye upande wa mazingira mabaya, kulikuwa na mambo ya rushwa pia ambayo yalikuwa yanakimbiza wawekezaji, kulikuwa na mambo ya rushwa yaliyokuwa yanatengeza mazingira mabaya ya biashara ambayo tayari Serikali imeshachukua hatua na hata ukiongea na wawekezaji na wafanyabiashara wanakiri kwamba, kusikilizwa wanapokwenda kwenye ofisi za umma kumekuwa kwa hali ya juu ambapo inatia matumaini kwamba hata hili ambalo Mbunge amelisemea litafanyiwa kazi.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami nisingependa Waziri achukuliwe shilingi yake, lakini wangetuambia hiyo *blue print* kwa sababu katika bajeti ya mwaka jana tuliambiwa kwamba *blue print* iko tayari na tulioneshwa *draft*, lakini mwaka mzima hiyo *blue print* ilishindikana kutoka. Labda kwa vile Mheshimiwa Mwijage amesimama atatusaidia kutuambia alikwama wapi na labda pale alipokwama atamsadia mwenzake kumweleza atatokatokaje. Ahsante. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salome Makamba.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Mheshimiwa Waziri lazima akumbuke kwamba sasa tuko kwenye Sera ya Tanzania ya Viwanda na kwa sababu hiyo lazima atengeneze mazingira rafiki haraka sana kuhakikisha kwamba *by 2020* tumefikia lengo hilo. Kwa mfano, mtu anataka kufungua kiwanda cha maziwa, tozo na kodi ni zaidi ya 28, Taasisi za Udhhibiti zaidi ya 11, kwangu Kahama pale wafanyabiashara wa maduka ya jumla wamekamatwa mbele ya *TV* na Mkuu wa Mkoa. Wamewekwa ndani leo ni zaidi ya miezi saba wako ndani bila dhamana, hivi

tunasemaje kwamba tunasaidia mazingira bora ya uwekezaji na biashara ndani ya nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba mifumo inafanyika, lakini *by 2020* tulitegemea ahadi ya Chama cha Mapinduzi ya kwamba tunakwenda kwenye Tanzania ya Viwanda iwe imesha-*favour* wafanya biashara wa nchi hii kwa kiasi ambacho tunazalisha malighafi ya kutosha, kwa kiasi ambacho wafanyabiashara wanaweza kufanya biashara ya kutosha kwa ajili ya kuweza kuchangia kodi tuweze kuendesha miradi ya nchi hii. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri alete *commitment* yake, nini mkakati wa karibu na wa mbele kwa ajili ya kuboresha mazingira ya wafanyabiashara katika hii nchi. Maduka mengi yamefungwa tunaongea leo hii ni kwa sababu ya ukiritimba unaofanywa na watumishi wa Serikali. Biashara nyingi zimefungwa kwa sababu ya kodi kubwa wanazopewa wafanyabiashara. Kwa hiyo siyo jambo dogo kama tunavyoliona. Miradi ya biashara *from Private Sector* ndiyo inayosaidia kwenye kodi na uendeshaji wa hii nchi kupitia ushuru... (*Makofi*)

(*Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

MWENYEKITI: Muda wako umekwisha Mheshimiwa, ahsante sana. Mheshimiwa Shangazi.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Suala siyo *blue print* peke yake, yapo matatizo mengine wala siyo ya kisheria, yapo matatizo kwa mfano barabarani, kuanzia bandarini unakutana na mizani kila baada ya hatua kadhaa, unakutana na polisi kila baada ya hatua kadhaa wanauliza jambo lile lile. Kimsingi ni kwamba, bado inaonekana kwamba hakuna dhamira na utashi wa kumaliza tatizo hili. Kwa hiyo ukiondoa matatizo ambayo ni ya kisheria lakini yapo mengine ambayo *overnight* yanaweza yakaondoka, kuanzisha *check point* maalum ambazo zitakuwa zinakagua magari yanayosafirisha mizigo ni jambo ambalo linawezekana. Hapa kinachoonekana ni utashi na

utayari wa kuondoa vikwazo katika biashara, ahsante.
(Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mtulia.

MHE. MAULID S. A. MTULIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nakushukuru kwa kupata fursa hii na naunga mkono hoja ya kaka yangu Vuma. Sisi watu wa Dar es Salaam kama mnavyofahamu sasa hivi Makao Makuu ya nchi yako Dodoma na Watendaji wa Serikali wengi, wafanyakazi wanahamia Dodoma, sisi tutabaki na biashara na mazingira magumu ya biashara yanakwenda kutufanya watu wa Dar es Salaam kuwa maskini. Biashara zinafungwa, kwa kweli hii hoja iko wazi, lazima Waziri, kama hiyo *blue print, blue print* inakuja na dawa ya namna gani biashara zetu zitakuwa hai, zitaboreka, kwa kweli hilo ndiyo jambo tunalohitaji, hakuna namna ya kufanya Watanzania wakaagiza bidhaa kutoka Uganda ilihali sisi tuna bandari, hiyo namna hakuna. Hakuna namna ya Kariakoo ya zamani iliyokuwa inaleta watu kutoka East Africa yote na Central Africa kuwa leo watu hawaji. Sasa hii lazima tu, tatizo ni kubwa hili...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana, kengele imeshagonga Mheshimiwa. Mheshimiwa Anatropia.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naunga mkono hoja ya kaka yangu hapo, lakini kama kuna kitu hatupaswi kujidanganya nacho kwamba *blue print* itakuja kumaliza matatizo ya wafanyabiashara na changamoto za biashara hapa nchini, siyo kweli. Tunachokihitaji leo ni Sera ya Biashara, tunaendaje, sisi kama Taifa ni namna gani tunataka biashara zetu ziende. Tunavyoongea leo hatujulikani sisi ni wajamaa au sisi ni wabepari au tuko wapi. Tukishapata sera, tukishabainisha hiyo sera, sera itaeleza, unataka kufanya biashara, utapokelewa vipi katika nchi ya Tanzania, utafanya moja, mbili, tatu. Unavyoongelea *blue print* haina tofauti na

unavyotoka mfano ukitoka Dar es Salaam utapita sijui kwenye *bus stop*, utakutana na *check point*, utakuja utafika Dumila, halafu utakuja Dodoma. Tusijidanganye na *blue print*, tuangalie changamoto kubwa zinazokabili sekta ya biashara nchini ikiwa ni pamoja na mlolongo wa tozo. Mlolongo wa tozo haziishi kwa kuandika kwamba usitoze moja, mbili, tatu, no! Tunahitaji utayari, tunahitaji *mental transformation* ya Watanzania. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Mary Nagu.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nami nakubaliana na Mheshimiwa Vuma kwamba urahisi wa biashara unaifanya nchi iwe na ushindani mkubwa na nchi nyingine na vilevile inaleta ufanisi. Namwomba arudishe shilingi ya Waziri kwa sababu kuna mipango mikubwa mingi ikiwa ni pamoja na *blue print*. Kwenye *blue print* kuna namna ambavyo Serikali itafanya ili iweze kufanya biashara iwe rahisi. Siyo hivyo tu, wakati tukijadili bajeti hii tulisema namna pekee ya kuifanya biashara iwe rahisi ni kuwa na *one stop centre* na tukasema tayari Rwanda inayo, tunaweza kwenda kucheki pale na sikusikia Waziri akikataa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba wengine wote ambao wanataka kung'ang'ania shilingi ya Mheshimiwa Waziri huyu, wajaribu kuirudisha ili aifanyie kazi Wizara hii, siyo rahisi, lakini kwa Dokta huyu anafanya kazi kwa bidii, nina hakika biashara itakuwa rahisi na anajua kwa nini anataka kuifanya kuwa rahisi. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Charles Mwijage.

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nasimama kumwomba ndugu yangu Mheshimiwa Vuma arudishe shilingi na maelezo yangu nikianza na Mheshimiwa Hawa aliyenitaka nizungumze, arejea ukurasa wa pili wa kitabu hiki, aya namba nne. *Blue Print Regulatory Form* kama alivyosema Mheshimiwa Kairuki ina *roadmap*, vile vilivyoainishwa na kama alivyosema

Mheshimiwa Anatropia ni kwamba tuta-*change mindset*, ukiangalia ile picha nzima ya *blue print* kila mtu ameguswa. Hata wewe Mtanzania unayenuna unasababisha mazingira ya biashara yawe mabaya, hata wewe usiyemsalimia mwekezaji, tutazaliwa upya. *Blue print* kwenye *roadmap* itatubadilisha wote Watanzania, wageni wote, wawekezaji wa ndani na nje itabidi wote tuwe wazuri, tuzaliwe upya, ndiyo tuweze kuwekeza hapa. Namwomba sana Mheshimiwa Mbunge amrudishie Mheshimiwa Waziri shilingi yake akafanye kazi, pale siyo mchezo. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Angella Kairuki.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI):

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Napenda tu kusema kwamba kwa kweli wamrudishie Mheshimiwa Waziri shilingi yake na hapo ukiangalia hoja kubwa walikuwa wakitaka kujua kuna mkakati gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Waziri ameeleza na Naibu wake mkakati uliopo katika Serikali, lakini pia nami katika maelezo yangu wakati nachangia nimeeleza. Mtu anasema kwamba *blue print* siyo suluhusho, ndani ya *document* hiyo ya *blue print* kwanza ilikuwa ni kubainisha changamoto na vikwazo ni vipi na kwa sasa ambacho Wizara ya Viwanda na Biashara inakifanya, inaandaa mpango kazi au *blue print action plan* ambao ndiyo mkakati wenyewe wa utekelezaji. Tayari wamefikia katika hatua ya mwisho, wakati wowote itatoka, tena nilidhani tungepaswa kupongezwa kama Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba mpango kazi bado haujapita, juzi wamemsikia Waziri wa Afya tayari yenyewe *on her own volition* ameshakuwa yuko yatari kupitia Kanuni ambazo yeye ameziandaa, wamefuta takribani tozo 25 kama nitakuwa sijasahau vizuri kupitia *TFDA*. Nimeeleza asubuhi pia, kupitia Bodi ya Nyama, Bodi ya Maziwa, *TBS*, Mheshimiwa Jenista tayari kupitia *OSHA* amefuta zaidi ya tozo tano, katika madini pia uzalishaji wa chumvi tumefuta zaidi ya tozo tisa, zote hizi ni hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia la pili, tumeeleza, Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye kwa sasa ndiyo anasimamia masuala ya uwekezaji, ameitisha kikao tarehe 17 Aprili, lakini na Jumamosi hii pia tuna kikao siku nzima, Mawaziri wote ambao tumeguswa katika *blue print* ile, tunaenda kuangalia pia kwa kina, mapendekezo ambayo yalitolewa katika *blue print* pamoja na kwamba bado *action plan* haijamalizika, nini kifanyike kwa haraka wakati huo *action plan* pia inamalizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la tatu, Mawaziri pia kupitia Kanuni ambazo wanaziandaa na kwenyewe pia wanaziangalia ili kuweza kuona ni vitu gani ambavyo wanaweza wakaviondoa ambavyo vimekuwa vikileta mkwamo. Pia vilevile Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Mawaziri husika kupitia uongozi wa Mheshimiwa Jenista wamekuwa wakifanya vikao kuangalia ni kwa namna gani pia taasisi za udhibiti ambazo zimekuwa zikiwa na mwingiliano nini kifanyike ili kuweza kuondoa baadhi ya majukumu kupitia taasisi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano katika *TBS*, *TBS* na *TFDA* kumekuwa kuna mwingiliano wa majukumu katika udhibiti wa vyakula na lenyewe pia ni muhimu liangaliwe. Kama ni katika suala la udhibiti wa sukari, nini kifanyike na Bodi ya Sukari, nini kifanyike na *TFDA*, nini kifanyike pamoja na *TBS*. Kwa upande wa wepesi wa kufanya biashara, kuna viashiria zaidi ya 11, imeelezwa vizuri sana. Sisi tumechukua *rank* namba 144 katika nchi 190, lakini ukiangalia kila tunapofanya maboresho na *improvement* mbalimbali katika wepesi wa kufanya biashara, tukumbuke pia kwamba na nchi za wenzetu nao hawajalala na wenyewe pia wanafanya maboresho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo unaweza ukajikuta leo una namba 144, kesho ukawa 145 muhimu ni kuhakikisha kwamba tunapiga hatua, tunaboresha huduma zetu tunazozitoa kwa wafanyabiashara na wawekezaji, lakini zaidi kuhakikisha kwamba katika vile viashiria kama ni katika suala zima la kufunga masuala ya ufilisi, kama ni katika suala la

kuanzisha biashara, kama ni katika suala la kusajili *property* au mali yako hatua zipi zimewekwa. Nipende kusema kama ambavyo nimeendelea kuisitiza, muhimu tu na sisi kama Wabunge tunapokuja kuombwa maoni na wale wanaofanya tafiti kupitia Benki ya Dunia basi hebu tutoe maoni ambayo ni mazuri kwa sababu watakuja kuwahoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapokuwa wanatoa taarifa ambazo si nzuri, unakuta labda *TRA* wamefanya maboresho yao kupitia malipo ya kodi, wao wakisema chochote vibaya pia ndiyo wanavyovirekodi na ndiyo vinavyokuwa *determine* katika *rank* yetu kama Taifa. Kwa hiyo, naomba wote tuwe wazalendo na tuweze kusemea yake mazuri ambayo yanafanywa na Taifa letu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jenista Mhagama.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, ameliweka vizuri sana suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kubwa ambalo limenifurahisha, kazi ya *blue print* imefanywa kwa kiasi kikubwa sana na Mheshimiwa Charles Mwijage ambaye amezungumza hapa karibuni. Amesema hapa, ukiitazama *blue print* maana yake halisi ni kufanya mabadiliko yote ya kiseru, ya kisheria, ya kimitazamo wa nchi yetu na kutupelekea sasa kutengeneza mazingira wezeshi ya kusaidia suala zima la ufanyaji biashara liwe sawasawa ndani ya nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *blue print* naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, kila hoja ambayo ilikuwa inakwamisha mazingira wezeshi ya uwekezaji na ufanyaji wa biashara nchini, *blue print* ime-address maeneo hayo yote. Sasa shida hapa kubwa ninachokiona ambacho sisi kama Serikali ni lazima tuchukue sasa jukumu letu, ni *commitment* yetu ya kuhakikisha tunaisimamia *blue print* kwa

kiasi cha kutosha na kwa haraka iwezekanavyo. Tukifanya hivyo, naamini kama tutaisimamia vizuri *blue print* tutakapofika hapa mwakani, hoja hii ya mazingira wezeshi ya ufanyaji wa biashara nchini itakuwa imekwisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, kutambua matatizo hiyo ni hatua kubwa sana na wanapaswa kuipongeza Serikali na wamemshuhudia Mheshimiwa Rais wetu, kila mwaka amekuwa akiitisha Baraza la Taifa la Biashara na kuzungumza na wafanyabiashara na wawekezaji mbalimbali ili kuendelea kuzitambua kero mbalimbali kwenye eneo zima la ufanyaji biashara na uwekezaji nchini. Kwa hiyo naomba niwahakikishie Wabunge, Rais wetu na Serikali yetu tumejizatiti, kwa kweli hata sisi tusingependa kuona kwamba Taifa letu linakuwa ni eneo ambalo si zuri na halina sifa ya ufanyaji biashara na uwekezaji kwa sababu *private sector* ni nguzo muhimu sana ya kujenga uchumi katika Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawahakikishia tukianza kuitekeleza *blue print* na kuisimamia, habari zote za vibali vya ajira, tozo na mambo mengine yote tutakuwa tumeweza kuyashughulikia kwa kiasi kikubwa. Mheshimiwa Vuma kwa heshima kubwa sana, naomba amrudishie shilingi mzee akaanze kufanya kazi ya kusimamia *blue print* na uwekezaji na ufanyaji biashara wepesi katika Taifa letu. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Augustine Holle Vuma, hitimisha hoja yako.

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli niseme kaka yangu Mwijage amenishawishi na dada yangu Kairuki amenishawishi, lakini *Chief Whip* pia amenishawishi. Niseme kwa ujumla nimeelewa hoja za msingi za Serikali ya Chama cha Mapinduzi, sasa naachia shilingi. Ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda nadhani utusaidie Waheshimiwa Wabunge wakipata nakala za hiyo *blue print* ili na wao wawe

wanasoma waweze kuangalia Serikali inaelekea wapi. Ili na wao wakati wanashauri, wawe wanashauri wakiwa wanajua sasa tumefikia hapa, tunaielekea hapa. Kwa hiyo nadhani ulitaka kusema unataka kutupa nakala! Nadhani ulitaka kusimama.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokea ushauri huo, tutagawa *blue print* kabla ya tarehe 31 Mei, 2019. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, sasa Waheshimiwa Wabunge tusipige tu makofi halafu tusisome, tusome ili tuweze kuishauri Serikali vizuri.

Waheshimiwa Wabunge basi tunaendelea, nimuite sasa Mheshimiwa Cecil Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nakusudia kushika shilingi mpaka nikipata ufafanuzi wa kutosha kabisa majadiliano na Mheshimiwa Waziri aweze kutueleza. Suala langu kubwa sana linahusiana na masuala ya *value addition* hasa zaidi kwenye zao la pamba kwa maana ya *cotton to cloth* pamoja na masuala ya korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao haya mawili niliyoyataja ni mazao makubwa kabisa ya kimkakati Tanzania, lakini kwenye suala la *cotton to cloth* ndiyo ambapo hasa nataka niweke hoja yangu kwamba kwa muda mrefu sana na tutaitaka Serikali itueleze kwa sababu tumeona hata leo majibu yaliyokuwa yanatolewa kuhusiana na masuala ya mafuta kuna ugomvi na watu wanaoingiza mafuta na wawekezaji na wengine. Sasa tunataka tuone mpango mahususi kabisa na hapa Mheshimiwa Waziri alikuja akatueleza kwamba sasa hivi anatushauri hata sisi Wabunge tuanze kuvaa nguo zinazotengenezwa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri chote kama ambavyo amefanya miaka yote, amekuja tu na hadithi nzuri kabisa, lakini hakuna *proper*

narrations zinazoonisha sasa tunakwenda *from cotton to cloth* na mazao yake yale mengine yote pale katikati ikiwemo mafuta pamoja na mbegu. Sasa Waziri nataka atueleze kinaga ubaga na atoe hapa *commitment* yako mpango huu wa *cotton to cloth* unaanza kutekelezwa lini Tanzania. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, ufafanuzi.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza katika hilo nakubaliana na Mheshimiwa Mwambe kwamba Tanzania ina *potential* kubwa ya kupata mafanikio kupitia *value addition* katika mazao ya kimkakati na hususan hili zao la pamba. Kimsingi upo mkakati wa *C to C* ambao unaainishwa pia na kusaidiwa na mpango wa *ASDP II* ambao tunataka kuangalia toka uzalishaji. Mbegu ziweze kupatikana ambazo zinaweza kutoa manufaa mazuri kama ni pamba, pamba nyeupe yenye vinyoleo vile yaani vyenye tija, lakini vilevile kupata mazao makubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunaangalia katika uwezekano wa kuendelea kufufua viwanda vilivyokuwepo, lakini pia kuwahamasisha wawekezaji kuja kuwekeza katika maeneo mbalimbali ambayo tunayaainisha katika Kanda hiyo hususan maeneo ya Mwanza, Shinyanga mpaka Tabora na Simiyu. Nampongeza sana Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Simiyu kwa jitihada ambazo pia ameshazianza katika kilimo cha pamba lakini pia hata Mkoa wa Kagera na kuweza kuvutia uwekezaji zaidi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunaendelea kutoa mafunzo kwa wananchi kupitia hawa wawekezaji ambao wamekuja kuwekeza nchini. Kwa mfano, katika sekta ya nguo wananchi wengi wanapata mafunzo ya ushonaji, wanashona kwenye viwanda vile lakini baadaye wanaweza kufungua viwanda vyao vidogo vidogo vya ushonaji kupitia vitambaa vinavyozalishwa nchini na kuendelea kuhamasisha wawekezaji wengine kuwekeza hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kimsingi ni mpango mkubwa na uko *complicated* lakini kwa sababu una ushirikiano mkubwa wa wananchi wenyewe, tunaamini kwa jitihada hii ya pamoja kati ya Kambi ya Upinzani, upande huu wa Chama Tawala na tukiendelea na moyo huu wa pamoja wa kuleta mawazo chanya, naamini kabisa tutafanikiwa. Kwa hilo, nampongeza sana Mheshimiwa Mwambe. Nimwombe kwa dhati kabisa, Mzee Cecil, Mstaafu wa Chama cha Mapinduzi ambaye tunamwomba urudi tena, tunaomba atuachie shilingi. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cecil Mwambe, naona umesimama.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, sisemi suala hili kwa ajili ya manufaa yangu mimi na watoto wangu bali ni kwa ajili ya manufaa ya Taifa hili kwamba hata siku za nyuma, Tanzania ni kati ya nchi ambazo zilikuwa zinazalisha pamba nyingi sana lakini tumeacha hii *opportunity* sasa hivi imeachiwa Sudan na maeneo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe hoja ili Wabunge waniunge mkono, tujadili jambo hili kwa sababu maelezo anayotoa Mheshimiwa bado siyo ya kimkakati ambayo tunataka tuyaone wazi yanakwendaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono. Naomba Waheshimiwa Wabunge wanaotaka kuchangia ndiyo waendeleo kusimama. Mheshimiwa Mgumba, Mheshimiwa Mashimba Ndaki, Mheshimiwa Upendo Peneza, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda na Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

Waheshimiwa Wabunge, sijui kama muda utatosha, wengi kweli mmesimama. Mheshimiwa Nyongo na

Mheshimiwa Ally Saleh. Nadhani hawa wanatosha. Tuanze na Mheshimiwa Mashimba Ndaki.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niseme tu kwamba mkakati wa C2C unaendelea na umeanza kuzaa matunda. Moja, zao la pamba miaka ya hivi karibuni limeanza kuongezeka kulimwa lakini pia linapovunwa limeongezeka. Mwaka juzi lilikuwa kidogo, mwaka jana limeongezeka, mwaka huu pamba iliyolimwa ni nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa C2C inaanzia kwenye pamba kuelekea kwenye nguo kama alivyosema Mheshimiwa Mwambe. Mimi nilikuwa nataka nimsihi Mheshimiwa Mwambe kwamba C2C kwa sababu imeanza kuonesha matunda kuanzia kwa mkulima mwenyewe ambaye ndiye ambaye analengwa hasa ili kipato chake kiweze kuongezeka, tuiache Serikali kwa sababu imeanza kutekeleza mkakati huu kupitia ASDP // iendelee halafu tutaipima baada ya ASDP // kuisha kuona kama mkakati huu umefeli au umefaulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mwambe arudishe shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu asipoirudisha mkakati mzima unakwama, hautafikia mwisho na hatutaona matunda yake. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Upendo Peneza.

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala ambalo liko mbele yetu kwa maana ya kutoka kwenye pamba mpaka kufika kwenye nguo tunazungumzia *value chain* yote ambayo inahusika mpaka pale ambapo unapata hizo nguo zenyewe. Suala hili ni la msingi sana kuhakikisha kwamba kama Wizara inaweza ikalifanyia kazi kuanzia kwa wakulima wenyewe mpaka kufika kwenye huo uzalishaji wenyewe mpaka upate hizo nguo kwa sababu ni jambo kubwa ambalo kwanza litawasaidia wakulima wetu katika maeneo ambayo tunatoka lakini litalisha viwanda ambapo

hata sasa hivi Kanda ya Ziwa watu wangeweza kuwekeza kwa kiasi kikubwa lakini hata pamba yenyewe haitoshi na uzalishaji wote ambao ungetokea ungeweza kusaidia upande mzima wa ajira. Kwa hiyo, niseme tu kwamba ni lazima Serikali itoe *commitment* na ni kwa kiasi gani hasa inapanga kuboresha hiyo *value chain* yenyewe mpaka kuweza kuzipata hizo nguo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa kuongelea mikakati ambayo ipo ambayo pia imesemwa na Mheshimiwa Ndaki, cha kujuliza hiyo mikakati ambayo ipo ina pesa kiasi gani? Hiyo mikakati ambayo ipo kama nchi tumetenga hela kiasi gani kuisaidia miradi hiyo unaona hakuna pesa.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa, kengele imegonga. Mheshimiwa Saleh.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hapana shaka pamba inalimwa sana nchini Tanzania na wakulima wako kwa maelfu na nchi hii ilikuwa na viwanda vingi, ilikuwa inavaa nguo za viwanda vyetu lakini ilikuwa ina viwanda vingi vya mafuta na mambo mengine. Hoja aliyoleta Mheshimiwa Mwambe ni muhimu kama alivyosema Mheshimiwa Upendo, tunachozungumzia hapa ni *value chain* ionekane. Kila *section* ionekane ina faida yake, inavyotoa ajira au mazao ili iweze kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kama Serikali imeweza kuzungumzia suala hili lakini mtoa hoja anachotaka ni kusikia Serikali ikisema *what is the next step* baada ya kusema nini kimetetelezwa mpaka sasa hivi na tunakwenda wapi ili *value chain* na mapato yaongezeke kwa wananchi lakini pia Serikali iweze kupata kodi zaidi. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi namuunga mkono mtoa hoja Mheshimiwa Cecil Mwambe kwa sababu tumesema Taifa letu linaenda kwenye viwanda na ni kweli kabisa tunashukuru muasisi wa Taifa hili aliweza kuanzisha viwanda vingi sana *MWATEX*, Mbeya tulikuwa tuna kiwanda cha nguo na viwanda vinginevyo. Wizara hii haituambii, pamoja na mkakati tulionao wa kuwa na viwanda vingi, vile vilivyokuwepo tumefikia wapi? Hili zao la pamba ambalo ni la muhimu sana, tulikuwa na malalamiko makubwa ya kuwa na pamba isiyokuwa na thamani, wameisimamiaje kama Wizara, wamelipaje wakulima waweze kutoa kitu chenye thamani ambacho kinaweza kikatusaidia sisi katika kupata hizo nguo na vitu vingine ambavyo tunavizungumzia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama wananchi wa Tanzania pamoja na Serikali ni lazima tuwekeze, tuhakikishe kwamba kile ambacho tunakikusudia kinatendeka. Wamezungumza wenzangu *value chain* inakuwaje pale, kutoka kwa mkulima mpaka kutokea nguo kamili, hapa katikati waliofaidia ni watu wa aina gani? Sasa hivi tuna malalamiko ya ajira kwa vijana, je, hivi viwanda vidogo vidogo au hata wale wanaoshughulikia suala la pamba lenyewe wamefaidikaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi namuunga mkono, naomba Serikali iweze...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Kengele imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana. Mheshimiwa Omary Mgumba.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza na mimi nimuombe Mheshimiwa Cecil Mwambe amuachie tu Mheshimiwa Waziri shilingi yake. Kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, suala hili tunalitekeleza katika mpango wa *ASDP II* na kuna Wizara zaidi ya sita tukiwepo sisi

Wizara ya Kilimo, Viwanda, TAMISEMI, Waziri Mkuu pamoja na Wizara ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi gharama za uzalishaji ni kubwa kwa hiyo pamba nyingi inakwenda nje kwa sababu wana-*offer* bei kubwa. Kwa mfano, viwanda vyetu vya ndani, *ginnery* zilizokuwepo zina uwezo wa ku-*process* pamba tani 900,000 lakini uzalishaji wetu ndiyo umeweza kuongezeka tani 200,000 tu mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wizara ya Kilimo na Serikali kwa ujumla mipango yetu ni kuongeza uzalishaji wenye tija kufikia tani 1,000,000 ndani ya miaka miwili ili kuweza ku-*feed* viwanda vyetu hivi na kuwavutia wawekezaji wengi waje kuwekeza kwa ajili ya huo mnyororo wa thamani. Ni nia ya Serikali yetu kutengeneza mpango mzuri ili mnyororo wa thamani ukamilike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa tuliyokuwa nayo katika kilimo ni tija ndogo na ndiyo maana kama Seriakli tumeanza kufanya tathmini ya udongo nchi nzima ili kujua mahitaji ya afya ya udongo, udongo unaumwa nini ili kuupa mbolea sahihi ili wakulima hawa waongeze uzalishaji tuweze kuvipa *material* ya kutosha viwanda vyetu. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Stanslaus Nyongo.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nami niungane na wenzangu kumuomba Mheshimiwa Cecil Mwambe amuchie shilingi Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kusema kwamba katika ule mpango ambao amezungumza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo hapa, *ASDP* ina mikakati mikubwa minne. Mwanzo inashughulika zaidi na masuala ya *production*, wamejikita kuangalia namna ya ku-*increase production* kwa mazao yote. Katika *level* hiyo wanafanya

research and development kuangalia ni namna gani ya kuongeza *production*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kingine walichojikita katika programu hii ni masuala ya *processing*, kuangalia ni namna gani wataweza kuchakata mazao yanayotokana na kilimo. Kwa hiyo, katika pamba tayari kuna mikakati mizuri ambayo imekwishaanza na mfano mzuri katika Mkoa wetu wa Simiyu tumeingia mkataba na makampuni ya Uturuki kuangalia namna ya kuweza kuchakata mazao ya pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ukizungumzia C2C ndani yake kuna *textile industry* na *textile industry* inahitaji *coordination* ya Serikali kwa maana ya kuwawezesha wale wafanyabiashara au wawekezaji kuwekeza katika maeneo tofauti tofauti kufanikisha *production* ya nguo. Ukiangalia hata ku-*produce* shati kunahitajika kiwanda cha kifungo, cha nyuzi na cha rangi, kwa hiyo, kuna mambo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili kuweza kufanikisha ile *production* nzima ni kwamba ni lazima Serikali iweze ku-*coordinate* na tayari mkakati huo umeshafanyika. ASDP imeangalia hadi namna ya kuweza kufanya *promotion* ya mazao mbalimbali na kufanya *environmental protection*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimjulishe Mheshimiwa Cecil Mwambe kwamba masuala haya yanafanyiwa kazi na yamekwisha kuanza. Naomba tu atuachie shilingi Mheshimiwa Waziri aendelee kufanya kazi yake. Ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Concern* ya Mheshimiwa Mwambe na Waheshimiwa Wabunge wenzangu ni kuona *value chain* ya pamba inatekelezwa kupitia hii sera ya *Cotton to Cloth (C2C)*. Kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri mwenza, pacha wangu

Mheshimiwa Mgumba pamoja na Mheshimiwa Mashimba Ndaki, Mheshimiwa Nyongo na wengine, hatua ya kwanza ya Serikali ya utekelezaji wa C2C ni ile hamasa ambayo tumeiweka kwenye kilimo cha pamba. Mwaka jana uzalishaji wa pamba ulikuwa ni tani 222,000 lakini msimu huu ambao tumeuzindua tarehe 1 Mei, tunategemea kuvuna zaidi ya tani 400,000. Kwa hiyo, hatua ya kwanza ni kuhakikisha tunahamasisha wakulima tupate pamba ya kutosha kwa ajili ya kuchakata viwanda vya pamba nyuzi pamoja na viwanda vya ngu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kwamba tumehakikisha viwanda 18 (*ginneries*) vinafanya kazi kupembua mbegu pamoja na nyuzi za pamba ambazo tunazihitaji kwa ajili ya kujenga uchumi wa viwanda. Sambamba na hilo, Serikali imeshatuma *delegation* Ethiopia kuangalia wenzetu walivyofanya mageuzi ya kufungamanisha kilimo cha pamba na viwanda. Wao wana *industrial parks* zisizopungua 50 na tayari kwenye maazimio ya mkutano wa wadau ambao tumefanya mwezi huu na sisi tutashirikiana na Wizara ya Viwanda kuhakikisha tunatenga haya maeneo maalum...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 104 sasa tunaingia kwenye kupitisha mafungu yote kwa pamoja. Katibu!

Kif. 1001 – *Administration and Human Resources Management*.....Sh. 12,929,375,000/=

Kif. 1002 – *Finance and Accounts*Sh.397,870,000/=

Kif. 1003 – *Policy and Planning* Sh.1,153,972,000/=

Kif. 1004 – *Gvt. Comm. Unit*Sh.128,048,000/=

Kif. 1005 – Internal Audit Unit.....	Sh.198,520,000/=
Kif. 1006 – Legal Services Unit.....	Sh.195,268,000/=
Kif. 1007 – Mgt Information System.....	Sh.240,836,000/=
Kif. 1008 – Procurement Mgt. Unit.....	Sh.221,753,000/=
Kif. 2001 – Industry.....	Sh. 6,595,559,000/=
Kif. 2002 – Small & Medium Enterprises Division.....	Sh.5,488,251,000/=
Kif. 4001 – Statistics.....	Sh.100,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 60 – Biashara

Kif. 3001 – Commerce Division.....	Sh.1,401,952,437/=
Kif. 3002 – Investment Division.....	Sh. 0
Kif. 4002 – Commodity Market Development Division.....	Sh.19,833,335,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 44 – Viwanda

Kif. 1001 – Administration and Human Resources Management.....	Sh.1,800,000,000/=
Kif. 1003 – Policy and Planning Unit.....	Sh.6,540,000,000/=
Kif. 2001 – Industry.....	Sh.37,160,000,000/=
Kif. 2002 – Small and Medium Enterprises Division.....	Sh.6,000,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 60 – Biashara

Kif. 4002 – Commodity Market Development Division.....	Sh. 0
--	-------

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge lllirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja, taarifa.

T A A R I F A

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 104(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake zote. Naomba sasa taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa utaratibu wetu, sasa nitahoji kuhusu hoja ya Waziri wa Viwanda na Biashara kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Viwanda na Biashara yalipitishwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nianze kwa kuwashukuru sana kwa kazi nzuri mliyoifanya kuanzia ngazi ya Kamati lakini pia humu ndani wale ambao siyo wajumbe wa Kamati husika kwa michango yote mliyoitoa na namna ambavyo Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wameipokea michango yenu na namna itakavyoboresha utendaji kazi wao.

Waheshimiwa Wabunge, pia kwa namna ya kipekee, niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na Watendaji wenu huko maofisini kwa maana ya Makatibu Wakuu na Manaibu wao, kwa kazi nzuri mliyokwisha kuifanya lakini na ambayo mtaenda sasa kuifanya kwa fedha hizi ambazo mmeidhinishiwa na Bunge. Tunaamini kama ambavyo mmetuahidi kwamba mawazo ya Waheshimiwa Wabunge mtaenda kuyafanyia kazi kwa maana ya kuboresha pale ambapo Wabunge wameonesha malalamiko kutoka kwa wananchi wao wanaowawakilisha humu ndani. Maadam watendaji kazi wenu pia wako hapa, naamini mengine watakuwa na wao wameyachukua na mtaenda kuyafanyia kazi kwa pamoja. Tunaamini mtakapokuja wakati mwingine basi mambo mengi ambayo Wabunge wamelalamikia mtakuwa mmeshayarekebisha. Tunawatakiya kila la kheri kwenye utekelezaji wa Bajeti ya 2019/2020. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe leo tunao mwaliko wa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa futari mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge, itafanyika hapo kwenye viwanja vya Bunge. Kwa hiyo, mtakapotoka tu hapa tuelekee hapo, wengine wataanza kwa sala na wengine wale ambao kidogo tumevaa kwa *style* ambazo pengine hazijakaa kifutari tutakuwa tukijitengeneza vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, kuna mambo machache ya kukumbushana kidogo hasa kuhusu matumizi ya lugha, mchanganyiko wa lugha wakati mwingine umezidi sana mpaka Taarifa Rasmi za Bunge hazikai sawasawa. Kwa hiyo, kama ambavyo sisi tunapata fursa ya kwenda huko kwa wenzetu tumeona hakuna mtu huko kwa wenzetu

anayechanganya na lugha ya Kiswahili anapozungumza lugha yao. Kwa hivyo, hata sisi tunapozungumza lugha yetu tujaribu kuongea kwa taratibu, huna haja ya kuongea haraka sana mpaka unachanganya na lugha nyingine na kufanya mchango wako mzima unakuwa kama hauko rasmi. Kwa hiyo, tujitahidi kwa sababu tunataka kukuza vya kwetu ni pamoja na lugha yetu sisi wenyewe. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kuna misamiati ambayo ni mirahisi kabisa wala haina sababu ya kuchanganywa. Kwa hiyo, tujitahidi kwa sababu jumba letu hili ni rasmi sana na sisi tujitahidi kutumia lugha rasmi. Tunapochanganya sana kila sentensi umeshachomeka humo maneno inaonekana lugha yetu haijitoshelezi. Kwa hiyo, tufuate Kanuni zetu Waheshimiwa Wabunge, tujitahidi kadri tunavyoweza, ndivyo Kanuni zetu zinavyosema lakini tukilifanya ni jambo la kawaida basi Kiswahili chetu hakitakua kama sisi hapa Bungeni tunachanganya mambo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine la jumla, kuna malalamiko kidogo hasa kutokea upande wa Kambi ya CUF. Makatibu Mezani niwakumbushe sisi tunapokea taarifa kutoka kwa viongozi rasmi wanaotambulika na Bunge, tofauti na hapo kila mtu akituletea ujumbe hapa mbele, ukiniletea mimi sawa ninao uwezo wa kufanya maamuzi lakini ukiwaandikia Makatibu moja kwa moja halafu ikatokea tukaita majina yale ambayo hayakuletwa na viongozi rasmi inakuwa ni shida kidogo. Ukiniletea mimi maana yake mimi natumia muda wangu ama mamlaka niliyonayo kumpa huyo mtu fursa ya kuzungumza lakini tuandikiane hapa Mezani kwa kufuata utaratibu kutoka kwenye kambi zetu zote. Asichukue mtu hatua ya kujiandikia yeye mwenyewe kuleta hapa mbele unawachanganya Makatibu Mezani halafu tunaleta malalamiko ambayo hayana sababu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, lingine kwa sababu muda wetu umeshafika, kwa upande wa Wizara na wataalam wenu wako hapa pamoja na kupenda vile vitu vyetu vya nyumbani nadhani yale yote mliyoyazungumza na naamini kwa sababu hiyo *blue print*, sijamaliza kusoma lakini

nimeshaanza kusoma naamini kuna mahali patakuwa panazungumzia mlolongo mzima wa zile kodi, ushuru na tozo unafanya uzalishaji unakuwa juu sana na kwa hivyo gharama za vitu vyetu vya ndani zinakuwa juu.

Kwa hiyo, mtu anaona ni afadhali akanunue kile cha nje kwa sababu gharama yake iko chini kuliko kile cha ndani hata kama thamani yake inaendana kabisa na ule uzito wa hicho kitu chenyewe ama ile thamani ya utengenezaji lakini gharama ikiwa juu sana mtu anaona ni afadhali anunue kile anachoweza kununua.

Kwa hiyo, mtusaidie ili gharama ziwe za kawaida lakini hapa lilishawahi kuulizwa swali kuhusu vipimo pia. Khanga zetu hapa zimepungua vipimo kwa hiyo sisi ambao Mwenyezi Mungu ametujaalia, kidogo zile khanga zinakuwa hazitutoshi vizuri. Kwa hiyo, hayo nayo myaangalie, naamini hilo liko ndani ya uwezo wenu pia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, niwatakie futari njema. Naamini tutaonana hapo nje.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.02 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,
Tarehe 16 Mei, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*